

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 7 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NDG. JUSTINE MONKO – K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 186

**Faida na Changamoto za Mfumo wa Vyama Vingi**

**MHE. ALI SALIM KHAMIS (K.n.y. MHE. ABDALLAH HAJI ALI)** aliuliza:-

Mfumo wa vyama vingi Tanzania ulirudishwa nchini hata baada ya Tume ya Nyalali kubaini ni asilimia ishirini tu ya Watanzania ndio waliotaka mabadiliko.

(a) Je, baada ya miongo miwili na nusu ni faida gani za mfumo huo zilizopatikana?

(b) Je, ni changamoto zipi ambazo zimejitokeza na kuwa mtihani katika suala hili la vyama vingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kama ilivyokuwa mfumo wa demokrasia ya chama kimoja cha siasa una faida na changamoto zake. Tangu mfumo huo uliporejeshwa mwaka 1992 kumekuwa na faida zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; mfumo umewezesha kupanuka kwa wigo wa demokrasia ya siasa ya vyama vingi ambapo hadi sasa kuna vyama vya siasa 19 vyenye usajili wa kudumu.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi katika chaguzi za kisiasa kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; kumekuwepo kwa ongezeko la uhuru wa kuchagua wagombea wa vyama vya siasa vilivyonadi na kushindanisha sera zao wakati wa kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; ni kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza zikiambatana na mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; ni kuongezeka kwa gharama za kuendesha chaguzi za kisiasa katika ngazi mbalimbali za uchaguzi. Aidha, kuongezeka kwa gharama za ruzuku ya Serikali kwa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu na uwakilishi Bungeni na katika ngazi ya Serikali za Mitaa wawakilishi katika Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kuibuka kwa makundi ndani ya baadhi ya vyama vya siasa ambapo viongozi wamekuwa hawafanyi siasa za kistaarabu na kuchochea vurugu katika jamii, hasa nyakati za Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge, Chaguzi ndogo za marudio pamoja na Chaguzi za ngazi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; ni kushuka kwa uzalendo wa wananchi kutokana na baadhi ya wanasiasa kushabikia mitazamo na kampeni hasi dhidi ya Serikali iliyopo madarakani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali Salim.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimuulize Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Waziri kwamba mfumo wa vyama vingi ni mfumo wa kidemokrasia. Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Tanzania inaelezwa kwamba ni haki ya kila chama kufanya kazi zake za kisiasa wakati wote kwa kutumia sheria na kanuni ambazo zimewekwa. Je, ni kwa nini Serikali imezuia harakati na mikutano ya kisiasa ili vyama visifanye kazi yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwa nini Msajili anaingilia mwenendo wa vyama vya siasa hali ya kuwa vinafanya kazi zake kikanuni, kikatiba kwa kufanya maamuzi kupitia Ofisi ya Msajili na kukataa maamuzi ya vikao halali vya vyama vya siasa kama vile Chama cha Wananchi (CUF). Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni sheria ipi ambayo inampa mamlaka hayo Msajili ya kutengua vikao halali vya chama ambavyo vimefanywa kwa mujibu wa kanuni na katiba na sheria za nchi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na la kwanza, si kweli kwamba Serikali imezuia harakati za kisiasa. Kama ambavyo yamekuwa yakijibiwa humu ndani bungeni, umewekwa utaratibu maalum wa kufanya siasa kutokana na sheria mbalimbali hasa ambazo zinaongoza utaratibu wa vyama vya siasa kushughulika katika shughuli za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba Serikali haijakataza vyama kufanya harakati za kisiasa lakini zimeruhusu vyama kufanya harakati za kisiasa kwa mujibu wa taratibu na sheria ambazo zimewekwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Msajili wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa sheria; ukisoma Sheria ya Vyama vya Siasa Sura namba 258 iliyorejewa mwaka 2002 na sheria ya vyama vya siasa iliyofanyiwa mabadiliko namba 7 ya mwaka 2009 inampa mamlaka Msajili kama mlezi wa vyama vya siasa kuhakikisha anavilea vyama vya siasa na pale panapotokea

matatizo awe sehemu ya kusaidia kurudisha *harmony* katika vyama vya siasa akiwa kama mlezi wa vyama vya siasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Vyama vya Siasa imeweka masharti ya wazi na yaliyo kamilika namna ambavyo vyama vitapata wanachama wake na vitaeneza sera na itikadi yake, lakini kwa sasa polisi wamekuwa na desturi ya kuzuia vikao vya vyama vya siasa hata vikao vya ndani vinavyopanga mipango ya uendelezaji wa chama. Sasa Serikali haioni kwamba badala ya kusimamia sheria Serikali yenyewe kwa kutumia vyombo vyake inavunja sheria; na kama inataka hayo masharti ya sasa yaendeleo ilete hiyo sheria hapa Bungeni ili kuweza kuweka hayo masharti mapya, badala ya kutumika kwa ajili ya kuwapiga wanasiasa mitaani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea majibu yangu ya awali kwamba si kweli kwamba Serikali inazuia harakati za kisiasa na hata sheria aliyoisema, sheria hii imetoa uhuru kwa vyama kutafuta wanachama na kufanya mikutano, lakini iko *subject* na sheria zinginezo ikiwepo sheria ya *Police Force* na *Auxiliary Service Act* ambayo pia imeweka masharti katika *section* namba 44 na 45 ya namna vyama vya siasa vinaweza vikafanya kazi zao hasa katika mikutano na maandamano mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka 2002 mpaka 2004 tulikubaliana kati ya wadau wa vyama vya siasa na Serikali tuwe na chuo cha kitaifa cha kuandaa viongozi bila kuangalia itikadi za vyama wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu. Je, Serikali imefikia wapi kuhakikisha tunakuwa na Chuo cha Kitaifa cha

kuandaa viongozi kwa ajili ya uzalendo wa kitaifa bila kuangalia itikadi za vyama vya siasa ili tuwe na Taifa moja lenye malengo yanayofanana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ni swali jipya lakini jibu tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali nia na dhamira ni kuendelea kukuza demokrasia ndani ya nchi na makubaliano hayo ya mwaka 2002 tutaendelea kuyafanyia kazi na kuyafuatilia ili lengo hili liweze kutimia la kuwa na chuo cha kuoka wanasiasa ambao tunaamini kabisa kupitia chuo hicho basi tutakuwa tumejenga Taifa la watu wenye uzalendo na ambao watakuwa na ari ya kweli ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Joyce Sokombi.

Na. 187

### **Wafanyakazi wa Mgodhi wa Nyamongo**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Wafanyakazi katika Mgodhi wa Nyamongo hawalipwi mshahara bali posho tu.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya wafanyakazi hao?

(b) Je, kwa nini wafanyakazi hao hawalipwi mishahara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta

Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodhi wa Dhahabu wa Nyamongo unamilikiwa na Kampuni ya ACACIA. Kwenye mgodi huo kuna makundi ya aina mbili ya wafanyakazi. Kwanza, kuna wafanyakazi walioajiriwa na Kampuni ya ACACIA na pili kuna wafanyakazi walioajiriwa na makampuni yanayopewa kazi na ACACIA (*Sub-Contractors*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wafanyakazi walioajiriwa na ACACIA wao hawalipwi posho bali hulipwa mishahara kwa mwezi. Kwa wafanyakazi walioajiriwa na makampuni mengine (*Sub-Contractors*) wao hulipwa mishahara kwa kuzingatia aina ya mkataba wa ajira na asili ya kazi anayofanya mfanyakazi kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yangu kupitia Idara ya Kazi itaendelea kufanya kaguzi za kazi katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini ikiwemo Kampuni ya ACACIA kwa lengo la kuwatambua waajiri ambao hawazingatii matakwa ya sheria za kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Imekuwa ni kawaida sana kwa migodi mingi na makampuni mengi kukaa na wafanyakazi bila kuwaajiri. Mheshimiwa Waziri umejibu kwamba wale wafanyakazi wameajiriwa, si kweli, wale wafanyakazi hawajaajiriwa. Hii inapelekea wafanyakazi wengi kukosa stahiki zao. Kwa hiyo basi, je, Serikali itaweka mkakati gani madhubuti wa kuhakiki migodi yote na makampuni yote kuhakikisha wafanyakazi hawa wamelipwa stahiki zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Sheria ya Ajira na kanuni zake ya 2003 inasema kwamba; mfanyakazi yeyote anapokuwa anafanya kazi sehemu yoyote kwa muda wa miezi sita anatakiwa aajiriwe na apewe haki zake za kimsingi.

Sasa swali langu linakuja, ni kwamba, Serikali haioni inapoteza mapato kwa kutowaajiri wafanyakazi hao kwa kuwafanya vibarua muda mrefu. Kwa nini Serikali isiingilie kati kuhakikisha wafanyakazi wa migodi wanapata haki zao za kimsingi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema si kweli kwamba wafanyakazi hao wameajiriwa. Nitamuomba tu Mheshimiwa Mbunge kama anayo taarifa nyingine tofauti atuwasilishie, lakini tarehe 28/4/2018 wakaguzi kutoka Ofisi ya Idara ya Kazi walikwenda kufanya ukaguzi katika Kampuni ya *ACACIA* na wakagundua idadi ya wafanyakazi na walio na mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna taarifa tofauti Mheshimiwa Mbunge anaweza kutuwasilishia katika ofisi yetu ili tuweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuhusu lini tutafanya uhakiki katika migodi. Idara ya Kazi mara zote imekuwa ikifanya kaguzi mbalimbali kuhakikisha kwamba waajiri wote nchi wanafuata sheria ya ajira na mahusiano kazini sheria Namba 6 ya mwaka 2004. Ni kazi yetu kama Serikali kuhakikisha kwamba *work places* zote hizi tunazitembelea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ameshakuelewa umejibu vizuri...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Ally Seif Ungando.



Na. 188

**Uhaba wa Vituo vya Afya Jimbo la Kibiti**

**MHE. ALLY S. UNGANDO** aliuliza:-

Ufunguzi wa Kituo cha Afya Mbwera ulifanyika tarehe 27/8/1994 na aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, wakati huo Dkt. John Samwel Malecela lakini hadi sasa kituo hicho hakina hadhi hiyo ya kuitwa Kituo cha Afya.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri mwenyewe haoni haja ya kwenda Mbwera kuona hali halisi ya kituo hicho baada ya kupokea taarifa kutoka kwa wataalamu wake kuona kama kimekamilika?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha kwani wanaotakiwa ni 39 na sasa waliopo ni wanne tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Afya Mbwera kilifunguliwa muda mrefu na kinakabiliwa na uchakavu wa miundombinu na uhaba mkubwa wa watumishi ikiwemo madaktari, tabibu na wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imepeleka jumla ya shilingi 560,000,000, kati ya fedha hizo shilingi 400,000,000 zimetolewa na Serikali kupitia wadau wa maendeleo wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (*Health Basket Funds*) na shilingi 160,000,000, zimetolewa na Serikali ya Watu wa Korea kwa lengo la kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na kujenga chumba cha upasuaji, nyumba ya mtumishi, wodi ya wazazi

(*maternity ward*), jengo la maabara, kurekebisha mfumo wa maji safi na maji taka, chumba cha kuhifadha maiti (*mortuary*) na kichomea taka (*incinerator*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa jengo la wodi ya wazazi na jengo la upasuaji yapo katika hatua ya msingi na ujenzi unaendelea kwa kutumia mfumo wa *force account*. Vilevile shilingi milioni 300 zimepelekwa bohari ya madawa (*MSD*) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Kituo cha Afya Mbwera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watumishi wa afya Serikali inalitambua na mnamo mwezi Novemba, 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti ilipewa watumishi wapya 11 wa kada mbalimbali za afya. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti imepanga kuajiri watumishi wapya wa kada mbalimbali za afya 199.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ungando.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto, je, Waziri sasa yuko tayari kufuatana na mimi kwenda Kituo cha Afya Mbwera kwenda kubaini baadhi ya changamoto za huu ujenzi unaoendelea hivi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwamba hali ya Kituo cha Afya Kibiti majengo yake kwa kweli uchakavu wake hauridhishi. Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ya kufanya ukarabati Kituo hiki cha Afya Kibiti ili kiweze kutoa huduma yenye tija kwa wananchi wa Kibiti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE):** Mheshimiwa

Mwneyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ungando Mwenyekiti wa Wandengereko (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko tayari kwa sababu wanasema *seeing is believing* kama ambavyo juzi nilipata fursa ya kwenda Dar es Salaam kutembelea Kituo cha Afya Buguruni na kule inakojengwa Hospitali ya Wilaya kwa Mheshimiwa Waitara, niko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kukarabati kituo kingine cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge anaomba, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunakamilisha na kukarabati vituo vya afya vingi kadri iwezekanavyo ili kusogeza huduma ya afya na hasa afya ya mama na mtoto kwa kadri itakavyowezekana. Kwa hiyo, kadri bajeti inavyoruhusu naomba nimhakikishie Mbunge kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba ukarabati unafanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kituo cha Afya Kakonko kimeelemewa sana na wagonjwa. Kituo hiki cha Afya Kakonko Waziri wa TAMISEMI akiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo, aliwahi kukitembelea akaona ukubwa wa kazi inayofanyika katika kituo kile. Kinapata mgao wa dawa sawa na Kituo cha Afya, kinatoa huduma kama Hospitali ya Wilaya. Sasa ni lini Serikali kwa makusudi kabisa itajenga Hospitali ya Wilaya ya Kakonko ili kuondoa mzigo kwenye Kituo cha Afya cha Kakonko? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba maeneo yote ambayo kuna Vituo vya Afya na hakuna Hospitali za Wilaya, hivyo Vituo vya Afya ndivyo ambavyo vimekuwa huduma kama Hospitali

za Wilaya. Ni ukweli usiopingika kwamba sifa ya kituo cha afya na sifa ya Hospitali ya Wilaya ni tofauti. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo hakuna Hospitali ya Wilaya tunajenga na ndio maana tumeanza na hizo hospitali 67. Ni azma kuhakikisha Wilaya zote Tanzania zinakuwa na Hospitali za Wilaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Jay.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Ulaya kinatumika kwa wananchi wote wa Kata za Zombo, Muhenda pamoja na Ulaya, lakini kina upungufu mkubwa sana wa watumishi na hali mbaya sana ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatupia macho kwenye Kituo cha Afya cha Ulaya ili wananchi wa pale kwenye Tarafa ya Ulaya waweze kupata tiba bora kwa mama na watoto, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Bonny.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE)** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya hicho Kituo cha Afya ambacho Mheshimiwa Mbunge anakitaja cha Ulaya sijapata fursa ya kukitembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ni ukweli usiopingika kwamba miongoni mwa mikoa ambayo imepata Vituo vya Afya vya kutosha katika awamu hizi ni pamoja na Mkoa wa Morogoro pamoja na Hospitali ya Wilaya. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Vituo vya Afya vyote ambavyo vinafanya kazi kama Vituo vya Afya, lakini havina hadhi ya Vituo vya Afya tunaenda kuvikarabati na kuviboresha ili vifanane na hadhi ya Vituo vya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni azma ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na yeye na pale alichombeza akaimba na wimbo nina amini hatutamsahau.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba uniruhusu niwape pole sana wenzetu wa Yanga kwa sababu msiba wa jirani yako ni msiba wa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na wasiwasi, naomba awe na subira mwaka 2018/2019 hii inakuja tutashughulikia suala lake la Ulaya.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bonny.

**MHE. BONIPHACE P. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuwe na utulivu, Yanga ni timu ya Taifa. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE P. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ujenzi wa Vituo vya Afya katika nchi yetu kwa maeneo mbalimbali. Kuna vituo vimepata shilingi milioni 500 na kuna vituo vimepata shilingi milioni 400. Sasa huwa najjuliza na wanasema vituo vyote vimepata shilingi milioni 700; shilingi milioni 200 kwa vituo vilivyopata shilingi milioni 500 inaenda MSD na shilingi milioni 300 kwa vituo vilivyopata shilingi milioni 400 imeenda MSD. Sasa huwa najjuliza...

**MWENYEKITI:** Swali!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tofauti ya fedha za kwenda kununua vifaa *MSD* ya shilingi milioni 300 na shilingi milioni 200 na shirika ni lile lile, la Serikali tofauti yake inatokana na nini? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili linajirudia kwa mara nyingine na nikiwa hapa niliwahi kutoa ufafanuzi kwamba kwanza inategemeana na *source of fund*; kuna maeneo mbalimbali ambayo tumepata fedha.

Kwa hiyo, inategemea shilingi milioni 500 au shilingi milioni 400, kama ni Benki ya Dunia, Canada, Serikali ya Tanzania lakini pia inategemeana na hali ya Kituo cha Afya husika kwa sababu kuna baadhi ya Vituo vya Afya vinahitaji ukarabati mdogo, vingine ukarabati wake ni mkubwa. Kwa hiyo, tumekuwa tukifanya *scope* kujua uhalisia ili Kituo cha Afya kiweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la pesa ambazo zinapelekwa *MSD*, majibu yake hayana tofauti sana na hili jibu la mwanzo kwa sababu ukienda Kituo cha Afya Manyamanyama ambacho labda kina *x-ray center* haiwezi kuwa sawa na kituo cha afya kingine ambacho hakina mashine kama hiyo.

Kwa hiyo, Serikali tumekuwa tukiyazingatia hayo wakati tunapeleka fedha, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Kilimo swali linaulizwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 189

## Taasisi Zinazoendelea Kununua Mazao kwa Mkopo

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Zipo taasisi bado zinaendelea kununua mazao kwa mkopo, jambo linalosababisha malalamiko kwa wakulima.

(a) Je, Serikali inaliujua jambo hilo?

(b) Je, ni lini utaratibu huu wa kununua mazao kwa mkopo utaisha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za Serikali zinazohusika na ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima ni Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*CPB*). Hata hivyo, taasisi hizi kwa miaka mitatu ya 2015/2016, 2016/2017 na 2017/2018 zimeweza kununua mazao toka kwa wakulima bila kuwakopa hivyo kutopata malalamiko yoyote kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulinunua mahindi tani 22,335,157, mwaka wa fedha 2016/2017 tani 62,099,319 na mwaka wa fedha 2017/2018 tani 26,038,643.

Aidha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilinunua mahindi tani 3,300 kwa mwaka wa fedha 2015/2016, tani 1,971.5 mwaka wa fedha 2016/2017 na tani 2,250 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka kwa wakulima. Manunuzi yote haya yalifanyika kwa fedha taslimu bila ya kuwakopa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, Serikali inaendelea kusisitiza uimarishwaji wa vyama vya Msingi vya Ushirika na Vyama Vikuu vya Ushirika ili kupitia vyama hivyo wakulima waweze kuuza mazao yao na kujihakikishia soko. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha mfumo wa uuzaji wa mazao katika Soko la Bidhaa za Kilimo (*Tanzania Mercantile Commodity Exchange*) kupitia mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani (*Warehouse Receipts System*) unaosimamiwa na Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi (*Warehouse Receipts Regulatory Board*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali itasimamia uuzaji wa mazao ya wakulima kwa njia ya minada ili kuweka ushindani wa bei na kumwezesha mkulima kupata bei kubwa kama ilivyo katika zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zitamhakikishia mkulima kuwa na soko la uhakika na hivyo kuongeza kipato chake. Aidha, Serikali inapenda kuwaomba wanunuzi binafsi wa mazao mbalimbali ya wakulima kujizuia au kuacha kabisa kuwakopa wakulima kwani vitendo ya namna hiyo huwakatisha tamaa wakulima na kusababisha kushuka kwa uzalishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomar.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu swali lake vizuri na linatia faida kwa wananchi. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake amelezea kwamba Serikali itasimamia uuzaji wa mazao ya wakulima kwa njia ya mnada ili kuweka ushindani. Sasa mimi nataka kumuuliza hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa nini Serikali isiweke masoko huria ili mkulima aweze kuuza mazao yake popote atakapo kwa kujiridhisha na bei itakayokuwepo kwa faida yake? (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza mtindo baadhi ya wakulima kuuza mazao yao bado yakiwa yangali shambani ili kukidhi matakwaa ya haja yake wakati inapomkumba na yeye fedha hana.

Je, Serikali itachukua hatua gani ili kusitisha tabia hiyo ambayo inamnyonya mkulima anapouza mazao yake shambani, na kwamba anatajirika ambaye yule anayekwenda kununua mazao shambani na akavuna mazao yake na kwamba wakati mkulima anapata hasara kwa pesa anayopata ni ndogo na mazao yake yote yameshamilikiwa na mtu mwingine? Ningeomba tamko la Serikali linasemaje. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye swali lake la kwanza amezungumzia Serikali kama tunaweza tukaruhusu mazao haya kuuzwa katika soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi nimesema kabisa kwamba Serikali imejipanga kuwa na mfumo rasmi wa uuzaji kupitia ile *TMX* kwa maana ya kwamba tutakuwa na soko huria lakini kupitia mfumo rasmi wa uuzaji kupitia chombo hiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali naomba nitoe rai na onyo kwa wanunuzi kwa wakulima wote ni marufuku kuuza mazao yakiwa bado kondeni/shambani, wote watakaopatikana na hilo jambo watachukuliwa hatua stahiki za kisheria, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Qambalo, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Mwanne.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika msimu huu wa kilimo...

**MBUNGE FULANI:** Washa *microphone*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Qambalo vipi?

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru katika msimu huu wa kilimo tumeshuhudia wakulima wa zao la mahindi mazao yao yameshambuliwa na viwavi jeshi aina ya *fall army worms* na viwavi jeshi hao bado ni tatizo. Nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba viwavi jeshi hao wanatokomezwa? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, ni lini, anataka kujua tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumejipanga na sasa hivi ninapozungumza Shirika la *WFP* wameshatoa dola 250,000 na Serikali pia imeweza kutoa pesa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba viwavi jeshi vinatokomezwa katika msimu huu wa kilimo, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali kupitia Bodi ya Korosho waliingia mkataba na baadhi ya wakulima kuzalisha mbegu za korosho na miche hii hawa wakulima wakaisambaza lakini mpaka sasa tunavyoongea wakulima hawa hawajalipwa na hii ni baada ya Bodi ya Korosho kuchukua kazi iliyokuwa inafanywa na Mfuko wa Pembejeo ambao walikuwa wakizalisha watu wanalipwa kwa wakati.

Sasa ni lini Serikali itaisimamia Bodi ya Korosho kuhakikisha inawalipa hawa wazalishaji wa mbegu za korosho waliofanya kazi ya kizalendo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli Serikali tunaelewa kwamba zao la korosho ni mojawapo ya zao la kimkakati na ni kweli kabisa kwamba

kuna wakulima hawa ambao wanaidai Bodi ya Korosho. Hata hivyo Serikali tumejipanga kwamba pesa hizi zinafuatiliwa na wakati wa bajeti Mheshimiwa Nape ataelewa majibu haya ya uhakika na ya kweli tunaweza kumpatia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanne, ajiandae Mheshimiwa Malocha na ajiandae Mheshimiwa Bobali.

**MHE. MWANNE J. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 wakulima wa tumbaku wa Mkoa wa Tabora walisumbuliwa sana katika suala la ununuzi wa bei ya tumbaku. Je, Serikali imejipangaje kuhusu suala la ununuzi wa tumbaku kwa bei nzuri ili isijirudie kama ilivyokuwa mwaka 2007?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu, ajiandae Mheshimiwa Malocha, ajiandae Mheshimiwa Bobali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi kwa upande wa zao la tumbaku tuna wanunuzi wakuu wanne. Hata hivyo kama Serikali tumejipanga kutafuta masoko mengine nje ya nchi, tumeweza kuongea na nchi ya Vietnam, China na Singapore; na naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako tukufu kwamba mpaka sasa hivi nchi ya Singapore tumeweza kufanikiwa na watanunua tani 1,000 kwa msimu huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Malocha atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika majibu ya msingi ya Serikali imeeleza kwamba tani 62,000 za mahindi zilinunuliwa mwaka 2016/2017 na tani 26,000 zilinunuliwa mwaka 2017/2018. Unaona kwamba kiwango kinapungua badala ya

kuongezeka wakati uzalishaji umeongezeka maradufu na wakulima wanaozesha mazao kwenye maghala. Ni zipi sababu zinafanya kiwango hiki kishuke? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi alivyozungumza ni kweli imekuwa ikishuka, mazao yetu yamekuwa yakishuka, lakini naomba niseme tu kwa kipindi cha mwaka wa fedha uliopita bajeti ilikuwa ndogo na tunategemea mwaka huu bajeti itaongezeka na hivyo tatizo zima hilo litakuwa limeshakamilika, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bobali, ajiandae Mheshimiwa Haonga

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikubaliana na Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi kwamba zao la ufuta mwaka huu litanunuliwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini mpaka hivi sasa tunapozungumza hakuna mipango ama mikakati yoyote ambayo tayari Serikali wameshaiweka tuanze kununua kwa stakabadhi ghalani na ufuta upo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, kwamba tunakwenda na stakabadhi ghalani ama tunatumia mfumo wa kawaida ili wakulima sasa waache kuyumba kuona kwamba mfumo gani utatumika mwaka huu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuli-*commit* kwamba msimu huu tutajitahidi kadri iwezekanavyo tuweze kuanza kuuza au kununua ufuta kwa mfumo wa stakabadhi ghalani na maandalizi yanaendelea na hivi kesho tutakuwa na kikao cha Wakuu wa Mikoa yote

inayozalisha ufuta ili tuone maandalizi yamefika kiasi gani na tuweze kutangaza rasmi lini tunaanzisha mfumo huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenitaja ulikuwa umesahau, ulisema Haonga.

**MWENYEKITI:** *Ooh sorry* Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka jana mahindi yalishuka bei sana kutokana na Serikali kufunga mipaka hivyo kuwasababishia wananchi hasara kubwa sana kutoka bei waliyouza mahindi awali shilingi 20,000 wakauza shilingi 3,500.

Je, Serikali ipo tayari sasa mwaka huu kuhakikisha kwamba haifungi mipaka ili wananchi waweze kuuza mahindi kwa bei nzuri? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kwamba Serikali ndiyo inasababisha mahindi yashuke bei bali ni kwa sababu mahindi ni mengi yamezalishwa *across region* yote wamezalisha vizuri msimu uliopita lakini kwa sababu hili jambo linahitaji umakini katika kulishughulikia majibu mazuri tutayatoa katika hotuba yetu ya bajeti.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 190

**Juhudi za Serikali katika Zao la Pamba**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Zao la Pamba limeendelea kupoteza mwelekeo kila kukicha na hivi karibuni mbegu walizoletewa wakulima wa Geita hazikuota kwa asilimia 30.

Je, ni nini juhudi za Serikali katika kutatua tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba ulibadilika kuanzia miaka ya 1990 baada ya soko huria kuanza. Kutokana na kutokuwepo mfumo rasmi wa utayarishaji wa mbegu za pamba kwa mujibu wa Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003, wakulima walikuwa wakiendelea kutumia mbegu aina ya *UK 91* ambayo kwa mara ya kwanza ilitolewa mwaka 1991 na imekuwa ikitumika kwa zaidi ya miaka 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuwepo kwa magonjwa na wadudu, aina hii ya mbegu ya *UK 91* imekwisha poteza sifa za kuendelea kutumika hivyo kuendelea kutumia aina hii ya mbegu ndio chanzo kikubwa cha uzalishaji na tija duni ya zao la pamba. Aidha, kwa kuwa mbegu hiyo hutunzwa na viwanda vya kuchambulia pamba, mara nyingine utunzaji wake huwa duni, hali ambayo hufifisha ubora wa mbegu na kusababisha utoaji wake pia kuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kurekebisha mfumo wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba kwa kufuata

vigezo vyote vya ubora kwa mujibu wa Sheria ya Mbegu Na. 18 ya mwaka 2003. Aidha, juhudi zilizofanyika na zinazoendelea kufanyika sasa ni kuzalisha kwa wingi mbegu aina ya *UKM 08* chini ya uratibu wa Kituo cha Utafiti cha Ukiriguru kwa kushirikiana na sekta binafsi na Bodi ya Pamba. Vilevile aina mbili za mbegu mpya za *UK 171* na *UK 173* zitaanza kupatikana kwa wakulima kuanzia msimu wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni kwamba mbegu iliyosambazwa kwa wakulima Mkoani Geita haikuwa na tatizo lolote la kuota na hatukuwahi kupokea malalamiko kutoka kwa mtu yoyote kuhusu kutoota kwa mbegu hizo. Tumuombe Mheshimiwa Mbunge pia kama anao ushahidi wa mbegu wa hizo kutoota utupatie ili tufanye utafiti kujua tatizo hilo litakuwa limetokeaje. Aidha, maoteo ya uzalishaji wa pamba msimu huu wa 2017/2018 yanatarajiwa kuwa makubwa sana ambapo kiasi cha tani 600,000 zinatarajiwa kuvunwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Tanzania ni nchi pekee ambayo mwakilishi wa nchi akifungwa, Waziri anakuja anashangilia Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lilikuwa *relevant* kwenye msimu wa 2016/2017 na limechelewa. Lakini naomba niishukuru Wizara kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu huu wa 2018/2019 katika Kata za Ihanamilo, Nyanguku na Bulela nilimjulisha Mheshimiwa Waziri kwamba limekuwepo tatizo la pamba kurefuka na hazitoi matunda. Kutokana na sababu hiyo wakulima katika maeneo hayo wameshindwa kufahamu kama utafiti huu wa mbegu za pamba ulikuwa *universal* katika nchi nzima.

Sasa swali langu ni lini Wizara itatuma wataalam kwenda katika maeneo hayo ili tuweze kufahamu sababu za kwa nini pamba hiyo imerefuka tu na imeshindwa kuzaa matunda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wakulima katika maeneo yao walikopeshwa pembejeo na msimu wa ununuzi wa pamba umeanza na uzalishaji ulikuwa mbaya na ni lazima wakatwe, ni nini kauli ya Serikali katika suala hilo? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Kanyasu kwa kusema kweli kwamba swali lenyewe la msingi lilikuwa limepitwa na wakati kwa sababu katika msimu huu hatukuwa na ushahidi wa mahali popote kwamba mbegu tuliyoisambaza ilishindwa kuota, taarifa tuliyokuwa nayo ni kwamba imeota vizuri maeneo yote na kwa hiyo namshukuru sana kwa uungwana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika maswali yake ya nyongeza, ni kweli taarifa kwamba pamba imerefuka kuliko ilivyotarajiwa ipo maeneo mengi, na tumewatuma tayari watafiti wetu wa Chuo cha Ukiriguru kwenda maeneo mbalimbali kujionea wenyewe na kutafiti ni sababu gani inayosababisha pamba ile irefuke. Suala ambalo kwa tafiti ya awali wamesema ni kuongezeka kwa mvua, mvua imenyeshwa nyingi kuliko ilivyokuwa kawaida kwa hiyo pamba imerefuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukosa vitumba, yapo maeneo ambako viuadudu vilichelewa kufika na wakulima wa maeneo hayo hawakuwa wamepulizia kwa wakati kwa hiyo vitumba vingi vikawa vimekwishaharibiwa na ndiyo maana huenda pamba ile inarefuka. Wale ambao hawakuvuna vizuri, tsubiri kwanza kwa sababu sasa hivi baada ya mvua kuanza kupungua pamba nyingine bado iko inatoa matunda na huenda pia mavuno yao yakawa



mazuri tu bila tatizo lolote ingawa tayari watafiti wetu wako maeneo mbalimbali wanafuatilia jambo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Justin Monko, ajiandae Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida pia tumehamasika sana kulima pamba na katika Jimbo langu la Singida Kaskazini pamba imelimwa kwa ekari 1,300 na tulipata pembejeo kutoka Serikalini ikiwemo dawa. Dawa hii ambayo tuliitumia kulingana na maelekezo ya wataalam; pamoja na Bodi ya Pamba kuja kupiga kwenye pamba lakini pamba hiyo imepukutisha majani na hivi sasa ninavyozungumza wananchi wa Kata za Ilongero, Ughandi, Mtonge, Kinyeto, Muhunga na Msange wanashindwa kabisa kupata mazao katika pamba ambayo wamelima katika msimu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuuliza Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na hasara hii ambayo wananchi wameipata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kuwapa pole sana wananchi wa jimbo lake kutokana na tatizo lililojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama alivyosema ni kwamba sisi kama Serikali tutatuma wataalam wetu kwenda kwenye jimbo lake kwanza kuthibitisha kama tatizo hilo limetokea, na kama ni kweli limetokea basi ninaagiza Bodi ya Pamba, na sisi tuna mfuko wetu kwenye Bodi ya Pamba kwamba maeneo yote ambayo yamelimwa pamba tutatoa vile viuatilifu kwa bure isipokuwa mbegu wataendelea kununua. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la Serikali ni kumuwezesha mkulima huyu wa pamba ili aweze kupata thamani ya pamba yake na kwa kuwa pamba hii imekuwa na gharama kubwa sana kwa mkulima kutokana na bidhaa ya pamba inayoingizwa kutoka nje. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka zuio la makusudi ili pamba inayozalishwa hapa nchini itumike kuzalisha bidhaa za pamba hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Masala.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezekano huo upo kama mazingira ya matumizi ya pamba hapa ndani yatakuwa mazuri yanayoweza kutumia pamba yote inayozalishwa hapa nchini. Kwa sasa hivi uwezo wa kutumia pamba yote tunayozalisha hapa nchini ni mdogo na kwa hiyo wafanyabiashara wanalazimika kupeleka hii pamba nje ya nchi, ndiyo maana sasa hivi tunafanya jitihada kubwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda kuhakikisha kwamba viwanda vya kutengeneza nguo, viwanda vya kutengeneza bidhaa za pamba vinajengwa hapa nchini ili soko la ndani liwe kubwa kuliko soko la nje kwa bidhaa zinazotokana na pamba.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu mazuri; Mheshimiwa Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba kupata kauli ya Wizara juu ya ubora wa *sulphur* ambayo safari hii wakulima wetu wa zao la korosho watakwenda kupata. Ukirejea ripoti ya CAG msimu wa mwaka jana *sulphur* ambayo imesambazwa kwa sehemu kubwa ubora wake ulikuwa na

mashaka makubwa sana; naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli, safari hii *sulphur* iko katika kiwango gani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sulphur* ni kiuatilifu kinachotumika kwenye zao la korosho na taratibu za uingizaji wa *sulphur* hapa nchini ziko kwa mujibu wa sheria. Tunacho chombo chetu cha *TPRI cha* kuhakiki ubora wa *sulphur* kabla ya kuruhusu *sulphur* hiyo kuingia hapa nchini. Kwa hiyo naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara kupitia *TPRI* inajitahidi kuhakikisha kwamba *sulphur* inayoingizwa nchini ina ubora unaokubalika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo; wageni wa Mheshimiwa Spika waliopo kwenye *gallery* ya Spika ni Bwana Aashutosh Agarwal, Mkurugenzi Mkuu wa *Gabon Special Economic Zone* akiambatana na Bwana Sharik Choughule kutoka Gabon na wanatakiwa wamuone Mheshimiwa Spika, mkiitwa mnasimama, *could you please stand up, you are supposed to be meeting the Speaker at ten this morning, could you kindly please proceed to his lounge now. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mary Deo Muro sasa aulize swali lake.

Na. 191

### **Shamba la Vikuge Kugeuzwa Pori – Kibaha**

**MHE. MARY D. MURO** aliuliza:-

Shamba la Vikuge lilikuwa mkombozi kwa wananchi wa Kibaha na Dar es Salaam kujipatia majani ya kulisha mifugo yao, lakini kwa sasa shamba hilo limegeuka pori.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu shamba hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** nlijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba la kuzalisha mbegu bora za malisho la Vikuge - Kibaha, ni moja wapo kati ya mashamba saba ya Wizara yanayozalisha mbegu bora za malisho. Mbegu hizo huuzwa kwa wafugaji na wadau wengine ili kuwekeza katika uzalishaji wa malisho kwa ajili ya kuwa na ufugaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili pia huzalisha hei na kuwauzia wafugaji wa Kibaha, Dar es Salaam na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba lina ukubwa wa jumla ya hekta 515 ambapo eneo la hekta 30 ni makazi, hekta 20 ni hifadhi ya vyanzo vya maji na eneo linaloendelezwa ni hekta 250. Eneo lililobaki si pori bali ni eneo la akiba lenye malisho ya asilia ambalo huwa linafyekwa vichaka na kuvunwa malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2017/2018 shamba la Vikuge limezalisha jumla ya marobota ya hei 26,000 na mbegu bora za malisho kilo 1,500 ambazo zinauzwa kwa wadau wa malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba la Vikuge katika mwaka wa 2018/2019 Serikali imejipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za malisho na hei kwa kuendeleza eneo jipya la hekta 20.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muro.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa hekta 270 za shamba hilo kuongezwa haziwezi kukidhi mahitaji ya wananchi wa Mkoa wa Pwani pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam wanaotumia majani hayo, je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza zaidi ya hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hei imekuwa bei aghali, je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ili kuvutia wananchi wengi kutumia majani hayo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza anataka kujua kwamba hizi ekari 270 ni ndogo kuweza kukidhi haja ya mahitaji ya chakula cha mifugo kwa Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es Salaam, je, Serikali tumejipangaje? Jibu la swali hili ni kwamba Serikali tumejipanga vizuri na ndiyo maana tumehakikisha kwamba maeneo yetu ambayo ni ya mifugo likiwemo hili la Vikuge na mengineyo yale ya *Holding Grounds* na hata maeneo yetu ya *NARCO* pale Ruvu tunawekeza sana sasa hivi katika kuhakikisha kwamba tunapata maliso ya kutosha ili kuweza kuwa-*supply* wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swali la pili ni juu ya bei; ni kweli, bado bei za hei na mbegu za malisho ziko juu. Hivi sasa tupo katika hatua ya mwisho kama Serikali ya ku-*certify* mbegu za malisho ili nazo ziweze kuuzwa kama zinavyouzwa mbegu za mahindi, mpunga na mazao mengine ili kuwawezesha wafugaji wetu waweze kupata mbegu hizo kwa bei nafuu. Hivi sasa bei ya kilo moja ya mbegu za malisho ni takribani shilingi 17,000. Mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba zinashuka ili ziweze kuwasaidia wafugaji walio wengi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, kwa niaba yake Mheshimiwa Chatanda.

Na. 192

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Njia ya Mradi wa Umeme na Gesi**

**MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y. MHE. HAMOUD A. JUMAA)** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuwapa fidia wananchi waliopisha njia ya mradi wa umeme wa gesi toka Kinyerezi kwenda Arusha, Awamu ya Kwanza hadi Chalinze lakini hadi sasa wananchi hao hawajalipwa fedha zao.

Je, ni lini wananchi wa Kibaha watalipwa fidia kutoka katika fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano shilingi bilioni mbili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Arusha. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 664 pamoja na kilometa 40 kutoka Kibaha hadi Zinga na kilometa 60 kutoka Segera hadi Kange, Tanga. Mradi huu unahusisha ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme vya Chalinze, Segera, Kange na Zinga, Bagamoyo. Mradi huu utajengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Exim ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 kazi ya utathmini wa mali za wananchi wa Kibaha na Chalinze ilifanyika ili waweze kulipwa fidia na kupisha ujenzi wa mradi. Kazi inayofanyika kwa sasa ni kukamilisha taratibu za malipo kwa wananchi waliohakikiwa. Zaidi ya shilingi bilioni 21.56

zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wanaopitiwa na mradi katika maeneo ya Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na maeneo mengine yanayopitiwa na mradi kutoka Kinyerezi hadi Chalinze. Fidia kwa wananchi hao italipwa mara tu baada ya taratibu za malipo hayo kukamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nimpongeze vilevile yeye mwenyewe kama Naibu Waziri na Waziri wake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba wanawapatia wananchi umeme. Nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu unaonekana utakwenda hadi Arusha, na kwa kuwa tayari wananchi wa Kibaha wao wameshafanyiwa tathmini ya kuhakikisha kwamba wanapata hizi fedha ambazo zimetengwa. Je, hawa wananchi wengine ambao watapitiwa na umeme hadi Arusha ni lini sasa watafanyiwa tathmini hiyo ili nao waweze kulipwa fidia zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Korogwe Mjini tunapata umeme ambao unawaka na kuzimika au unachezacheza, nini tatizo la umeme huo Korogwe Mjini? Naomba nipatiwe majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya msingi katika swali la Mheshimiwa Mbunge, nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini napenda sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mary Pius Chatanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa tathmini imefanyika katika awamu mbili, awamu ya kwanza

imefanyika kutoka Kibaha na Chalinze na Chalinze hadi Segera na kadhalika imefanyika kutoka Segera hadi kwenda mpaka Arusha ambapo tathmini imepatikana. Kwa awamu ya kwanza shilingi bilioni 5.2 na lile eneo la pili mpaka Tanga shilingi bilioni 10.6. Kwa hiyo tathmini zote mbili zimeshafanyika na malipo yatafanyika kwa pamoja mara baada ya uhakiki kukamilika mapema iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na umeme kutokuwa imara katika maeneo ya Tanga na maeneo mengine, nipende tu kumpa taarifa Mheshimiwa Chatanda na kumshukuru sana kwa kuunga mkono juhudi za Serikali, kinachofanyika la kwanza ni kuhakikisha kwamba maeneo yote yanayopitiwa na miundombinu yanafanyiwa ukarabati. Tumeshianza kusafisha njia kutoka Tanga katika maeneo yote ya Korogwe, Lushoto mpaka Muheza na mwisho wa mwezi huu itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na maeneo ya pili ni kurekebisha nguzo pamoja na nyaya ambayo itakamilika mwezi huu wa Mei. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Chatanda baada ya mwezi Mei, hali ya umeme kwa Korogwe itaimarika sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo, maswali yote ya nishati yatasubiri bajeti inayokuja. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu.

Na. 193

## **Maeneo yaliyofikiwa na Umeme wa REA Nchi Nzima**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Mradi wa kupeleka Umeme Vijijini (REA) ni mradi ambao unaendelea kwa kasi kubwa nchi nzima.



Je, Serikali inaweza kutuambia ni kwa kiasi gani umeme huu umesambazwa nchi nzima (*coverage*) tangu mradi huu ulipoanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa *REA I* ambapo utekelezaji wake ulijumuisha ujenzi wa miundombinu ya umeme wa msongo wa kilovoti 11/33 wenye urefu wa kilometa 1,700; umeme wa msongo wa kilovoti 0.4/0.23 wenye urefu wa kilometa 800 na ufungaji wa transfoma 386. Jumla ya vijiji 231 vilipatiwa umeme na jumla ya wateja 22,100 waliunganishwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mradi wa *REA II* ulijumuisha ujenzi wa miundombinu ya umeme wa msongo wa kilovoti 11/33 wenye urefu wa kilometa 17,740; ujenzi wa umeme wa msongo wa kilovoti 0.4/0.23 wenye urefu wa kilometa 10,970; ufungaji wa transfoma 4,100 za ukubwa tofauti na kuvipatia umeme vijiji 2,500 na kuunganishia umeme kwa jumla ya wateja 178,641 ambao ni sawa na asilimia 71.46 ya matarajio ya wateja 250,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa azma ya Serikali ni kupeleka umeme katika vijiji vyote kufika mwaka 2020/2021, Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*) mwezi Julai 2017 ilianza kutekeleza mradi wa *REA III* kupitia *grid extension* na *Densification* itayopeleka umeme maeneo ambayo yaliyorukwa katika utekelezaji wa *REA I* na *II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganisha umeme maeneo ya pembezoni mwa miji (*Peri-urban, electrification program*), kusambaza umeme katika vijiji vyote ikiwa ni pamoja vilivyo pembezoni mwa mkuza wa njia ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga na utekelezaji

wa miradi ya nishati jadidifu. Utekelezaji wa miradi ya *REA III* kwa mzunguko wa kwanza unajumuisha ufunguji wa miundombinu ya umeme ya msongo wa kilovoti 11/ 33 yenye urefu wa kilometa 16,420; njia za umeme wa msongo wa kilo vote 0.4 lenye urefu wa kilometa 15,600; ufungaji wa transformi 6,700 na kuvipatia umeme vijiji zaidi 3,559 na kuwaunganisha wateja 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme vijijini nchini umechangia kufikia matumizi jumla ya umeme nchini (*overall access*) kufikia asilimia 67.5 kwa vijijini ambapo vijijini ni asilimia 49.5 kutoka asilimia mbili iliyokuwepo wakati wakala unanza kutekeleza majukumu yake mwaka 2007 na mijini ni asilimia 97. 3.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hija.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza na mimi nipongeze Wizara kwa *speed* nzuri wanayochukua ya kusambaza umeme vijijini. Hata hivyo nina suala moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri ametueleza pia kuna taasisi za Serikali ambazo Mheshimiwa Waziri hakuzitaja. Je, nini mikakati ya kuziunganishia taasisi za Serikali, umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kw kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Hija kwa pongezi zake kwenye swali lake; la nyongeza ameuliza mkakati wa Serikali wakusambazia umeme taasisi za Kiserikali. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la mzingi katika utekelezaji wa *REA I* na *II* kulikuwa na mapungufu ya kuruka baadhi ya maeneo na hususani Taasisi za Kiserikali utekelezaji wa *REA III* kama Serikali tumetoa maelekezo kwamba taasisi zote za Serikali zipatiwe

kipaumbele na napenda kuwashukuru wakandarasi wote wamekuwa wakitekeleza maelekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo napenda nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwa sasa kwa makandarasi wameendelea kuunganisha maeneo ya Kiserikali iwe ya zahanati, miradi ya maji, vituo vya afya na hospitali. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** ahsante Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kemirembe kwa niaba ya Mheshimiwa Mabura.

Na. 194

### **Ukosefu wa Umeme wa Uhakika Kata za Wilaya ya Nyamagana**

**MHE. STANLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. KEMIREMBE J. LWOTA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha umeme wa uhakika kwenye Kata za Wilaya ya Nyamagana, Mkoa wa Mwanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishari napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kimirembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyamagana ina jumla ya Kata 18 ambazo ni Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Rwanhima, Mkuyuni, Mabatini, Luchelele, Igogo, Pamba, Nyamagana, Mirongo, Isamilo, Mbungani, Mahina, Igoma, Butimba, Muhandu na Kishiri. Kata zote hizi zinapata umeme wa Gridi ya Taifa japo baadhi ya maeneo ya Kata hayana umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kujenga miundombinu ya umeme na kusambaza umeme katika maeneo yote ya nchi yetu. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Shirika la Umeme (*TANESCO*) limetenga

jumla ya shilingi bilioni nane na milioni mia saba thelathini kwa ajili ya kujenga, kukarabati na kuboresha miundombinu ya umeme ya Mkoa wa Mwanza ikiwepo Wilaya ya Nyamagana na Kata zake ili kuhakikisha umeme unapatikana kwa uhakika. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 jumla ya nguzo 519 za umeme wa kati wenye msongo wa kilovoti 11 na 33 na nguzo 188 za msongo wa voti 400 katika Kata za Nyamagana na maeneo mengine ya jiji la Mwanza vimebadilishwa, pia vikombe 807 vilikuwa vimevunjika vimebadilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kilometa 33 za msongo wa kati na madogo zimesafishwa kwa kukata miti pamoja na kubalisha waya kwa kilometa 22 zilizokuwa zimechakaa. Zoezi hili la ukarabati linaendelea ili kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho hayo yamewezesha kuimarika kwa upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Mwanza ukilinganisha na kipindi cha nyuma. Aidha, kukamilika kwa mradi mkubwa wa kusafirisha umeme wa msongo kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga kumechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa umeme katika Mkoa wa Mwanza. Zoezi la ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya umeme ni endelevu na kiasi cha fedha shilingi bilioni nne kimependekeza katika bajeti ya mwaka huu 2018/2019 kwa ajili kuboresha miundombinu ya umeme ya uhakika Jijini Mwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba niulize maswli mawili madogo ya nyongeza na moja ni kwa sababu Serikali bado yako maeneo kwenye Jiji la Mwanza na hasa Wilaya ya Nyamagana kama Kata za Kishiri, Lwanima na Buhongwa bado hayajapata umeme wa uhakika.

Ni lini sasa Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* itahakikisha maeneo hayo yanapata umeme wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Mji wa Mwanza bado unayo maeneo yenye taswira ya vijiji ikiwemo Jimbo la Ilemela. Ni nini mpango wa Serikali kupitisha umeme kwenye maeneo hayo hasa maeneo ambayo tayari yamebaki sambamba na Kata za Sangabuye, Bugogwa, Kahama na Shibula ili kuhakisha Mwanza yote inapata umeme wa uhakika? Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kwa kifupi, Mheshimiwa Waziri musika.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya swali la msingi, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mabula pia katika kufuatilia maeneo ya vijiji hivi 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tulitenga fedha shilingi bilioni 8.7 kwa ajili ya kupeleka vijiji tisa katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge vipya, kupitia mradi wa *TANESCO*. Na nimwambie tu Mheshimiwa Mabula nimpongeze sana hivi sasa *TANESCO* wanapeleka umeme katika kijiji cha Lwanima na wakimaliza Lwanima wanakwenda Kanema, pamoja na Bukaga, Nyakwagwe watapeleka. Pia watapeleka mpaka Kigogo pamoja Isebanda na wakimaliza Isebanda Mheshimiwa wanakwenda pia kwenye kijiji cha Kigodo pamoja Nyangwi pamoja na mtaa wako wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimpe uhakika Mheshimiwa Mabula kwamba hadi kufika mwezi Juni ambapo mradi unakamilika wananchi wote wa vijiji vyote vinane, umbali wa kilometa 9.2 utakuwa umefikishiwa umeme na Mwanza itakuwa inapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swala lake la pili, ni kweli yako maeneo ambayo yako mjini na visiwani na vijiji. Tuna mradi wa (*Peri-urban*) ambao Jiji la Mwanza katika maeneo ya Kishiri, Buhongwa Pamoja na Kata za Lwanima pia ziko kwenye mpango huo. Kwa hiyo, watapelekewa

kupitia mradi wa (*Peri-urban*) lakini pamoja na mradi wa *Densification* utakaoanza Julai mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea maswala yote ya REA mtasubiri kwenye bajeti, Wizara ya Viwanda, Biashara Uwekezaji, Mheshimiwa Oliver.

Na. 195

### **Viwanda vya Kusindika Matunda**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Mkoa wa Kagera unazalisha matunda ya aina mbalimbali kama vile ndizi, nanasi, parachichi, embe na kadhalika. Kwa kuwa kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha uchumi wa viwanda nchini.

Je, Serikali inaweza kuweka wazi mikakati madhubuti iliyoandaliwa ya ujenzi wa viwanda vya kusindika matunda katika Wilaya ya Ngara, Karagwe na Bukoba katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016/2020?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Katika mpango huu imebainishwa wazi kuwa ni jukumu la sekta binafsi kujenga viwanda na Serikali ibaki na jukumu la kuweka mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji biashara. Pia katika mpango huo tunalenga kuanzisha viwanda vinavyotumia malighafi zitokanazo na mazao ya wananchi, viwanda vinavyoajiri watu wengi na viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika kwa vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumueleza Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Wabunge wote wa Kagera na Wana Kagera wote kwa ujumla kuwa Serikali inasimamia mikakati ifuatayo katika ujenzi wa viwanda vinavyosindika matunda Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuimiza Serikali ngazi ya Kijiji, Kata na Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kuhakisha maeneo hayo yanawekewa miundombinu wezeshi na saidizi; tatu, kupitia *SIDO* kutoa mafunzo ya kusindika malighafi za shamba ikiwemo matunda; nne, kujenga majengo ya viwanda (*industrial sheds*) ambapo wajawasiamali watapata mafunzo ya kuchaka na kusindika mazao yao ya shamba; na tano kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia uwekezaji Mkoa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa mwitikio ni mzuri kwani viwanda vinavyosindika matunda vimeanza kujengwa, hii ni pamoja na kiwanda cha Mayawa kilichopo Bukoba Mjini, kiwanda cha kusindika nyanya kilichoko lbwera kinachomilikiwa na Mheshimiwa Dkt. Samsoni Rweikiza Mbunge wa Bukoba vijijini, kiwanda cha mvinyo wa ndizi cha Salum Said Seif kilichoko Mulemba na kiwanda cha mvinyo cha ndizi kilichopo Karagwe kwa kutaja baadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri; ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa za viwanda tunazosisoma na kuzisikiliza kila siku, kwa jibu ni kuwa Kagera bado tuko nyuma katika viwanda. Sasa nini mpango wa Wizara yako kushirikiana na mimi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kagera kuhamasisha ujenzi wa viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wananchi wa Kagera wajasiriamali wadogo wadogo ili waweze kupata mikopo ya riba nafuu ili waweze kufungua viwanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za uhamasishaji zinaendelea, shughuli zinazofanywa na Wizara ya Mifugo za kuondoa uvuvi haramu zinalenga kuona kwamba katika ziwa letu tunapata samaki wa kutosha ili viwanda vya samaki viweze kujengwa. Lakini yako makampuni ambayo tumeshawasiliana nayo, kiwanda cha kutengeneza maziwa kitajengwa Kagera. Pia kampuni moja kutoka Uganda ya Uvan inataka kujenga kiwanda cha vanilla. Suala la uhamasishaji ni endelevu.

Nipende kukuahidi wewe na Wabunge wenzangu na wananchi katika Mikoa ambayo nataka kufanya kazi nayo ya uhamasishaji ni pamoja na Kagera, Kigoma, Mara, Katavi na Ruvuma. Katika miezi minne ijayo tutafanya kampeni kubwa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...ya mazao ya shamba ambayo tunataka kuyaimiza yaweze kuzalisha bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwawezesha wananchi akina mama na akina dada kifedha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tunao mfuko wa *NADef*. Jambo la muhimu si pesa, jambo la muhimu ni kwenda kupata *idea* na kupata mawazo *SIDO*. Mkishapata mawazo kupitia *SIDO* mtanufaika na mfuko wa *NADef* lakini iko mifuko mingine ambayo iko chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nitakapozindua kitabu cha mwongozo wa kujenga viwanda kwa *local government* katika bajeti yangu siku ya Alhamisi



kitabu hicho kitagawiwa mtaweza kujua pesa zinapatikana wapi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Balazi Mwamoto.

Na. 196

### Hati Miliki za Kimila

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Je, ni nini faida ya hati miliki za kimila?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa fungu la 18, 28 hadi 47 la Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba tano ya mwaka 1999 hati ya hakimiliki za hati ya kumiliki ardhi kwa kuzingatia mila na desturi kwa raia wa Tanzania na ina hadhi sawa na hakimiliki nyingine inayotolewa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida nyingi za hati za hakimiliki ya kimila, miongoni mwa faida hizo ni pamoja na kuwa na usalama wa miliki, kupunguza migogoro baina ya watumiaji ardhi, kutumika kama dhamana katika taasisi za fedha na vyombo vya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya hatimiliki za kimila 56,506 zimeandaliwa katika maeneo mbalimbali nchini. Wananchi katika maeneo hayo wamenufaika kiuchumi kutokana na mikopo waliyoipata katika taasisi za kifedha kwa kutumia hati za hatimiliki za kimila kama dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Juni, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 59.2 zimekopeshwa kwa wananchi kwa kutumia hati za hakimiliki za kimila kama dhamana kutoka mabenki na taasisi za kifedha. Miongoni mwa taasisi hizo ni pamoja *NMB PLC, CRDB PLC, Stanbic Bank, SIDO, PSPF, Agriculture Trust Fund, Meru Community* na Mfuko wa Pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi wote kutoa ushirikiano katika miradi ya utoaji hati za hakimiliki za kimila inayoendelezwa katika maeneo yao ili ziweze kuwanufaisha kwa ustawi wa kiuchumi na kijamii.

**MWENYEKITI:** Balozi Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ukiangalia majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba waliokopeshwa kwa kutumia hatimiliki za kimila takribani ni shilingi bilioni 59, lakini ukiangalia idadi ya wanaomiliki hati hizo miliki za kijiji wako wengi, sasa hii inaonesha kwamba kuna tatizo katika wakopeshaji.

Sasa je, Waziri atakubali kulifuatilia jambo hili ili kuhakikisha kwamba wale wanyonge ambao hasa ndiyo wanalengwa kwa sasa wanapata mikopo bila usumbufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Sheria Namba Nne na Namba Tano ya mwaka 1999 ya Ardhi ya Vijiji iko wazi na inatakiwa marekebisho kwa sababu wanaokwenda kutoa haki inapotokea matatizo ya ardhi vijijini ni mabaraza ya kata. Lakini kwa kuwa kuna tatizo pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi swali.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Je, Waziri atakuwa tayari kukutana na Waziri wa TAMISEMI na yeye Waziri wa

Ardhi ili kurekebisha kwa sababu haki haitendeki kama ambavyo inatajikana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema imeonekana ni wazi kwamba wahitaji wa mikopo ni wengi, lakini wanaokopeshwa ni wachache. Hapa kuna mambo mawili kuna *either* watu kuogopa kwenda kuchukua mikopo au benki kutokubali zile hatimiliki za kimila.

Napenda nimthibitishie tu kwa sababu elimu inayotolewa wanapopewa zile hati za haki miliki za kimila wanaambiwa zina sifa sawa sawa na hati zingine na ndiyo maana benki 11 zimeweza kutoa hizo shilingi bilioni tisa na ninawapongeza sana watu wa Mbozi ambao ndiyo wanaongoza kwa kutoa mikopo kwa kutumia hati miliki za kimila. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili ambalo amelizungumzia naomba tu niseme kwamba kweli tunayo changamoto hiyo na hasa ya uelewa, kwa maana katika maeneo mengi tunahitaji kuwa na watu ambao ni waajiriwa wanaoweza kufanya kazi hiyo ya kusimamia Mabaraza ya Ardhi. Sasa kama hilo linaonekana ni tatizo nadhani bado tunaweza tukaliangalia. Ni kweli kuna shida na maeneo mengi Mabaraza ya Ardhi ya Kata hayafanyi kazi yake vizuri pengine kutokana uelewa mdogo au kutokuwa na *manpower* ya kutosha, kwa hiyo, hili tunalichukua tatalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika wageni 116 wa Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwelwe, Mbunge na Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni Profesa Kitila Mkumbo - Katibu Mkuu; *Engineer*

Emmanuel Kalombelo - Naibu Katibu Mkuu; Balozi Job Lusinde Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji, Dodoma; Ndugu Vicent Mrisho - Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Maji na Profesa Tolly Mbwette - Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam. Wameambatana na Maafisa wa Mabonde ya Maji, Maafisa wa Maabara ya Maji, Wahandisi wa Maji wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji pamoja Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Kamwelwe ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Mlele wakiongozwa na Mheshimiwa Deus Bundala, Mwenyekiti Halmashauri ya Mlele. Pia ipo familia yake ikiongozwa Ndugu Bora Isack Kamwelwe ambaye ni mke wake. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 30 wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambao ni wachezaji wa Timu ya *Ilala Veterans* kutoka Ilala Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti wa timu hiyo ambaye ni Mwenyekiti Kibunge Tito na Diwani Fatuma Abubakar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambayo ni familia yake kutoka Pangani Mkoani Tanga wakiongozwa na Bi. Kauthar Aweso ambaye ni mke wake. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Eng. Atashasta Nditiye, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango-Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wakiongozwa na Mheshimiwa Mwalingo Kisemba. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Juma Othman Hija ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo la Tumbatu, Ndugu Khamis Haji. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Hassan Masala (Mbunge) ambae ni Ndugu Anzigar Chilumba kutoka Nachingwea Mkoani Lindi. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Ulanga Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Andrew Chenge ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Mkoani Simiyu wakiongozwa na Mheshimiwa Robert Lweyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni Ndugu Martina Bartholomwe. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 90 na walimu watatu kutoka shule ya msingi Canon Andrea Mwaka ya hapa Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 72 na walimu watano kutoka shule ya sekondari ya wavulana ya Feza ya Jijini Dar es salaam. *(Makofi)*

Tangazo, Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, matokeo ya mechi zilizochezwa mwishoni mwa wiki kati ya *Ndugai Boys* na *Bank of Africa* iliyochezwa tarehe 5 Mei, 2018 *Ndugai Boys* walipata goli moja na *Bank of Africa* walipata sifuri. Goli la *Ndugai Boys* lilifungwa na Mheshimiwa Cosato Chumi na nyota wa mchezo katika mechi hiyo alikuwa ni Mheshimiwa Salum Rehani. *(Makofi)*

Aidha anafurahi kuwatangazia kuwa tarehe 6 Mei, 2018 timu ya soka ya *Bunge Sports Club* ambayo kwa umaarufu inaitwa *Ndugai Boys* iliwashangaza wakongwe waliowahi kutamba miaka ya zamani wanaocheza *Ilala Veterans* baada ya kutoka sare na kutokufungana katika

mchezo uliochezwa jana tarehe 6 Mei, 2018 katika uwanja wa Jamhuri. Wakongwe hao wakiongozwa na Dua Said, Mwanamtwa Kiwelu, Shabani Ramadhani, Abdallah Waswa na wengineo wa *Ilala Veterans* walishindwa kabisa kuipenya ngome ya *Ndugai Boys* iliyokuwa ikiongozwa na Abdallah Ally, Salum Rehani na William Ngeleja. Nyota wa mchezo wa *Ndugai Boys* alikuwa ni Mheshimiwa Flatei Massay ambaye aling'ara vilivyo. (Makofi)

Anawashukuru Wabunge wote na wananchi waliofika kushuhudia pambano hilo. Kipekee anamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Zungu kwa kuendelea kuunga mkono *Ndugai Boys* kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika mechi zote hizo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge ni ukweli timu ya Ilala ilicheza na *Bunge Sports* na timu ya Ilala ilipata *penalty* lakini ilikuwa ni maelekezo yangu niliwaambia wasifunge kwa sababu tunacheza na timu ya Spika na isije biashara ikaharibika. (Kicheko/Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, jana nchini Algeria timu ya Yanga iliiwakilisha Tanzania katika michuano. Naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na wananchi tuendeleo kui-*support* timu yetu ya Tanzania, kuteleza siyo kuanguka. (Makofi/Kicheko)

Ndugu Athuman Kwikima, Mkurugenzi wa Utawala anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa katika eneo la maonesho ya Bunge lililopo nyuma ya Jengo la Utawala, mkabala na Idara ya Habari kuna maonyesho yafuatayo:-

Wajasiriamali waliokweda nchini Uganda kupeperusha bendera ya Taifa letu wapo hapa Bungeni kuonesha na kuuza bidhaa mbalimbali. Mnaombwa kutembelea maonesho hayo na kuunga mkono. Kampuni ya Mabati ALAF pia wapo wakionyesha mabati ya aina mbalimbali waliyotengeneza na kuuza kwa bei nafuu. Aidha, Kampuni ya Simu ya *TTCL* wapo na vifaa mbalimbali

vinavyotengenezwa na wanahitaji muone na kuwaunga mkono.

Pia wataalam kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma watakuwepo pia katika viwanja hivyo kuanzia saa 7:00 mchana kwa ajili ya kuuza viwanja vilivyopo maeneo ya Mtumba na Iyumbu hivyo mnaombwa kufika na kuchangua viwanja mnavyohitaji kwa bei nafuu.

Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kufika katika viwanja hivyo ili muweze kujipatia huduma hizo. Katibu.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Jambo la kuahirisha shughuli za Bunge.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa Nkamia subiri kwanza, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Kubenea. Haya Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niombe Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na kwa sababu ya muda naomba nisiisome.

Leo wakati Mheshimiwa Waziri akijibu swali namba 190 la Mheshimiwa Constantine Kanyasu kuhusu ubora wa mbegu za pamba, nilikuwa naomba mwongozo wako, mbegu za pamba ni miongoni mwa mbegu ambazo zinatoa mafuta ya kula. Kuanzia jana na leo vyombo vingi vya habari hasa magazeti vimekuwa vikiandika juu ya kuadimika kwa mafuta ya kula hapa nchini hali ambayo inasababisha baadhi ya mafuta yanayouzwa kupanda bei kwa haraka.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mwongozo wako, Serikali itoe maelezo, je, taarifa hizi zina ukweli gani na kuwaondolea wananchi hofu kwa sababu baadhi ya wazalishaji wa mafuta wanadaiwa wamefunga viwanda, inawezekana ikawa ni janja ya kutaka kupandisha bei ya mafuta ili wananchi waweze kuumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Muongozo wako, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe!

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kutumia Kanuni ya 69 kama utaridhia ili angalau tuweze kuahirisha shughuli za Bunge angalau kwa dakika 30 tuweze kujadili jambo moja tu kwamba mwezi wa Ramadhani unakaribia na kama alivyoanza kusema Mheshimiwa Nkamia bei ya mafuta ya kula imepanda, bei ya sukari imepanda, lakini nchi zilizotuzunguka zimefuta kodi katika moja ya chakula ambacho huliwa sana na Waislamu kipindi cha mwezi wa Ramadhani na ni *sunna* wakati wa kufuturu ni tende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ili Serikali iweze kukubaliana na kama Bunge litaazimia kufutia kodi tende ili kuwapunguzia mzigo Waislamu mwezi wa Ramadhani *considering* bei ya mafuta imepanda, bei ya sukari imepanda sasa na tende kuwa na kodi na yenyewe gharama yake itakuwa kubwa ili kuweza kuupunguza mzigo huu, kama utaridhia tuahirishe angalau kwa nusu saa Bunge lijadili tuweze kufanya azimio la kuitaka Serikali ifute kodi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie Kanuni ya 68 kuhusu utaratibu kuanzia fasili ya (1) mpaka ya (7) na kuokoa muda sitaisma ili nitumie Kanuni ya 31 ya Dua ndani ya Bunge hili pamoja na Kanuni ya 101 na 103 lakini sitazisoma zote.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 31 ni ya Dua na ule mstari wa pili unasema; “ili haki yako itendeke, uhuru, umoja, haki na amani na kufanya maamuzi sahihi kwa manufaa ya Taifa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Kanuni ya 101 inazungumzia kuhusu mjadala katika Kamati ya Matumizi. Fasili ya 3 inasema; “Mbunge atakaeamua kutumia kifungu hiki itakuwa ni suala la sera, mshahara wa Waziri ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahususi la sera” ile ya 4 ndiyo inayosema kwamba; “kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 3, Kamati ya Vyama zitawasilisha kwa Spika majina ya Wabunge watakaomba kupata ufafanuzi wa suala mahususi la kisera na Spika atatoa nafasi hiyo kwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano” pamoja na ile ya 103 yote ya kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tarehe 3 Mei, Mheshimiwa Esther Matiko naye aliomba tena muongozo haa kuhusu utaratibu wa Kamati ya Matumizi, Kiti chako hakina utaratibu unaofanana, inategemea ni nani yuko hapo. Wakati mwingine aliyeko hapo kwenye kiti cha Spika anasema uwiano watatoka Wabunge wanne upande wa Chama Tawala na wawili upande wa huku lakini kwa mzunguko, akitoka mmoja kule anafuata CHADEMA *then* wanafuata CUF. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona mara mbili hapa, tarehe 3 Mei, tarehe 2 Mei wote wakitoka upande mmoja, Ijumaa tuliona kwamba wakitoka upande huku wanne halafu wakaenda CUF na kile chama kinachofuata kikapewa mmoja sasa tusiposimamia kanuni hizi na hasa Kiti kisipoongoza kusimamia kanuni hizi itakuwa ni fujo ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu kwamba nimesema mpaka ile ya 68(7) ili kiti kitoe utaratibu na hasa suala la, ni Wajumbe wangapi wanaounga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiti kinasema wakati mwingine wewe ni mmoja, wakati mwingine wanasema wawe 10 Kiti hicho hicho wanasema akiomba kutoa hoja

wakati wa kutoa shilingi wanasema ni 10 wengine ni mmoja. Kwa hiyo, namaliza kwa kuomba kwamba tunaomba sasa tupate mwongozo sahihi wa Kiti kuhusu matumizi ya Kanuni hizi kwenye Kanuni zote nilizozisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nipate muongozo, wakati Naibu Waziri wa Kilimo akijibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari, swali la nyongeza kuhusiana na kununua mazao mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate Mwongozo wako kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa tamko la Kiserikali ambalo kwa sisi tunaotoka Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hasa Iringa ni tamko kali na ningepata nipate Mwongozo wako kwa sababu kule Iringa kwa mfano, kuna mahindi haya tunayoyaita Gobo huwa yananunuliwa na yanavunwa yakiwa shambani, sasa Naibu Waziri amesema ni marufuku kabisa kuchukua mazao shambani na hii naona ni kuingilia uhuru wa wakulima na mimi kama mkulima vilevile naona naingiliwa katika uhuru wa kuvuna na kuuza mazao yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate Mwongozo wako, je, ni halali kwa Serikali kutoa matamko kama haya kwa wakulima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo na nimesimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63(2) inasema; "Bunge ndiyo

chombo kikuu cha wananchi cha kusimamia Serikali” na Ibara ya 3(1) inasema; “Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina dini.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali hii ambayo haina dini na Katiba yetu inatambua Bunge kwamba ndiyo chombo kikuu cha kusimamia Serikali kwa niaba ya wananchi, Serikali imetoa mamlaka ya kusimamia suala zima la *Hijja* kwa chombo kimoja cha Waislamu kinaitwa BAKWATA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina taasisi zaidi ya 11 zilizosajiliwa zenye haki sawa na BAKWATA na kwa msingi huo kuwachukua Waislamu wote, kuwaambia waungane, waende kutumia BAKWATA kama chombo chao cha kuwapeleka *Hijja* inakiuka Katiba ya nchi inayotoa uhuru wa kuabudu na kila mtu kuwa na uhuru wa kuabudu na kujiunga na taasisi yoyote anayotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako kwamba Kiti kiliwahi kutoa uamuzi ndani ya Bunge kwamba mambo ya dini yasijadiliwe ndani ya Bunge, lakini Serikali ambayo haina dini inajiingiza katika mambo ya dini kwa kulazimisha chombo kimoja kisimamie masuala ya *Hijja* ambayo ni imani ya Waislamu na mimi nazungumza haya kwa sababu moja, nimepokea malalamiko kutoka kwa Masheikh na Maimamu wa Misikiti ya Dar es Salaam na Jimbo la Ubungo na pili, mimi mwenyewe ni muislamu na BAKWATA iliwahi kuwapeleka waislamu *Hijja* ikawaweka *airport* siku 10 miaka mitano iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba mwongozo wako, je, ni halali Serikali isiyokuwa na dini kusimamia mambo ya dini? Na kwamba je, Bunge hili haliwezi kujadili kwa niaba ya wananchi mambo ya dini ambayo Serikali imejiingiza yenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwongozo wa Mheshimiwa Nkamia, Waziri wa Kilimo uko hapa ujibu pamoja na la Mheshimiwa Msigwa maana siku hizi tumeanzisha miongozo hii imekuwa ni kipindi kingine cha maswali na majibu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nitoe ufafanuzi juu ya mambo mawili ambayo Waheshimiwa Wabunge wameomba Mwongozo wako. Nianze na hili la Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu za pamba kutumika kukamua mafuta linafahamika lakini kwa mavuno ya pamba ya msimu uliopita tulivuna tani laki 133 ya pamba mbegu. Ukiifanya *GOT* ya asilimia 32 kwamba ndiyo *news* unabakiza kama tani 92,000 kuwa mbegu. Katika mbegu hizo tuliondoa tani 25,000 kwa ajili ya kupanda mbegu za msimu huu na kwa hivyo zikabaki tani 67,000 kama mbegu iliyokamuliwa mafuta. Ukikamua mafuta tani 67,000 kwa wastani wa *40 percent extraction rate* unajiona kwamba mafuta yaliyopatikana na pamba ni kidogo sana, ni kama tani 26,000 tu. Kwa hiyo, suala la mafuta yanayotokana na pamba kwa uhakika kwa msimu huu hayakutarajiwa kuwa mengi kwa sababu ya mavuno yenyewe ya pamba yalikuwa kidogo.

Sasa Serikali inachokifanya kwa kawaida huwa inaruhusu mafuta kutoka nje ya nchi kuingizwa ndani na mafuta yanayoingizwa kwa wingi zaidi ni *crude palm oil* ambayo yanakuja kuwa *refined* hapa ndani na kusaidia walaji kupata mafuta kama mahitaji yalivyo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba suala la mafuta linafahamika na Serikali inalifanyiakazi kuhakikisha kwamba wananchi hawatakosha mafuta au hayatapanda bei sana kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anataka kutia wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili la Mheshimiwa Msigwa kuhusu zuio la wafanyabiashara kuingia mashambani na kununua mazao ya wakulima, ukimsikilza

Mheshimiwa Fakharia Shomari alivyouliza swali lake la nyongeza alionesha wazi kwamba kitendo hicho kinawaonea wakulima na sisi tumekuwa tukisema pia kwamba unaponunua shambani hata kipimo cha kununua hakipo. Mtu anatazama tu shamba anasema hapa nitakupa shilingi 60,000 kumbe mavuno halisi yatakatayokuja kupatikana pale ni shilingi 200,000.

Kwa hiyo, tunachokifanya ni kuweka tu utaratibu ambao utahakikisha kwamba mkulima haonewi na mfanyabiashara haonewi, haki bin haki. Wewe kama una shida mkopeshe pesa, auze mazao yake akulipe pesa kuliko kukadiria kwamba hapa utavuna tani moja kumbe shambani iko tani tano na una *-take advantage* ya umaskini wa mtu kumfanyia biashara ambayo siyo halali. Kwa hiyo, ndiyo maana utaratibu unawekwa wa masoko ambao utazingatia usawa na haki kwa pande zote mbili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru. Nichukue fursa hii kuwaeleza Waheshimiwa wabunge na Bunge lako tukufu kwamba sasa hivi kwenye hifadhi ya matenki pale Da es Salaam kuna *CPO* takribani tani 40,000 na Meli zilizoko nje zina *CPO* takribani *crude palm oil* au mafuta ghafi ya Mawese takribani 50,000; meli zilizoko nje na zilizoko ndani wastani wa takribani tani 90,000. Kinacholeta tatizo ni kutokukubaliana katika viwango vya kodi. Ukileta mafuta kwa Sheria tuliyopitisha (*CPO*) ile *crude palm oil* kwa Sheria tulizopitisha sisi Tanzania tunamtoza muagizaji asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipimo vilivyopimwa, vinamuonesha Kamishna wa *Customs*, kwamba hii sio *crude oil* wala hii siyo *finished oil*, ambayo inamuonesha kamishna kwamba basi hii ni mafuta safi anataka kutoza asilimia 25. Serikali tumeichukua hili na watalaam wa Serikali watatoa majibu kati ya leo na kesho ili tuweze kujua hii ni *crude* au si-*crude* twende asilimia 10 au 25 lakini kama nilivyowaeleza tunayo hazina ya kutosha si-*crude oil* tani 90,000 na kwa hiyo

niwahakikishe katika mwezi mtukufu wa Ramadhani tutakwenda kufunga vizuri tutakula vyakula vyetu vyenye mafuta ya kutosha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mtajibu na hilo la tende. Waziri wa Fedha yupo hapo? Jibu la tende la Mhe. Hussein M. Bashe.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tende ni suala la kwenda kuzungumza na Waziri wa Fedha na kuna kikao tulifanya juzi, kwa sababu hakikuwepo kwenye sheria yetu tuliyoipitisha. Baada ya kuona lile tangazo la nchi ya jirani ndo likawa linazunguka katika vikao visivyo rasmi na mimi nimeliona. Kwa hiyo, tutalipeleka kwa Waziri wa Fedha tuweze kwenda kumshawishi kwenye busara hii kusudi katika mwezi huu Bunge lichume thawabu na nchi ichume thawabu, tutamshauri Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sawa lakini miaka ya nyuma tende huwa inapaa *exemption* jaribuni kulitizama hilo.

Waheshimiwa suala la Mheshimiwa James Mbatia, kanuni zetu ziko *clear*. Kiti hakihojiwi ndani ya Bunge, kama kuna jambo lolote, Mbunge yeyote. Kanuni ya 5(4) inasema; "Mbunge yoyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika."

Sasa ni vema mkaandika iwe *on record* majibu mtajibiwa. Ni mara nyingi sana kipindi cha maswali hasa kipindi hiki cha Kamati ya Matumizi kunatokea sitofahamu ya Wabunge hasa ni vizuri mkamwandika Katibu malalamiko yote mliyoainisha ili Katibu aweze kuwajibu na kila mtu ajue.

Ni kama vile mimi mara nyingi sana nakupeni mifano rahisi sana, *referee* akiwa mpirani hahojiwi na mchezaji namna gani anavyofanya maamuzi isipokuwa kuna kamati ya masaa 72, hali kadharika na hapa, kwa hiyo, ninyi andikeni barua kwa mujibu wa Kanuni ya 5(4) mpate majibu sahihi

Mheshimiwa Saed Kubenea hili nalichukua sababu lazima nilifanyie kazi ili nilitizame taratibu zake zilivyo. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MWENYEKITI:** Samahani, Samahani kidogo, kuna Waheshimiwa Wabunge majina ya wageni wao yalikuwa yamesahaulika, Mheshimiwa Chikambo, anaomba kuwatambulisha wageni wake ambao ni Ndugu zake, Hamis Said Mkali, Issa Yusuph Simba, Rajabu Kassim Kamili, Said Khalifa Selemani.

Pia Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Aweso anaomba kuwatambulisha wadau wa Shirika wa Maendeleo ya Maji wamo kwenye ukumbi, karibu sana. Katibu. (*Makofi*)

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa neema na baraka kwa kutujalia uhai na afya njema, kuweza kuwepo mahala hapa kujadili mapitio ya utekelezaji wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kuiteua kuwa Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Wizara inayomgusa kila mwananchi, napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais pamoja na Bunge lako tukufu kuwa nitafanya kazi kwa bidii, maarifa na uadilifu mkubwa, ili kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuwapatia Watanzania huduma ya maji safi na salama pamoja na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri ili kuziongoza Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza na kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa kazi za Serikali. Nawapongeza pia Mawaziri wenzangu waliotangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa maoni, ushauri, na ushirikiano walioutoa wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mbunge kupitia Jimbo la Siha; Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge kupitia Jimbo la Kinondoni; Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Mbunge kupitia Jimbo la Longido; Mheshimiwa Dkt. Justin Joseph Monko, Mbunge kupitia Jimbo la Singida Kaskazini na Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge kupitia Jimbo la Songea Mjini. Naahidi kushirikiana nao katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu kupitia Sekta ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa, taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Leonidas Tutubet Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini. Napenda kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa msiba huo mkubwa, Mwenyezi Mungu aweke roho ya marehemu mahali pema pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuchukua fursa hii, kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ambayo inatoa taarifa hali ya sekta ya Maji na Umwagili nchini. Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na malengo ya sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, changamoto na hatua zilizochukuliwa pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka 2018/2019. Maelezo yatakayotolewa katika hotuba hii yamezingatia serana mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa pamoja na sheria, kanuni na miongozo inayohusiana na sekta ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda niliopangiwa, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sekta ya maji na umwagiliaji nchini, maji ni rasilimali muhimu kwa maendeleo

ya jamii, na sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwemo viwanda, kilimo, uvuvi, na utalii. Vilevile upatikanaji wa maji wa kutosha ambayo ni safi na salama kwa ajili ya matumizi ya majumbani ni usafi wa mazingira ni muhimu katika kulinda afya za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi maji safi na salama, pamoja na kuiwezesha nchi yetu kuwa na uchumi wa kati kufikia mwaka 2025 Wizara yangu inatekeleza mipango Serikali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2000 ambayo itakwenda mpaka mwaka 2025. Malengo ya maendeleo endelevu ambayo yanaanza mwaka 2016 - 2030; Awamu ya Pili ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano kati ya mwaka 2016/2017 na 2020/2021; Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi mwaka 2020 na ahadi mbalimbali za Serikali. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kupitia Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi katika sekta hizo ni kama ifuatavyo; sekta ya maji, Wizara inaendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo utekelezaji wake inahusisha programu ndogo tano ambazo ni usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma ya maji vijijini, huduma ya maji mijini, kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira na kujenga uwezo wa taasisi zinazosimamia utekelezaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; nchi yetu inapata mvua katika vipindi viwili ambavyo ni vya masika kati ya mwezi Machi na Mei na mvua za vuli kati ya mwezi Oktoba na Novemba. Hata hivyo kuna baadhi ya maeneo ambayo yanapata mvua mara moja ambayo ni Disemba hadi Aprili. Kiwango cha mvua katika maeneo mengi nchini kwa mwaka ni wastani ni mm 900 hadi mm1200. Katika maeneo ya katikati ya nchi ni wastani wa

mm 550 na maeneo ya nyanda za juu kusini na maeneo ya milima ya Usambara ni wastani wa mm. 2200 hadi 2500 kwa mwaka kulingana na hali ya hewa ya maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kiasi kinachopatikana nchini rasilimali za maji juu ya ardhi zinazofaa kwa matumizi mbalimbali ni wastani wa kilometa za ujazo 92.7, na hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi inakadiriwa kilometa za ujazo 30. Hata hivyo, mtawanyiko na upatikanaji wa rasilimali hizo nchini haulingani katika maeneo yote kutokana na tofauti ya hali ya hewa, jiografia na jiojiojia. Kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu ni wastani wa mita za ujazo 1800 kwa mwaka na kuiweka nchi yetu katika nafasi ya kwanza Afrika Mashariki na nne Barani Afrika ikitanguliwa na Zambia, Msumbiji na Sudani Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni wastani wa mita za ujazo 1700 chini ya kiwango hicho hali hiyo hujulikana kama uhaba wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na rasilimali za maji za kutosha kwa sasa, rasilimali hizo zimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la idadi ya watu.

Aidha, uharibifu wa mazingira ambao husababisha vyanzo vya maji kukauka, mabadiliko ya tabia ya nchi na uchafuzi wa vyanzo vinaharibu ubora wa maji, iwapo hali hiyo haitadhibitiwa kiwango hicho kitaendelea kushuka na kuhatarisha ukuaji wa sekta za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ubora wa maji katika nchi yetu hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine na kunatokana na hali ya miamba ya asili, shughuli za kibinadamu, jiografia ya eneo na mabadiliko ya tabia ya nchi. Wizara imeainisha viashiria vya ubora wa maji ambavyo ni changamoto katika baadhi ya maeneo nchini. Changamoto kubwa kwa maji juu ya ardhi ni uwepo wa kiwango kikubwa cha madini ya *nitrogen*, *phosphorous*, tope pamoja na

vimelea vya vijidudu vinavyosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji chini ya ardhi changamoto ni uwepo wa kiwango kikubwa cha madini ya chumvichumvi, tindikali, *nitrate*, madini ya *flouride*, chuma, manganese na *chloride*. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa miradi ya maji inayotekelezwa nchini inawekewa miundombinu ya kutibu na kusafisha maji ili kulinda afya za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za maji vijijini, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inaelekeza kuwapatia wananchi waishio vijijini maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji. Lengo ni kufikia asilimia 85 ya wananchi waopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2020. Hadi sasa miundombinu ya maji iliyojengwa, ina jumla ya vituo vya kuchotea maji 125,086 ambavyo vina uwezo wa kuhudumia watu 30,972,000 sawa na asilimia 85.2 ya wananchi 36,344,505 waishio vijijini; kati ya hivyo vituo 86,877 tu ndivyo vinavyofanya kazi ya kutoa huduma kwa watu 21,719,250 sawa na asilimia 59.76 ya wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo imesababishwa na changamoto ya mfumo uliopo wa usimamizi na uendelezaji wa miradi ya maji. Katika kuwapunguzia wananchi gharama za uendeshaji, na matengenezo Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza kubadilisha mitambo inayotumia nishati ya disel kusukuma maji na kufunga mitambo inayotumia nishati ya jua.

Vilevile Serikali inaandaa mifumo itakayofaa kusimamia na kuendeleza miradi ya maji ikiwa ni pamoja na kuvimarisha vyombo vya watumiaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji mijini; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika jiji la Dar es Salaam. Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo pamoja na Miji na vijiji vinavyohudumiwa na miradi ya maji ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ni kama ifuatavyo; kwanza ni uzalishaji wa mahitaji ya maji nchini; kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji katika kipindi cha mwezi Machi, 2017 hadi mwezi Machi, 2018 kumeongeza uzalishaji wa maji katika Miji Mikuu ya Mikoa kutoka lita milioni 400 kwa siku hadi lita milioni 404 ikilinganishwa na mahitaji ya lita milioni 646. Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo kutoka lita milioni 99.7 hadi lita milioni 100.6 ikilinganishwa na mahitaji ya lita milioni 277.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji ya kitaifa, uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita milioni 59.5 kwa siku hadi lita milioni 67.2 kwa siku ikilinganishwa na mahitaji halisi ya lita milioni 125.6. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita milioni 300 kwa siku hadi lita milioni 504 ikilinganishwa na mahitaji ya lita milioni 544.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji; hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa ni wastani asilimia 78. Kiwango hicho kimeshuka ikilinganishwa na asilimia 86 ya mwaka 2016/2017 kutokana na kuongezeka na eneo la utoaji wa huduma baada ya upanuzi wa mipaka ya baadhi ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa miji mipya pamoja na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji; katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ni wastani wa asilimia 60. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ni asilimia 75. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 inaelekeza kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma mijini kufikia asilimia 95 katika miji mikuu ya mikoa na Dar es Salaam na asilimia 90 katika

miji mikuu ya wilaya. Miji midogo na miradi ya kitaifa azma ya Serikali ni kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uondoaji maji taka mijini miundombinu imejengwa ya Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Songea, Tabora na Tanga. Kwa miji mingine kwa huduma ya uondoaji wa maji taka inatolewa kwa kutumia magari ya maji taka na kutiririsha kwenye mabwawa au maeneo yaliyotengwa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya uondoaji maji taka kwa kujenga, kukarabati na kupanua mifumo ya uondoaji maji taka pamoja na ununuzi wa magari ya uondoaji maji taka. Lengo ni kuboresha upatikanaji wa huduma hiyo mijini hadi kufikia asilimia 30 itakapofika mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya umwagilaji; nchi yetu ina eneo la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagilaji, ambapo hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, hekta milioni 4.8 zina uwezekano wa kati na hekta milioni 22.3 zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kujenga miundombinu yenye jumla ya hekta milioni moja katika *scheme* za wakulima wadogo, wakati na wakubwa ifikapo mwaka 2020/2021. Hadi mwezi Machi, 2018 jumla hekta 475,052 zinamwagiliwa sawa na asilimia 47.44 ya lengo na asilimia 1.6 ya eneo lote linalofaa kwa umwagilaji. Ili kuhakikisha lengo linafikwa, Serikali inaendelea kukarabati miundombinu ya *scheme* zilizoharibika kukamilisha ujenzi wa *scheme* pamoja na kufanya upembeuzi yakinifu, usanifu pamoja na kujenga *scheme* na mabwawa mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018 na mpango wa mwaka

2018/2019 fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Fungu 49 - Wizara ya Maji na umwagiliaji iliidhinishwa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 648.06 na kati ya fedha hizo shilingi bilioni 24.046 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 623.61 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili, 2018 jumla ya shilingi bilioni 359.9 sawa na asilimia 58 ya fedha za maendeleo zimepokelewa na shilingi bilioni 12.83 sawa na asilimia 52.45 ya fedha za matumizi ya kawaida zimepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliidhinishwa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 24.61 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 4.06 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 20.1 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili, 2018 jumla ya shilingi bilioni 2.47 sawa na asilimia 12.13 za fedha za maendeleo zimepokelewa na shilingi bilioni 2.6 sawa na asilimia 65.07 ya fedha za matumizi ya kawaida zimepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika mwaka 2017/2018 na malengo ya mwaka 2018/2019; usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini. Utekelezaji wa majukumu hayo, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji; ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa rasilimali za maji katika mwaka wa fedha 2017/2018 vyanzo sita vya maji vimewekewa mipaka na kuongeza idadi ya vyanzo vya maji vilivyowekewa mipaka kufikia 88; vilevile vyanzo 18 vimetangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji na taratibu ya kungaza maeneo zaidi zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imepanga kutangaza vyanzo 45 kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji Wizara hufanya ukaguzi wa ubora wa maji taka yanayotiririshwa kwenye vyanzo vya maji. Hadi mwezi Machi, 2018 jumla ya viwanda 22, migodi saba na taasisi nne zilifanyiwa ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi yalibaini kuwepo kwa uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji unaotokana na utiririshaji wa maji taka na wahusika walichukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya vibali 13 vilizolewa kwa ajili ya kutiririsha maji taka yanayokidhi viwango kwenye vyanzo vya maji. Katika mwaka fedha 2018/2019 jumla ya vibali 30 vya kutiririsha maji taka vimepangwa kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda, Farkwa na Ndembela; katika kuhakikisha uwepo wa maji ya kutosha kwa matumizi mbalimbali kwa kipindi chote kwa mwaka, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda - Mororogo, Farkwa - Dodoma na Ndembela - Iringa. Bwawa la Farkwa litatumika kwa ajili ya usambazaji wa maji katika mji wa Dodoma na Wilaya za Chemba na Kondo, pamoja na Kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kidunda litatumika kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruvu unakuwa na maji katika kipindi chote cha mwaka. Kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji umeme, Bwawa la Ndembela litatumika kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruaha unakuwa na maji katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme; hadi sasa usanifu wa mabwawa hayo umekalimika ikiwa ni pamoja na tathmini za kimazingira na kijamii pamoja na uthamini wa mali, pamoja na kulipa fidia wananchi watakaopisha ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo. Hadi mwezi Machi, 2018 ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda



umekamilika na unaendelea kwa mabwawa ya Farkwa na Ndembela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kunusuru vyanzo vya maji kupitia mpango endelevu wa matumizi bora ya ardhi katika mabonde madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu. Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) pamoja na Mfuko wa Mazingira Duniani (*Global Environmental Facility*) inatekeleza mradi wa kunusuru vyanzo vya maji kupitia mpango endelevu wa matumizi bora ya ardhi katika mabonde madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu ambao utagharimu dola za Marekani milioni 27.65. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 ambapo jumla ya vijiji 20 katika Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Mvomero, Muheza, Mkinga na Korogwe vitanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2018 kazi zilizotekelezwa ni uanishaji wa maeneo yatakasaidia kutoa taarifa za msingi kuhusu wingi na ubora wa maji katika mabonde hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa misitu hekta mia moja hamsini na moja pointi tatu nane, kwenye hifadhi ya Mlima Uruguru, na hekta mia moja na kumi na tano kwenye hifadhi ya Msitu wa Amani, zilizokuwa zimeharibiwa kwa kiasi kikubwa na shughuri za kilimo na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kuwapatia wananchi shughuli mbadala za kujipatia kipato na kuunda jumuiya nne za watumiaji maji.

Aidha, mradi huo umejenga miundombinu ya kusambaza maji yenye urefu wa kilometa 3.8 katika vijiji vya Mashewa, Shembekeza na Kimbo ambapo wananchi wapatao 3700 wananufaika. Katika mwaka fedha 2018/2019

Serikali itaendelekeza mradi huo ili kunusuru vyanzo vya maji katika Bonde dogo la Mto Zigi na Mto Ruvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi, nchi yetu ina mabonde saba yanayovuka mipaka ya nchi na hivyo kulazimika kushirikiana na nchi nyingine 17 katika kutunza rasilimali za maji zilizopo katika kwenye mabonde hayo. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Elitrea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendela kushirikiana na nchi hizo kupitia vyombo vya pamoja vilivyoundwa ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwa kutelekeza progamu na miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda iliendelea kutelekeza Awamu ya Pili ya Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira ya Ziwa Victoria, ambayo muda wake ulimalizika mwezi Desemba, 2017. Kazi zilizokamilika yaani ukarabati na upanuzi wa maabara za maji Mwanza, Musoma na Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa machinjio ya Mwanza, ujenzi wa mfumo wa maji taka katika machinjio ya Jiji Mwanza ambao uko kwenye hatua za majaribio, utekelezaji wa miradi 295 ya kijamii inayonufaisha wakazi 505,550 na uondoaji wa hekta 9 .39 za gugumaji katika Ziwa Victoria. Vilevile huduma ya usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza umeboreshwa kwa kuongeza kilometa 7.9 za mtandao wa maji taka na kuunganisha wateja 290 kweye mtandao huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaandaa andiko kwa ajili ya Awamu ya Tatu ya miradi ambayo itahusisha kukamilisha miradi ya kijamii, upanuzi wa miundombinu ya maji taka pamoja na upanuzi wa miradi

inayozingatia usafi wa mazingira katika maeneo ya Simiyu na maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria pamoja na Miji ya Geita, Chato, Kayanga, Umulushaka, Buseresere, Katoro, Bunazi na Buchosa. Maelezo ya kina kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimaji nchini yameanishwa kuanzia ukurasa wa 13 hadi ukurasa wa 27 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ubora na usafi wa maji; maji safi na salama ni muhimu katika kulinda afya za wanachi dhidi ya magonjwa yatokanayo na maji. Wizara yangu inajukumu la kuhakikisha na kufatilia ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji. Mitandao ya kusambaza maji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam ambao husaidia kutoa maamuzi kuhusu matumizi ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya sampuli ya 3471 za maji safi kwa matumizi mbalimbali na sampuli 256 za maji taka zilikusanywa na kuchunguzwa. Kati ya sampuli hizo asilimia 76 ya sampuli za maji kwa matumizi ya majumbani na asilimia 100 ya sampuli ya maji kwa ajili ya matumizi ya viwanda ujenzi, umwagiliaji na utafiti zilikidhi viwango.

Vilevile asilimia 35 ya sampuli ya maji taka zilikidhi viwango vinavyokubalika kutirishwa kwenye mazingira. Kwa upande wa sampuli ambazo hazikukidhi viwango vinavyokubalika Serikali ilitoa ushauri wa kitaalam kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora wa madawa ya kusafisha maji ya kutibu maji, katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya sampuli 12 za madawa ya kusafisha na kutibu maji zilichukuliwa. Sampuli hizo ni za dawa za aina ya *Calcium Hypocroside* kwa ajili ya kutibu maji na *Aluminium Sulphate* au shabu, *Polymerblend* na *Soda Ash* kwa ajili ya kusafisha maji. Matokeo ya uchanguzi yalionyesha madawa hayo kukidhi viwango vilivyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uondoaji wa madini ya *floride* katika maji ya kunywa na kupikia, Wizara imeendelea mkakati wa uondoaji wa madini ya *floride* kwenye maji ya kunywa na kupikia katika maeneo ya yaliyoathirika na madini hayo. Hadi mwezi Machi, 2018 jumla ya mitambo midogo 210 inayotumika katika ngazi ya kaya imesambazwa katika Mikoa ya Arusha na mwanza ambapo wananchi 1700 wananufaika. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara imepanga kutengenea na kusambaza mitambo midogo 1,000 ya kuondoa madini ya *floride* akwenye maji katika ngazi kaya kwenye maeneo yaliyoathiriwa na madini hayo. Maelezo ya kina kuhusu huduma za ubora na usafi wa maji nchini, yameanishwa kuanzia ukurasa wa 27 hadi ukurasa wa 33 wa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji vijijini, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini unahusisha ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo na hadi mwezi Machi, 2018, jumla ya miradi 1,493 imetekelezwa na inawanufaisha wananchi 21,321,500 waishio vijijini. Aidha, miradi 366 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu Serikali inaendelea programu tatu, ambao ni mfumo wa malipo kwa matokeo (*payment by result*), kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini na matumizi ya teknolojia ya nishati jadidifu. Lengo la programu hizo ni kuimarisha utekelezaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Utekelezaji wa programu hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Mfumo wa Malipo kwa Matokeo; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (*DFID*) inatekeleza mfumo wa malipo kwa matokeo ili kutoa motisha ya fedha katika utekelezaji wa miradi kwenye Halmashauri kwa lengo la kuongeza kasi ya undeshaji na matengenezo ya miradi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mfumo huo malipo ya paundi 50 hutolewa kwa kila kituo cha kuchotea maji kitakachokarabatiwa na kufanya kazi na paundi 1500 kwa kituo kipya kitakachojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya mpango ulikamilika mwezi jJuni, 2017 na jumla ya Halmashauri 57 zilikidhi vigezo vya kupata malipo hayo ambapo shilingi bilioni 3.93 zilipelekwa katika Halmashauri hizo kati ya shilingi bilioni sita zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Pili inaendelea ambapo jumla ya Halmashauri 72 zimekidhi vigezo kwa kupata malipo shilingi bilioni 8.55 kati ya shilingi bilioni 53.6 zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2017/18. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 shilingi bilioni 54.5 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini; Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itaanza kutekeleza programu ya kuendeleza na kuimarisha huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwa kutumia mfumo wa malipo kwa matokeo kwa kipindi cha miaka sita, kuanzia mwaka 2018/2024 kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni mia tatu. Programu hiyo inatarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai, 2018 na itatekelezwa katika mikoa 17 ya Tabora, Katavi, Rukwa, Lindi, Geita, Shinyanga, Singida, Kagera, Mwanza, Manyara, Mtwara, Simiyu, Iringa, Mara, Ruvuma, Kigoma na Songwe. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni 23.5 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya teknolojia ya nishati jadidifu, Serikali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ohio cha Marekani inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya majaribio ya nishati jadidifu katika vijiji vya Ghalunyangu na Mughangha katika Halmashauri ya Singida iliyoanza kutekelezwa mwezi Novemba, 2017. Aidha, Serikali

inaendelea na mazungumzo na Chuo hicho ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwenye vijiji 36 katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Mara, Tabora, Singida na Dodoma. Lengo ni kutekeleza miradi ya matumizi ya nishati jadidifu katika vijiji 125 katika maeneo mbalimbali nchini ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji; katika mwaka wa fedha 2017/2018 utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji vijijini umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unatarajia kutoa maji kutoka kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu na kuhudumia miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, *OFID*, *Saudi Fund* na *Kuwait Fund* na umegawanyika katika awamu mbili na utekelezaji wa awamu ya kwanza umegawanyika katika vipande vinne. Hadi mwezi Machi, 2018, utekelezaji wa kipande cha kwanza umefikia asilimia 68 na kipande cha nne asilimia 37. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza kipande cha pili na cha tatu. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni 35 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mradi huo. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao 456,931 wa Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa vijiji 100 vilivyopo kandokando ya bomba kuu la *KASHWASA*; Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa vijiji 100 vilivyopo kandokando ya bomba kuu la maji la *KASHWASA*. Ujenzi wa miradi kwenye vijiji 14 umekamilika na kunufaisha wananchi wapatao 38,348 wa vijiji vya Runele, Gatuli, Nyashimbi, Magobeko, Kakulu, Butegwa, Nyang'homango, Ng'homango, Jimondoli, Kadoto, Lyabusalu, Mwajiji, Ichongo na Bukamba. Aidha, utekelezaji wa mradi unaendelea katika vijiji vya Mwasekagi na Mwakatola. Katika mwaka 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni saba kwa

ajili ya kuendelea na usanifu na ujenzi wa miradi kwenye vijiji vilivyobaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Maji wa Ntomoko; Mradi wa maji wa Ntomoko ulilenga kutoa huduma katika vijiji 18 vya Wilaya za Kondoza na Chemba. Kutokana na uwezo wa chanzo kuonekana kutokidhi mahitaji, mwezi Novemba, 2017 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliunda timu ya pamoja ya wataalam kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina wa mradi pamoja na kutafuta chanzo kingine cha maji kwa ajili ya kuongeza wingi wa maji utakaokidhi mahitaji ya maji katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hiyo ilibaini kuwa chanzo cha Ntomoko kina uwezo wa kuhudumia vijiji vitatu tu. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bwawa lenye mita za ujazo milioni 2.8 litakalojengwa kwenye eneo la Kisangaji ili kukidhi mahitaji ya vijiji vilivyobaki ambavyo kwa sasa havipati huduma ya maji. Usanifu wa bwawa hilo pamoja na bomba kuu kutoka katika chanzo cha bwawa hadi makutano ya kijiji cha Lusangi umekamilika na utekelezaji wa mradi huo utasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (*DUWASA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati na ujenzi wa mabwawa, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini hususan kwenye maeneo kame kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2018 ujenzi wa bwawa la Matwiga lililopo Wilaya ya Chunya umekamilika na linatarajiwa kuhudumia vijiji 15. Kwa upande wa bwawa la Mwanjoro lililopo Wilayani Meatu, utekelezaji wa ujenzi umefikia asilimia 91. Bwawa hilo likikamilika litahudumia vijiji vitatu vya Mwanjoro, Jinamo na Mbushi vilivyopo Wilayani Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha uwepo wa vyanzo vya maji vya uhakika hususan kwenye maeneo kame, Serikali imeendelea kufanya utafiti ili kubaini maeneo mbalimbali yanayofaa kujengwa mabwawa nchini. Hadi mwezi Machi, 2018, usanifu wa Bwawa la Nsekwa katika Halmashauri ya Mlele umekamilika na taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea. Kwa upande wa Bwawa la Dongo litakalohudumia Halmashauri za Kiteto, Gairo na Kongwa taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo zinaendelea. Vilevile timu ya pamoja ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na usanifu wa Bwawa la Kidete lililopo Wilaya ya Kilosa. Aidha, utafiti kwa ajili ya maeneo yanayofaa kujenga mabwawa mapya unaendelea katika Halmashauri za Bahi, Mpwapwa na Chemba. Katika mwaka 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 3.87 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba ni muhimu kutokana na uhaba wa upatikanaji wa maji hususan katika maeneo kame. Kutokana na umuhimu huo, Serikali inaendelea kuzihamasisha taasisi za kijamii, asasi na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao. Vilevile Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wananchi kuhusiana na uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia rahisi kupitia mapaa ya majengo kwa kujenga matanki ya mfano kwenye maeneo ya shule, zahanati na masoko katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji katika maeneo ya maziwa makuu; katika kutatua changamoto ya uhaba wa huduma ya maji kwenye baadhi ya maeneo ya pembezoni mwa maziwa makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali ili kuhakikisha huduma hiyo inapatikana katika maeneo hayo. Hadi mwezi Machi, 2018 Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji kwenye maeneo hayo amepatikana. Kazi hiyo itafanyika katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo jumla ya shilingi milioni



500 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo. Maelezo ya kina kuhusu huduma ya maji vijijini yameainishwa kuanzia ukurasa wa 33 hadi ukurasa wa 44 wa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji mijini; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutekeleza Programu Ndogo ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mijini. Miradi inayotekelezwa inahusu ujenzi, ukarabati na upanuzi wa mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji. Miradi hiyo hutekelezwa kwa kutoa maji kutoka vyanzo vya maziwa, mito, chemchem, visima na mabwawa. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kutoa maji Ziwa Victoria, miji ya Isaka na Kagongwa; Serikali inatekeleza mradi wa maji kutoka bomba kuu la *KASHWASA* kwenda katika miji ya Isaka na Kagongwa. Mradi huo umegawanyika katika vipande viwili ambapo kipande cha kwanza kinahusu ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilometa 52.84 kutoka eneo la Kinaga hadi Kagongwa na kinagharimu shilingi bilioni 11.91.

Kipande cha pili kinahusu ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilometa 47 katika miji ya Isaka na Kagongwa na kinagharimu shilingi bilioni 12.81. Hadi mwezi Machi 2018 utekelezaji wa kipande cha kwanza umefikia asilimia 44 na kipande cha pili asilimia 20. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao 115,000 wa miji hiyo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 6.5 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mradi wa maji kutoka bomba kuu la *KASHWASA* kupeleka katika miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui pamoja na vijiji 110 vilivyopo kilometa 12 kutoka bomba kuu. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya dola za Marekani milioni

268.35. Hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 15 na utakapokamilika utahudumia wananchi wapatao milioni 1.1. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Mwanza na Miji ya Lamadi, Magu na Misungwi; Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa inaendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi kwa gharama ya *euro* milioni 104.5. Hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji wa mradi wa maji umefikia asilimia 15 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2018/2019. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao 105,649 wanaoishi maeneo ya Nyasaka, Bugarika, Nyegezi, Capripoint, Mjimwema, Nyakabungo na Kitangiri. Aidha, mradi wa uboreshaji wa huduma ya usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza umefikia asilimia 80 na utakamilika mwezi Mei 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika miji ya Magu, Misungwi na Lamadi utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi 92,195 wa miji ya Misungwi, Magu na Lamadi pamoja vijiji vya Ilungu na Kipeja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Musoma kwa gharama ya shilingi bilioni 45. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 10.14 za sasa hadi lita milioni 34 kwa siku. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 98 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018 ambapo wakazi wapatao 145,288 wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kwenda Manispaa ya Kigoma unatekelezwa na Serikali kwa ushirikiano na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa

Ulaya kwa gharama ya *Euro* milioni 16.32. Hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 83 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2018 na utakapokamilika utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 1.3 za sasa kwa siku na kufikia lita milioni 42 na kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kutoka asilimia 65 za sasa hadi asilimia 95 na kuwanufaisha wakazi wapatao 348,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji katika miji mbalimbali inayotumia vyanzo vya visima virefu. Jiji la Arusha, ili kuondoa kero ya uhaba wa majisafi na uondoaji majitaka katika Jiji la Arusha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka unaogharimu dola za Marekani milioni 233.9. Hadi mwezi Machi, 2018, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia tatu na unatarajiwa kukamilika Mwaka wa fedha 2020 na kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 kwa siku za sasa hadi kufikia lita milioni 200 kwa siku. Aidha, huduma ya uondoaji wa majitaka itaongezeka kutoka asilimia 7.6 za sasa hadi kufikia asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza mradi wa maji katika Manispaa ya Lindi kwa gharama ya *Euro* milioni 11.7. Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 90. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 1.5 kwa siku za sasa hadi lita milioni tisa na kuwanufaisha wakazi wapatao 81,343 wa mji huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji katika miji ya mikoa mipya; kwanza ni Mji wa Geita; Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika inaendelea kutekeleza Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (katika Mji wa Geita kwa gharama ya shilingi bilioni 6.67. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 3.8 kwa siku hadi lita milioni 5.7 na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 35 za sasa hadi asilimia 70 kwa wakazi wapatao 135,359 wa Mji wa Geita. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuboresha hali ya huduma ya maji katika mji huo wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji ya mserereko kutoka chemchemi ya Kanoge hadi tanki la Manga kwa gharama ya shilingi milioni 607.12 katika Mji wa Mpanda. Mradi huo umeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 3.2 hadi lita milioni 8.6 kwa siku pamoja na kuwanufaisha wakazi wapatao 10,000 wa maeneo ya Makanyagio, Madukani na Majengo B. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.5 ili kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka chemchem ya Kibena kwenda Mji wa Njombe kwa gharama ya shilingi bilioni 1.1 katika Mji wa Njombe. Hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95 na mradi utakapokamilika utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Hospitali ya Kibena, Chuo cha Uuguzi na maeneo ya Nyamyuya, Ofisi za Mkoa na Mgendela. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa kutekeleza mradi wa maji katika Mji wa Bariadi. Mradi utahusisha ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilometa 3.4 katika maeneo ya Malinoni, Kigangoni na Kisesa, ufungaji wa pampu tano za kusukuma maji pamoja na kupeleka umeme eneo la visima. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Kimbiji na Mpera unahusisha uchimbaji wa visima virefu 20 kwa gharama ya shilingi bilioni 18 ambavyo vinatarajiwa kuzalisha maji lita milioni 260 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2018 visima 19 vimechimbwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kusambaza maji kutoka kwenye visima hivyo kupeleka katika maeneo ya Gongo la Mboto, Chanika, Luzando, Pugu, Mpera, Chamanzi, Kitunda, Ukonga, Kinyerezi, Uwanja wa Ndege Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Tandika, Keko na Chang'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha miundombinu ya uondoaji majitaka. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini, Shirika la Maendeleo la Ufaransa na Benki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muda wako unaisha. Jitahidi umalize, kama unaona haiwezekani, yaingize kwenye *Hansard* nenda kwenye ukurasa wa 102 uombe pesa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowaeleza awali, hotuba yangu yote naomba iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru nchi wahisani, mashirika ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha ambazo zimechangia katika utekelezaji wa miradi ya sekta za maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wahisani ni pamoja na Korea Kusini, China, Uingereza, Marekani, Ujerumani, Japan, Uholanzi, Hispania, Ubelgiji, Ufaransa, India na Misri. Taasisi za

fedha za kimataifa na mashirika ya kimaendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Africa, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani, Benki ya Maendeleo ya Ufaransa, Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza, Shirika la Maendeleo la Ujerumani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, Shirika la Maendeleo ya Ubelgiji, Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa, Shirika la Misaada la Marekani na *Green Climate Fund*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuyashukuru mashirika na taasisi za kidini za *CARITAS, Adventist Development Relief Agency, Norwegian Church Aid, Livingwater International, World Islamic League*, Shirika la *Ahmadiyya Muslim Jamaat, Tanzania Islamic Foundation*, BAKWATA, KKKT, Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nazishukuru taasisi zisizo za kiserikali za *TAWASANET, ATAWAS*, Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya, *WaterAid, World Vision, WWF, Water Resources Integration Development Initiatives, Plan International, Concern Worldwide, Water Mission (T)* na Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji; Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Katibu Mkuu; Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelo - Naibu Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 727,345,768,677kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2018/2019 ili

Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 49 katika mwaka 2018/2019 jumla ya shilingi 697,577,902,677 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya sekta ya maji. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi 24,363,869,000 ambapo shilingi 6,266,714,000 sawa na asilimia 26 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo na shilingi 18,097,155,000 sawa na asilimia 74 ni kwa ajili ya kulipa mishahara.

Aidha, shilingi 673,214,033,677 ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya fedha hiyo, shilingi 443,214,034,677 sawa na asilimia 66 ni fedha za ndani na shilingi 229,999,999,000 sawa na asilimia 34 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 05; katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi 29,767,866,000 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya sekta ya umwagiliaji. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi 3,947,408,000 ambapo shilingi 585,184,000 sawa na asilimia 14.82 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo na shilingi 3,362,224,000 sawa na asilimia 85.18 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 25,820,458,000 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 6,000,000,000 sawa na asilimia 23.20 ni fedha za ndani na shilingi 19,820,458,000 sawa na asilimia 76.80 ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI MHE. ENG. ISACK ALOYCE KAMWELWE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KWA MWAKA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, **Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini**, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2018/2019.

2. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji** kwa maoni, ushauri na ushirikiano waliutoa wakati wa uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2018/2019. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli**, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Wizara inayomgusa kila mwananchi. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa nitafanya kazi kwa bidii, maarifa na uadilifu mkubwa ili kufikia malengo tuliyojiwekea ya kutoa huduma ya maji kwa matumizi mbalimbali, pamoja na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri ili kuziongoza Wizara mbalimbali.



4. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wabunge hao ni **Mhe. Dkt. Godwin Aloyce Mollel (Mb)**, kupitia Jimbo la Siha, **Mhe. Maulid Said Mtulia (Mb)**, kupitia Jimbo la Kinondoni; **Mhe. Dkt. Stephen Kiluswa (Mb)**, kupitia Jimbo la Longido; **Mhe. Dkt. Justin Joseph Monko (Mb)**, kupitia Jimbo la Singida Kaskazini na **Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb)**, kupitia Jimbo la Songea Mjini. Naahidi kushirikiana nao katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu kupitia Sekta za Maji na Umwagiliaji.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Nawapongeza pia Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

6. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa, taarifa ya kifo cha **Mhe. Leonidas Tutubert Gama**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini. Napenda kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa msiba huo mkubwa. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. **Amina.**

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ambayo inatoa taarifa ya hali ya sekta za maji na umwagiliaji nchini; mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na malengo ya sekta hizo kwa mwaka 2018/2019; changamoto na hatua zilizochukuliwa; pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka 2018/2019. Maelezo yatakayotolewa katika hotuba hii yamezingatia Sera na Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa; pamoja na Sheria, Kanuni na Miongozo inayohusiana na Sekta za Maji na Umwagiliaji.

## **2.0 HALI YA SEKTA ZA MAJI NA UMWAGILIAJI NCHINI**

**8. Mheshimiwa Spika**, maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya binadamu na maendeleo ya jamii na sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwemo viwanda, kilimo, uvuvi na utalii. Katika kufikia azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi majisafi na salama pamoja na kuiwezesha nchi yetu kuwa ya uchumi wa kati kufikia mwaka 2025, Wizara inatekeleza mipango ya Serikali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030); Awamu ya Pili ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020; na ahadi mbalimbali za Serikali.

Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kupitia Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2010. Hali halisi katika sekta hizo ni kama ifuatavyo:-

### **2.1 SEKTA YA MAJI**

**9. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo utekelezaji wake unahusisha Programu ndogo tano, ambazo ni Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji, Huduma ya Maji Vijijini, Huduma ya Maji Mijini, Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira na Kujenga Uwezo wa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Programu hiyo. Hali ya sekta ya maji ni kama ifuatavyo:-

#### **2.1.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**10. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ipo kusini mwa mstari wa Ikweta katika Latitudo 1° na 12° na Longitudo 29° na 41° Mashariki na inapata mvua katika vipindi viwili vya masika na vuli. Baadhi ya maeneo yanapata mvua mara moja (Desemba – Aprili) na mengine yanapata mvua mara mbili (Oktoba – Desemba na Machi - Mei) kwa mwaka. Kiwango cha wastani wa mvua katika maeneo mengi nchini kwa mwaka ni **milimita 900** hadi milimita 1200, wastani wa mvua

katika maeneo ya katikati ya nchi ni kati ya wastani wa **milimita 300** hadi **milimita 550**; na maeneo ya Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya milima ya Usambara ni wastani wa **milimita 2,200** hadi **milimita 2,500** kwa mwaka kulingana na hali ya hewa ya maeneo husika.

Kutokana na kiasi cha mvua kinachopatikana nchini, rasilimali za maji juu ya ardhi zinazofaa kwa matumizi mbalimbali ni wastani wa **kilomita za ujazo 92.27** na hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi inakadiriwa kuwa **kilomita za ujazo 30**. Hata hivyo, mtawanyiko na upatikanaji wa rasilimali hizo nchini haulingani katika maeneo yote kutokana na tofauti ya hali ya hewa, jiografia na jiolojia. Kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu ni wastani wa **mita za ujazo 1,800** kwa mwaka na kuiweka nchi yetu katika nafasi ya kwanza Afrika Mashariki kwa kiwango cha maji kilichopo kwa mtu kwa mwaka na ya nne Barani Afrika ikitanguliwa na Zambia, Msumbiji na Sudan Kusini. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni wastani wa **mita za ujazo 1,700**. Chini ya kiwango hicho, nchi huungia katika hali inayoitwa uhaba wa maji (water stress).

**11. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa na rasilimali za maji za kutosha kwa sasa, rasilimali hizo zimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka 1962 kiwango cha maji kwa mtu kilikuwa wastani wa **mita za ujazo 7,862** kwa mwaka (wakati Tanzania ikikadiriwa kuwa na watu milioni 10.6), kiwango hicho kimeshuka hadi kufikia wastani wa **mita za ujazo 1,800** mwaka 2018 ambapo idadi ya watu inakadiriwa kufikia **milioni 54**. Hali hiyo inasababishwa na ongezeko la idadi ya watu, uharibifu wa mazingira ambao husababisha vyanzo vya maji kukauka, mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa vyanzo unaoharibu ubora wa maji. Iwapo hali hiyo haitadhibitiwa, kiwango hicho kitaendelea kushuka na kuhatarisha ukuaji wa sekta za kiuchumi na kijamii.

### **2.1.2 Ubora wa Maji**

**12. Mheshimiwa Spika**, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inaelekeza kufanyika kwa tathmini za mara kwa mara

za kuhakiki ubora wa maji ili kubaini hali halisi na kuchukua hatua stahiki pale ambapo ubora wa maji utabainika kupungua. Zoezi la kuhakiki ubora wa maji linatekezwa na Wizara yangu kupitia maabara **16** za ubora wa maji zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini. Maabara hizo huhakiki ubora wa maji kwa kufanya uchunguzi wa kibaiolojia, kifizikia pamoja na kikemia katika maji. Matokeo ya uchunguzi hulinganishwa na viwango vya ubora wa maji (Water Quality Standards) kwa matumizi mbalimbali ili kubaini kama maji yanakidhi viwango vya ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**13. Mheshimiwa Spika**, uchunguzi wa ubora wa maji katika nchi yetu unaonesha hali ya ubora wa maji kutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Kutofautiana huko kunatokana na hali ya miamba ya asili, shughuli za binadamu, jioografia ya eneo na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kutumia takwimu za ubora wa maji zilizopo, Wizara imeweza kuainisha viashiria vya ubora wa maji ambavyo ni changamoto katika baadhi ya maeneo nchini.

Changamoto kubwa kwa maji juu ya ardhi (surface water) ni uwepo wa kiwango kikubwa cha Nitrogen, Phosphorous, tope (turbidity) pamoja na vimelea vya vijidudu vinavyosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji. Kwa upande wa maji chini ya ardhi (groundwater) changamoto ni uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi, tindikali (acidity), Nitrate, madini ya Flouride, Chuma, Manganese na Chloride. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa miradi ya maji inayotekelezwa nchini inawekewa miundombinu ya kutibu na kusafisha maji ili kulinda afya za wananchi. **Kiambatisho Na. 1** kinaonesha viashiria vya ubora wa maji katika maeneo mbalimbali nchini.

### 2.1.3 Huduma ya Maji Vijijini

**14. Mheshimiwa Spika**, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inaelekeza kuwapatia wananchi waishio vijijini maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana

na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji. Lengo ni kufikia asilimia 85 ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2020. Hadi sasa, miundombinu ya maji iliyojengwa ina jumla ya vituo vya kuchotea maji **123,888** ambavyo vina uwezo wa kuhudumia watu **30,972,000** sawa na **asilimia 85.2** ya wananchi **36,344,509** waishio vijijini.

Hata hivyo, kati ya hivyo, vituo **85,286** tu ndivyo vinavyofanya kazi na kutoa huduma kwa watu **21,321,500** sawa na **asilimia 58.7** ya wananchi waishio vijijini. Hali hiyo imechangiwa na changamoto ya mfumo uliopo wa usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji. Katika kuwapunguzia wananchi gharama za uendeshaji na matengenezo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza kubadilisha mitambo inayotumia nishati ya dizeli kusukuma maji na kufunga mitambo inayotumia nishati ya jua. Vilevile, Serikali inaandaa mifumo itakayofaa kusimamia na kuendesha miradi ya maji ikiwa ni pamoja na kuviimarisha Vyombo vya Watumiaji Maji.

#### **2.1.4 Huduma ya Maji Mijini**

**15. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wakazi waishio mijini wanapata huduma bora ya majisafi na usafi wa mazingira, Sera ya Maji inaelekeza kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na majitaka ili iweze kutoa huduma endelevu kwa wakazi waishio mijini na pembezoni mwa miji. Ili kufikia malengo hayo, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo pamoja na miji na vijiji vinavyohudumiwa na Miradi ya Maji ya Kitaifa. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ni kama ifuatavyo:-

##### **(a) Uzalishaji na mahitaji ya maji mijini**

**16. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji katika kipindi cha mwezi Machi 2017 hadi mwezi

Machi 2018, kumeongeza uzalishaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa kutoka **lita milioni 400** kwa siku hadi **lita milioni 404** ikilinganishwa na mahitaji ya **lita milioni 646**; Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo kutoka **lita milioni 99.7** hadi **lita milioni 100.6** ikilinganishwa na mahitaji ya **lita milioni 277.8**; na miradi ya maji ya Kitaifa, uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka **lita milioni 59.5** kwa siku hadi **lita milioni 67.2** ikilinganishwa na mahitaji ya **lita milioni 125.6**. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka **lita milioni 300** kwa siku hadi **lita milioni 504** ikilinganishwa na mahitaji ya **lita milioni 544**.

**(b) Upatikanaji wa huduma ya maji**

17. **Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa ni wastani wa **asilimia 78**. Kiwango hicho kimeshuka ikilinganishwa na **asilimia 86** ya mwaka 2016/2017 kutokana na kuongezeka kwa eneo la utoaji wa huduma baada ya upanuzi wa mipaka ya baadhi ya miji, kuanzishwa kwa miji mipya pamoja na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji. Katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ni wastani wa **asilimia 60**. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ni **asilimia 75**. Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) inaelekeza kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini kufikia **asilimia 95** katika miji mikuu ya mikoa na Dar es Salaam; na **asilimia 90** katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Azma ya Serikali ni kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya miji nchini.

**(c) Wateja waliunganishwa kwenye huduma ya maji**

18. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wakazi wengi zaidi wa maeneo ya mijini wanaunganishwa kwenye mtandao wa majisafi, Serikali imeweka malengo yanayotekelezwa kila mwaka ya kuunganisha wateja wapya **40,000** katika Miji Mikuu ya Mikoa, **22,000** Miji Mikuu ya Wilaya,

Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa na wateja 100,000 katika Jiji la Dar es Salaam. Hadi mwezi Machi 2018, wateja wapya **35,369** katika Miji Mikuu ya Mikoa, wateja **13,405** katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa na wateja **105,512** katika Jiji la Dar es Salaam wameunganishwa kwenye mtandao wa majisafi. Serikali itaendelea kuhakikisha wakazi wengi zaidi wanaunganishwa ili kuweza kufikia malengo tuliyojiwekea.

**(d) Upotevu wa maji**

**19. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo, Miradi ya Kitaifa pamoja na Jiji la Dar es Salaam zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya upotevu mkubwa wa maji ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika Kimataifa cha **asilimia 20**. Hadi mwezi Machi 2018, wastani wa upotevu wa maji katika Miji Mikuu ya Mikoa ni **asilimia 32**; Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa ni **asilimia 39**; na kwa Jiji la Dar es Salaam ni **asilimia 49**. Serikali inaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya majisafi pamoja na kuweka mikakati ya kupunguza upotevu wa maji hadi kufikia kiwango kinachokubalika.

**(e) Uondoaji wa majitaka**

**20. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa huduma ya uondoaji majitaka mijini, miundombinu imejengwa katika miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Songea, Tabora na Tanga. Kwa miji mingine huduma ya uondoaji wa majitaka inatolewa kwa kutumia magari ya majitaka na kutiririshwa kwenye mabwawa au maeneo yaliyotengwa na Halmashauri husika. Serikali inaendelea kuboresha huduma ya uondoaji majitaka kwa kujenga, kukarabati na kupanua mifumo ya uondoaji majitaka na ununuzi wa magari ya uondoaji majitaka. Lengo ni kuboresha upatikanaji wa huduma hiyo mijini hadi kufikia **asilimia 30** ifikapo mwaka 2020.

### 2.1.5 Kujenga uwezo wa Taasisi

21. **Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo ya Serikali ya kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama pamoja na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, Wizara imeendelea kujenga uwezo wa Taasisi zinazotekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Sekta ya Kilimo kwa upande wa Umwagiliaji. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imeajiri watumishi **106** wa sekta ya maji ambao wamepangiwa kazi katika vituo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Ofisi za Maji za Mabonde na Makao Makuu ya Wizara. Kwa upande wa Sekta ya Umwagiliaji, watumishi **34** wameajiriwa na kupangiwa kazi kwenye Ofisi za Kanda za Umwagiliaji na Makao Makuu. Vilevile, ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi za Wizara na maabara **10** za maji umefanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi na kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

## 2.2 SEKTA YA UMWAGILIAJI

22. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina eneo la **hekta milioni 29.4** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ambapo **hekta milioni 2.3** zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, **hekta milioni 4.8** zina uwezekano wa kati na hekta milioni 22.3 zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa. Lengo la Serikali ni kujenga miundombinu yenye jumla ya **hekta 1,000,000** katika skimu za wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ifikapo mwaka 2020/2021. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya hekta 475,052 zinamwagiliwa sawa na **asilimia 47.44** ya lengo na **asilimia 1.6** ya eneo lote linalofaa kwa umwagiliaji. Aidha, maeneo yenye skimu zilizoendelezwa yameongeza uzalishaji na tija kutoka wastani wa **tani 1.8 – 2.0** kwa hekta hadi kufikia wastani wa **tani 4.0 – 5.0** kwa hekta kwa zao la mpunga na hivyo kuchangia **asilimia 24** ya mahitaji yote ya chakula nchini. Ili kuhakikisha lengo linafikiwa Serikali inaendelea kukarabati miundombinu ya skimu zilizoharibika, kukamilisha ujenzi wa skimu pamoja na kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na kujenga skimu na mabwawa mapya.



**3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 NA MPANGO WA MWAKA 2018/2019**

**3.1 FEDHA ZILIZOIDHINISHWA NA ZILIZOPOKELEWA KATIKA MWAKA 2017/2018**

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 648,064,207,757** na kati ya fedha hizo **Shilingi 24,457,459,705** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 623,606,748,052** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya **Shilingi 347,500,300,527** sawa na **asilimia 56** ya fedha za maendeleo zimepokelewa; na **Shilingi 12,827,935,743** sawa na **asilimia 52.45** ya fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa.

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 24,158,893,232**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,055,481,082** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 20,103,412,150** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya **Shilingi 2,468,524,645** sawa na **asilimia 12.13** ya fedha za maendeleo zimepokelewa; na **Shilingi 2,928,687,064** sawa na **asilimia 72.23** ya fedha za matumizi ya kawaida zimepokelewa.

**3.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI NA PROGRAMU MBALIMBALI KATIKA MWAKA 2017/2018 NA MALENGO YA MWAKA 2018/2019**

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, sekta za maji na umwagiliaji zilitekeleza miradi inayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini; usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; ufuatiliaji wa ubora wa maji; uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji; na kutekeleza masuala mtambuka. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018 na mpango wa mwaka 2018/2019 umeelezwa kwa kina kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

26. **Mheshimwa Spika**, majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji kwa kuchunguza na kutathmini rasilimali za maji, kuhakikisha rasilimali za maji zinatunzwa na kuendelezwa, pamoja na kusimamia rasilimali za majishirikishi. Utekelezaji wa majukumu hayo umeelezwa kwa kina kama ifuatavyo:-

#### 3.2.1.1 Mwenendo wa Rasilimali za Maji

27. **Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa takwimu na taarifa za mwenendo wa rasilimali za maji ni muhimu katika kutambua hali ya maji kwa nyakati tofauti kwenye maeneo mbalimbali nchini. Takwimu na taarifa hizo hutumika katika usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji, umwagiliaji, mabwawa na usanifu wa madaraja. Hadi mwezi Machi 2018, takwimu za maji zimekusanywa kwenye vituo **475** vya kupima mwenendo wa rasilimali za maji nchini na kuchakatwa. Vituo hivyo vinajumuisha vituo **220** vya kupima mtiririko wa maji mitoni, vituo **13** vya kupima kina cha maji katika mabwawa ya Mindu, Mtera, Kihansi, Kidatu na Nyumba ya Mungu, vituo **sita (6)** vya kupima kina cha maji katika maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa, vituo **152** vya kupima mvua, vituo **65** vya kupima hali ya hewa na vituo **19** vya kupima mwenendo wa maji chini ya ardhi.

28. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na takwimu zilizokusanywa, mwenendo wa rasilimali za maji umeonesha kupungua kwa mvua zilizonyesha katika mwaka wa kihaidrolojia unaoanzia mwezi Novemba 2016 hadi mwezi Oktoba 2017 ikilinganishwa na wastani wa mvua katika mwaka uliopita wa kihaidrolojia na kusababisha kupungua kwa viwango vya maji katika baadhi ya mito, maziwa na mabwawa. **Kiambatisho Na. 2** kinaonesha kiwango cha maji katika mito, maziwa na mabwawa mbalimbali nchini.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mwenendo wa rasilimali za maji nchini, jumla ya vituo **sita (6)** vya kupima mtiririko wa maji kwenye mito

(*hydrometric stations*) na vituo **sita (6)** vya hali ya hewa (*mini weather stations*) vimejengwa katika mabonde ya Ziwa Nyasa na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini. Aidha, ukarabati ulifanyika katika vituo **30** vya kupima mwenendo wa rasilimali za maji nchini. Katika mwaka 2018/2019, Wizara yangu itaendelea na ujenzi wa vituo **35** kwenye mito na ukarabati wa vituo **45** vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji pamoja na kukusanya takwimu kwenye mabonde yote nchini.

### 3.2.1.2 Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji

**30. Mheshimiwa Spika**, ongezeko la shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo vya maji limekuwa ni changamoto inayosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira. Jumla ya vyanzo 298 vya maji vilibainishwa kuwa katika hatari ya kuharibika na kuathirika. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara inaendelea kutekeleza Mpango wa miaka mitano wa Utunzaji wa Rasilimali za Maji wa mwaka 2014 – 2020 kwa lengo la kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji pamoja na kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia rasilimali za maji nchini. Katika mwaka 2017/2018, vyanzo **sita (6)** vya maji vimewekewa mipaka na kuongeza idadi ya vyanzo vya maji vilivyowekewa mipaka kufikia **84**. Vilevile, jumla ya vyanzo 18 vimetangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji na taratibu za kutangaza maeneo zaidi zinaendelea. **Kiambatisho Na. 3** kinaonesha vyanzo vya maji vilivyotangazwa kuwa maeneo tengefu. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imepanga kutangaza vyanzo **45** kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji. Vilevile, jumla ya Jumuiya za Watumia Maji (*Water User Associations*) **20** zimepewa mafunzo pamoja na vitendea kazi ili ziweze kusimamia rasilimali za maji kwa ufanisi zaidi. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imepanga kuunda Jumuiya **33** za Watumia Maji na kuziimarisha zilizopo.

### 3.2.1.3 Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

**31. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, Wizara hufanya ukaguzi wa ubora wa

majitaka yanayotiririshwa kwenye vyanzo vya maji. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya viwanda **22**, migodi **saba (7)** na taasisi **nne (4)** zilifanyiwa ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi yalibaini kuwepo kwa uchafuzi mkubwa wa vyanzo vya maji unaotokana na utiririshwaji wa majitaka ambapo wahusika walichukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kupewa onyo, kutakiwa kusitisha utiririshaji wa majitaka, kuagizwa kuboresha miundombinu ya majitaka katika shughuli zao na kufuata maelekezo yaliyopo kwenye mipango yao ya usimamizi wa mazingira (*Environmental Management Plans*). Vilevile, ukaguzi wa miundombinu ya majitaka hufanyika mara kwa mara ili kuhakikisha viwanda, migodi na taasisi zinazotiririsha majitaka kwenye vyanzo vya maji zinafuata taratibu na kupata vibali. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya vibali **13** vilitolewa kati ya **30** vilivyopangwa kwa ajili ya kutiririsha majitaka yanayokidhi viwango kwenye vyanzo vya maji katika Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Victoria (5), Wami/Ruvu (**4**), Mto Rufiji (**3**) na Mto Pangani kibali **kimoja (1)**. Viwanda, migodi na taasisi hizo ziliagizwa kuzingatia masharti ya vibali vya kutiririsha majitaka kwenye vyanzo vya maji. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya vibali **30** vya kutiririsha majitaka vimepangwa kutolewa.

#### 3.2.1.4 Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji

**32. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutafuta vyanzo vipya vya maji pamoja na kufanya tathmini na usanifu katika vyanzo vilivyobainishwa ili viweze kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya maeneo **179** yanayofaa kuchimbwa visima yalitambuliwa katika Bonde la Mto Pangani maeneo **37**, Ruvuma na Pwani ya Kusini (**90**), Ziwa Victoria (**16**), Rufiji (**10**), Bonde la Kati (**11**), Wami-Ruvu (**11**) na Ziwa Rukwa maeneo **manne (4)**. Aidha, Serikali inaendelea kutambua vyanzo vya maji vinavyofaa kufanyiwa usanifu na kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo mengi zaidi ili kuongeza upatikanaji wa maji nchini.

#### 3.2.1.5 Ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati33.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha uwepo wa maji ya

kutosha kwa matumizi mbalimbali kwa kipindi chote cha mwaka, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro) na Ndembera (Iringa). Bwawa la Farkwa litatumika kwa ajili ya usambazaji wa maji katika Mji wa Dodoma na Wilaya za Chemba na Kondoza pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Bwawa la Kidunda litatumika kwa ajili kuhakikisha Mto Ruvu unakuwa na maji katika kipindi chote cha mwaka, kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa umeme.

Bwawa la Ndembera litatumika kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruaha unakuwa na maji katika kipindi chote cha mwaka, kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme. Hadi sasa usanifu wa mabwawa hayo umekamilika ikiwa ni pamoja na tathmini za kimazingira na kijamii pamoja na uthamini wa mali kwa ajili ya kulipa fidia wananchi watakaopisha ujenzi wa mabwawa hayo. Hadi mwezi Machi 2018, ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa bwawa la Kidunda umekamilika na unaendelea kwa mabwawa ya Farkwa na Ndembera. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo.

### 3.2.1.6 Udhhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima

**34. Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kudhibiti uchimbaji holela wa visima vya maji kwa kuzipatia leseni kampuni zinazohusika na shughuli za utafiti na uchimbaji wa visima. Hatua hiyo husaidia kuzitambua na kufuatilia utendaji kazi wa kampuni hizo. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya kampuni **43** ziliomba kupatiwa leseni ambapo leseni **34** zilitolewa kwa kampuni za uchimbaji visima vya maji na leseni saba (7) kwa kampuni za utafiti wa maji chini ya ardhi.

Kampuni **mbili (2)** hazikupewa leseni kwa kuwa hazikukidhi vigezo vinavyokubalika. Vilevile, leseni **30** zilitolewa kwa wataalam wa uchimbaji wa visima. Aidha, visima vya maji **608** vilichimbwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hivyo, visima **184** vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima

na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) na visima **424** vilichimbwa na kampuni binafsi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutoa leseni za uchimbaji visima kwa kampuni na wataalam wanaokidhi vigezo pamoja na kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na.11** ya mwaka 2009 na Kanuni zake kwa lengo la kudhibiti uchimbaji holela wa visima vya maji nchini.

### **3.2.1.7 Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji na Udhibiti wa Migogoro**

**35. Mheshimiwa Spika**, Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu umuhimu wa kuwa na vibali vya kutumia maji na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya vibali vipya **688** vilitolewa katika Bonde la Mto Pangani (**31**), Mto Rufiji (**309**), Wami/Ruvu (**216**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**18**), Bonde la Kati (**71**) na Ziwa Victoria vibali **43**. Vilevile, jumla ya maombi mapya **178** ya kutumia maji yaliwasilishwa na taratibu za kutoa vibali hivyo zinaendelea. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imepanga kutoa vibali **600** vya kutumia maji kwa lengo la kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji nchini. Aidha, kwa upande wa udhibiti wa migogoro ambayo hutokea miongoni mwa watumiaji wa rasilimali za maji, Bodi za Maji za Mabonde kwa kushirikiana na Jumuiya za Watumia Maji zimeendelea kutoa ushauri wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya migogoro **21** ya watumia maji ilijitokeza katika Bonde la Mto Pangani (**9**), Mto Rufiji (**1**), Wami/Ruvu (**6**), Ziwa Rukwa (**1**), Ziwa Nyasa (**3**), na Bonde la Kati mgogoro mmoja (**1**). Kati ya hiyo, migogoro 17 imesuluhishwa; na migogoro minne (**4**) katika Bonde la Mto Pangani (**3**) na Wami/Ruvu (**1**) ipo katika hatua mbalimbali za usuluhishi.

### **3.2.1.8 Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**36. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kukamilisha Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ili kuhakikisha rasilimali hizo zinasimamiwa kwa

pamoja na wadau wote wanaohusika na matumizi ya maji. Wizara imekamilisha uandaaji wa mipango hiyo kwa mabonde **sita (6)** ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Mto Rufiji na Bonde la Kati. Hadi mwezi Machi 2018, tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii (*Strategic Environment and Social Assessment*) imekamilika kwa Bonde la Rufiji. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii kwa mabonde yaliyobaki. Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji kwa mabonde ya Pangani, Ziwa Victoria na Bonde la Wami/Ruvu imeanza kuandaliwa na inatarajiwa kukamilika mwaka 2018/2019.

### 3.2.1.9 Kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde

**37. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuziimarisha Bodi za Maji za Mabonde **tisa (9)** nchini kwa kujenga ofisi, kuzipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi. Bodi hizo zina jukumu la kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Hadi mwezi Machi 2018, ujenzi wa ofisi za Bodi za Maji za Bonde la Ziwa Tanganyika umekamilika, Ziwa Rukwa umefikia **asilimia 85**, Bonde la Kati asilimia 90, Ruvuma na Pwani ya Kusini asilimia 85 na Bonde la Ziwa Nyasa **asilimia 40**. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

### 3.2.1.10 Mradi wa Kunusuru Vyanzo vya Maji kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Mabonde Madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu

**38. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) pamoja na Mfuko wa Mazingira Duniani (*Global Environment Facility - GEF*) inatekeleza Mradi wa Kunusuru Vyanzo vya Maji kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi katika mabonde madogo ya Mto Zigi (Bonde la Pangani) na Mto Ruvu (Bonde la Wami-Ruvu). Gharama za mradi ni **Dola za**

**Marekani milioni 27.65.** Mradi huo una maeneo mawili ya utekelezaji, ambayo ni kujenga uwezo wa taasisi na kukuza uratibu wa masuala ya rasilimali za maji miongoni mwa mamlaka za mabonde hayo na wadau wengine pamoja na kutekeleza shughuli za usimamizi endelevu wa ardhi zinazolenga kupunguza uharibifu wa vyanzo vya maji na kuboresha maisha ya jamii. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 ambapo jumla ya vijiji 20 katika Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Mvomero, Muheza, Mkinga na Korogwe vitanufaika.

**39. Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Machi 2018, kazi zilizotekelezwa kupitia mradi huo ni uainishaji wa maeneo yatakayosaidia kutoa taarifa za msingi kuhusu wingi na ubora wa maji katika mabonde hayo; utunzaji wa misitu **hekta 151.38** kwenye hifadhi ya Mlima Uluguru na **hekta 115** kwenye hifadhi ya msitu wa Amani zilizokuwa zimeharibiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kilimo na uchimbaji wa madini. Uhifadhi wa misitu ulihusisha uimarishaji wa doria kwa kujenga kituo cha polisi katika msitu wa Amani, kuwaondoa wananchi waliovamia maeneo ya vyanzo; kupanda miti ili kurudisha uoto wa asili; na kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kuwapatia wananchi shughuli mbadala za kujipatia kipato ikiwemo kuwapatia mizinga ya nyuki. Vilevile, vijiji **vinne (4)** vipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mipango ya matumizi bora ya ardhi; na Jumuiya **nne (4)** za Watumia Maji ziliundwa katika maeneo ya mradi ambapo Jumuiya **tatu (3)** zipo katika bonde dogo la Mto Zigi na Jumuiya **moja (1)** katika bonde dogo la Mto Ruvu. Aidha, mradi huo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga umejenga miundombinu ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 3.4** katika vijiji vya Mashewa, Shembekeza na Kimbo kwa gharama ya Shilingi **milioni 103** na kunufaisha wananchi wapatao **3,700** wa vijiji hivyo.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji **12** vilivyopo katika maeneo ya mradi; kuunda na kuziimarisha Jumuiya za Watumia Maji kwa kuzijengea ofisi na kutoa mafunzo; kuainisha watumiaji



wa maji waliopo katika maeneo ya mabonde madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu; kununua vifaa vya kupima mwenendo wa maji; kuweka mipaka kwenye eneo la **kilomita 20** katika Mto Zigi na Mto Ruvu; kuunda Jumuiya **tatu (3)** za watumiaji maji katika bonde dogo la Mto Ruvu, kujenga vidakio vya maji katika vijiji vya Mnyanza na Tangeni, kukarabati mradi wa maji katika kijiji cha Newyork, kujenga vituo sita vya kunyweshea mifugo, kuanzisha vitalu vya miti; na kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kuwapatia wananchi shughuli mbadala za kujipatia kipato.

### **3.2.1.11 Mradi wa Kuimarisha Taasisi Zinazosimamia Rasilimali za Maji**

**41. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeanza kutekeleza mradi wa kuimarisha taasisi zinazosimamia rasilimali za maji kwa kuboresha ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za rasilimali za maji pamoja na kutekeleza miradi itakayohakikisha uwepo wa maji ya kutosha na uhifadhi wa rasilimali za maji katika mabonde yote nchini. Katika bonde la Wami-Ruvu mradi huo umelenga kukamilisha mpango shirikishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika bonde la Wami-Ruvu, ujenzi wa ofisi na maabara, uundaji wa jumuiya za watumia maji, uanzishaji wa kamati za mabonde madogo na kuhifadhi vyanzo vya maji. Mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 50**. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya **Shilingi bilioni 10.18** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

### **3.2.1.12 Ukusanyaji wa Maduhuli**

**42. Mheshimiwa Spika**, maduhuli yanayokusanywa na Bodi za Maji za Mabonde kupitia vibali na ada za matumizi ya maji, vibali vya utiririshaji wa majitaka na faini hutumika kwa ajili ya kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za maji katika mabonde husika. Lengo ni kuziimarisha Bodi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hadi mwezi Machi 2018, **Shilingi bilioni 4.65** zilikusanywa ambazo ni sawa

na **asilimia 112** ya lengo la **Shilingi bilioni 4.15** zilizopangwa kukusanywa katika mwaka 2017/2018. Katika mwaka 2018/2019, Bodi za Maji za Mabonde zimepanga kukusanya **Shilingi bilioni 4.44** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. **Kiambatisho Na. 4** kinaonesha makadirio na ukusanyaji wa maduhuli katika Bodi za Maji za Mabonde.

### 3.2.1.13 Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi

43. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina mabonde saba yanayovuka mipaka ya nchi na hivyo kulazimika kushirikiana na nchi nyingine **17** katika kutunza rasilimali za maji zilizopo kwenye mabonde hayo. Ushirikiano baina ya Tanzania na nchi nyingine unatekelezwa kupitia mikataba na makubaliano ambayo yameanzisha Kamisheni na Taasisi mbalimbali.

Nchi hizo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Eritrea. Wizara imeendelea kushirikiana na nchi hizo kupitia vyombo vya pamoja vilivyoundwa ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo kwa kutekeleza programu na miradi mbalimbali kama ifuatavyo:-

#### (a) Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda iliendelea kutekeleza awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Project – LVEMP II*) ambayo muda wake ulimalizika mwezi Desemba, 2017. Kazi zilizokamilika ni ukarabati na upanuzi wa maabara za maji za Mwanza, Musoma na Bukoba; ukarabati wa machinjio ya Mwanza; ujenzi wa mfumo wa majitaka katika machinjio ya Jiji la Mwanza ambao uko kwenye hatua za majaribio; utekelezaji wa miradi **295** ya kijamii inayonufaisha wakazi **505,550**; na uondoaji wa **hekta 9.39** za gugumaji katika Ziwa Victoria. Vilevile, huduma ya usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza imeboreshwa kwa kuongeza **kilomita 7.9** za

mtandao wa majitaka na kuunganisha wateja 290 kwenye mtandao huo. Aidha, Serikali inaandaa andiko kwa ajili ya awamu ya tatu ya mradi ambayo itahusisha kukamilisha miradi ya kijamii, upanuzi wa miundombinu ya majitaka pamoja na upanuzi wa miradi inayozingatia usafi wa mazingira katika eneo la Simiyu na maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria pamoja na miji ya Geita, Chato, Kayanga/ Omurushaka, Buseresere, Katoro na Bunazi.

**(b) Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe**

**45. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi imeendelea kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe. Katika mwaka 2017/2018, Azimio la kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe (*Convention for Establishment of Songwe River Basin Commission*) liliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 07/09/2017. Vilevile, Serikali za Malawi na Tanzania zimepata fedha za kutekeleza mradi wa utunzaji wa mazingira ya Mto Songwe kutoka *Global Environment Facility (GEF)* ambapo Mtaalam Mshauri yuko katika hatua za kukamilisha andiko la mradi. Mradi huo umekadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 6.4** na utatekelezwa chini ya Sekretarieti ya Mpito inayosimamia Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe. Aidha, taratibu zimefanyika za kumpata Mtaalam Mshauri (*Transaction Advisor*) kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa bwawa la Songwe Chini kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali za Malawi na Tanzania zitaanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Bonde la Mto Songwe ambayo pamoja na mambo mengine itatekeleza miradi ya utunzaji wa mazingira na ya kusambaza maji kwa vijiji vilivyopo katika Bonde hilo.

**(c) Bonde la Mto Zambezi**

**46. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Bonde la Mto Zambezi ambazo ni Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zambia na

Zimbabwe katika kutekeleza Mkataba wa Bonde hilo (Zambezi Water Course Commission - ZAMCOM). Lengo la Mkataba huo ni kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji ya Bonde la Mto Zambezi. Katika mwaka 2017/2018, kazi zilizotekelezwa ni kukamilisha nyaraka inayoelekeza utaratibu wa kupeana taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo inaweza kuwa na athari kwa nchi wanachama; kuandaa mfumo wa kuhifadhi na kubadilishana takwimu (data sharing) baina ya nchi wanachama; na maandalizi ya Mpango Mkakati wa ZAMCOM.

Vilevile, Tanzania ilishiriki katika mkutano wa tano wa Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Zambezi ambao ulifanyika mwezi Februari, 2018 nchini Namibia. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni, suala la michango ya nchi wanachama pamoja na kupitisha makadirio ya bajeti kwa mwaka 2018/2019. Aidha, mkutano huo uliazimia kuwa mkutano wa sita wa Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Mto Zambezi ufanyike nchini Tanzania.

**(d) Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Ruvuma**

**47. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mkataba wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Ruvuma kati ya nchi yetu na Msumbiji. Katika mwaka 2017/2018, Mkutano wa tatu wa Kamisheni hiyo ulifanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Novemba, 2017 kwa lengo la kujadili hali halisi ya utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa pili wa Kamisheni uliofanyika Maputo Msumbiji mwaka 2010 pamoja na kujadili na kutoa mapendekezo ya namna bora ya utekelezaji wa shughuli za Kamisheni. Mkutano huo uliazimia kutekeleza miradi iliyoainishwa katika Mkakati wa Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji (UPARAMA) na kujifunza kutoka kwenye Kamisheni za mabonde mengine ili kupata uzoefu.

**(e) Mkutano wa Mawaziri wa Maji na Nishati wa SADC**

**48. Mheshimiwa Spika**, mkutano wa mwaka wa Mawaziri wa Maji pamoja na Nishati wa nchi wanachama

wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), ulifanyika tarehe 09 – 13 Julai, 2017 katika Jiji la Ezulwini nchini Swaziland. Mkutano huo ulijadili utekelezaji wa Programu ya Maji ya SADC, taarifa ya Mkutano Mkuu wa Marais uliopita, pamoja na kupitia mpango kazi wa utafutaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya nne ya Programu hiyo. Aidha, mkutano huo ulifanyika sambamba na Jukwaa la Uwekezaji la nchi wanachama wa SADC ambapo wadau mbalimbali wa maendeleo walihudhuria wakiwemo GIZ na AfDB. Katika Jukwaa hilo miradi miwili kutoka nchini Tanzania iliwasilishwa kwa ajili ya kutafutiwa fedha za utekelezaji. Miradi hiyo ni Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe na Mradi wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Nakonde - Tunduma.

### 3.2.2 Huduma za Ubora na Usafi wa Maji

**49. Mheshimiwa Spika**, maji safi na salama ni muhimu katika kulinda afya za wananchi dhidi ya magonjwa yatokanayo na maji. Wizara yangu ina jukumu la kuhakiki na kufuatilia ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji, mitandao ya kusambaza maji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Vyombo vya Watumiaji Maji, Bodi za Maji za Mabonde, Taasisi mbalimbali pamoja na watu binafsi. Uhakiki wa ubora wa maji husaidia katika kutoa maamuzi kuhusu matumizi mbalimbali ya maji na utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

**50. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha maji yanayotumika kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii yanakidhi viwango vinavyohitajika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji maji. Katika mwaka 2017/2018 jumla ya sampuli **10,000** za majisafi na sampuli **1,500** za majitaka zilipangwa kuchunguzwa. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya sampuli **4,295** za majisafi zilikusanywa na kuchunguzwa, kati ya hizo sampuli **3,513** ni kwa ajili ya matumizi ya maji majumbani, viwandani **(356)**, kuratibu mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo

(309), shughuli za utafiti (41), umwagiliaji (66) na sampuli 10 za maji kwa ajili ya ujenzi. Kwa upande wa majitaka jumla ya sampuli 256 zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizo na hali ya ubora wa maji kwa matumizi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

### 3.2.2.1 Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani

51. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilihakiki hali ya ubora wa maji kwa matumizi ya majumbani kutoka katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji kwenye Halmashauri, Mamlaka za Maji, Taasisi mbalimbali pamoja na vyanzo vya maji vya watu binafsi. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli 2,814 sawa na asilimia 80 zilikidhi viwango vinavyokubalika na sampuli 699 sawa na asilimia 20 hazikukidhi. Sampuli ambazo hazikukidhi viwango zilitokana na uwepo wa viwango vikubwa vya madini ya chuma na manganese kwenye sampuli zilizochukuliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi na vijidudu kwenye sampuli kutoka Halmashauri za Pangani, Handeni na Mbeya. Kwa maeneo ambayo ubora wa maji haukukidhi viwango, ushauri wa kitaalam ulitolewa na kuzingatiwa hivyo kudhibiti athari ambazo zingeweza kutokea kutokana na matumizi ya maji yasiyo salama.

### 3.2.2.2 Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda, Ujenzi, Umwagiliaji na Utafiti

52. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakiki ubora wa maji yanayotumika kwa ajili ya shughuli za viwandani, ujenzi, umwagiliaji na utafiti, sampuli za maji 473 zilikusanywa na kuchunguzwa. Kati ya hizo, sampuli zilizochunguzwa kwa ajili ya matumizi ya viwandani ni 356, ujenzi (sampuli 10), umwagiliaji (sampuli 66) na sampuli 41 zilichunguzwa kwa ajili ya shughuli za utafiti. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli zote zilikidhi viwango vya ubora kwa matumizi husika. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kufuatilia ubora wa maji yanayotumika kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya shughuli za kiuchumi.

### 3.2.2.3 Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa kwenye Mazingira

**53. Mheshimiwa Spika**, vyanzo vya maji vinaweza kuathiriwa kutokana na majitaka yanayozalishwa viwandani na majumbani kutiririshwa katika vyanzo vya maji bila kuzingatia miongozo ya utiririshaji majitaka kwenye mazingira. Katika kutathmini ubora wa majitaka yanayotiririshwa, Maabara za Maji huchunguza ubora wa majitaka hayo na kutoa ushauri kwa Mamlaka husika.

Hadi mwezi Machi, 2018, jumla ya sampuli **256** za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uhakiki yalibaini kuwa sampuli **167** sawa na **asilimia 65** hazikukidhi viwango vya ubora unaokubalika. Matokeo hayo yanaashiria kuwepo kwa kiwango kikubwa cha uchafuzi wa mazingira. Kutokana na hali hiyo, Wizara imetoa ushauri wa kitaalam katika miji, viwanda na Taasisi mbalimbali kuhusu uboreshaji wa mabwawa na mifumo ya kusafisha majitaka. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa majitaka katika miji, viwanda na taasisi mbalimbali kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

### 3.2.2.4 Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji

**54. Mheshimiwa Spika**, viwango vya ubora wa madawa yanayotumika kusafisha na kutibu maji hutakiwa kuthibitishwa kabla ya matumizi husika kwa lengo la kulinda afya za wananchi na usalama wa maji kwa ujumla. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya sampuli **12** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Taasisi **3** zilichunguzwa. Sampuli hizo ni za dawa aina ya *Calcium Hypochlorite* sampuli **4** kwa ajili ya kutibu maji; na *Aluminium Sulphate*(Shabu) (**4**), *Polymerblend* (**3**) na Soda Ash sampuli **1** kwa ajili ya kusafisha maji. Matokeo ya uchunguzi yalionesha madawa hayo kukidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kusimamia Miongozo inayohusu ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji.

### 3.2.2.5 Utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji na Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa

55. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji (*Water Safety Plans*) kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma ya majisafi na salama kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na Vyombo vya Watumiaji Maji (*COWSOs*).

Utekelezaji wa Mipango hiyo umeanza kwa Mamlaka ya Maji Kigoma na *COWSO* ya Mbande - Kongwa kama maeneo ya majaribio (*pilot sites*). Katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa *COWSO* ya Mbande, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Afya Duniani limeidhinisha **Shilingi milioni 125** kwa ajili ya kutafuta vyanzo zaidi vya maji ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika eneo hilo.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa (*National Guideline for Monitoring Drinking Water Quality*). Lengo la Mwongozo huo ni kuhakikisha watoa huduma ya maji ya kunywa wanazingatia viwango vya ubora vinavyokubalika ili kulinda afya za wananchi. Hadi mwezi Machi 2018, mikoa ya Dar es salaam, Kigoma, Njombe, Mbeya na Dodoma imejengewa uwezo kuhusu utekelezaji wa Mwongozo huo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya Mwongozo na kuratibu utekelezaji wake kwa mikoa yote nchini.

### 3.2.2.6 Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika Maji ya Kunywa na Kupikia

57. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika maji ya kunywa na kupikia katika maeneo yaliyoathirika na madini hayo. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya mitambo midogo



**210** inayotumika katika ngazi ya Kaya (*household deflouridation unit*) imesambazwa katika mikoa ya Arusha na Mwanza kwenye maeneo yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa na uwepo wa madini ya *fluoride* katika maji. Matumizi ya teknolojia hiyo yamenufaisha wananchi **1,700** wa maeneo hayo kwa kuwapatia majisafi na salama. Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia teknolojia hiyo ya kutibu maji ili yafikie kiwango cha madini ya *fluoride* kinachokubalika. Vilevile, Madiwani **23** kutoka katika Halmashauri za Meru, Arusha na Ngorongoro wamepatywa mafunzo na wanashiriki kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi ya teknolojia ya uondoaji wa madini ya *fluoride* kwenye maji.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imepanga kutengeneza na kusambaza mitambo midogo **1,000** ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji katika ngazi ya Kaya. Aidha, ili kukidhi mahitaji ya bone char na activated carbon, Serikali itaboresha mfumo wa ukusanyaji malighafi ambayo ni mifupa ya ng'ombe na kuongeza uzalishaji wa born char.

### **3.2.2.7 Maabara za Maji kupata Ithibati (Accreditation)**

**59. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha maabara zote za ubora wa maji nchini zinapata ithibati ili ziweze kutambulika kitaifa na kimataifa. Lengo ni kuongeza idadi ya maabara zenye ithibati (*accreditation*) kutoka moja iliyopo hadi maabara tano ifikapo mwaka 2019.

Jitihada zinazofanyika ili kufikia lengo hilo ni pamoja na ujenzi wa majengo ya maabara yanayokidhi vigezo vya maabara za uchunguzi (*testing laboratories*), ununuzi wa vifaa vya kufanya uchunguzi, kutoa mafunzo na kushiriki katika mazoezi ya kujipima uwezo (*Proficiency Test*) kwa maabara zote **16** za Ubora wa Maji. Hadi mwezi Machi 2018, Mwongozo wa Usimamizi wa Ubora wa Maji kwa ajili ya Maabara za Dar es Salaam na Iringa unatumika na mafunzo kuhusu Mwongozo huo yanatolewa kwa watumishi wa maabara husika.

Aidha, taarifa ya tathmini ya utendaji kazi za kiuchunguzi kwa kila maabara inaonesha kuwa maabara zimeendelea kufanya vizuri katika upimaji wa viashiria mbalimbali vya kemikali na vijidudu kwenye maji. Taarifa hiyo inaonesha maabara za maji zinajengewa uwezo kwa kutoa takwimu sahihi zinazotumika katika kutoa maamuzi kuhusu uendelezaji wa miradi ya maji na utoaji wa huduma za maji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Maabara ya Ubora wa Maji Mwanza ambayo ina Ithibati, *Southern African Development Accreditation Service (SADCAS)* imeendelea kuifanyia ukaguzi (*Laboratory Technical Audit*) na tathmini ya matokeo imeonesha maabara ya Mwanza itaendelea kuwa na ithibati hadi mwaka 2019. Katika mwaka 2018/2019 taratibu za kuwasilisha maombi katika Bodi ya Ithibati (*Accreditation Board*) kwa maabara ya Dar es Salaam na Iringa zitafanyika.

### 3.2.2.8 Ujenzi na Ukarabati wa Maabara za Maji

**60. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati maabara za ubora wa maji nchini ili kuhakikisha kuwa maabara hizo zinakidhi mahitaji ya Mwongozo wa Viwango vya Kimataifa vya *ISO 17025:2017*. Hadi mwezi Machi 2018, Wizara imekamilisha ujenzi wa maabara ya Mwanza, Musoma na Kigoma. Vilevile, upanuzi na ukarabati wa majengo ya maabara za maji kwa Dar es Salaam umefikia **asilimia 98** na Songea **asilimia 45**. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa majengo mapya ya maabara ya Singida ambapo ujenzi umefikia **asilimia 80**, Bukoba (**99**), Sumbawanga (**75**), Mbeya (**65**) na Mtwara **asilimia 80**. Katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za ubora wa maji kwa kujijengea uwezo maabara za maji kote nchini ili kukidhi mahitaji ya mwongozo wa *ISO 17025:2017* na kulinda afya za watumishi.

**61. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kusimamia ubora wa maji na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji ambapo **sampuli 10,000** za maji kutoka vyanzo mbalimbali na sampuli 1,500

za majitaka kutoka katika viwanda, migodi na Taasisi mbalimbali zitachunguzwa.

### 3.2.3 Huduma ya Maji Vijijini

**62. Mheshimiwa Spika**, miradi ya maji vijijini inatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utekelezaji wa miradi hiyo unahusisha ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya miradi **1,493** imetekelezwa na inawanufaisha wananchi **21,321,500** waishio vijijini. Aidha, miradi **366** inaendelea kutekelezwa na imefikia hatua mbalimbali. Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji vijijini pamoja na kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji pamoja na programu hizo ni kama ifuatavyo:-

#### 3.2.3.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maji

**63. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini umefikia hatua mbalimbali kama inavyoelezwa katika aya zifuatazo:-

##### (a) Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe

**64. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unatarajia kutoa maji bwawa la Nyumba ya Mungu na kuhudumia miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji **38** vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, *OFID*, *SAUDI Fund* na *Kuwait Fund* na umegawanyika katika awamu mbili.

Awamu ya kwanza inatekelezwa katika vipande vinne vinavyohusisha ujenzi wa kidakio cha maji, mitambo ya kusafisha maji na miundombinu ya kupeleka na kusambaza maji katika miji ya Mwanga na Same pamoja na vijiji **tisa (9)**

vilivyopo kandokando ya bomba kuu. Awamu ya pili ya mradi itahusu kupeleka maji kwenye vijiji **29** vilivyobaki. Mradi utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **264,793** wa Wilaya ya Same, Mwanga (**177,085**) na Korogwe wananchi **15,053**.

**65. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa kipande cha kwanza unahusisha ujenzi wa kidakio cha maji, mtambo wa kutibu na kusafisha maji katika Kijiji cha Njiapanda, tanki la maji eneo la Kisangara pamoja na ulazaji wa bomba kutoka kwenye chanzo hadi tanki la maji litakalojengwa Kisangara. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 68**. Vilevile, utekelezaji wa kipande cha nne unahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita **milioni 9**, matanki mawili ya ujazo wa **lita 300,000** kila moja pamoja na ulazaji wa mabomba. Hadi mwezi Machi, 2018 ujenzi wa kipande hicho umefikia **asilimia 37**.

**66. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza kipande cha pili cha mradi kinachohusu ujenzi wa miundombinu katika vijiji **tisa (9)** vinavyozunguka mradi. Vilevile, utekelezaji wa kipande cha tatu unahusu ujenzi wa mtambo wa kusukuma maji kutoka kwenye tanki la Kisangara hadi Kiverenge, miundombinu ya matanki ya kuhifadhi maji na mabomba ya kusambaza maji katika Mji wa Mwanga. Hadi mwezi Machi 2018, kibali cha kuendelea na ujenzi kimepatikana kutoka Serikali ya KUWAIT na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Katika mwaka 2018/2019 jumla ya Shilingi bilioni 35 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mradi huo.

**(b) Mradi wa Maji wa Masoko**

**67. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Masoko unatekelezwa katika Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya na unahusisha ujenzi wa vituo **335** vya kuchotea maji, vidakio vya maji, matanki **sita (6)** ya kuhifadhi maji na ulazaji wa mtandao wa mabomba wenye urefu wa **kilomita 204.7**. Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika vipande (*lots*) vitano. Kipande cha kwanza kinahusisha ujenzi wa kidakio

cha maji katika Mto Mbaka, tanki la ujazo wa **lita 90,000**, vituo **vitano (5)** vya kuchotea maji, ulazaji wa mtandao wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 12.6** na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 370,000**. Ujenzi wa kipande hicho unagharimu **Shilingi milioni 552.2** na hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji umefikia **asilimia 50**. Kipande cha pili kinahusisha ujenzi wa kidakio cha maji, ujenzi wa chujo la maji, ujenzi wa vituo **40** vya kuchotea maji, ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 19.1** na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 290,000**. Kipande hicho kinagharimu **Shilingi milioni 851.6** na ujenzi wake umefikia **asilimia 30**.

**68. Mheshimiwa Spika**, kipande cha tatu kinahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 600,000**, ujenzi wa vituo **112** vya kuchotea maji na ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 61.9**. Kipande hicho kinagharimu **Shilingi bilioni 1.26** na hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji umefikia **asilimia 35**. Kipande cha nne kinahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 550,000**, ujenzi wa vituo **111** vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 80.6**. Kipande hicho kinagharimu **Shilingi bilioni 2.4** na ujenzi wake umefikia **asilimia 15**. Kipande cha tano kinahusisha uboreshaji wa kidakio cha maji, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 90,000**, ujenzi wa vituo **67** vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 30.5**. Kipande hicho kinagharimu **Shilingi milioni 552.4** na ujenzi wake umefikia **asilimia 45**.

**69. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi wa maji wa Masoko kutaongeza huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wapatao **19,624** wanaoishi katika vijiji vya Bulongwe, Ngaseke, Igembe, Ntandabala, Lupando, Bujesi, Lufumbi, Nsyasa, Ikama, Itagata, Busisya, Mbaka, Isabula, Lwifa na Nsanga. Katika mwaka 2018/2019 Wizara imetenga **Shilingi milioni 420** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

**(c) Mradi wa Maji wa Vijiji 100 Vilivyopo Kando ya Bomba Kuu la KASHWASA**

**70. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa vijiji **100** vilivyopo kandokando ya bomba

kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi umepangwa katika vijiji **40** ambapo vijiji **33** vimefanyiwa usanifu.

Kati ya vijiji vilivyofanyiwa usanifu, ujenzi wa miradi kwenye vijiji **14** umekamilika na kunufaisha wananchi wapatao **38,348**. Vijiji hivyo ni Runele, Gatuli, Nyashimbi, Magobeko, Kakulu, Butegwa, Nyang'homango, Ng'homango, Jimondoli, Kadoto, Lyabusalu, Mwajiji, Ichongo na Bukamba. Aidha, utekelezaji wa mradi unaendelea katika vijiji vya Mwasekagi na Mwakatola. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi bilioni 7 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mradi kwenye vijiji vilivyobaki.

#### **(d) Mradi wa Maji wa Ntomoko**

**71. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Ntomoko ulilenga kutoa huduma katika vijiji **18** vya Wilaya za Kondoa na Chemba. Kutokana na uwezo wa chanzo kuonekana kutokukidhi mahitaji, mnamo mwezi Novemba, 2017 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliunda timu ya pamoja ya wataalam kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina wa mradi pamoja na kutafuta chanzo kingine cha maji kwa ajili ya kuongeza wingi wa maji utakaokidhi mahitaji ya maji katika vijiji hivyo. Timu hiyo ilibaini kuwa chanzo cha Ntomoko kina uwezo wa kuhudumia vijiji vitatu tu. Kwa sasa wananchi wapatao **9,408** wa vijiji vya Makirinya na Lusangi wanaendelea kupata huduma ya maji kutoka mradi wa maji Ntomoko. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bwawa lenye mita za ujazo milioni **2.8** litakalojengwa kwenye eneo la Kisangaji ili kukidhi mahitaji ya vijiji vilivyobaki ambavyo kwa sasa havipati huduma ya maji. Usanifu wa bwawa hilo pamoja na bomba kuu kutoka katika chanzo cha bwawa hadi makutano ya kijiji cha Lusangi umekamilika. Vilevile, ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huo, usimamizi na ujenzi wa mradi utafanywa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

(e) **Mradi wa Maji Chiwambo**

**72. Mheshimiwa Spika**, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha upanuzi na ukarabati wa mradi wa maji wa Chiwambo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi utakaogharimu **Shilingi bilioni 4.49**. Utekelezaji wa mradi huo unahusisha ukarabati wa matanki na miundombinu ya maji iliyochakaa, ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji, upanuzi wa miundombinu ya kusambaza maji na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi wa Chiwambo umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha huduma ya maji kwa wakazi wapatao **84,082** wa Kata za Lulindi, Lupumbulu, Namalenga, Chiungutwa, Sindano, Mchauru na Mbuyuni.

(f) **Ukarabati na Ujenzi wa Mabwawa**

**73. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini hususan kwenye maeneo kame kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo wanapata huduma ya maji safi na salama. Hadi mwezi Machi 2018, ujenzi wa bwawa la Matwiga lililopo Wilayani Chunya umekamilika na linatarajiwa kuhudumia vijiji **15**. Kwa upande wa bwawa la Mwanjoro lililopo Wilayani Meatu, utekelezaji wa ujenzi umefikia **asilimia 91** ambapo kazi inayoendelea ni kukamilisha ujenzi wa utoro wa maji (*spillway*). Bwawa hilo likikamilika litahudumia vijiji **vitatu (3)** vya Mwanjoro, Jinamo na Mbushi vilivyopo Wlayani Meatu.

**74. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha uwepo wa vyanzo vya maji vya uhakika hususan kwenye maeneo kame, Serikali imeendelea kufanya utafiti wa maeneo mbalimbali yanayofaa kujengwa mabwawa nchini. Hadi mwezi Machi 2018, usanifu wa bwawa la Nsekwa katika Halmashauri ya Mlele umekamilika na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Kwa upande wa bwawa la Dongo litakalohudumia Halmashauri za Kiteto, Gairo na Kongwa, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya usanifu

wa kina kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo zinaendelea. Kwa bwawa la Kidete lililopo Wilayani Kilosa, timu ya pamoja ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeanza ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya usanifu wa bwawa ambalo pamoja na matumizi mengine litatumika kuzuia mafuriko yanayotokana na kiwango kikubwa cha maji kwenye Mto Kinyasungwe. Utekelezaji wa mabwawa ya Dongo na Kidete utasimamiwa na Wataalam wa Wizara. Aidha, utafiti kwa ajili ya maeneo yanayofaa kujenga mabwawa mapya unaendelea katika Halmashauri za Bahi, Mpwapwa na Chemba. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 3.87** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa.

### **3.2.3.2 Programu za Kuimarisha Uendeleu wa Huduma ya Maji Vijijini**

**75. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu, Serikali imetoa mwongozo kwa Halmashauri kuhusu usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs) ambavyo vinapaswa kusimamia uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya COWSOs **2,796** katika vijiji **3,435** zimeundwa na kusajiliwa katika Halmashauri mbalimbali nchini pamoja na kupatiwa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa miradi na fedha. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuimarisha uendeleu wa huduma ya maji vijijini kupitia Programu zifuatazo:-

#### **(a) Mfumo wa Malipo kwa Matokeo (Payment by Results - PbR)**

**76. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa DFID, inatekeleza mfumo wa malipo kwa matokeo ili kutoa motisha ya fedha katika utekelezaji wa miradi kwenye Halmashauri kwa lengo la kuongeza kasi ya uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Kupitia mfumo huo, malipo ya Paundi **50** hutolewa kwa kila kituo cha kuchotea maji kitakachokarabatiwa na kufanya kazi na Paundi **1,500**



kwa kituo kipya kitakachojengwa. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango ulikamilika mwezi Juni, 2017 na jumla ya Halmashauri **57** zilikidhi vigezo vya kupata malipo hayo ambapo **Shilingi bilioni 3.93** zilipelekwa katika Halmashauri hizo kati ya **Shilingi bilioni 6** zilizopangwa katika mwaka 2016/2017.

Awamu ya pili inaendelea ambapo jumla ya Halmashauri **72** zimekidhi vigezo vya kupata malipo ya **Shilingi bilioni 8.55** kati ya **Shilingi bilioni 53.6** zilizopangwa katika mwaka 2017/2018. Katika mwaka 2018/2019 **Shilingi bilioni 54.5** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo.

**(b) Programu ya Kuimarisha Uendeleu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

**77. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itaanza kutekeleza Programu ya Kuimarisha Uendeleu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kutumia mfumo wa malipo kwa matokeo (*Payment for Results – PforR*) kwa kipindi cha miaka **sita (6)** kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2024 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni **300**. Programu hiyo inatarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai, 2018 na itatekelezwa katika mikoa **17** ya Tabora, Katavi, Rukwa, Lindi, Geita, Shinyanga, Singida, Kagera, Mwanza, Manyara, Mtwara, Simiyu, Iringa, Mara, Ruvuma, Kigoma na Songwe. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya **Shilingi bilioni 23.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza programu hiyo.

**(c) Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (Renewable Energy)**

**78. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ohio (*Ohio State University - OSU*) cha Marekani inaendelea kutekeleza miradi miwili ya majaribio ya nishati jadidifu katika vijiji vya Ghalunyangu na Mughangha katika Halmashauri ya Singida iliyoanza kutekelezwa mwezi Novemba 2017. Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na *OSU* ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwenye vijiji **36** katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Mara,

Tabora, Singida na Dodoma. Lengo ni kutekeleza miradi ya matumizi ya nishati jadidifu katika vijiji 125 katika maeneo mbalimbali nchini ifikapo mwaka 2020.

**(d) Uvunaji wa Maji ya Mvua**

**79. Mheshimiwa Spika**, uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba ni muhimu kutokana na uhaba wa upatikanaji wa maji hususan katika maeneo kame. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuzihamasisha Taasisi za Kijamii, Asasi na Watu Binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wananchi kuhusiana na uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia rahisi kupitia mapaa ya majengo kwa kujenga matanki ya mfano kwenye maeneo ya shule, zahanati na masoko katika Halmashauri mbalimbali nchini.

**3.2.3.3 Miradi Mingine ya Maji Vijijini Inayotarajiwa Kutekelezwa**

**(a) Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Mkoani Kigoma**

**80. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji na usafi wa mazingira mkoani Kigoma unatarajiwa kuhudumia wakazi wapatao **200,000** katika vijiji 26 vya Mkoa huo. Mradi huo utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji kwa gharama ya **Euro milioni 8.8**. Hadi mwezi Machi 2018, Meneja wa Mradi amepatikana na taratibu za kuajiri watumishi wengine wa kutekeleza mradi huo zinaendelea. Vilevile, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya usanifu na usimamizi wa mradi zinaendelea. Ujenzi wa mradi huo unatarajia kuanza baada ya usanifu kukamilika. Katika mwaka 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

**(b) Miradi ya Maji katika Maeneo ya Maziwa Makuu**

**81. Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto ya uhaba wa huduma ya maji kwenye baadhi ya maeneo ya

pembezeni mwa maziwa makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali ili kuhakikisha huduma hiyo inapatikana katika maeneo hayo. Hadi mwezi Machi 2018, Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji kwenye maeneo hayo amepatikana. Kazi hiyo itafanyika katika mwaka 2018/2019 na jumla ya Shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

**(c) Mradi wa Maji wa Lukululu**

**82. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji Lukululu utatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na utahusisha vijiji vya Lukululu, Mbewe, Mlangali, Shomola, Shaji na Ndolezi katika Kata ya Mlangali na vijiji vya Igunda, Mahenje, Mbulu, Myovizi, Ichesa na Ivugula katika Kata ya Myovizi. Mradi huo utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Hispania kupitia *Debt Swap Program between Tanzania and Spain* na utagharimu **Shilingi bilioni 5**. Hadi mwezi Machi 2018, Mkataba kati ya Wizara na kampuni ya ONGAWA ambayo itafanya mapitio ya usanifu na kusimamia ujenzi wa mradi umeandaliwa na unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2018. Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Hispania kwa ajili ya kutekeleza mradi huo ambao utahudumia wananchi **35,277** wa Kata hizo. Katika mwaka 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 1.89** kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

**(d) Mradi wa Pamoja na Mgodhi wa Bulyanhulu**

**83. Mheshimiwa Spika**, mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Kampuni inayomiliki Mgodhi wa Dhahabu wa Bulyanhulu (*ACACIA*). Mradi una lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika vijiji **14** vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Shinyanga, Nyang'hwale na Msalala. Utekelezaji wa mradi unahusu kutoa maji kutoka bomba kuu la KASHWASA na kuyapeleka kwenye vijiji vya Mwenge, Nyugwa, Kharumwa, Mwamakiliga, Izunya, Kafita, Lushimba, Rwabakanga, Kakola **Namba 9**, Bushing'we, Kakola, Bugarama, Igudija na Ilogi. Maandalizi

ya ujenzi yameanza na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018. Kukamilika kwa mradi kutawanufaisha wananchi wapatao **100,243** wa Halmashauri hizo.

**84. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhakikisha wananchi waishio vijijini wanapata huduma endelevu ya majisafi na salama. Jumla ya **Shilingi bilioni 358.4** zimepangwa kutekeleza miradi ya maji vijijini ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 230** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 128.4**. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 5**.

### **3.2.4 Huduma ya Maji Mijini**

**85. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutekeleza Programu Ndogo ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini kwa kujenga, kukarabati na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji. Miradi hiyo hutekelezwa kwa kutoa maji kutoka vyanzo vya maziwa, mito, chemichemi, visima na mabwawa. Lengo likiwa ni kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini ikiwemo miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya na miji midogo. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo:-

#### **3.2.4.1 Miradi Inayotumia chanzo cha Maji Kutoka Maziwa (Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika) kupeleka kwenye Miji Mbalimbali**

##### **(a) Miradi ya Kutoa Maji Ziwa Victoria**

##### **(i) Miji ya Isaka na Kagongwa**

**86. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa maji kutoka bomba kuu la KASHWASA kwenda katika miji ya Isaka na Kagongwa. Mradi huo umegawanyika katika vipande viwili ambapo kipande cha kwanza kinagharimu **Shilingi**

**bilioni 11.91** na kipande cha pili **Shilingi bilioni 12.81**. Utekelezaji wa kipande cha kwanza unahusisha ulazaji wa bomba kuu kutoka Kinaga hadi Kagongwa lenye urefu wa kilomita **52.84** na ujenzi wa chemba. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 44**. Utekelezaji katika kipande cha pili unahusu ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **24** katika Mji wa Kagongwa na kilomita **23** katika Mji wa Isaka pamoja na ujenzi wa matanki **mawili (2)** ya chuma kwa kila mji na vituo **16** vya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 20**. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **115,000** wa miji ya Isaka na Kagongwa ambapo hali ya upatikanaji wa huduma ya maji itaongezeka kutoka **asilimia 26** hadi **asilimia 90** kwa Mji wa Isaka na **asilimia 24** hadi **asilimia 95** kwa Mji wa Kagongwa. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 6.5** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

**(ii) Miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo**

**87. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga (KASHWASA) imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ulazaji wa mabomba ya maji katika miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo pamoja na ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita milioni 1.2** katika Mji wa Kishapu. Mradi huo umegharimu **Shilingi bilioni 15.2** na umewezesha wananchi **58,155** kupata huduma ya maji safi na salama katika maeneo hayo.

**(iii) Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui**

**88. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa maji kutoka bomba kuu la KASHWASA wenye malengo ya muda mrefu ya kuwapatia huduma ya maji ya uhakika wananchi wapatao milioni **1.1** wa miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui pamoja na vijiji **110** vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka bomba kuu. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 268.35**, fedha kutoka

Serikali ya India kama mkopo wa masharti nafuu. Kazi zinazotekelezwa ni ulazaji wa bomba kuu, mabomba ya kusambaza maji pamoja na ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji. Mradi umegawanyika katika vipande vitatu ambapo kipande cha kwanza kinaanzia Kijiji cha Solwa (kilichopo Wilayani Shinyanga Vijijini) hadi Mji wa Nzega; kipande cha pili kinaanzia Nzega mjini hadi Manispaa ya Tabora kupitia Wilaya ya Uyui; na kipande cha tatu kinaanzia Nzega mjini hadi Igunga mjini. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 15** na utakapokamilika upatikanaji wa huduma ya maji katika miji hiyo utakuwa **asilimia 100**.

**(iv) Jiji la Mwanza na Miji ya Lamadi, Magu na Misungwi**

**89. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB*) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) inaendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi kwa gharama ya **Euro milioni 104.5**. Kwa upande wa Jiji la Mwanza, kazi zinazotekelezwa ni ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **64.82**; ujenzi wa matanki **sita (6)** katika maeneo ya Kitangiri **lita 500,000**, Nyasaka (**lita 1,000,000**), Mjimwema/Nyakabungo (**lita 1,200,000**), Nyegezi (**lita 1,200,000**) na Bugarika matanki mawili yenye ujazo wa **lita 800,000** na **lita 200,000**; kubadilisha mabomba yaliyochakaa; kuongeza mtandao wa mabomba katika maeneo ya barabara ya Kenyata, Makongoro na Nyakato yenye urefu wa kilomita **15.77**; na ujenzi wa mtambo wa kutibu maji.

**90. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi wa majisafi umefikia **asilimia 15** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2018/2019. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **105,649** wanaoishi maeneo ya milimani ambao hawapati huduma ya maji kwa sasa. Maeneo hayo ni Nyasaka, Bugarika, Nyegezi, Capripoint, Mjimwema, Nyakabungo na Kitangiri. Aidha, uboreshaji wa huduma ya usafi wa mazingira katika

Jiji la Mwanza hususan kwenye maeneo ya milimani pamoja na ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoaji wa majitaka unaendelea na hadi mwezi Machi, 2018 utekelezaji umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2018.

**91. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika miji ya Magu, Misungwi na Lamadi, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kujenga mifumo mipya ya kusafisha na kutibu maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa matanki; ujenzi wa vituo vya kuchotea maji na ununuzi wa vitendea kazi (magari na pikipiki). Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 10** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi **23,315** waishio Misungwi Mjini na Kijiji cha Nyahiti; wakazi **45,340** waishio Magu Mjini na vijiji vya Ilungu na Kipeja; na wakazi **23,540** wa Lamadi Mjini.

**(v) Manispaa ya Musoma**

**92. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Musoma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 45**. Kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa chanzo cha kutoa maji kutoka Ziwa Victoria ambacho kimeweza kuongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 10.14** hadi **lita milioni 36** kwa siku ambazo zitakidhi mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Musoma hadi mwaka 2025. Mradi umekamilika na upo kwenye kipindi cha uangalizi. Kukamilika kwa mradi huo kumewanufaisha wakazi wapatao **145,288** wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

**(b) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika kwenda Manispaa ya Kigoma**

**93. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa maji unaohusu usambazaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Kigoma unatekelezwa kwa gharama ya **Euro milioni 16.32** kwa ushirikiano wa Serikali na

Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa matanki **matano (5)** yenye ujazo wa **lita milioni 2** kila moja na tanki moja lenye ujazo wa **lita 500,000**; ujenzi wa tanki (*balance tank*) lenye ujazo wa **lita milioni 2**; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji chenye pampu **9**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji urefu wa kilomita **122.8**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **22**; ujenzi wa vituo **70** vya kuchota maji; ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la kutoa huduma ya uondoaji majitaka. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 83** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018 na utakapokamilika utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 1.3** za sasa hadi **lita milioni 42** na kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kutoka **asilimia 65** za sasa hadi asilimia 95 na kuwanufaisha wakazi wapatao **384,501**.

#### 3.2.4.2 Miradi Inayopata Maji kutoka Vyanzo vya Mito Kupeleka Miji Mbalimbali

##### (a) Mji wa Orkesumet

94. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Mji wa Orkesumet unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (*BADEA*) na Mfuko wa Nchi zinazozalisha mafuta kwa Maendeleo ya Kimataifa (*OFID*). Mradi huo ambao unapata maji kutoka Mto Pangani umegawanyika katika vipande (*lots*) viwili ambapo kipande cha kwanza kitagharimu **Shilingi bilioni 12.99** na kipande cha pili **Shilingi bilioni 25.02**. Utekelezaji wa kipande cha kwanza unaohusu ujenzi wa kidakio cha maji na mtambo wa kutibu na kusafisha maji utaanza mwezi Mei, 2018. Vilevile, utekelezaji wa kipande cha pili umeanza na unahusisha ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa vituo vya kuchotea maji; na miundombinu ya kunyweshea mifugo. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kazi hizo umefikia **asilimia 36** na kazi zilizobaki zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2018. Mradi



utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kutoka **asilimia 48** hadi **asilimia 100** na kuwanufaisha wakazi wapatao **52,000** wa Mji wa Orkesument pamoja na mifugo yao.

**(b) Mji wa Longido**

**95. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Longido. Mradi huo umegawanyika katika vipande **vinne (4)**. Utekelezaji wa kipande cha kwanza unaogharimu **Shilingi bilioni 10.89** unahusu ujenzi wa chanzo katika Mto Simba, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **63.02** kutoka Mto Simba hadi kwenye tanki la Longido mjini na ujenzi wa chemba **nne (4)** za kupunguza msukumo wa maji. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 40**. Utekelezaji wa kipande cha pili utagharimu **Shilingi bilioni 2.54** na unahusisha ulazaji wa bomba la kusafirisha maji kutoka Longido hadi Kijiji cha Engikaret pamoja na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 42**.

**96. Mheshimiwa Spika**, kipande cha tatu kinachogharimu **Shilingi milioni 276.36** kinahusisha ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji litakalojengwa katika Mji wa Longido, ukarabati wa matanki matatu, ukarabati wa miundombinu ya kunyweshea mifugo na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika Kijiji cha Engikaret. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 90**. Kipande cha nne kinahusu ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika Mji wa Longido kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.09** ambapo utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 75**. Kukamilika kwa mradi wa Longido kutawezesha wananchi wapatao **16,712** kupata huduma ya maji safi na salama. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi bilioni 6 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

**(c) Miji ya Vwawa na Mlowo**

**97. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya

majisafi katika Miji ya Vwawa na Mlowo katika Mkoa mpya wa Songwe. Mradi wa maji katika Mji wa Vwawa unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.47** ambapo kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa kidakio cha maji kwenye Mto Mantengu, ufungaji wa mitambo ya kutibu maji, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **17.1**, ulazaji wa mtandao wa kusambaza maji wenye urefu wa kilomita **12.56** na ununuzi wa dira za maji **1,200**. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefika **asilimia 70**.

**98. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Mlowo unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 466** kwa kutumia chanzo cha Mto Mlowo. Kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa matanki **mawili (2)** yenye jumla ya ujazo wa **lita 200,000**, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **2**, upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji wenye urefu wa kilomita **15**, ufungaji wa mtambo wa kusuma maji na ununuzi wa dira za maji **200**. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 60**.

**99. Mheshimiwa Spika**, miradi yote ikikamilika katika Miji ya Vwawa na Mlowo itaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 38.4** hadi **asilimia 56.4** na kunufaisha wakazi **10,171** wa Mji wa Vwawa na **9,154** wa Mji wa Mlowo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2.5** kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.

#### **3.2.4.3 Miradi inayopata Maji kutoka kwenye Visima Kupeleka Miji Mbalimbali**

##### **(a) Jiji la Arusha**

**100. Mheshimiwa Spika**, ili kuondoa kero ya uhaba wa majisafi na uondoaji majitaka katika Jiji la Arusha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka unaogharimu **Dola za Marekani milioni 233.9**. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu **56**; ujenzi wa matanki **10**; ujenzi wa mtambo wa kutibu na

kusafisha maji; upanuzi na ukarabati wa mtandao wa mabomba ya majisafi; upanuzi na ukarabati wa mtandao wa majitaka, ujenzi wa mabwawa mapya **18** ya majitaka; ujenzi wa ofisi ya Mamlaka; ununuzi wa vitendea kazi na kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 3** na unatarajiwa kukamilika mwaka 2020. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 200** kwa siku. Vilevile, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi utaongezeka kutoka saa **12** za sasa hadi saa **24** kwa siku pamoja na kuongeza huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**.

**(b) Manispaa ya Lindi**

**101. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza mradi wa maji katika Manispaa ya Lindi kwa gharama ya **Euro Milioni 11.7**. Kazi zinazotekelezwa ni uchimbaji wa visima virefu 10; ujenzi wa chujio la maji lenye uwezo wa kusafisha maji **lita milioni 7.5** kwa siku; ujenzi wa matanki mawili ya maji yenye ujazo wa **lita milioni 3** na **lita milioni 2**; ulazaji wa bomba kuu la maji lenye urefu wa kilomita **11.5**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **27**; ujenzi wa vituo **85** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la huduma ya uondoaji majitaka. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 90**. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 1.5** za sasa hadi **lita milioni 9** na kuwanufaisha wakazi wapatao **81,343** wa Mji wa Lindi.

**(c) Mji wa Geita**

**102. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) inaendelea kutekeleza mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LWATSAN II*) katika Mji wa Geita kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.67**. Mradi huo unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza. Kazi zinazotekelezwa ni uchimbaji wa

visima virefu **vitatu (3)** ambapo visima **viwili (2)** vimefungiwa pampu; ufungaji wa pampu kwenye visima **vitano (5)** vya zamani; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **16**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **38**; ununuzi wa dira za maji **4,090**; pamoja na ujenzi wa matanki **manne (4)** yenye jumla ya ujazo wa **lita 815,000** katika maeneo ya Kagera, Buhalahala, Shule ya Waja na Stendi ya Mabasi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 3.8** kwa siku hadi **lita milioni 5.7** kwa siku na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kutoka **asilimia 35** hadi asilimia 70 kwa wakazi wapatao **135,359** wa Mji wa Geita.

**103. Mheshimiwa Spika**, vilevile, mradi huo unahusisha uboreshaji wa huduma za usafi wa mazingira ambapo ujenzi wa vyoo **viwili (2)** katika Shule za Msingi Mbugani na Nyankumbu umekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka na ujenzi wa dampo la kisasa la kutupa taka ngumu kwenye eneo la Usindakwe. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya usafi wa mazingira umefikia **asilimia 75**. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kuendelea kuboresha hali ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Geita.

#### **3.2.41.4 Miradi Inayotumia chanzo cha Maji kutoka kwenye Chemchemi Kupeleka Miji Mbalimbali**

##### **(a) Mji wa Mpanda**

**104. Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa mserereko kutoka katika chemchemi ya Kanoge hadi tanki la Manga kwa gharama ya **Shilingi milioni 607.12**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 3.2** hadi **lita milioni 4.6** kwa siku pamoja na kuwanufaisha wakazi wapatao 10,000 wa maeneo ya Makanyagio, Madukani na Majengo B. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.5** ili kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mpanda.

**(b) Mji wa Njombe**

**105. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Njombe, Serikali inatekeleza mradi unaopata maji kutoka Chemchemi ya Kibena kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.1**. Hadi mwezi Machi 2018, kazi zilizokamilika ni ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **2.2**, ujenzi wa kidakio cha maji, ununuzi wa dira za maji na ufungaji wa pampu mbili za kusukuma maji zenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo **72** kwa saa. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 90** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2018. Mradi huo utakapokamilika utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 480,000** hadi **lita 864,000** kwa siku na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Hospitali ya Kibena, Chuo cha Uuguzi na maeneo ya Nyamyuya, Ofisi za Mkoa na Mgendela. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

**3.2.4.5 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo**

**106. Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji majitaka katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na miji ya Kibaha na Bagamoyo. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

**(a) Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera**

**107. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera unahusu uchimbaji wa visima virefu **20** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 18** ambavyo vinatarajiwa kuzalisha maji **lita milioni 260** kwa siku. Hadi mwezi Machi 2018, visima **19** vimechimbwa na kati ya hivyo visima **15** vimekamilika na uchimbaji wa visima **vinne (4)** unaendelea. Kazi ya uchimbaji wa visima vyote **20** itakamilika mwezi Mei, 2018. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kiasi cha **Dola za Marekani milioni 158** kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kusambaza maji

kutoka kwenye visima vya Mpera ili kupeleka maji katika maeneo ya Gongo la Mboto, Chanika, Luzando, Pugu, Mpera, Chamanzi, Kitunda, Ukonga, Kinyerezi na Uwanja wa Ndege. Kwa upande wa visima vya Kimbiji, gharama ya miundombinu ya kusambaza maji ni Dola za Marekani milioni 307 na maeneo yatakayonufaika ni Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Tandika, Keko na Chang'ombe.

**(b) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

**108. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza majisafi katika maeneo ya Tegeta hadi Mpiji, Mpiji hadi Bagamoyo na Mbezi hadi Kiluvya kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 32.93**. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 81**. Kazi zilizotekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **283.3** kati ya kilomita **511.6** zilizopangwa; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa **lita milioni 5** katika eneo la Salasala; na ujenzi wa matanki **manne (4)** yenye ujazo wa **lita milioni 6** kila moja katika maeneo ya Changanyikeni, Wazo, Bunju na Bagamoyo. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wakazi wa Mji wa Bagamoyo na vitongoji vyake, eneo la uwekezaji la Bagamoyo (*EPZ*), Mpiji, Bunju, Mabwepande, Boko, Mbweni, Tegeta, Ununio, Wazo, Salasala, Kinzudi, Matosa, Mbezi Juu, Goba, Changanyikeni, Makongo, Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Msakuzi, Makabe, Malamba mawili na Msigani. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi bilioni 38.5 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji.

**(c) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

**109. Mheshimiwa Spika**, usanifu wa ujenzi wa bwawa la Kidunda pamoja na ulipaji wa fidia kwa wakazi watakaopisha ujenzi wa bwawa hilo umekamilika. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 215**. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa bwawa lenye mita za ujazo milioni **190**

kwa ajili ya kuhifadhi maji yatakayotumika katika mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini; ujenzi wa kituo cha kufua **Megawati 20** za umeme; ujenzi wa njia ya msongo mkubwa wa umeme kutoka Kidunda hadi Chalinze; na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita **76** kutoka Ngerengere hadi Kidunda. Lengo la mradi huo ni kuhakikisha kuwa maji katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikubwa cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka. Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na *NSSF* kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

**(d) Kuboresha Miundombinu ya Uondoaji Majitaka**

**110. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na uboreshaji wa usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam kwa kupanua mtandao wa uondoaji majitaka na kujenga miundombinu ya kusafisha majitaka. Lengo ni kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya uondoaji majitaka kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 30** ifikapo mwaka 2020. Katika kutimiza lengo hilo Serikali itatekeleza ujenzi wa miradi katika maeneo matatu ya Jangwani, Kurasini na Mbezi Beach.

**(i) Eneo la Jangwani**

**111. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 90.09**. Mradi huo utahusisha ujenzi wa mfumo wa majitaka wenye mabomba yenye urefu wa kilomita **376** kutoka maeneo ya Ubungo, Kinondoni, Magomeni, Mwananyamala, Msasani, katikati ya Jiji na Ilala hadi kwenye mtambo wa kusafisha majitaka utakaojengwa eneo la Jangwani. Vilevile, ujenzi wa mradi utahusisha kubadili mwelekeo wa bomba linalomwaga majitaka baharini na kuyapeleka kwenye mtambo wa Jangwani. Mtambo huo utakuwa na uwezo wa kusafisha lita milioni 200 za majitaka kwa siku. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka 2018/2019.

**(ii) Eneo la Kurasini**

**112. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) itatekeleza mradi wa

kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika eneo la Kurasini. Mradi huo unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 100** ambapo majadiliano ya mkataba wa kifedha yanaendelea. Mradi utahusisha ujenzi wa mfumo wa mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita **90** katika maeneo ya Keko, Chang'ombe, Kurasini, Temeke na Uwanja wa Taifa. Majitaka kutoka katika maeneo hayo yatasafishwa katika mtambo mpya utakaojengwa maeneo ya Kurasini yalipo mabwawa ya kusafisha majitaka. Mtambo wa Kurasini utakuwa na uwezo wa kusafisha majitaka **lita milioni 11** kwa siku. Kwa sasa eneo la Kurasini halitoshi kwa ujenzi, hivyo Serikali inaendelea kulipa fidia kwa wakazi watakaopisha upanuzi wa eneo la mradi huo. Gharama za ulipaji fidia ni **Shilingi bilioni 7** na hadi mwezi Machi 2018, **Shilingi bilioni 4** zimelipwa.

### (iii) Eneo la Mbezi Beach

**113. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika maeneo ya *Mbezi Beach*, Kawe na Kilongawima kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 65**. Mradi huo utahusisha ujenzi wa mtambo mpya utakaojengwa eneo la *Mbezi Beach* utakaokuwa na uwezo wa kusafisha **lita milioni 16** kwa siku pamoja na mfumo wa mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita **97**. Mradi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa taratibu za umiliki wa eneo la mradi.

#### 3.2.4.6 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Dodoma

**114. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeweka mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Dodoma ili kuendana na uhitaji mkubwa wa maji unaotokana na ukuaji wa kasi wa mji huo ambao ni Makao Makuu ya Serikali. Mikakati hiyo imeelezwa kwa kina kama ifuatavyo:-



(a) Mikakati ya Muda Mfupi

(i) Utafutaji wa Maeneo ya Kuchimba Visima karibu na Mji Mpya wa Serikali

115. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi (*geophysical survey*) katika maeneo ya Ihumwa na Kikombo yaliyomo pembezoni mwa Mji wa Dodoma. Lengo la utafiti huo ni kuwezesha upatikanaji wa maji kwa shughuli za ujenzi wa Mji wa Serikali unaotarajiwa kujengwa eneo la Ihumwa pamoja na kuyapatia maji maeneo ya pembezoni mwa mji. Hadi mwezi Machi 2018, uchimbaji wa kisima **kimoja (1)** kilichopo Ihumwa umekamilika na maandalizi ya kuchimba visima vingine yanaendelea.

(ii) Miradi ya Kusambaza Maji Kwenye Maeneo Yasiyo na Huduma

116. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa mitandao ya kusambaza majisafi katika maeneo yasiyo na huduma katika Mji wa Dodoma, Serikali itatekeleza miradi ya kusambaza maji katika maeneo ya Chidachi, Ndachi, Nzuguni Njedengwa/Medeli, Kizota na Mwangaza itakayogharimu **Shilingi bilioni 1.5**. Ili kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (*DUWASA*) inaendelea na taratibu za kupata fedha kupitia Mfuko wa Investment Financing Facilities (*IFF-OBA*) unaofadhiliwa na *KfW*.

(b) Mikakati ya Muda Mrefu

(i) Mradi wa Bwawa la Farkwa

117. **Mheshimiwa Spika**, mkakati wa muda mrefu wa Serikali ni kujenga bwawa la Farkwa katika Wilaya ya Chemba ili kupata chanzo cha maji cha nyongeza kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa Mji wa Dodoma. Bwawa hilo litaongeza uzalishaji wa maji kwa zaidi ya ujazo wa **lita milioni 120** kwa siku, kiasi ambacho kitatosheleza mahitaji

ya maji ya watu zaidi ya milioni 1 wa Mji huo. Hadi mwezi Machi 2018 tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi imekamilika.

(ii) **Mradi wa Uboreshaji Huduma za Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma na Chamwino Ikulu**

**118. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na taratibu za kuajiri Mtaalam Mshauri ambaye atafanya upembuzi yakinifu, tathmini ya athari ya kimazingira na kijamii na usanifu wa kina wa mradi wa uboreshaji huduma za majisafi na majitaka Mjini Dodoma na Chamwino Ikulu. Lengo la mradi ni kupata mahitaji halisi ya majisafi na huduma ya uondoaji wa majitaka katika Miji ya Dodoma na Chamwino Ikulu. Aidha, Mtaalam Mshauri atafanya kazi ya kutafuta vyanzo vingine vya maji kwa maeneo ya pembezoni mwa Mji wa Dodoma.

(iii) **Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Uondoaji Majitaka**

**119. Mheshimiwa Spika**, Serikali itatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya uondoaji majitaka unaokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 56**. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2019/2020. Hadi mwezi Machi 2018, eneo la ujenzi wa mabwawa mapya ya kusafisha majitaka limepatikana katika eneo la Nzuguni ambapo **Shilingi milioni 611** zimetumika katika ulipaji wa fidia kwa ajili ya eneo hilo lenye ukubwa wa **hekta 60**. Aidha, mitandao ya kukusanya majitaka itajengwa kwenye maeneo ya Area A, Chadulu, Chinangali, Kikuyu, Makole, Ipagala, *Urban Renewal East and West*, Viwanda, Mlimani, Medeli, Ilazo, Kisasa, *NCC* na Nkuhungu. Vilevile, ukarabati wa mtandao wa majitaka kwenye maeneo ya *Area C* na *Area D* utafanyika.

**120. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuhakikisha wananchi wa Mji wa Dodoma wanapata huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma hizo unakidhi mahitaji ya wakazi wa Mji wa

Dodoma. Aidha, Serikali inaziomba taasisi na wadau mbalimbali kutoa ushirikiano katika kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Dodoma. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 9.5** kwa ajili ya kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Dodoma.

### 3.2.4.7 Miradi ya Maji ya Kitaifa

**121. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maji ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Maji ya Kitaifa. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Mradi wa Maji Chalinze

**122. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inatekeleza awamu ya tatu ya mradi wa majisafi wa Chalinze kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 41.3**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni upanuzi wa kidakio cha maji kwenye Mto Wami kitakachoongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5** kwa siku hadi **lita milioni 9**; ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji katika vijiji **20**; ulazaji wa bomba kuu na upanuzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **921.72**; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 2** katika Mlima Mazizi; na ujenzi wa vituo **496** vya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na huduma ya maji wakati wa ujenzi wa awamu ya kwanza na ya pili ya mradi. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 73**. Hata hivyo, ujenzi wa mradi huo umesimama kwa sasa kufuatia kusitishwa kwa mkataba kutokana na mkandarasi kukiuka masharti ya mkataba. Hatua za kimkataba zinaendelea katika kutatua changamoto zilizojitokeza. Inatarajiwa kazi zilizobaki zikamilike ndani ya miezi **tisa (9)** tangu ujenzi utakapoanza tena. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wa Chalinze wapatao **397,384**. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2.3** kwa ajili ya kuendelea kutekeleza mradi huo.

**(b) Mradi wa Mugango - Kiabakari**

**123. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development - SFD*) itatekeleza mradi wa maji utakaohudumia maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na upanuzi wa kidakio cha maji katika Ziwa Victoria; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji iliyopo Kiabakari; ujenzi wa matanki **matatu (3)** katika maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mugango kwenda Kiabakari hadi Butiama lenye urefu wa kilomita **32**; na ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji kutoka Butiama hadi Bisarye. Usanifu wa kina wa mradi unaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao **80,000** waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka eneo la bomba kuu. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 6.5** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**(c) Mradi wa Makonde**

**124. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya muda mfupi ya uboreshaji wa huduma ya upatikanaji wa maji katika mradi wa maji wa Kitaifa wa Makonde. Hadi mwezi Machi 2018, pampu **10** za kusukuma maji kutoka kwenye visima zimenunuliwa na zitafungwa katika vituo vya Mkunya Bondeni (**pampu 2**), Mkunya Kati (**1**), Makote (**1**), Mahuta (**1**), Mitama-Nanda (**2**), Mitema-Mtongowele (**2**) na Mtongowele-Chihangu pampu **moja (1)**. Ununuzi na ufungaji wa pampu unagharimu Shilingi milioni 710.29.

Vilevile, mradi wa ukarabati wa mabomba yaliyochakaa yenye urefu wa kilomita **24** katika maeneo ya Makote-Nanguruwe, Mahuta-Nanyuwila, Ghana Juu-Lukokoda, Nanda - Kitangali, Chihangu - Mnyambe unaendelea na hadi

mwezi Machi, 2018 ununuzi wa mabomba yenye gharama ya **Shilingi milioni 864.06** umefanyika. Hatua inayofuata ni ulazaji wa mabomba hayo. Miradi hiyo itakapokamilika itaongeza uzalishaji wa maji pamoja na kupunguza upotevu wa maji, hivyo kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi huo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.

**(d) Mradi wa Handeni Trunk Main (HTM)**

**125. Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya Wilaya za Handeni na Korogwe yanayohudumiwa na Mradi wa Maji wa Kitaifa wa *HTM* kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2**. Kazi zitakazotekelezwa ni kununua na kufunga mitambo ya kusukuma maji kwenye kidakio cha Mandera kilichopo Mto Pangani; kubadilisha mabomba chakavu; kukarabati tanki la kuhifadhi maji katika eneo la Bongi; kupeleka umeme kwenye mitambo ya kusukuma maji na kukarabati machujio ya maji. Hadi mwezi Machi 2018, Mkandarasi wa kutekeleza mradi huo amepatikana na yupo katika hatua za maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi (*mobilization*). Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapatao **237,600** wa maeneo yanayohudumiwa na mradi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.5** ili kuanza utekelezaji wa mradi huo.

**(e) Mradi wa Wanging'ombe**

**126. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mradi wa Maji wa Kitaifa wa Wanging'ombe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.93**. Kazi zinazotekelezwa ni ukarabati wa matanki **44**, ukarabati wa mbauti **59** za kunyweshea mifugo, pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 65** na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018. Kukamilika kwa mradi huo kutapunguza kero ya uhaba wa maji katika maeneo yanayohudumiwa

na mradi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mradi huo.

**(f) Mradi wa Maji wa Masasi-Nachingwea**

**127. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji ya Mradi wa Kitaifa wa Masasi – Nachingwea (*MANAWASA*). Mradi huo unagharimu **Shilingi milioni 870.74** na kazi zinazotekelewa ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika vijiji **12** vilivyomo umbali wa kilomita **5** kutoka kwenye bomba kuu, ujenzi wa vituo vya muda vya kuchotea maji (stand pipes) na ujenzi wa vioski. Hadi mwezi Machi 2018, ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2018. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapatao **24,077** wa vijiji vya Mtepeche, Magereza, Mailisita, Mkotokuyana na Naipanga vilivyopo Wilayani Nachingwea; vijiji vya Chiyapi, Nandanga, Ipingo, Lucheregwa, Mbecha na Litama vilivyopo Wilayani Ruangwa na kijiji cha Chikunja kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Masasi.

Aidha, Serikali itajenga mtambo wa kutibu na kusafisha maji katika Chemchemi ya Mbwinji ambapo taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu zinaendelea. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa maeneo yanayohudumiwa na mradi wa maji wa Kitaifa wa Masasi-Nachingwea.

**(g) Mradi wa Maji wa Maswa**

**128. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji katika Bwawa la New Sola utakaohudumia Mji wa Maswa na vijiji vya Zanzui, Malita, Bayubi, Dodoma, Hinduki, Mwasita, Mwabayanda, Ng'wigwa na Mwabujiku kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.35**. Hadi mwezi Machi 2018, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 78** na unatarajiwa kukamilika mwezi

Mei 2018. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5.9** hadi **lita milioni 10.37**. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa Kitaifa wa Maswa.

**(h) Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo**

**129. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo. Hali ya utekelezaji wa miradi katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 6**. Aidha, katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 20.5** kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ambayo upatikanaji wa huduma ya maji siyo wa kuridhisha. **Kiambatisho Na. 7** kinaonesha mgawanyo wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

**3.2.4.9 Miradi ya Maji Inayotarajiwa Kutekelezwa katika Maeneo Mbalimbali Mijini**

**(a) Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma Kupeleka Manispaa ya Mtwara – Mikindani**

**130. Mheshimiwa Spika**, Serikali itatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara – Mikindani na vijiji **26** pamoja na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka eneo la bomba kuu utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 189.9**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji; mtambo wa kusafisha na kutibu maji; nyumba ya mtambo wa kusukuma maji; matanki madogo **26** na tanki kubwa la ujazo wa **lita milioni 30** ambalo litajengwa eneo la Mangamba; vituo vya kuchotea maji **234**; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **63**. Hadi mwezi Machi 2018, Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo amepatikana na Serikali inaendelea na majadiliano na

Serikali ya China kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa mradi huo. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9** hadi **lita milioni 120** kwa siku na kutosheleza mahitaji ya maji katika Manispaa ya Mtwara.

**(b) Mradi wa Kutoa Maji Mto Malagarasi Kwenda Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka**

**131. Mheshimiwa Spika**, Wizara imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Mto Malagarasi kupeleka miji ya Urambo, Kaliua, Nguruka, Usoke pamoja na vijiji **68** vilivyopo kando ya bomba kuu. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji, ujenzi wa mitambo ya kusafisha na kutibu maji, ujenzi wa matanki ya maji, ulazaji wa bomba kuu kutoka Mto Malagarasi hadi miji ya Urambo na Kaliua na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji kwenye miji hiyo. Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa mradi huo. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo unaokadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 331.91. Mradi unatarajiwa kunufaisha wakazi wapatao 607,086 wa Miji ya Urambo, Kaliua, Nguruka na Usoke pamoja na vijiji 68.

**(c) Mradi wa Maji katika Miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi**

**132. Mheshimiwa Spika**, Serikali itatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika miji ya Nyashimo (Busega), Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi kwa gharama ya **Euro milioni 313**. Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kina wa mradi na anatarajia kukamilisha kazi hiyo mwezi Mei, 2018. Mradi utatekelezwa katika awamu mbili na utakapokamilika utahudumia wakazi **834,204** wa miji hiyo. Awamu ya kwanza itagharimu **Euro milioni 105** ambapo Benki ya KfW ya Ujerumani itatoa Euro milioni 25 na *Green Climate Fund (GCF)* **Euro milioni 80**. Awamu hiyo itahusisha miji ya Nyashimo (Busega), Bariadi, Lagangabilili pamoja na vijiji vipatavyo **170** vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka bomba kuu. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na *Green Climate Fund*



kwa ajili ya kupata fedha kiasi cha **Euro milioni 208** za kutekeleza awamu ya pili ya mradi itakayohusisha miji ya Mwanhuzi na Maswa pamoja na vijiji vipatavyo **83**.

**(d) Mradi wa Maji Morogoro Mjini**

**133. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo la *AFD* itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Manispaa ya Morogoro. Lengo la mradi huo ni kuongeza ujazo wa maji ya bwawa la Mindu kutoka **lita bilioni 12** hadi kufikia lita bilioni 20. Kazi zitakazotekelezwa ni kuongeza kina cha bwawa la Mindu kwa kuongeza urefu wa tuta kwa **mita 2.5**; ujenzi wa mtambo wenye uwezo wa kusafisha na kutibu maji **lita milioni 54** kwa siku; upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji; ukarabati wa mabwawa ya majitaka katika eneo la Mafisa ambayo yanapokea majitaka kutoka viwandani na majumbani; ukarabati wa miundombinu ya majisafi; ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka Tumbaku hadi Kingolwira; na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 450,000**. Vilevile, utafiti wa vyanzo vipya vya maji vitakavyotosheleza mahitaji ya maji hadi kufikia mwaka 2035 utafanyika. Gharama ya mradi ni **Euro milioni 70** na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu wa kina na usimamizi wa mradi zinaendelea. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 8** ili kutekeleza mradi huo.

**(e) Mji wa Bariadi**

**134. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha mradi wa kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Bariadi. Kazi zitakazotekelezwa ni ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita **3.4** katika maeneo ya Malinoni, Kigangoni na Kisesa na kupeleka umeme kwenye eneo la visima vipya **vitano (5)** pamoja na kufunga pampu katika visima hivyo. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kutekeleza mradi huo zinaendelea. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.5** ili kutekeleza mradi huo.

**(f) Miji ya Mtwara na Babati**

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Serikali itakamilisha usanifu wa kina pamoja na kuanza ujenzi wa

miradi ya kusambaza majisafi katika miji ya Mtwara na Babati kwa gharama ya **Euro milioni 18.9**. Mradi huo utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya. Utekelezaji wa mradi huo utaboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji hiyo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi bilioni 6 ili kutekeleza miradi kwenye miji hiyo.

**(g) Miji ya Musoma na Bukoba**

**136. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) itatekeleza miradi ya uondoaji majitaka katika miji ya Musoma na Bukoba, itakayogharimu **Shilingi bilioni 24.87**. Hadi mwezi Machi 2018, Mkandarasi amepatikana kwa Mji wa Musoma na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2018. Kwa upande wa Mji wa Bukoba taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri wa kupitia usanifu pamoja na kusimamia ujenzi zinaendelea.

**(h) Miradi ya Maji katika Miji 17**

**137. Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa muda mrefu wa kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mbalimbali nchini, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India, itatekeleza miradi ya maji katika miji **17** ikiwemo Zanzibar. Gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ni **Dola za Marekani milioni 500**. Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya India ili kukubaliana mkataba wa fedha. Orodha ya miji hiyo na mchanganuo wa gharama umeainishwa katika **Kiambatisho Na. 8**, katika Manispaa ya Kigoma. Hadi mwezi Desemba 2017, kujenzi wa mradi unatekelezwa kwa gharama ya **Euro Milioni 16.32** umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi April 2018. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja ujenzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa matanki **matano (5)** yenye ujazo wa **lita milioni 2** kila moja na tanki moja lenye ujazo wa **lita 500,000**; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 2** (*balance tank*); ujenzi wa kituo cha kusukuma maji chenye pampu **9** ; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji urefu wa kilomita **122.8**; ulazaji wa bomba

kuu lenye urefu wa kilomita **22**; ujenzi wa vituo **70** vya kuchotea maji ; ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la huduma ya uondoaji majitaka. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kutoka Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Dodoma

#### **3.2.4.10 Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini**

**138. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali imeanza ujenzi wa Ofisi za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Mpanda na Geita. Hadi mwezi Machi 2018, ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Maji Geita umefikia **asilimia 45** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2018. Kwa upande wa Mamlaka ya Maji Mpanda, ujenzi umefikia **asilimia 92** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2018. Vilevile, ofisi za Mamlaka zitajengwa katika miradi ya uboreshaji wa huduma ya maji inayoendelea kutekelezwa katika Jiji la Arusha pamoja na miji ya Tabora, Igunga na Nzega. Kukamilika kwa ofisi hizo kutaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini ili kuwaongezea ujuzi katika utendaji wao wa kazi.

#### **3.2.4.11 Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Mijini**

**139. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi waishio mijini kwa kujenga miradi mipya, kupanua miradi, kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa pamoja na kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa miundombinu ya miradi ya maji. Jumla ya **Shilingi bilioni 322.2** zimepangwa kutumika kutekeleza miradi ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 155** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 167.2**. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mijini umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 9**.

### 3.2.5 Huduma ya Umwagiliaji

#### 3.2.5.1 Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo

**140. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program - ASDP*) kwa kujenga, kukarabati na kufanya usanifu wa skimu na mabwawa ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Machi 2018, Wizara imekamilisha ujenzi wa utoro wa maji (*spillway*) katika mabwawa ya Ussoke Mlimani lililopo katika Halmashauri ya Urambo lenye uwezo wa kumwagilia **hekta 530**; na Dongobesh lililopo katika Halmashauri ya Mbulu; ujenzi wa kivuko cha mifugo, makingamaji **matatu (3)** na usakafaji wa mifereji yenye urefu wa **mita 100** kwenye Skimu ya Mforo (Halmashauri ya Mwanga) yenye **hekta 290**; uchimbaji na usakafaji wa mfereji mkuu wenye urefu wa **mita 740** kwenye Skimu ya Hangangadinda (Mji mdogo wa Madaba) yenye **hekta 250**; uchimbaji na usakafaji wa mfereji mkuu wenye urefu wa **mita 115** pamoja na ujenzi wa vigawa maji **saba (7)** kwenye Skimu ya Igongwa iliyopo katika Halmashauri ya Misungwi yenye **hekta 300**.

**141. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu za Luiche (Kigoma Ujiji), Ibanda (Sengerema/Geita), Gidahababieg (Hanang’); pamoja na kufanya uchunguzi wa kitaalam (geotechnical investigations) katika bwawa la Lwanyo (Mbarali). Aidha, taratibu za kupata Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Skimu za Igenge (Misungwi) yenye **hekta 95** na Skimu ya Kirya (Mwanga) yenye **hekta 600** pamoja na Wataalam Washauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu katika Skimu za Lupiro (Ulanga), Mwamkulu (Mpanda Mji) na Muhongo (Ngara) zinaendelea. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imetenga **Shilingi bilioni 5** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya Itagata na Kongogo; Skimu **tano (5)** za Kirya, Nyamitita, Rudewa, Endagaw na Igenge; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu katika Skimu za Luiche, Ibanda, Gidahababierg

na bwawa la Lwanyo pamoja na kuanza upembuzi yakinifu na usanifu katika Skimu za Mwamkulu, Lupiro na Muhongo.

### 3.2.5.2 Mradi wa Kuendeleza Zao la Mpunga (Expanded Rice Productivity Project - ERPP)

**142. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza kilimo cha zao la mpunga, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imekamilisha usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye Skimu ya Msolwa Ujamaa yenye **hekta 270** na Skimu ya Njage yenye **hekta 175** katika Halmashauri ya Kilombero; Skimu ya Mvumi (Halmashauri ya Kilosa) yenye **hekta 293**; na Skimu za Kigugu (**hekta 480**) na Mbogo (**hekta 250**) zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Hadi mwezi Machi 2018, taarifa za usanifu wa skimu hizo zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali (*no objection*) cha kutangaza zabuni za ujenzi. Aidha, wakulima viongozi **50** wanaounda kamati za uendeshaji na utatuzi wa migogoro ya ndani na nje ya skimu walipatiwa mafunzo. Wakulima viongozi hao walitoka katika Skimu za Mbogo, Kigugu na Mvumi. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imetenga **Shilingi bilioni 7.26** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

### 3.2.5.3 Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (Small Scale Irrigation Development Project – SSIDP)

**143. Mheshimiwa Spika**, mradi wa *SSIDP* unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*). Lengo la mradi ni kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga kwenye skimu **119** za wakulima wadogo. Utekelezaji wa mradi huo umegawanywa katika makundi matatu (*three batches*) ambapo kundi la kwanza linahusisha skimu **45**, kundi la pili skimu **63** na kundi la tatu litahusisha skimu **11**. Hadi mwezi Machi 2018, ukarabati na ujenzi wa skimu za kundi la kwanza umekamilika. Vilevile, ujenzi na ukarabati wa skimu za kundi la pili unaendelea na umefikia **asilimia 79**. Utekelezaji wa mradi kwa kila skimu umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 10**. Aidha, mradi wa

SSIDP unahusisha kujenga uwezo wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambapo mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi umesainiwa na vifaa hivyo vinatarajiwa kukabidhiwa mwezi Juni 2018. Vifaa hivyo ni *bulldozer, Track Excavator, Wheel Loader, Vibrator Compact, Motor Grader, Low bed Loader, Mobile (Truck) Concrete Mixer, Water Bowser na Tipper Trucks*. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 8.9** kwa ajili ya utekelezaji wa skimu **11** za kundi la tatu la mradi. Skimu hizo ni Mwisa katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Nyida (Shinyanga), Katelantaba na Mbata (Busokelo), Mgambalenga (Kilolo), Mwalunili (Igunga), Ngongowele (Liwale), Nanganga (Ruangwa), Ngage (Simanjiro), Kituani Mwenzae na Kwemgiriti katika Halmashauri ya Lushoto.

#### **3.2.5.4 Programu ya Kukabiliana na Changamoto za Uhaba wa Chakula Duniani (Feed the Future)**

**144. Mheshimiwa Spika**, kupitia programu ya *Feed the Future*, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani inaendelea kuboresha miundombinu katika Skimu ya Dakawa (Mvomero) yenye **hekta 2000**. Mradi huo uligawanywa katika vipande **vinne (4)** na utekelezaji umefikia hatua mbalimbali. Utekelezaji wa kipande cha kwanza umekamilika na ulihusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa mita **800** kutoka barabara kuu ya Turiani kwenda kwenye pampu za kusukuma maji, kujenga nyumba mpya ya pampu na kuweka uzio kwenye eneo lenye nyumba za pampu; kipande cha pili kilihusu ununuzi na ufungaji wa pampu **6** ambapo zote zimenunuliwa na pampu **3** zimefungwa; kipande cha tatu kilihusu ujenzi wa nyumba mbili za ofisi, mfereji wa matupio wenye urefu wa kilomita **11.5** na kukarabati tuta la kuzuia mafuriko lenye urefu wa mita **360** ambapo utekelezaji wake umekamilika; na kipande cha nne kilihusu kukarabati barabara za mashambani zenye urefu wa kilomita **35** kwa kiwango cha changarawe, kujenga miundombinu ya mashambani zaidi ya **50**, kujenga mfereji mkuu kilomita **7.3** na kusakafia mifereji ya kati yenye jumla ya urefu wa kilomita **6.5**, kwa ujumla utekelezaji wa kazi za kipande cha nne umefikia asilimia **85**.

### 3.2.5.6 Mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji

**145. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo (*JICA*) inafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ili kubaini maeneo halisi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini. Chimbuko la mapitio ya mpango huo ni ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa matumizi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Mapitio hayo yanazingatia Mipango Shirikishi ya Maendeleo ya Rasilimali za Maji ambayo imeainisha kiasi cha maji kinachoweza kutumika katika umwagiliaji nchini. Vilevile, mapitio yatabaini hali halisi ya sekta ya umwagiliaji, maeneo na skimu za umwagiliaji zitakazoendelezwa ili kufikia lengo la **hekta milioni 1** ifikapo mwaka 2025. Aidha, mapitio ya mpango huo yatahusisha uandaaji wa mpango mkakati wa utekelezaji na mahitaji halisi ya gharama za uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa mtambuka katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2025. Utekelezaji wa mpango huo utaongeza kasi ya sekta ya umwagiliaji katika kuchangia kufikia nchi ya uchumi wa kati na “Tanzania ya Viwanda”.

### 3.2.5.6 Mradi wa Kujenga Uwezo katika Kuendeleza Umwagiliaji Nchini (Tanzania Capacity Building for Irrigation Development - TANCAID)

**146. Mheshimiwa Spika**, mradi wa *TANCAID* unahusu kujenga uwezo kwa Wataalam wa Kanda za Umwagiliaji, Halmashauri za Wilaya na Wakulima kwa kutumia Mwongozo Yakinifu wa Umwagiliaji (*Comprehensive Guidelines*). Hadi mwezi Machi 2018, Mwongozo huo umetafsiriwa katika lugha rahisi ili uweze kueleweka na kutumika kwa Wakulima. Vilevile, “*Standard Design Manual for Irrigation Canal and Rehabilitation Manual*”; “*Site Handbook Supervision Manual*”; pamoja na vitini vya mafunzo ya uendeshaji wa mafunzo ya skimu vinavyoendana na Mwongozo wa Umwagiliaji vimeandaliwa. Aidha, mafunzo kuhusu matumizi ya Mwongozo katika kuandaa, kuendesha na kusimamia skimu

za umwagiliaji yametolewa kwa wataalam **42** kutoka Kanda **saba (7)** za umwagiliaji na wataalam **14** kutoka Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Shinyanga, Manyoni, Simanjiro, Sikonge, Urambo na Manispaa ya Tabora.

### 3.2.6 Taasisi zilizo Chini ya Wizara

#### 3.2.6.1 Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji

**147. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji ni Taasisi iliyoanzishwa kwa lengo la kusaidia uwekezaji kwenye miradi ya utoaji wa huduma ya maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidakio vya maji, kipaumbele ikiwa ni kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa huduma ya maji hususan maji vijijini. Taasisi hiyo ina jukumu la kukusanya mapato, kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi yake.

**148. Mheshimiwa Spika**, pamoja na Sheria ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 kuainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya Mfuko, hadi sasa chanzo pekee kimeendelea kuwa tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya petroli. Fedha zinazopatikana kutoka chanzo hicho zimesaidia uwekezaji kwenye miradi ya kusambaza maji na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini.

**149. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2018, Mfuko umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 117.1** sawa na **asilimia 73.9** ya makadirio ya mapato kwa mwaka 2017/2018. Fedha hizo zimetumwa kwa watekelezaji mbalimbali wa miradi ya maji zikiwemo Halmashauri **106**, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira **36**; na miradi inayosimamiwa na Wizara ikiwemo ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya kimkakati. Lengo ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini pamoja na maeneo ya Miji Midogo na Miji Mkuu ya Wilaya. **Kiambatisho Na. 11** kinaonesha fedha zilizotumwa katika Halmashauri, Mamlaka za Maji na miradi inayosimamiwa na Wizara.



**150. Mheshimiwa Spika**, kiasi cha fedha kinachopatikana kutokana na tozo ya mafuta bado hakikidhi mahitaji ya uwekezaji kwenye miradi ya maji nchini. Mahitaji ya maji yameendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la watu pamoja na ongezeko la shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali zikiwemo uzalishaji viwandani, kilimo cha umwagiliaji, uchimbaji madini na uvuvi. Aidha, pamoja na ongezeko hilo la mahitaji, rasilimali za maji zimeendelea kupungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uharibifu wa mazingira unaochangia kukauka kwa vyanzo vya maji. Kutokana na hali hiyo na kwa kuzingatia kuwa sekta ya maji ni muhimu katika kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Tanzania ya Viwanda, upo umuhimu mkubwa wa kuongeza wigo wa mapato ya fedha za Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji ili kuongeza zaidi uwekezaji kwenye miradi ya maji pamoja na miradi ya kulinda na kutunza vyanzo vya maji.

### **3.2.6.2 Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)**

**151. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) una jukumu la kuchimba visima, kujenga mabwawa, kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na kuchunguza ubora wa udongo kwa ajili ya shughuli za ujenzi nchini. Hadi mwezi Machi 2018, Wakala umeendelea kutekeleza mikataba ya kuchimba visima virefu **225**, umekarabati visima **21** na kufunga pampu **6** za mkono na umeme na kufanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **195** kwa ajili ya uchimbaji wa visima. **Kiambatisho Na. 12** kinaonesha orodha ya visima vilivyochimbwa katika mwaka 2017/2018.

**152. Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika mwaka 2017/2018, Wakala umeendelea kutekeleza mikataba ya ujenzi wa mabwawa ya ujazo wa kati ya Mwamapalala, Sawida na Nhobola yaliyopo Wilayani Itilima; Dongobeshi (Mbulu); na bwawa la Mbangala lililopo Wilayani Songwe. Aidha, Wakala umeendelea kutoa ushauri wa kitaalam katika usanifu wa mabwawa ya Lukuledi, Chingulungulu na Mihima

yatakayojengwa katika Wilaya ya Masasi; kufanya uchunguzi wa udongo kwa ajili ya shughuli za ujenzi katika maeneo **6**; kujenga mfumo wa kusambaza maji katika maeneo **mawili (2)**; na kupima ubora wa mabomba ya kusambaza maji katika miradi **mitano (5)** kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*).

**153. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wakala umepanga kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **400**, kuchimba visima **400**, kukarabati visima **50**, kufunga pampu za maji **35**, kujenga bwawa la ujazo wa kati **1**, kujenga bwawa dogo **1**, kukarabati mabwawa ya ujazo wa kati **manne (4)**, kujenga mifumo ya kusambaza maji kwenye maeneo **manne (4)** na kufanya uchunguzi wa udongo kwa ajili ya shughuli za ujenzi katika maeneo **20**.

### **3.2.6.3 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA)**

**154. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ni Mamlaka ya udhibiti wa sekta kuu mbili za maji na nishati na ina majukumu ya kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao. Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake, *EWURA* imeimarisha Ofisi katika Kanda nne ambazo ni Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Kati (Dodoma) na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya).

**155. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2017/2018, kwa upande wa sekta ya maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini, ambapo ilitoa leseni **3** za kutoa huduma ya majisafi na majitaka kwa Mamlaka za Maji za Miji ya Chato, Mikumi na Maganzo. Vilevile, *EWURA* ilitathmini na kuidhinisha bei mpya za huduma ya maji kwa Mamlaka **saba (7)** kati ya maombi **tisa (9)** yaliyopokelewa. Mamlaka zilizoidhinishwa bei ni

Nansio, Biharamulo, Maganzo, Kishapu, Nzega, Tabora na Manyoni. Maombi ya bei za Mamlaka mbili za Mtwara na Lindi yanaendelea na taratibu za kupatiwa bei mpya. Aidha, *EWURA* iliidhinisha mikataba **17** ya huduma kwa mteja kwa Mamlaka za Maji za Ruangwa, MANAWASA, Bukoba, Kigoma, Karagwe, Ngara, *DAWASCO*, Babati, Dodoma, Tabora, Iringa, Sumbawanga, Shinyanga, Muleba, Geita, Bariadi na Lollondo na kupitisha Mipango ya Kibiashara kwa Mamlaka **17** za Majisafi na Usafi wa Mazingira.

**156. Mheshimiwa Spika**, *EWURA* ilikagua miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na majitaka katika Mamlaka **70** na kuzishauri kuhusu taratibu bora za uendeshaji, matengenezo, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu kwa huduma endelevu. Vilevile, *EWURA* ilifanya uhakiki wa ubora wa majisafi katika Mamlaka **60** na uhakiki wa ubora wa majitaka yanayotoka katika mabwawa ya kusafisha majitaka katika Mamlaka **10** ili kujiridhisha kama majitaka hayo yanakidhi viwango vya ubora unaokubalika kurudishwa kwenye mazingira. Aidha, *EWURA* imetoa taarifa za utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka 2016/17. Taarifa hizo husaidia Wizara pamoja na Wadau wa sekta ya maji katika kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

**157. Mheshimiwa Spika**, *EWURA* imeandaa Mwongozo na Kanuni za Kufanya Mapitio ya Bei na Tozo za Maji. Aidha, *EWURA* kwa kushirikiana na *GIZ* imeratibu uandaaji wa Mwongozo wa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma ya maji (*Water Sector PPP Guidelines*). Mwongozo huo unaelekeza jinsi Sekta ya Umma na Sekta Binafsi zinavyoweza kushirikiana katika kuboresha utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira ambapo Sekta Binafsi inaweza kuwekeza kwenye miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na uendeshaji.

**158. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ndogo ya umeme, *EWURA* iliendelea kupanua wigo wa utoaji huduma hiyo kwa kuidhinisha leseni **nne (4)** za muda mfupi kwa ajili

ya miradi ya kuzalisha umeme. Vilevile, *EWURA* ilitoa leseni **380** za ufungaji mifumo ya umeme. Katika kuhakikisha miundombinu ya umeme inajengwa na kuendeshwa katika ubora unaotakiwa ili kuweza kupunguza uwezakano wa kuleta madhara kwa watu, mali na mazingira, *EWURA* ilikagua miundombinu hiyo katika mikoa **12** ambapo mapendekezo ya kuboresha miundombinu iliyokaguliwa yaliwasilishwa kwa watoa huduma. Aidha, kwa upande wa Sekta Ndogo ya Gesi Asilia, *EWURA* imeendelea kukagua miundombinu ya kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia ili kubaini miundombinu hiyo inakuwa salama kwa matumizi na mazingira.

**159. Mheshimiwa Spika**, katika sekta ndogo ya mafuta, *EWURA* imeendelea kutoa leseni za biashara ya mafuta pamoja na kupanga bei kikomo za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa na kuendelea kupima ubora wa mafuta hayo, ili watumiaji waweze kutumia mafuta yaliyo bora na kwa bei ambayo imepangwa na *EWURA*. Hadi Machi 2018, *EWURA* imetoa leseni **1,467** kwa vituo vipya vya mafuta; leseni 124 za biashara ya kuagiza kwa jumla mafuta ya petroli; leseni **moja (1)** kwa kiwanda cha kusafisha mafuta ya petroli; leseni 28 za uagizaji na usambazaji wa jumla wa vilainishi (lubricants); leseni **tisa (9)** kwa viwanda vyenye miundombinu ya mafuta kwa ajili ya matumizi binafsi na leseni **tisa (9)** kwa ajili ya uagizaji na usambazaji wa gesi ya *LPG*. Katika mwaka 2018/2019, *EWURA* itahakikisha mtumiaji anauziwa mafuta yaliyo bora na kwa bei ambayo siyo zaidi ya bei kikomo.

**160. Mheshimiwa Spika**, *EWURA* itaendeleza ushirikiano wa karibu kwa kupokea na kutekeleza miongozo inayotolewa na Wizara zinazosimamia sekta za maji na nishati kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

#### 3.2.6.4 Chuo cha Maji

**161. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Maji ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa kwa lengo la kuendeleza na kutoa wataalam wanaohitajika katika sekta za maji na umwagiliaji. Wakala huo ulianzishwa mwaka 2008 kutokana na mabadiliko

yaliyotokea kwenye sekta ya umma ambayo yalilenga kuboresha utoaji wa huduma. Majukumu mengine ya Chuo ni kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kwa kuzingatia sera na miongozo ya sekta za maji na umwagiliaji pamoja na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi (NACTE).

**162. Mheshimiwa Spika**, Chuo hutoa mafunzo katika fani **tano (5)** kwa ngazi ya Stashahada na fani moja katika ngazi ya Shahada. Fani zitolewazo katika ngazi ya Stashahada ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*), Haidrolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*), Haidrojiolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*), Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*), pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*); na katika ngazi ya Shahada, Chuo kinatoa fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation Engineering*). Vilevile, Chuo hutoa mafunzo ya muda mfupi kulingana na matakwa ya wadau kwenye sekta za maji na umwagiliaji.

**163. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Chuo kilidahili wanafunzi 583 wa Stashahada na wanafunzi **167** wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji na kufanya jumla ya wanafunzi wote chuoni kufikia **2,027**. Kati ya hao wanafunzi **1,422** wako katika mafunzo ya ngazi ya Stashahada na wanafunzi **605** ni wa ngazi ya Shahada ya Kwanza.

Aidha, wanafunzi **248** wa Stashahada katika fani mbalimbali na wanafunzi **54** wa Shahada walihitimu mafunzo yao. Vilevile, Mfuko wa Mafundi Sanifu (*Water Technicians Fund*) ulifadhili jumla ya wanafunzi **105** na kati yao wanafunzi wa kike ni **49**. Hii imewezesha kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike Chuoni na kufikia **547** sawa na **asilimia 27** ya wanafunzi wote kutoka wanafunzi **489**, mwaka 2016/2017. Aidha, Chuo kinaendelea kufanya utafiti kuhusu upotevu wa maji katika mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa na uendelevu wa miradi ya maji vijijini (*Sustainability of rural water supply schemes*).

**164. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Chuo kimeboresha miundombinu mbalimbali ya kutolea taaluma ikiwemo ukarabati wa majengo **manne (4)** ya ofisi, pamoja na ununuzi wa vitabu mbalimbali 855 vya rejea na vifaa vya maabara ya udongo. Aidha, Chuo kimeboresha maktaba kwa kutengeneza chumba maalum chenye kompyuta kwa ajili ya huduma za kimtandao kwa wanafunzi ili kupanua zaidi wigo wao kitaaluma. Vilevile, Chuo kipo katika hatua za mwisho za kusaini mikataba kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara za haidrolojia, haidrojiolojia na uchimbaji wa visima ili kuboresha mazingira ya kufundishia.

**165. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2018, Chuo kina watumishi 89 na kati ya hao watumishi **60** ni wakufunzi na **29** wanahusika na masuala ya utawala. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya watumishi **23** waliendelea na mafunzo ya muda mrefu ambapo kati ya hao **13** wako katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*), **saba (7)** ni wa Shahada ya Uzamili na watumishi **watatu (3)** wapo katika mafunzo ya Shahada ya Kwanza. Vilevile, watumishi **wanne (4)** wamehitimu masomo yao ambapo waliohitimu katika Shahada za uzamivu ni mtumishi **mmoja (1)**; uzamili **(2)** na Shahada ya **Kwanza (1)**. Pia, watumishi **28** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali.

**166. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019 Chuo kina lengo la kudahili wanafunzi **1,000**; kukarabati majengo ikiwemo madarasa, karakana za mafunzo na nyumba za wafanyakazi; kununua vifaa vya kufundishia katika maabara na vitabu mbalimbali vya rejea. Vilevile, Chuo kitaendelea kufanya tafiti mbalimbali, kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

### **3.2.7 Masuala Mtambuka**

#### **3.2.7.1. Sheria**

**167. Mheshimiwa Spika**, katika kukidhi mahitaji ya kissekta, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya Sheria zake

pamoja na kutoa elimu ya Sheria za Maji na Umwagiliaji na kanuni zake kwa wadau mbalimbali ambao ni Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji na jamii kwa ujumla. Elimu hiyo hutolewa kupitia vyombo vya habari, warsha, mikutano, semina, mafunzo na makongamano. Hadi mwezi Machi 2018, Wizara imekamilisha uandaaji wa marekebisho madogo (*miscellaneous amendments*) kwenye kifungu cha **6** cha Sheria ya DAWASA **Na. 20** ya mwaka 2001 kinachohusu majukumu ya DAWASA na kupitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 12/09/2017.

**168. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mfumo na kuongeza ufanisi kwenye usimamizi wa rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji, Wizara imekamilisha kuandaa *Order 6* na *Notice 3* ambazo ni *Water Resources Management (Mbwinji Catchment) Order, 2017; Water Resources Management (Momba Catchment) Order, 2017; Water Resources Management (Katuma Catchment) Order, 2017; Water Resources Management (Luiche-Muze Catchment) Order, 2017; Water Resources Management (Rungwa Catchment) Order, 2017; Water Resources Management (Songwe Catchment) Order, 2017; Water Supply and Sanitation (Mbeya Urban Water Supply and Sanitation Authority)(Extension of Service Area) Notice, 2017; Water Supply and Sanitation (Establishment of Chato Water Supply and Sanitation Authority) Notice, 2017; na Water Supply and Sanitation (Establishment of Mbambabay, Madaba, Newala, Tandahimba, Mahuta na Nanyamba Water Supply and Sanitation Authorities) Notice, 2017.*

**169. Mheshimiwa Spika**, vilevile, rasimu za Kanuni **9** zimeandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio na ushauri wa kisheria kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kutumika. Kanuni hizo ni *Water Resources Management (Water Resources Classification System) Regulations, 2017; Water Resources Management (Control and Management of Storm Water) Water Resources Management (Control And Management of Storm Water) Regulations, 2017; Transfer of Water Use, Discharge and Groundwater Permits Regulations,*

2017; *Water Resources Management (Water Well Quality Monitoring) Regulations, 2017; Water Supply and Sanitation (Licensing Board) Regulations, 2017; Water Supply and Sanitation (Water Bowser Services) Regulations, 2017; DAWASA (Water Bowser Services) Regulations, 2017; Water Supply and Sanitation (Provision and Management of Sewage and Wastewater Services) Regulations, 2017; na Water Supply and Sanitation (Delegation of Powers to Local Government Authorities) Notice, 2017.* Aidha, maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusu maboresho ya Kanuni **2** zinazohusiana na Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji za mwaka 2013 (*The National Water Investment Fund Regulations*) pamoja na *Water Supply and Sanitation (Declaration and Establishment of Water Quality Laboratories) Regulations, 2018* yamekusanywa na yanaendelea kufanyiwa kazi kabla ya kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio (*vetting*), ushauri wa kisheria na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**170. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018 Wizara imeandaa rasimu ya mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** ya mwaka 2009; Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 na Sheria ya DAWASA **Na. 20** ya mwaka 2001. Vilevile, Wizara imeendelea kupitia na kutoa maoni ya kitaalam kwenye Mikataba na Randama za Makubaliano (*Conventions and Protocols*) zinazohusu majishirikishi. Hadi mwezi Machi 2018, Mikataba na Randama za Makubaliano 136 zimepitiwa na kutolewa maoni. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefuatilia na kusimamia mashauri 25 yaliyopo mahakamani na kwenye Baraza la Usuluhishi na Uamuzi ambapo mashauri **matano (5)** kati ya hayo yametolewa uamuzi.

**171. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019 Wizara itaendelea na utayarishaji wa Kanuni za Sheria za Maji na Umwagiliaji na kuziboresha zilizopo ili kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hizo. Vilevile, itaendelea kutoa ushauri wa kisheria na miongozo kwa wadau wa Sekta za Maji na Umwagiliaji pamoja na kukamilisha mchakato wa



marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** ya mwaka 2009, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009, Sheria ya DAWASA **Na. 20** ya mwaka 2001 na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji **Na. 5** ya mwaka 2013 ili kuboresha huduma za maji na umwagiliaji nchini.

### 3.2.7.2 Maendeleo ya Rasilimali Watu

**172. Mheshimiwa Spika**, katika kuwajengea uwezo watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwapatia mafunzo katika fani na nyanja mbalimbali. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya watumishi **67** wamepata mafunzo ya ndani na nje ya nchi ambapo watumishi **30** walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi **37** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, mafunzo kuhusu utawala na uongozi yalitolewa kwa viongozi **43** wa Wizara. Aidha, Wizara ilipata kibali cha kuajiri watumishi **154**, kati ya hao Wahandisi ni **43**, Mafundi Sanifu Daraja la II (**52**), Mafundi Sanifu Wasaidizi (**48**) na Watumishi wa Fani Mtambuka (**11**). Hadi mwezi Machi 2018, watumishi **106** walijajiriwa, kati ya hao Wahandisi **43**, Mafundi Sanifu **52**, Mchumi **mmoja (1)**, Mtakwimu (**1**), Afisa Maendeleo ya Jamii (**1**) na Maderewa **wanane (8)** wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi. Wizara inaendelea kufuatilia mabadiliko ya kibali cha Mafundi Sanifu Wasaidizi **48** ili kuweza kuajiri Mafundi Sanifu Daraja la II ambao ndio wanaohitajika kwa wingi. Kwa upande wa Sekta ya Umwagiliaji, watumishi **34** wameajiriwa na kupangiwa kazi kwenye Ofisi za Kanda za Umwagiliaji na Makao Makuu.

**173. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilipokea lkama ya watumishi **1,522** kati ya hizo, ajira mpya zilizoidhinishwa ni **148**, nafasi **nne (4)** za uteuzi, nafasi **17** za uhamisho, nafasi 17 za kubadili vyeo na nafasi **293** za kupandisha watumishi vyeo. Hadi mwezi Machi 2018, watumishi **43** kati ya **293** wamepandishwa vyeo na taratibu za kuwapandisha waliobaki zinaendelea. Aidha, watumishi **78** wameondoka kazini kutokana na sababu mbalimbali

ikiwemo kustaafu, kufariki, kuacha kazi na wengine kuondolewa kazini kutokana na utoro pamoja na vyeti vya kughushi. Wizara imewasilisha maombi ya kuajiri kwenye Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

### 3.2.7.3 Mapambano Dhidi ya Rushwa

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maelekezo kutoka Ofisi ya Rais Ikulu na kwa mujibu wa mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan - NACSAP III*) kuhusu mapambano dhidi ya rushwa katika Wizara na Taasisi zake, Wizara imeunda Kamati ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Kamati ya Uadilifu. Kamati hizo zimeandaa mipango kazi na kuiwasilisha Ofisi ya Rais Ikulu Kitengo cha Uratibu cha Utawala Bora. Vilevile, Wizara imefanya mapitio na kuboresha Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa mwaka 2012 kwa kuzingatia mabadiliko ya kitaasisi yaliyojitokeza katika Serikali.

### 3.2.7.4 UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY)

**174. Mheshimiwa Spika**, elimu kuhusu afya hususan kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza imetolewa kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Hadi mwezi Machi 2018, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi **sita (6)** waliotoa taarifa za kuathirika na magonjwa hayo, kwa kutoa posho maalumu ya chakula ili kuhakikisha wanapata lishe bora. Vilevile, Wizara imeendelea kufuatilia afya za watumishi hao kwa kuzingatia kazi wanazopangiwa kulingana na afya zao ili kutekeleza Mwongozo wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza.

### 3.2.7.5 Jinsia

**Mheshimiwa Spika**, suala la jinsia huzingatiwa katika uteuzi wa viongozi wa ngazi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zake kulingana na mpango wa kurithishana madaraka. Vilevile, uteuzi wa kamati na vikosi kazi mbalimbali huzingatia jinsia

ili kuhakikisha watumishi wote wanashiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao bila kujali jinsia zao. Aidha, Wizara inaandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Masuala ya Jinsia (*Gender Implementation Strategy*) kwa sekta ya maji ambao utatekelezwa na Wizara, Ofisi za Bonde, Mamlaka za Maji Mijini pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

#### 4.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

**175. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2017/2018, Wizara ilikabili na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji. Changamoto zilizojitokeza na hatua zinazochukuliwa kuzikabili ni kama ifuatavyo:-

##### 4.1 Uwekezaji mdogo kwenye miundombinu ya maji na umwagiliaji

**176. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha huduma za maji na umwagiliaji kwa kuwekeza katika miundombinu ya huduma hizo. Hata hivyo, kasi ya uwekezaji huo ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya huduma hizo katika Sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Sababu zilizochangia uwekezaji mdogo na hatua zinazochukuliwa ni kama ifuatavyo: -

##### (a) Upatikanaji Mdogo wa Fedha Kulinganisha na Bajeti

**177. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilikasimiwa jumla ya **Shilingi 643,710,160,202** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye sekta za maji na umwagiliaji. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 623,606,748,052** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa upande wa sekta ya maji na **Shilingi 20,103,412,150** kwa sekta ya umwagiliaji. Hadi mwezi Machi, 2018 jumla ya **Shilingi 349,968,825,172** sawa na **asilimia 54.37** ya bajeti ya maendeleo ya Wizara zimetolewa na kati ya fedha hizo, **Shilingi 347,500,300,527** sawa na **asilimia 56** zilitolewa kwa sekta ya maji na **Shilingi 2,468,524,64** sawa na

**asilimia 52.45** zilitolewa kwa sekta ya umwagiliaji. Hali hiyo imechangia kupungua kwa uwekezaji kwenye sekta hizo.

**178. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji zikiwemo kuwashawishi Washirika wa Maendeleo ambao wanaonesha nia ya kusaidia uwekezaji katika sekta za maji na umwagiliaji; kuendelea kushawishi sekta binafsi kushiriki katika kutekeleza miradi ya maji na umwagiliaji kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; pamoja na kuendelea kubuni vyanzo vipya vya fedha.

**(b) Ushiriki Mdogo wa Sekta Binafsi katika Uwekezaji kwenye Sekta za Maji na Umwagiliaji**

**179. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya kuboresha huduma za maji na umwagiliaji, mchango wa sekta binafsi kwenye uwekezaji katika kutoa huduma hizo bado si wa kuridhisha. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2009 na Sheria ya Ubia ya mwaka 2010 na Kanuni zake ili kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji. Vilevile, Wizara imeendelea kuwapatia wataalam wake mafunzo yanayohusu uwekezaji ikiwa ni pamoja na ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna ya kutekeleza miradi ya ubia.

**4.2 Kupungua kwa rasilimali za maji**

**180. Mheshimiwa Spika**, rasilimali za maji zimeendelea kupungua siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya tabianchi, uvamizi katika vyanzo vya maji, uchafuzi wa vyanzo vya maji na matumizi holela ya maji. Kupungua kwa rasilimali hiyo, kumeathiri shughuli za kijamii na kiuchumi na kusababisha migogoro kwenye vyanzo vya maji.

**181. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza na kusimamia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira. Kupitia nyenzo hizo, ukaguzi wa mara kwa mara hufanyika katika vyanzo vya maji, maeneo ya viwanda, migodi na mabwawa ya kutibu majitaka ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa na kuhifadhiwa na kuhakikisha utupaji wa majitaka unazingatia viwango vinavyotakiwa kisheria. Vilevile, Wizara inaendelea kuvitambua vyanzo vya maji, kuviwekea mipaka na kuvitangaza kuwa maeneo tengefu. Aidha, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Halmashauri, Jumuiya za Watumiaji Maji na Wadau wengine imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

**182. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa kutekeleza mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; kushirikiana na wadau mbalimbali katika kufanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana na athari zake; kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji, na kuhamasisha matumizi ya utaalim asilia (*Indigenous knowledge*) katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

#### **4.3 Upungufu wa Wataalam katika Sekta za Maji na Umwagiliaji**

**183. Mheshimiwa Spika**, sekta za maji na umwagiliaji zinakabiliwa na upungufu wa wataalam kutokana na baadhi yao kufariki, kustaafu, kuacha kazi na wataalam wengine kuachishwa kazi kutokana na sababu mbalimbali. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupata kibali cha kuajiri wataalam watakaokidhi mahitaji ya sekta za maji na umwagiliaji. Aidha, Wizara imeendelea kuwasiliana na Taasisi mbalimbali za elimu ya juu kwa ajili ya uanzishwaji wa fani zinazohusu maji

na umwagiliaji ili kuongeza idadi ya wataalam katika fani hizo.

#### 4.4 Uharibifu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji

**184. Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na hujuma za kuharibu miundombinu ya maji na umwagiliaji hali inayoathiri upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka na huduma za uhakika za umwagiliaji kwa wakulima. Hujuma hizo hufanywa na wananchi wasio waaminifu kupitia biashara ya chuma chakavu pamoja na wanaoharibu kwa makusudi miundombinu ya miradi ambayo imechelewa kukamilika.

**185. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Ofisi za Kanda za Umwagiliaji na Wahandisi wa Halmashauri wameendelea kushirikiana na uongozi wa Mikoa, Wilaya, Jeshi la Polisi pamoja na wananchi ili kubaini wananchi wanaojihusisha na hujuma hizo na kuchukua hatua stahiki pamoja na kutoa zawadi kwa watoa taarifa. Aidha, Wizara imeendelea kuzifanyia marekebisho Sheria za Maji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wahujumu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi shirikishi katika kulinda na kutunza miundombinu ya maji na umwagiliaji kupitia vipeperushi, maonesho na maigizo kwenye sherehe mbalimbali za kitaifa pamoja na vipindi kwenye runinga na radio.

#### 4.5 Kiwango kikubwa cha upotevu wa maji

**186. Mheshimiwa Spika**, sekta ya maji inakabiliwa na changamoto ya upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu iliyojengwa miaka mingi iliyopita, wizi wa maji kwa wateja wasiokuwa waaminifu kujipatia huduma ya maji kinyume na taratibu (*by-pass, and illegal connection*) pamoja na udanganyifu wa wateja kwa kuchezea dira za maji ili zisitoe taarifa sahihi za matumizi ya maji. Hadi mwezi Machi 2018, upotevu wa maji ni **asilimia 38** kwa *DAWASCO*

na wastani wa **asilimia 33** kwa Mamlaka za Maji zilizopo katika Miji Mikuu ya Mikoa, Wilaya, Miji Midogo pamoja na miradi ya Kitaifa. Viwango hivyo vya upotevu wa maji ni vikubwa ukilinganisha na kiwango kinachokubalika kimataifa cha **asilimia 20**. Hali hiyo inaathiri shughuli za uendeshaji katika Mamlaka hizo kutokana na upotevu wa mapato. Upotevu huo wa maji umeisababishia *DAWASCO* kupoteza wastani wa **Shilingi bilioni 2.5** kwa mwezi na Mamlaka nyingine kwa pamoja zimepoteza jumla ya **Shilingi bilioni 1.58** kwa mwezi.

**187. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kuwekeza kwenye miundombinu ya majisafi, ukarabati wa miundombinu chakavu, kuhakikisha wateja wote wanafungiwa dira za maji na kuzielekeza Mamlaka kuwa na mikakati ya kupunguza upotevu wa maji hadi kufikia **asilimia 20**. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji na umwagiliaji pamoja na kurekebisha Sheria za Maji na Umwagiliaji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji.

#### **4.6 Madeni makubwa ya ankara za maji kwa Taasisi za Serikali**

**188. Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu sasa, Taasisi na Idara za Serikali zimekuwa zikipata huduma ya maji bila kulipia gharama ya huduma hiyo kwa wakati na hivyo kulimbikiza madeni makubwa ya Ankara za matumizi ya maji. Hali hiyo, imesababisha Mamlaka za Maji nchini kushindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi ya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya maji. Hadi mwezi Machi 2018, madeni ya Ankara za maji kwa Taasisi za Serikali yalifikia **Shilingi bilioni 39**.

**189. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imewasilisha Wizara ya Fedha na Mipango orodha ya madeni ya ankara za maji za Taasisi na

Idara za Serikali ili madeni hayo yalipwe moja kwa moja kutoka HAZINA kwenda kwa Mamlaka za Maji husika. Vilevile, Wizara imeendelea kuziagiza Mamlaka za Maji kuanza kutumia dira za maji za mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*prepaid meters*) kwa lengo la kupunguza tatizo la malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji. Hadi mwezi Machi 2018, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Iringa, Songea, Dodoma, Tanga, Mbeya na Tabora zimeanza kutumia dira hizo na kuonesha mafanikio makubwa. Aidha, Mamlaka za Moshi na Mwanza zinaendelea na taratibu za kufunga dira hizo.

#### **4.7 Miradi ya maji na skimu za umwagiliaji kutokuwa endelevu**

**190. Mheshimiwa Spika**, miradi ya maji na umwagiliaji imekuwa na changamoto ya kutokuwa endelevu kutokana na Vyombo vya Watumia Maji na Vyama vya Wamwagiliaji kuwa na uwezo mdogo wa kusimamia miradi. Changamoto kubwa ipo katika ukusanyaji na usimamizi wa maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji pamoja na michango kwa ajili ya matumizi ya miundombinu ya umwagiliaji. Vilevile, uwepo wa migogoro katika matumizi ya maji kwenye vyanzo vya maji na miundombinu ya umwagiliaji baina ya watumiaji wa maji katika baadhi ya maeneo imeathiri upatikanaji wa huduma za maji na umwagiliaji.

**191. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kuunda na kuviimarisha Vyombo vya Watumiaji Maji (*COWSOs*) na Vyama vya Wamwagiliaji ili vyombo hivyo viweze kusimamia na kuendesha miradi ya maji na Skimu za umwagiliaji mtawalia. Vilevile, Wizara itaandaa mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa miradi ili miradi hiyo iwe endelevu pamoja na kuajiri wataalam wa kutosha wa Sekta za maji na umwagiliaji katika ngazi za Halmashauri za Wilaya. Aidha, Wizara ipo katika taratibu za kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini (*Rural Water Agency-RuWA*) ili kuhakikisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini inaboreshwa na kuwa endelevu.



## 5.0 SHUKRANI

**192. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyofikiwa katika kuendeleza sekta za maji na umwagiliaji yanatokana na michango inayoendelea kutolewa na wadau mbalimbali, hivyo napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia na kutuwezesha kufanikisha majukumu ya sekta hizo. Naamini kuwa mafanikio yaliyopatikana ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya kimataifa, Taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na Taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru nchi rafiki zikewemo Korea Kusini, China, Uingereza, Marekani, Ujerumani, Japan, Uholanzi, Hispania, Ubelgiji, Ufaransa, India na Misri.

**193. Mheshimiwa Spika**, vilevile, natoa shukrani kwa Taasisi za fedha za kimataifa na mashirika ya kimaendeleo kwa misaada ya fedha na ushirikiano wa kitaalam katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara. Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank-WB*), Benki ya Maendeleo ya *Africa (AfDB)*, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*), *Global Environment Facility (GEF)*, na *Green Climate Fund*.

**194. Mheshimiwa Spika**, Mashirika na Taasisi za Kidini yameendelea kuongeza hamasa katika kuyafikia malengo tuliyojiwekea. Hivyo, napenda kuyashukuru mashirika na Taasisi hizo ambazo ni *Catholic Agency for Overseas Aid and*

*Development (CARITAS), Adventist Development Relief Agency (ADRA), Norwegian Church Aid, Livingwater International, World Islamic League, Shirika la Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.*

Vilevile, nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali katika kuendeleza sekta za maji na umwagiliaji. Taasisi hizo ni pamoja na *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET); Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS), Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (WAMMA); WaterAid; World Vision; World Wide Fund for Nature (WWF); Water Resources Integration Development Initiatives (WARIDI) Netherlands Volunteers Services (SNV); Plan International; Concern Worldwide; Water Mission (T), Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (IUCM); African Medical Research Foundation (AMREF); Clinton HIV Aids Initiative; na Bill and Melinda Gates Foundation.*

**195. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb), Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji; Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Katibu Mkuu; Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelo, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji yanatimizwa.

Vilevile, naishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na msaada wao katika kipindi chote na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Aidha, ninayo furaha kubwa kuendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Katavi kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019

**196. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 727,345,768,677** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2018/2019, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

### (a) Fungu 49

**197. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, jumla ya **Shilingi 697,577,902,677** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya sekta ya maji. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 24,363,869,000** ambapo **Shilingi 6,266,714,000** sawa na **asilimia 26** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 18,097,155,000** sawa na **asilimia 74** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 673,214,033,677** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 443,214,034,677** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani na **Shilingi 229,999,999,000** sawa na **asilimia 34** ni fedha za nje.

### (b) Fungu 05

**198. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019 jumla ya **Shilingi 29,767,866,000** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya sekta ya umwagiliaji.

Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 3,947,408,000** ambapo **Shilingi 585,184,000** sawa na **asilimia 14.82** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 3,362,224,000** sawa na **asilimia 85.18** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 25,820,458,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 23.20** ni fedha za ndani na **Shilingi 19,820,458,000** sawa na **asilimia 76.80** ni fedha za nje.

**199. Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz).

**200. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. *(Makofi)*

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa afya ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji. Pia naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa ushirikiano wanaonipa katika kuongoza Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yetu ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard* kama ilivyo kwenye vitabu vya maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha

2017/2018 pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa madhumuni ya taarifa hii, Wizara ya Maji ina mafungu mawili ambayo ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji – Fungu 49 na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inafafanua mambo matano yafuatayo:-

Kwanza, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

Pili, mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

Tatu, mapitio ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

Nne, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na

Tano, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo yatakayotolewa ni matokeo ya mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, mahojiano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti

ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani matano kama yalivyoainishwa kwenye vitabu vyako vya kamati mlivyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa kikamilifu hususan kwenye ushauri uliohusu utoaji wa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge, kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na kuongeza Tozo kwenye mauzo ya mafuta ya dizeli na petroli kutoka shilingi hamsinihadi shilingi mia kwa lita ili kutunisha Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotekelezwa kwa ushauri wa Kamati kikamilifu kumepelekea athari katika sekta. Kwa mfano: kutoongezwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na diseli kutoka shilingi hamsini hadi shilingi mia moja kunaathiri ufanisi wa Mfuko wa Maji na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maji na hususan kwa maeneo ya vijijini. Pendekezo la kuongeza tozo kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli sio tu ni ushauri wa Kamati, pia ni agizo la Bunge lako Tukufu lililopitishwa kupitia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa katika Bunge lako tukufu Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inataka uamuzi wa agizo hili la Bunge lako Tukufu litekelezwa kutokana na kuridhika na mafanikio yaliyofikiwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ambapo asilimia 66 ya pesa zilizopatikana na kutumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo maji vijijini zilitokana na makusanyo ya Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka fedha 2017/2018 yalijielekeza katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopelekwa na kutumika na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka fedha 2017/2018 Wizara ya Maji na Umwagiliaji - Fungu 49 liliidhinishwa jumla ya shilingi 24,457,459,705; kati ya fedha hizo shilingi

6,636,518,705 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 17,820,941,000 ni mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi 623,606,748,052 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 408,617,643,052 sawa na asilimia 66 ni fedha za ndani ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 158,500,000,000 ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na shilingi 250,117,643,052 ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, shilingi 214,989,105,000 sawa na asilimia 34 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka fedha 2017/2018 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 24,158,893,232 kati ya fedha hizo shilingi 4,055,481,082 ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 585,184,082 ni fedha kwa ajili ya mishahara na shilingi 3,407,297,000 ni fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 20,103,412,150 kati ya hizo shilingi 5,600,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 14,503,412,150 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 Wizara ya Maji na Umwahiliaji - Fungu 49 lilikuwa limepokea fedha za matumizi mengineyo shilingi 2,939,365,387 sawa na asilimia 44 na mishahara shilingi 9,990,540,556 sawa na asilimia 55 ya kiasi kilichoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2018 zilikuwa shilingi 135,191,256,566 sawa na asilimia 22 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05 ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 483,040,684 kwa ajili ya matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 83 na shilingi 2,155,941,880 sawa na asilimia 62 zilitolewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi 2,468,524,644.66 zilitolewa ambazo ni sawa na asilimia 12 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji - Fungu 49 zilizotolewa ni

asilimia 42 tu ya mwaka huu. Mwenendo huu ni wa kusikitisha na hasa ukizingatia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa sehemu kubwa ni miradi ya maji. Mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa muda mrefu, ndiyo maana Bunge liliazimia Serikali kuongeza shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli ili kutunisha Mfuko wa Maji ambapo ni chanzo cha fedha cha uhakika na umeonesha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maji. Hata hivyo, azimio hili la Bunge halijatekelezwa hadi Kamati inapowasilisha taarifa hii na hakuna taarifa yoyote kutoka Serikalini kuelezea ni sababu zipi zilizopelekea azimio hili kutotekelezwa. Hii ni dharau kubwa kwa Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maduhuli, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 4,735,005,000. Hadi kufikia Machi, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 3,276,849,518 ambayo ni sawa na asilimia 69 ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo hata. Hivyo, Kamati inahimiza Wizara kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 99(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika miradi ya Mkoa wa Kigoma. Miradi iliyokaguliwa ni:-

(1) Mradi Namba 306 wa Maji Safi na wa Mazingira Kigoma, Ujiji *(KUWASA)*;

(2) Mradi wa Maji katika Kijiji cha Kagera Mkoani Kigoma;



(3) Mradi wa Maji wa Kalinzi;

(4) Mradi wa uendelezaji wa Bonde la Mto Luiche; na

(5) Mradi wa Majitaka Luiche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya ukaguzi wa miradi hiyo, imeainishwa katika Taarifa ya Kamati kuanzia ukurasa wa nane hadi ukurasa wa 13 ambapo maoni ya kila mradi yamefafanuliwa kwa kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa hii napenda kuwasilisha maoni ya jumla kuhusu ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha, Kamati imebaini miradi mingi ya maendeleo haikamiliki kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali kama vile:-

(1) Ucheleweshaji wa fedha kutoka Hazina kunaathiri utekelezaji wa miradi;

(2) Uwezo mdogo wa kandarasi;

(3) Makosa ya usanifu wa mradi hatua za mwanzo;

(4) Kukosekana kwa usimamizi madhubuti na makini kutoka kwa wataalam wa Serikali; na

(5) Kukosekana uwajibikaji wa pamoja wa ushirikiano miongoni mwa taasisi za mamlaka za Serikali. Kwa mfano, katika Mradi wa Maji wa Kalinzi Kamati ilibaini mkandarasi alikuwa hajamaliza ujenzi wa mradi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa umeme wa kutosha kwa ajili ya kuwashia *pump*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa wakati kumekuwa na madhara mbalimbali kwa Serikali na wananchi. Madhara hayo ni pamoja na moja,

kuongeza gharama za mradi; pili, kuanza kuchakaa kwa baadhi ya miundo kabla ya mradi kuanza kutumika na tatu, kuwakosesha na kuwachelewesha wananchi kupata huduma iliyokusudiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kamati ilipata nafasi ya kuchambua kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Taasisi zilizopo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilichambua mipango ya bajeti kwa mafungu mawili; Fungu Namba 49 na Fungu Namba 05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 5 linahusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambapo pamoja na majukumu mengine Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina jukumu la kuhakikisha Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inatekelezwa kwa vitendo. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 29,767,866,000; kati ya fedha hizo shilingi 3,947,408,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 25,820,458,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazoombwa zinakusudiwa kutumika kutekeleza kazi mbalimbali. Kimsingi fedha zinazoombwa kwa ajili ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na mambo mengine zitawezesha kujenga na kuboresha *scheme* ya umwagiliaji ili kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kutekelezwa kwenye eneo la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambapo mpaka sasa hekta zilizokwoshatumika ni hekta 466,338 ambayo ni sawa na 1.6% ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji, ndilo linalomwagiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa, pamoja na eneo dogo linalotumika kwa umwagiliaji na uzalishaji wa tija, imejionesha katika skimu ya umwagiliaji zilizoboreshwa kwa mazao yafuatayo; zao la mpunga uzalishaji umeongezeka kutoka tani nne mpaka tani tano kwa hekta kufikia tani 10 mpaka tani 12; zao la mahindi

uzalishaji umeongezeka kutoka tani 1.5 mpaka tani tano kwa hekta na zao la vitunguu kutoka tani 13 mpaka 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ili Wizara iweze kutekeleza azma ya Serikali, Serikali inapaswa kuiwezesha Tume ya Umwagiliaji kwa kutenga angalau shilingi trilioni tatu kila mwaka. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeidhinishiwa takribani shilingi bilioni 25 tu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha hizo ni sawa na 0.85% ya mahitaji. Tathmini ya Kamati imebaini pia, endapo Serikali itaendelea kuitengea Tume ya Taifa ya Umwagiliaji fedha kidogo kiasi hiki ikilinganishwa na mahitaji halisi ni wazi kuwa azma ya Serikali kuendeleza eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, labda hekta 100,000 itafikia mwaka 2025, haitafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu Namba 49 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 24,366,869,000 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,266,414,000 sawa na asilimia 26 ni kwa ajili ya gharama ya matumizi ya kawaida (*other charges*) na shilingi 18,097,155,000 sawa na asilimia 74 ni kwa ajili ya kulipa mishahara. Ili kutekeleza kazi zilizopangwa kwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 673,214,033,677. Kati ya fedha hizo, shilingi 443,214,034,677 sawa na asilimia 66 ni fedha za ndani na shilingi 229,999,000,000 sawa na asilimia 34 ni fedha za nje. Aidha, fedha nyingine za nje ni shilingi 96,405,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha, Wizara ya Maji na Umwagiliaji imepanga kukusanya shilingi 631,000,000 itakazozipata kutokana na makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2018/2019, maelezo ya ufafanuzi kuhusu maoni na ushauri wa Kamati yameelezwa kwa kirefu kuanzia ukurasa wa 25 hadi ukurasa wa 40 katika taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwenye maeneo nane, kama ifuatavyo:-

Moja, mtiririko usioridhisha wa fedha za Mmiradi ya maendeleo. Mwenendo usioridhisha wa utoaji fedha za miradi ya maendeleo umeendelea kuwa tatizo la kudumu katika sekta ya maji na umwagiliaji. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2017/ 2018 fedha ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na Bunge lako tukufu na kutolewa na Serikali kwa Fungu Namba 49 ni asilimia 16.8 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na asilimia 22 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa Fungu Namba 05 ni asilimia 8.4 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na asilimia 12 kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kiasi kidogo cha ongezeko la fedha kwa miradi ya maendeleo, kiasi cha kutokidhi kabisa mahitaji ya fedha zilizotolewa kwa kipindi tajwa, hazifiki hata nusu ya bajeti ya mwaka. Hivyo kwa sababu ya kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya maji na hivyo kuwanyima wananchi fursa ya kupata huduma ya maji safi na salama. Takwimu zinaonesha kuwa hadi Desemba, 2017 hali ya upatikanaji maji safi na salama kitaifa ni wastani wa asilimia 56 kwa vijijini na asilimia 69 kwa mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu usioridhisha unakwamisha kufikia kwa malengo ya upatikanaji maji safi na salama kufikia asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2021 kama ilivyoaidhinishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 hadi 2020/2021). Kamati inaishauri Serikali kutekeleza azma ya kuwapatia wananchi wote huduma ya majisafi kwa gharama nafuu na

kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kadri zilinavyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Pili, umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo; tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa ipo tija kubwa katika uzalishaji wa mazao kupitia kilimo cha umwagiliaji ikilinganishwa na kilimo cha kutegemea mvua ambapo kimeathiriwa na uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na tija inayojidhihirisha kwenye kilimo cha umwagiliaji, bado Serikali haijalipa suala la kilimo cha umwagiliaji msukumo stahiki kutokana na ukweli kwamba hekta 461,326 sawa na asilimia 1.6 tu ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ndilo linalotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwe na kilimo chenye tija, kuongeza uzalishaji wa malighafi za viwanda pamoja na utoshelezi wa chakula nchini, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili iweze kutekeleza Mipango kabambe ya Kitaifa ya Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan 2015*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuwathibitisha watendaji wa juu wa Tume ambao wengi wanakaimu nafasi hizo walizonazo kwa muda mrefu, hivyo kukosa uthubutu wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, Tume inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi ikilinganishwa na mahitaji halisi, hivyo Kamati inashauri tathimini ifanyike kubaini mahitaji halisi na kupatiwa vibali vya kuajiri kulingana na mahitaji.

Tatu, kuongeza tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na dizeli kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Maji ulikusanya shilingi bilioni 158 fedha ambayo imetumika ipasavyo na kuonesha mafanikio kwenye miradi ya maji vijijini. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa dhati kwa namna ambavyo imefanikisha miradi ya maji vijijini kupitia fedha za Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo na mafanikio yaliyofikiwa Kamati inaamini endapo Serikali itatekeleza azimio la Bunge lako Tukufu lililopitishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 la kuongeza tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na dizeli kutoka shilingi 50 hadi kufikia shilingi 100 fedha ambayo ingekusanywa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ingekuwa mara mbili ya fedha zilizokusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2018/2019 na 2019/2020 makusanyo yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 316 hatua ambayo itaongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini na hivyo kuiwezesha Serikali kufanikiwa lengo lake la kufikisha maji vijijini kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2020/2021 sambamba na adhima ya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza kwa dhati uamuzi wa Serikali kuunganisha *DAWASA* na *DAWASCO*. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na Wizara kushindwa kuwasilisha taarifa mabalimbali zinazoombwa na Kamati kwa lengo la kutoa ushauri na kuboresha. Kamati ilitaka kufahamu kabla ya kuunganisha *DAWASA* na *DAWASCO* ni kwa namna gani masuala ya msingi yafuatayo yamezingatiwa na kushughulikiwa?

Moja, namna madeni ya *DAWASA* na *DAWASCO* yalivyoshughulikiwa; pili, namna maslahi ya wafanyakazi wa *DAWASA* na *DAWASCO* yanavyoshughulikiwa; tatu, utaratibu wa ajira kwa wafanyakazi wa *DAWASA* na *DAWASCO* mara baada ya taasisi hizi kuunganishwa; nne, suala la malalamiko ya upotevu wa maji kwa *DAWASCO* na hatua zilizochukuliwa ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaka kupatiwa taarifa hizi kutokana na umuhimu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (*DAWASA*) na Shirika la Majitaka Dar es Salaam (*DAWASCO*) katika kutoa huduma za maji na kuzingatia kuwa, Dar es Salaam ni mji mkuu wa kibiashara na wenye idadi kubwa ya watu ukilinganisha na miji mingine.

Aidha, Kamati pia ilitaka kupata ufafanuzi wa hoja za Mdhibiti Mkuu kuhusu Hesabu ya Serikali ya 2016/2017 kuhusu kutokuzingatiwa kwa mkataba wa ukodishaji wa maji na miundombinu ya maji kati ya *DAWASCO* na *DAWASA*.

Moja, matumizi yasiyoridhisha ya shilingi bilioni 1.8 zilizotengwa kufanikisha uunganishaji wa maji kwa wateja wanya; pili, *DAWASCO* kushindwa kununua kifaa cha utambuzi wa uvunaji Maji, hivyo kushindwa kudhibiti upotevu wa maji ambao umefikia asilimia 47 na tatu, *DAWASCO* kufuta deni la shilingi bilioni 24.4 bila kuishirikiana na *DAWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa na kitendo cha Wizara ya Maji na Umwagiliaji kushindwa kuwasilisha taarifa hizi muhimu. Kitendo cha Wizara kushindwa kuwasilisha taarifa hizi muhimu kinadhihirisha malalamiko yaliyoko miongoni mwa Watumishi wa *DAWASA* na *DAWASCO* kuhusu mustakabali wa ajira, maslahi na haki zao mara taasisi hizi zitakapounganishwa. Kufuatia malalamiko haya, Kamati inaishauri Wizara kufuata taratibu zote za ajira ili kuepusha upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu maskini maeneo ya mijini wanagharimia zaidi kupata maji kuliko matajiri. Utafiti unaonesha kuwa watu maskini na wenye kipato kidogo wananunua maji kwa gharama kubwa mara kadhaa kuliko gharama zinazopatikana na watumiaji wenye kipato cha kati na kipato cha juu ambao hupata maji ya bomba kupitia mfumo rasmi majumbani. Halikadhalika, usambazaji wa maji kwenye mitaa ya watu masikini sio wa kuaminika na uhakika na kukosekana kwa maji ni kitu cha kawaida. Matokeo yake ni kwamba wale wenye uwezo mdogo zaidi wanapata maji kwa bei kubwa na kwa taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaonesha kuwa Kamati imebaini watu wa maeneo ya mijini wanaopata maji kutoka katika mfumo usio rasmi. Wanalipa hadi zaidi ya mara tano zaidi ya wale wanaopata maji majumbani kutokana na mtandao wa mabomba ukilinganisha na kiasi kidogo

wanacholipa tabaka la kati na wale wenye tabaka la juu.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hii, Kamati inaishauri Serikali kujengea uwezo Mamlaka za Maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na mazingira katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka hizo ili ziweze kujiendesha kibiashara pamoja na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imetoa miongozo kwa taasisi zake kuhusu namna ya kuvuna maji, miongozo hii iliyotolewa inazielekeza Halmashauri kutunga sheria ndogo zitakazoitaka taasisi za jamii na asasi za kiraia na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa sekta ya maji wanatabanaisha kuwa uvunaji wa maji ya mvua ni salama na rahisi zaidi kuliko uchimbaji wa visima. Endapo uvunaji wa maji ya mvua utawekewa mkazo utaisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi ambazo zimekuwa zikielekezwa kwenye uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa uvunaji wa maji uliolezwa katika bajeti, katika bajeti inayoombwa hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Kufuatia maelezo haya Kamati inaishauri Serikali, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ije na mkakati unaoonesha namna ilivyojipanga kuvuna maji ya mvua nchi nzima pamoja na mkakati unaooneshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miji 17 Itakayonufaika na mradi wa maji kupitia mkopo wa Serikali ya India, Kamati imetaarifiwa kuwa tararibu zote zilizokuwa zinakwamisha upatikanaji wa fedha hizo zimekamiliika na tayari Serikali ya Tanzania na India wamesaini mkataba kwa kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zinatarajiwa kupatikana na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha



2018/2019. Kwa sasa kinachosubiriwa ni utaratibu wa uchunguzi (*vetting*) kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutoa *exemption order* na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili fedha hizo zitolewe na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua hiyo iliyofikiwa na Serikali. Hata hivyo Kamati inaitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo sehemu iliyosalia ambayo inahusu ofisi yake, hatua ambayo itawezesha kuanza kwa utekelezaji na hivyo kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha inapeleka majisafi na salama katika miji mikubwa kwa asilimia 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

**1.1 MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Maji ina mafungu mawili ambayo ni:-

- Wizara ya Maji na Umwagiliaji – Fungu 49; na
- Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05.

## 1.2 MUUNDO WA TAARIFA

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

(e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, maoni na mapendekezo yatakayotolewa ni matokeo ya mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, mahojiano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.2 cha Sehemu ya Kwanza.

### 2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani matano (5) yafuatayo ya kipaumbele:

(a) Mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge;

(b) Mapendekezo ya kuongeza tozo ya shilingi hamsini kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli ili kutunisha Mfuko wa Maji;

(c) Kuiwezesha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kuiongezea bajeti ili iweze kujenga miundombinu ya umwagiliaji itakayokabili changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi;

(d) Umuhimu wa kuharakisha Mkakati wa Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda na;

(e) Umuhimu wa Wizara kuratibu fedha za miradi ya maji zinazokasimiwa kupitia mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa kikamilifu hususan kwenye ushauri uliohusu utoaji wa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge, kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na kuongeza Tozo kwenye mauzo ya mafuta ya dizeli na petroli kutoka shilingi

hamsini (50) hadi shilingi mia (100) kwa lita ili kutunisha Mfuko wa Maji.

**Mheshimiwa Spika**, kutotekelezwa kwa ushauri wa Kamati kikamilifu kumepelekea athari katika sekta. Kwa mfano: kutoongezwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na diseli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia moja (100) kunaathiri ufanisi wa Mfuko wa Maji na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maji na hususan kwa maeneo ya vijijini. Pendekezo la kuongeza tozo kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli sio tu ni ushauri wa Kamati, lakini pia agizo la Bunge lako Tukufu lililopitishwa kupitia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu Januari, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitaka uamuzi wa agizo hili la Bunge lako Tukufu litekelezwa kutokana na kuridhika na mafanikio yaliyofikiwa katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018 ambapo **asilimia 66** ya pesa zilizopatikana na kutumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo maji vijijini zilitokana na makusanyo ya Mfuko wa Maji.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yalijielekeza katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanyaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Machi, 2018.

### 2.2.1 Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ya Maji na Umwagiliaji- Fungu 49, lilidhinishwa jumla ya shilingi **24,457,459,705**. Kati ya fedha hizo shilingi **6,636,518,705** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **17,820,941,000** ni mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi **623,606,748,052** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **408,617,643,052** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani

ambapo kati ya fedha hizo, shilingi **158,500,000,000** ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na shilingi **250,117,643,052** ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, shilingi **214,989,105,000** sawa na **asilimia 34** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05 iliidhinishwa jumla ya shilingi **24,158,893,232** kati ya fedha hizo shilingi **4,055,481,082** ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo shilingi **585,184,082** ni fedha kwa ajili ya mishahara na shilingi **3,407,297,000** ni fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi **20,103,412,150** kati ya hizo shilingi **5,600,000,000** ni fedha za ndani na shilingi **14,503,412,150** ni fedha za nje.

## 2.2.2 Mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2018 Fungu 49 lilikuwa limepokea fedha za matumizi mengineyo shilingi **2,937,365,387** sawa na **asilimia 44**, na mishahara shilingi **9,890,570,356** sawa na **asilimia 55** ya kiasi kilichoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2018 zilikuwa shilingi **135,191,256,566** sawa na **asilimia 22** ya fedha zote za bajeti ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05 hadi kufikia Machi, 2018 fedha za matumizi ya mengineyo kiasi cha shilingi **483,040,684** ambayo ni sawa na **asilimia 83** zilipokelewa na shilingi **2, 155, 941, 880** sawa na **asilimia 62** zilitolewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi **2,468,524,644.66** zilitolewa ambazo ni sawa na **asilimia 12.3** ya fedha zilizoidhinishwa.

## 2.2.3 Maoni kuhusu Mwenendo wa Utolewaji Fedha

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika (2017/2018) fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji - Fungu 49 zilizotolewa ni **asilimia 22** tu. Mwenendo huu ni wa kusikitisha na hasa

ukizingatia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa sehemu kubwa ni miradi ya maji. Mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua changamoto ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa muda mrefu, ndio maana Bunge liliazimia Serikali kuongeza shilingi hamsini (50) kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli ili kutunisha Mfuko wa Maji ambao ni chanzo cha fedha cha uhakika na umeonyesha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maji, hata hivyo Azimio hili la Bunge halijatekelezwa hadi Kamati inapowasilisha taarifa hii na hakuna taarifa yoyote kutoka Serikalini kuelezea ni sababu zipi zilizopelekea azimio hili kutotekelezwa hii ni dharau kubwa kwa Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi **4,735,005,000**. Hadi kufikia Machi, 2018, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **3,276,849,518** ambayo ni sawa na **asilimia 69** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo hata hivyo, Kamati inahimiza Wizara kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo yaliyowekwa.

### **2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2017/2018), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika mkoa wa Kigoma. Miradi iliyokaguliwa ni: -

a) **Mradi Namba 3306 wa Maji Safi na usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji (KUWASA).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua mradi **Namba 3306** wa Maji Safi na usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji (KUWASA). Mradi ambao unatekelezwa chini ya program ya kitaifa ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Three Towns Urban Upgrading Project*) kwa ushirikiano kati ya Serikali (Wizara ya Maji) na *European Union Community* kwa gharama ya **EURO milioni 15,160,702.7**. Mradi unategemea kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 21** za sasa hadi kufikia lita **milioni 42**.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitegemewa kukamilika mwaka 2014 hata hivyo mradi haujakamilika kutokana na mkandarasi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati pamoja na marekebisho yaliyofanywa kwenye usanifu wa mradi ambayo yalipelekea kuongeza gharama za mradi kwa zaidi ya **EURO 1,162,449.97**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa kukosekana kwa usimamizi makini kumepelekea miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati na hivyo kusababisha hasara kwa gharama za miradi kuongezeka kama ilivyojitokeza katika mradi wa majisafi na usafi wa mazingira Kigoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu utekelezaji wa mradi huu:-

(i) Mamlaka ya Maji Kigoma (KUWASA) inapaswa kuwa na Mpango wa Biashara (*Business plan*) utakaowezesha Mradi kujiendesha kwa faida baada ya kukamilika. Kwa sasa KUWASA inakusanya kiasi cha shilingi **million 125** kwa mwezi. Mara mradi utakapokamilika gharama za kuzalisha umeme kwa ajili ya kuendeshea mradi zinatarajiwa kuwa kati ya shilingi **million 140 hadi shilingi million 247** kwa mwezi hivyo ni vyema KUWASA ikawa Mpango Biashara utakowezesha kujiendesha kwa tija.

(ii) Mpango wa Biashara utakaoandaliwa uzingatie umuhimu wa matumizi ya mita za malipo kabla (*pre paid*)

*meters*) na kwamba kila mteja lazima afungiwe na aunganishwe kwenye mfumo huu ili uisaidie Mamlaka kupata wepesi wa kukusanya ankara za maji.

(iii) Aidha, Kamati iliishauri Mamlaka za Maji kutumia vyanzo vingine vya umeme vyenye gharama nafuu kama umeme wa jua (*solar power*) ili kupunguza gharama za uendeshaji na kusaidia miradi kuwa endelevu.

#### **b) Mradi wa Maji katika kijiji cha Kagera mkoani Kigoma**

Mradi huu ulisainiwa kuanza ujenzi 01 April, 2014 na ulipangwa kukamilika tarehe 30 Januari, 2014 na gharama za mradi ni shilingi **942,837,710**. Hadi kufikia Machi, 2018 mradi ulikuwa haujakamilika kutokana na kutounganishwa na mtandao wa maji wa Mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Kigoma/Ujiji (KUWASA) ili tenki liweze kupokea maji na kusambaza kwenye maeneo yaliyokusudiwa, Hivyo miundombinu ya mradi huu imekabidhiwa KUWASA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa KUWASA imekosa fedha za kukamilisha ujenzi wa njia kuu ya maji kwenda tenki la Kagera **km 8.28** kutoka eneo la Mwanga. Ni vema Serikali ikaiwezesha KUWASA kupata kiasi cha fedha kinachohitajika shilingi **million 825** kwa ajili ya ujenzi wa njia kuu ya maji yenye urefu wa **km 8.28** kutokea eneo la Mwanga kwenda tanki la Kagera ili mtandao mzima wa maji uunganishwe tayari kwa kuanza kuwanufaisha wananchi.

#### **c) Mradi wa Maji wa Kalinzi**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji Kalinzi ni moja kati ya miradi ya maji inayotekelezwa na Halmashauri ya Kigoma tangu 30 Januari, 2017 kwa gharama za shilingi **786,642,000**. Mradi huu ulipangwa kukamilika tarehe 30 Septemba, 2017. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, mkandarasi alikua hajamaliza ujenzi wa mradi kutokana na sababu mbalimbali kama vile kukosekana kwa umeme wa kutosha kwa ajili ya kuwasha pampu na kutakiwa kubadilisha pampu zilizofungwa



kusukuma maji kuwa na uwezo mdogo. Kutokana na ucheleweshaji huu, baadhi ya miundombinu ya mradi kama vile mantenzi ya kuhifadhi maji vimeanza kuchakaa kabla ya mradi kuanza kutumika.

**d) Mradi wa Majitaka Luiche**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umesanifiwa kwa ajili ya kukusanya maji taka kutoka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji, mradi umepangwa kutekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi majitaka na chujio la majitaka, na awamu ya pili inahusisha ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji taka kutoka majumbani. Hadi Kamati ilipokuwa inakagua mradi huu sehemu ya mradi iliyotekelezwa ilikuwa ni ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi majitaka, machujio ya majitaka na baada ya awamu ya kwanza kukamilika yatapelekwa katika mabwawa kwa kutumia magari ya kubebea maji taka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhika na kupongeza jitihada na hatua iliyofikiwa katika kutekeleza mradi huu. Hata hivyo ni vema Manispaa ya Kigoma ikawa na mipango endelevu kwa kutambua na kutenga maeneo ambayo awamu ya pili ya mradi itapita na kuyahifadhi yasitumiwe kwa shughuli nyingine. Hatua hii itasaidia kuepuka gharama zitakazoendana na ubomoaji na ulipaji fidia hapo baadae hivyo ni vyema Manispaa ikasaidiana na Mamlaka nyingine kuwa na *Master Plan* ya majisafi na majitaka ili kila mpango utakaofanyika uwe ndani ya *Master Plan* hiyo.

**e) Mradi wa uendelezaji bonde la mto Luiche.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kutekeleza kilimo cha umwagiliaji katika bonde la mto Luiche ambapo miundombinu ya umwagiliaji itajengwa ili kuimarisha kilimo cha mazao ya mpunga, mahindi na mboga mboga katika eneo la jumla ya **hekta 3,000** ambao kwa upande wa kilimo cha mpunga uzalishaji unategemewa kuongezeka kutoka tani **2.5** hadi **tani 5.6** kwa hekta. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Kuwait kupitia Kuwait *Fund* na unategemea

kugharimu fedha za kitanzania zisizopungua shilingi **bilioni 34**.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Luiche umekuwa wa kususua kwa muda mrefu, pamoja na kususua kwa kuanza utekelezaji wa mradi huu kwa sasa hatua iliyofikiwa ni ya kupongezwa ambapo Serikali imeshasaini mkataba ambao utawezesha kuanza kwa kilimo cha umwagiliaji ambacho kitawezesha kukuza kilimo cha mazao ya mahindi, mpunga na mboga mboga na hivyo kutoa ajira kwa watanzania hususan wananchi wa kigoma na pia kuongeza pato la Taifa.

## **2.4 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 21 na 22 Machi, 2018 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi umezingatia Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Awamu II), Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV 2025), Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya Mwaka 2010.

### **2.4.1 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI (FUNGU 05)**

**Mheshimiwa Spika**, Fungu 05 linahusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ambapo pamoja na majukumu mengine Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina jukumu la kuhakikisha Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inatekelezwa kwa vitendo na kutoa mchango stahiki katika kuongeza tija za uzalishaji katika sekta ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inahimiza umuhimu wa kuendeleza eneo kubwa lililopo nchini linalofaa

kwa umwagiliaji kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo kwenye mazao ya chakula, biashara, malisho na kilimo cha majani<sup>1</sup>. Kwa muktadha huu, maombi ya fedha kwa mwaka **2018/2019** na utekelezaji wa bajeti unalenga kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Umwagiliaji ya Taifa pamoja na kufanikisha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji ambao unalenga kujenga miundombinu yenye jumla ya **hekta 1,000,000**, katika skimu za wakulima wadogo, kati na wakubwa ifikapo mwaka **2025** kwa makadirio ya takribani **shilingi trilioni 15**.

#### **2.4.1.1 Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019- Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (Fungu 5) kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019** inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **29,767,866,000**. Kati ya fedha hizo, shilingi **3,947,408,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **25,820,458,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha zinazooombwa zinakusudiwa kutumika kutekeleza pamoja na kazi zingine vipaumbele vifuatavyo: -

(a) Kukamilisha ujenzi wa skimu sita **(6)** za umwagiliaji ambazo ni pamoja na Nyamitita (Serengeti), Kirya (Mwanga), Ludewa (Kilosa), Lwanyo (Mbalali), Gidahabaieg (Hanang'), na Endagaw (Hanang');

(b) Kukamilisha ujenzi wa mabwawa matatu **(3)** ya umwagiliaji ambayo ni Dongobesh katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Kongongo (Bahi), na Itagata (Itigi);

(c) Kukamilisha skimu **11** za umwagiliaji ambazo ni Mwisa (Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe), Nyinda (Shinyanga), Katela Ntaba na Mbata (Busokelo), Mgambalenga (Kilolo), Mwalunili (Igunga), Ngongowe (Liwale), Nanganga

---

<sup>1</sup>Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya Mwaka 2010

(Ruangwa), Ngage (Simanjiro), na Katuani Mwenzae na Kwemgiriti (Lushoto);

(d) Kuimarisha Vyama vya Wamwagiliaji katika usimamizi wa skimu, kuanzisha chombo cha kusimamia vyama vya wamwagiliaji pamoja na kuhamasisha teknolojia za matumizi ya maji kwa ufanisi;

(e) Kutathimini mchango wa kilimo cha umwagiliaji katika usalama wa chakula nchini, ajira kwa vijana na ufanisi wa kilimo shadidi.

#### **2.4.1.2 Tathimini ya Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti na maombi ya fedha kwa Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba nchi yetu ina jumla ya **hekta milioni 29.4** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hadi mwezi **Februari 2017**, jumla ya **hekta 468,338** sawa na **asilimia 1.6** ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji ndio linamwagiliwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na eneo dogo linalotumika kwa umwagiliaji uzalishaji wa tija umejionyesha katika skimu za umwagiliaji zilizoboreshwa kwa mazao yafuatayo:-

- **Zao la mpunga uzalishaji umeongezeka** kutoka tani 4.0-5.0 **kwa** hekta **hadhi kufikia** tani 10.0 – tani 12.0 **kwa** hekta.
- **Zao la mahindi uzalishaji umeongezeka kutoka** tani 1.5 hadi 3.7 – 5.0 **kwa** hekta.
- **Zao la vitunguu kutoka** tani 13-26 **kwa** hekta **na**
- **Zao la nyanya kutoka** tani 5-18 **kwa** hekta. <sup>2</sup>

**Mheshimiwa Spika**, tija inayopatikana kutoka kwenye skimu za umwagiliaji zilizoboreshwa zinaweza kulima misimu miwili hadi mitatu tofauti na kilimo cha kutegemea mvua ambacho mara nyingi huwa ni cha msimu mmoja.

---

<sup>2</sup> Sera ya Maji ya Mwaka 2002

Kwa kutambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji ambao utekelezaji wake umepangwa kukamilika mwaka **2025** na umepangwa kutekelezwa katika kanda nane na unakadiliwa kugharimu takribani shilingi **trilioni 15**.

**Mheshimiwa Spika**, ili kufikia adhima hiyo, Serikali inapaswa kuiwezesha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kuitengea angalau shilingi **trilioni tatu** kila mwaka. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imehidhinishiwa takribani shilingi **bilioni 25** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo fedha hizo ni sawa na **asilimia 0.83** ya mahitaji.

Jedwali lifuatalo linafafanua gharama za uwekezaji zinazotakiwa kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ifikapo Mwaka 2025.

**JEDWALI NA.1**

<b>Na.</b>	<b>Kanda</b>	<b>Eneo linaloweza kumwagiliwa (ha)</b>	<b>Kiasi cha Fedha kinachohitajika</b>
1.	Kilimanjaro	212,299.00	1,752,878,380,000.00
2.	Mbeya	263,132.20	2,887,129,058,046.90
3.	Mwanza	317,611.70	2,849,526,590,950.00
4.	Katavi	115,096.00	1,112,355,650,000.00
5.	Morogoro	294,168.50	2,912,268,150,000.00
6.	Mtwara	118,095.30	1,146,164,073,468.00
7.	Tabara	73,578.00	612,337,022,588.50
8.	Dodoma	139,434.00	1,359,551,193.68
<b>Jumla Kuu</b>		<b>1,533,414.70</b>	<b>14,632,032,476,247.10</b>

**Mheshimiwa Spika**, tathimini ya Kamati imebaini kuwa endapo Serikali itaendelea kuitengea Tume ya Taifa ya Umwagiliaji fedha kidogo kiasi hiki ikilinganishwa na mahitaji halisi ni wazi kuwa adhima ya Serikali kuendeleza eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji la **hekta 1,000,000** ifikapo mwaka **2025** haitafikiwa

## **2.4.2 WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI (FUNGU 49)**

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inaeleza kuwa maji ni bidhaa muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Hivyo, upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mahitaji ya msingi kwa binadamu wote<sup>3</sup>. Kwa kutambua hilo ndio maana swala la maji limewekewa mkazo katika malengo mahususi ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo la sita la maendeleo endelevu linadhamiria kuona kuna upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote ifikapo 2030.

### **2.4.2.1 Umuhimu wa Maji kwa Maendeleo ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika**, juhudi zote hizo zinadhihirisha kuwa Maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kwamba kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa lakini bado upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini umethibitika kuwa mgumu hususan maeneo ya vijijini ambapo takwimu zinaonyesha ni **asilimia 56%** tu ya wakazi wa vijijini ndio wanaopata maji safi na salama na **asilimia 69%** kwa wakazi wa mjini.

### **2.4.2.2 Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 inatarajiwa kwenda kutekeleza miradi itakayosaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji safi na salama ili kuhakikisha kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ni:-

---

<sup>3</sup> Sera ya Maji ya Mwaka 2002

(a) Kuwa na huduma bora ya maji kwa wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025;

(b) Huduma bora za maji vijijini kwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi ifikapo mwaka 2025; na

(c) Kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuvilinda, kuvitunza, kuviendeleza na kutafuta vyanzo vipya vya maji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo, bajeti inayoombwa pia itatakeleza kazi zifuatazo: -

(i) Kukamilisha miradi 366 inayoendelea katika Halmashauri mbalimbali na kuanza miradi mipya ya maji vijijini;

(ii) Kujenga matenki na kulaza mabomba ya kusambaza maji kutoka mitambo ya Ruvu Chini, Ruvu Juu na Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera kwenda maeneo yanayohudumiwa na DAWASA;

(iii) ujenzi wa barabara iendayo eneo la Bwawa la Kidunda, njia ya umeme na ujenzi wa Bwawa la Kidunda;

(iv) Kuanza ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya uondoaji majitaka katika maeneo ya Mbezi *Beach*, Jangwani na Kurasini; na kupanua mtandao wa kuondoa majitaka;

(v) Kulipa fidia na kuanza ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati ya Farkwa (Dodoma) na Ndembera (Iringa);

(vi) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Tinde, Nzega, Igunga, Uyui, Sikonge pamoja na vijiji 89 vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu; na

(vii) Kuendelea na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na ufuatiliaji wa ubora maji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 24,366,869,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 6,266,714,000** sawa na **asilimia 26** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya kawaida (*Other Charges*) na **shilingi 18,097,155,000** sawa na **asilimia 74** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya Watumishi. Kati ya fedha za mishahara, shilingi **15,932,277,000** ni za mishahara ya Watumishi wa Wizara na shilingi **2,164,878,000** ni za mishahara ya Watumishi wa Chuo cha Maji.

#### **2.4.2.3 Fedha zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **673,214,033,677**. Kati ya fedha hizo, shilingi **443,214,034,677** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani na shilingi **229,999,999,000** sawa na asilimia 34 ni fedha za nje. Aidha, fedha zingine za nje shilingi **96,405,000,000** zimetengwa kupitia mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI kwa ajili ya miradi ya maji na kampeni za maji na usafi wa mazingira vijijini.

#### **2.4.2.4 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia **Fungu 49** imepanga kukusanya shilingi **631,001,000** itakazozipata kutokana na makadirio ya kukusanya maduhuli yatakayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji visima vya maji na tozo mbalimbali zitakazotozwa kwa wateja watakaopata huduma za maabara za ubora wa maji.

#### **2.4.2.5 Tathimini ya Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Fungu 49**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa Serikali imeendelea kutenga fedha nyingi za



ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo japo hazitoshi kulingana na mahitaji halisi, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Fungu 49 limetengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi **443,214,034,677** ambayo ni sawa na **asilimia 66** ya fedha zote za maendeleo. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati.

#### **2.4.3 TATHIMINI YA JUMLA YA MALENGO YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia, imechambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Malengo haya ni ya msingi na ya kuridhisha hata hivyo, Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 hayakidhi mahitaji makubwa ya Maji kama yalivyoelezwa katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano (Awamu ya I&II) ambao umebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji, viwanda, usafirishaji na uchukuzi na kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, tathimini ya Kamati inaonyesha kuwa ni kawaida kwa Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maendeleo na kushindwa kuzitoa kama zilivyoidhinishwa. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Bunge liliidhinisha shilingi **623,606,748,052** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia Machi, 2018 kiasi cha shilingi **135,191,256,566** sawa na asilimia 22 tu ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hali hii ina athari kubwa siyo tu katika maamuzi ya Bunge bali pia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayokusudiwa katika kipindi fulani kwa wananchi.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwenye maeneo nane (8) yafuatayo:-

#### 1) **MTIRIRIKO USIORIDHISHA WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo usioridhisha wa utoaji fedha za miradi ya maendeleo umeendelea kuwa tatizo la kudumu katika Sekta ya Maji na Umwagiliaji. Kwa mfano; kwa kipindi cha miaka miwili (2016/2017 hadi 2017/2018) fedha ambazo zimekuwa zikiidhinishwa na Bunge na kutolewa na Serikali kwa **Fungu 49** ni **asilimia 16.8** kwa Mwaka wa Fedha **2016/2017** na **asilimia 22** kwa Mwaka wa Fedha **2017/2018**. Na kwa **Fungu 5** ni **asilimia 8.4** kwa mwaka wa fedha **2016/2017** na **asilimia 12.3** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na kiasi kidogo cha ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha kutokidhi kabisa mahitaji, fedha zilizotolewa kwa kipindi tajwa hazifiki hata nusu ya bajeti ya mwaka mmoja hivyo kuwa sababu ya kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya maji na hivyo kuwanyima wananchi fursa ya kupata huduma za majisafi na salama. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi Desemba, 2017 hali ya upatikanaji maji safi na salama kitaifa ni wastani wa **asilimia 56** kwa **vijijini** na **asilimia 69** kwa **mijini**.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo huu usioridhisha unakwamisha kufikiwa kwa malengo ya upatikanaji maji safi na salama kufikia **asilimia 85 vijijini** na **asilimia 95 mijini** ifikapo **mwaka 2021** kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2016/2017 – 2020/2021). Kamati inaishauri Serikali kutekeleza adhima ya

kuwapatia wananchi wote huduma ya majisafi kwa gharama nafuu kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kadri zilizvyoidhinishwa na Bunge.

## 2) **UMUHIMU WA KILIMO CHA UMWAGILIAJI KATIKA KUONGEZA UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO**

**Mheshimiwa Spika**, tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa ipo tija kubwa katika uzalishaji wa mazao kupitia kilimo cha umwagiliaji ikilinganishwa na kilimo cha kutegemea mvua ambapo kimeathiriwa na uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano; katika utafiti uliofanywa katika skimu ya umwagiliaji ya Sakalio Rukwa, umeonyesha kuwa ulinganisho wa uzalishaji wa zao la mahindi kwa hekta kwa kupitia kilimo cha umwagiliaji ni **tani 3.75 kwa hekta** wakati kilimo cha kutegemea mvua ni **tani 2.7 kwa hekta**. Aidha, katika skimu ya umwagiliaji wa kilimo cha mpunga Mombo- Tanga uzalishaji kupitia kilimo cha umwagiliaji ni **tani 4.5 hadi tani 5.5** kwa hekta wakati kilimo cha kutegemea mvua ni **tani 2.2- 3 kwa hekta**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na tija inayojidhihirisha kwenye kilimo cha umwagiliaji, bado Serikali haijalipa suala la kilimo cha umwagiliaji msukumo stahiki kutokana na ukweli kwamba hekta **461,326** sawa na **asilimia 1.6** tu ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ndio linalotumika.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na kilimo chenye tija, kuongeza uzalishaji wa malighafi za viwanda pamoja na utoshelezi wa chakula nchini, Kamati inashauri Serikali kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili iweze kutekeleza Mpango kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan 2025*) ambao unaonyesha mahitaji ya fedha ni takribani shilingi **trilioni 15** zitakazotumika kujenga, kusimamia na kutunza miundombinu ya umwagiliaji itakayowezesha Taifa kujielekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji na hivyo kuwa na kilimo chenye tija.

**Mheshimiwa Spika**, ili Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, licha ya Kamati kuitaka Serikali iongezee Tume fedha za kutekeleza Mpango kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji, Kamati pia inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuwathibitisha watendaji wa juu wa Tume ambao wengi wao wanakaimu nafasi walizonazo kwa muda mrefu na hivyo kukosa uthubutu wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, Tume inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi ikilinganishwa na mahitaji halisi, hivyo Kamati inashauri tathimini ifanyike kubaini mahitaji halisi na kupatiwa vibali vya kuajili kulingana na mahitaji.

**3) KUONGEZA TOZO YA MAFUTA KWA KILA LITA YA PETROLI NA DISELI KUTOKA SHILINGI HAMSINI (50) HADI SHILINGI MIA MOJA (100)**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mfuko wa Maji ulikusanya shilingi **bilioni 158**, fedha ambayo imetumika ipasavyo na kuonyesha mafanikio kwenye miradi ya maji vijijini. Kamati inaipongeza Serikali kwa dhati kwa namna ambavyo imefanikisha miradi ya maji vijijini kupitia fedha za Mfuko wa Maji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo na mafanikio yaliyofikiwa, Kamati inaamini endapo Serikali ingetekeleza azimio la Bunge lako Tukufu lililopitishwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 la kuongeza tozo ya mafuta kwa kila litera ya petroli na diseli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia moja (100) fedha ambayo ingekusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ingekuwa mara mbili ya makusanyo yaliyopatikana na kwa miaka miwili (2018/ 2019 na 2019/2020) makusanyo yanakadiriwa kufikia shilingi **bilioni 316** hatua ambayo itaongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini na hivyo kuiwezesha Serikali kufanikisha lengo la kufikisha maji vijijini kwa **asilimia 85** ifikapo mwaka **2021** sambamba na adhima ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kumtua mama ndoo kichwani.

**4) KUUNGANISHWA KWA MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJI TAKA DAR ES SALAAM (DAWASA) NA SHIRIKA LA MAJI SAFI NA MAJITAKA DAR ES SALAAM (DAWASCO)**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu kuunganishwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASA) na Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASCO). Shughuli za huduma za majisafi na maji taka kwa jiji la Dar es salaam zimekuwa zikiendeshwa kupitia Mamlaka ya majisafi na majitaka Dar es salaam (DAWASA) na Shirika la majisafi na majitaka Dar es salaam (DAWASCO) tofauti na Mamlaka zingine za Maji za Miji Mikuu na Mikoa ambapo shughuli za aina hii hufanywa na Mamlaka moja.

**Mheshimiwa Spika**, umaalum huu wa uendeshaji huduma za majisafi na majitaka kwa Jiji la Dar es salaam ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na wingi wa idadi ya watu, uchakavu wa miundombinu ya majisafi na majitaka na huduma duni za upatikanaji wa maji safi kutokana na kukosekana uwekezaji wa muda mrefu. Changamoto hizo na zingine nyingi zilipelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya majisafi na majitaka Dar es salaam (DAWASA) kwa lengo la kujenga na kumiliki miundombinu, kusimamia utoaji wa hudumu ya maji safi na majitaka na kupanga mipango na kusimamia upanuzi wa huduma Wakati DAWASCO ina majukumu mbalimbali yakiwemo kuendesha shughuli za kutoa huduma za majisafi na majitaka, kutoa ankara za wateja na kukusanya maduhuli, kufanya matengenezo ya miundombinu pamoja na matengenezo makubwa yanayogharamiwa na DAWASA na kuunganisha wateja wapya na kudhibiti maji yasiyolipwa.

**Mheshimiwa Spika**, kuanzishwa kwa taasisi hizi kumepelekea upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa jiji la Dar es salaam kuongezeka kutoka **asilimia 58** mwaka **2003** na kufikia **asilimia 75** mwaka **2018**. Ongezeko la upatikanaji maji kwa jiji la Dar es salaam limepelekea kupungua kwa changamoto nyingi zilizofanya kuanzishwa kwa DAWASA na DAWASCO na hivyo Serikali kuona umuhimu wa kuunganisha majukumu

ya DAWASA na DAWASCO kwa lengo la kuboresha zaidi huduma na kupunguza gharama za uendeshaji ambapo takwimu za Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 zinaonyesha DAWASCO ndio Mamlaka ya Maji inayoongoza kutoza gharama kubwa kwa watumiaji maji maji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza kwa dhati uamuzi wa Serikali wa kuunganisha DAWASA na DAWASCO hata hivyo Kamati imesikitishwa na Wizara kushindwa kuwasilisha taarifa mabalimbali zilizoombwa na Kamati kwa lengo la kutoa ushauri wa kuboresha.

Kamati ilitaka kufahamu kabla ya kuunganisha DAWASA na DAWASCO ni kwa namna gani masuala ya msingi yafuatayo yamezingatiwa na kushughulikiwa:-

(a) Namna madeni ya DAWASA na DAWASCO yalivyoshughulikiwa;

(b) Namna maslahi ya wafanyakazi wa DAWASA na DAWASCO yanavyoshughulikiwa;

(c) Utaratibu wa ajira kwa wafanyakazi wa DAWASA na DAWASCO mara baada ya taasisi hizi kuunganishwa na

(d) Suala la malalamiko ya upotevu wa maji kwa DAWASCO na hatua zilizochukuliwa ili kukabiliana na changamoto hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kupatiwa taarifa hizi kutokana na umuhimu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASA) na Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASCO) katika kutoa huduma za maji na kwa kuzingatia kuwa Dar es salaam ni mji mkuu wa biashara na wenye idadi kubwa ya watu ukilinganisha na miji mingine. Aidha, Kamati pia ilitaka kupata ufafanuzi wa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2016/2017 kuhusu kutozingatiwa kwa mkataba wa ukodishaji wa maji na miundombinu ya maji kati ya DAWASA na DAWASCO kuhusu: -

(i) Matumizi yasiyoridhisha ya shilingi **bilioni 1.8** zilizotengwa kufanikisha uunganishaji wa maji kwa wateja wapya;

(ii) DAWASCO kushindwa kununua kifaa cha utambuzi wa uvunaji wa Maji hivyo kushindwa kudhibiti upotevu wa maji ambao umefikia **asilimia 47**;

(iii) DAWASCO kufuta deni la shilingi bilioni 24.9 bila kuishirikisha DAWASA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imesikitishwa na kitendo cha Wizara ya Maji na Umwagiliaji kushindwa kuwasilisha taarifa hizo muhimu, kitendo cha Wizara kushindwa kuwasilisha taarifa hizo kinadhihirisha malalamiko yalioko miongoni mwa Watumishi wa DAWASA na DAWASCO kuhusu mustakabali wa ajira, maslahi na haki zao mara taasisi hizi zitakapounganishwa. Kufuatia malalamiko hayo Kamati inaishauri Wizara kufuata taratibu zote za ajira ili kuepusha upendeleo, malumbano na ugomvi wa madaraka miongoni mwa menegementi na Watumishi wa DAWASA na DAWASCO.

#### **5) UANZISHWAJI WA WAKALA WA MAJI VIJIJINI NA UMUHIMU WAKE KATIKA KUHARAKISHA UPATIKANAJI WA MAJI VIJIJINI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa “Hati Idhini” iliyochapishwa kwenye gazeti la Serikali la tarehe 22/04/2016 inatamka kuwa pamoja na mambo mengine, Waziri wa Maji ndiye mwenye mamlaka ya kutoa huduma za maji nchi nzima, kutafuta fedha na kusimamia miradi yote inayohusu shughuli za maji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na tamko hilo la “Hati Idhini”, Miradi ya Maji inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na OR-TAMISEMI, ambapo Wizara ya Maji inawajibu wa kutoa miongozo na taratibu za uendeshaji miradi hiyo, wakati OR-TAMISEMI inawajibu wa kutekeleza miongozo iliyotolewa. Utaratibu huu wa ugatuaji madaraka umepelekea pamoja na mambo mengine, changamoto ya kimfumo ambapo Wizara ya Maji hukosa mamlaka ya moja

kwa moja kwa watekelezaji na wasimamizi wa miradi ya maji vijijini ambao wanasimamiwa na OR-TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hii imekuwa ikikwamisha utekelezaji thabiti wa miradi ya maji vijijini ikiwa ni pamoja na kampeni ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kumtua mama ndoo kichwani na hivyo kuchelewesha adhima ya Serikali ya kufikishia majisafi na salama vijijini kwa **asilimia 85** ifikapo mwaka **2021**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hii na zingine nyingi zimepelekea wadau wa sekta ya maji kuona umuhimu wa kuanzisha Wakala wa Maji vijijini ambao pamoja na mambo mengine, kiutawala na kiutendaji itaripoti kwa Waziri mwenye dhamana ya Maji na Umwagiliaji. Kuanzishwa kwa Wakala wa Maji vijijini kutawezesha utekelezaji wa miradi ya maji kwa ubora na ufanisi unaotakiwa kwa kuwa wataalam wataongezeka; uandaaji na utoaji taarifa utaimarika; usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi (*Value for Money*) utarahisishwa na uendelevu wa miradi ya maji utaimarika kwa kuwa kutakuwa na chombo kitakachohusika na masuala hayo na kushughulikia kikamilifu, masuala ya matengenezo na ukarabati wa miradi ya maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia faida zitakazotokana na uanzishwaji wa Mamlaka ya Maji Vijijini, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini kwa lengo la kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa maji katika maeneo mengi vijijini.

## **6) WATU MASIKINI MAENEO YA MIJINI WANAGHARIMIKA ZAIKI ILI KUPATA HUDUMA ZA MAJI**

**Mheshimiwa Spika**, utafiti unaonyesha watu masikini na wenye kipato kidogo wananunua maji kwa gharama kubwa mara kadha kuliko gharama wanazolipa watumiaji wenye kipato cha kati na cha juu ambao hupata maji ya bomba kupitia mfumo rasmi majumbani. Halikadhalika, usambazaji wa maji kwenye mitaa ya watu maskini sio wa kuaminika/



uhakika, na kukosekana kwa maji ni kitu cha kawaida. Matokeo yake ni kwamba wale wenye uwezo mdogo zaidi wanapata maji kwa bei kubwa na kwa tabu sana.

**Mheshimiwa Spika**, utafiti uliofanywa na Kamati umebaini watu wa maeneo ya mijini wanaopata maji kutoka katika mfumo usio rasmi, wanalipa hadi zaidi ya mara tano ya wale wanaopata maji ya majumbani kutoka kwenye mtandao wa mabomba ikilinganishwa na kiasi kidogo wanacholipa watu wa tabaka la kati na wale wenye kipato cha juu.

**Mheshimiwa Spika**, hii inathibitishwa na ukweli kwamba bei ya maji ya nyumbani kwa jiji la Dar es salaam yanayosambazwa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASA) huuzwa sh **1,663** kwa lita **1,000** wakati maji yanayonunuliwa nje ya mfumo wa mita hununuliwa kwa sh **10,000** kwa lita **1,000 (kwa ukokotozi wa ndoo ya lita 20 huuzwa kwa bei ya chini shilingi 200)**. Hii tafsiri yake ni kwamba wananchi wengi wanao uwezo wa kugharamia huduma za maji safi na salama zinazotolewa na Mamlaka mbalimbali za maji nchini. Changamoto iko kwa Mamlaka za Maji kukosa uwezo wa kufikisha majisafi na salama kwa wananchi wengi na hivyo kuwabebesha wananchi gharama kubwa za maji.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji mijini ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka hizo ili Mamlaka ziweze kujiendesha kibiashara pamoja na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

## **7) UMUHIMU WA UVUNAJI WA MAJI YA MVUA**

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha takriban watu **bilioni 1.5** duniani, hawapati huduma ya maji safi na salama. Idadi hiyo ni kubwa kuliko ya watu wote waliopo Afrika wanaokadiriwa kuwa **bilioni 1.2** sawa na **asilimia 16** ya dunia nzima kutokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu kwenye vyanzo vya maji pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, utafiti uliofanywa na Shirika la Mazingira Duniani (UNEP), unaonyesha ifikapo Mwaka 2050 takriban watu **bilioni 2** duniani watakuwa hawana uhakika wa kupata maji ya kutumia, Ifikapo mwaka huo maji yatakuwa bidhaa adimu katika mataifa mengi duniani. Aidha, ripoti mbalimbali zinaonyesha kiwango cha uchafuzi wa maji kimekuwa kikubwa, upungufu wa maji na mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuisumbua dunia.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na majanga ya asili na shughuli za binadamu kwenye vyanzo vya maji, maeneo mengi yamekuwa yakipata mvua chini au juu ya kiwango kilichotarajiwa. Ukame na mafuriko yamekuwa sehemu ya maisha ya binadamu wa leo. Ili kukabiliana na changamoto hii ni muhimu Serikali ikaweka mkazo kwenye programu za kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi na kutumika katika maeneo yenye ukame.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Serikali imetoa miongozo kwa taasisi zake kuhusu namna ya kuvuna maji, miongozo iliyotolewa inazielekeza Halmashauri kutunga sheria ndogo zitakazozitaka taasisi za jamii, asasi za kiraia na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji maji ya mvua kwenye majengo na maeneo yao. Ujenzi wa matenki ya kuvunia maji ya mvua yajengwe vituo vyote vya kutolea huduma za afya, taasisi za elimu, mahakama, ofisi zote za Serikali na miradi ya sekta binafsi. Pamoja na maelekezo hayo, kila halmashauri inatakiwa kila mwaka kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa angalau bwawa moja la kuvunia maji ya mvua.

**Mheshimiwa Spika**, utafiti uliofanywa na Kamati umebaini kuwa miongozo iliyotolewa haitekelezwi ipasavyo na hakuna ufuatiliaji unaofanywa na Serikali na hivyo kupelekea upotevu mkubwa wa maji. Kufuatia upotevu mkubwa wa maji ya mvua, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia utekelezaji wa miongozo inayotoa kama hatua muhimu ya kuhakikisha kuwa upatikanaji wa majisafi na salama kwa ajili ya binadamu, wanyama na mimea kipindi chote cha mwaka utakuwa wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika**, wataalamu wa sekta ya maji wanatabanaisha kuwa, uvunaji wa maji ya mvua ni salama na rahisi zaidi kuliko uchimbaji wa maji ardhini. Endapo uvunaji wa maji ya mvua utawekewa mkazo utaisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi ambazo zimekuwa zikielekezwa kwenye uchimbaji wa visima ambavyo utumia fedha nyingi na uhitaji nishati ya umeme kwa ajili ya kuyavuta, faida nyingine ni pamoja na uhakika wa upatikanaji wa maji hasa kipindi cha masika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa uvunaji wa maji uliolezwa, katika bajeti inayoombwa hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo, kufuatia maelezo hayo, Kamati inashauri Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ije na mkakati unaoonyesha namna ilivyojipanga kuvuna maji ya mvua nchi nzima pamoja na mkakati unaonyesha dhamira ya dhati ya kusimamia miongozo iliyoitoa kuhusu kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua katika majengo mbalimbali pamoja na kuhakikisha kila Halmashauri kutenga kila mwaka fedha kwa ajili ya ujenzi wa angalau bwawa moja la kuvunia maji ya mvua.

#### **8) MIJI 17 ITAKAYONUFAIKA NA MRADI WA MAJI KUPITIA MKOPO WA SERIKALI YA INDIA**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka 2017/2018 Serikali ilitangaza kupata mkopo wa ***Dola za Marekani milioni 500*** kutoka Serikali ya India fedha ambazo zitanufaisha miji 17 ambayo ni Mheza, HTM, Kayanga, Njombe, Makambako, Waging'ombe, Manyoni, Songea, Sikonge, Chunya, Rujewa, Kasulu, Kilwa – Masoko, Mgumu, Geita, Makonde na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha hizo umechelewa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Serikali ya India kusisitiza kuondolewa kwa aina zote za tozo na kodi ikiwemo VAT katika matumizi ya fedha hizo na kwa kuzingatia marekebisho kwenye Sheria ya VAT yaliyofanyiwa na Bunge mwezi Septemba, 2017 ambapo msamaha wa kodi hutolewa kwenye miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo.

Aidha, Bunge katika kipindi hicho, Bunge pia lilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, ambapo marekebisho yaliyofanyika yameweka utaratibu mpya ambao unamtaka Waziri wa Fedha na Mipango kabla ya kutoa misamaha ya kodi ya mapato ni sharti apate ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imetaarifiwa kuwa, tararibu zote zilizokuwa zinakwamisha upatikanaji wa fedha hizo zimekamilika na tayari Serikali ya Tanzania na India wamesaini mkataba wa kutoa fedha hizo. Fedha hizo zinatarajiwa kupatikana na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa sasa kinachosubiriwa ni utaratibu wa uchunguzi (*vetting*) kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutoa *exemption order* na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali ili fedha hizo zitolewe na kuanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua iliyofikiwa na Serikali, hata hivyo Kamati inaitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo sehemu iliyosalia ambayo inaihusu ofisi yake, hatua ambayo itawezesha kuanza kutekelezwa na hivyo kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha inapeleka majisafi na salama katika miji mikubwa kwa **asilimia 95**.

#### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mhe. Eng. Isaack A. Kamwelwe, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Katibu Mkuu Prof. Kitila Mkumbo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mгимwa Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb "
5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb "
6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb "
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb "
9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "
10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
11. Mhe. Lucy Simon Magereli, "
12. Mhe. Justine Joseph Monko "
13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb "
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb "
15. Mhe. Pascal Yohana Haonga "
16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb "
19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb "
21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb "
22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb "
23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb "

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Virgil Mtui, Ndg. Martha Chassama na Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)  
**MWENYEKITI,**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**  
**MIFUGO NA MAJI**

7 MEI, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye ukurasa wako 56 Mpango wa Maji Dar es Salaam, Ilala, Segerea, Kinondoni, hamna, lakini mpango wa maji taka Ilala umeuweka. Kwa hiyo, Ilala wanapokea majitaka, maji safi hakuna; Segerea hakuna. Kwa hiyo, mkija hapa mtujibu, Ilala, Segerea na maeneo mengi kama Kinondoni hakuna maji. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza kuchangia, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Julius Laizer na Mheshimiwa Adadi Rajab.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kwa moyo wa dhati kabisa kutokana na changamoto za maji nchini, Taarifa ya Kamati imeelezea changamoto kwa kina na Waheshimiwa Wabunge humu ndani wote tunajua umuhimu wa maji kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 174. Kwanza tu naomba nimwambie ukweli kwa sababu Mradi

wa Bunda maji ni kama mtoto wangu niliyemlea tangu nikiwa Mbunge wa Viti Maalum, naujua vizuri sana na kwa sababu nataka kulisaidia Taifa hili, nitasema ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, hivyo vituo ambavyo vinasemwa hapa vilivyojengwa ni Nyasura, Balili Msikitini, Balili Stoo na Kunzugu. Makubaliano katika ujenzi wa mradi huu wa maji, vituo vilikuwa vianzie kwenye chanzo cha maji Nyabehu. Hilo halijafanyika na kilichotokea Mamlaka yetu ya Maji Bunda ikaamua kujenga kituo kimoja Nyabehu. Vituo vingine vilivyokuwepo kama Tairo ni kituo ambacho chanzo chake ni ile miundombinu ya zamani, siyo mradi huu mpya, hilo Mheshimiwa Waziri naomba ulizingatie kweli kweli. Mradi huu wa maji Bunda kilikuwa kichaka cha watu kula fedha za Serikali ambazo ni kodi za wananchi kushirikiana na watoto wa vigogo na wewe unajua. Lazima tuseme haya, tunahitaji hii miradi ya maji ikamilike mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani miaka nane tunazungumzia chujio. Kuna habari nimezipata huko Wizarani kwako, aidha mmepigwa au mlikuwa mnataka kupigwa. Chujio la shilingi bilioni tatu mlikuwa mnaambiwa lijengwe kwa shilingi bilioni 12. Tunaipeleka wapi nchi hii? Kweli dhamira ya kumtua ndoo mwanamke kichwani itakamilika kwa ufisadi wa namna hii wakishirikiana na baadhi ya watendaji, ambao wengine mnawatoa Mtwara mnawaleta Bunda, mnawatoa Bunda mnawaleta Wizarani. Wizarani ambapo ndiyo kunasimamia miradi lukuki ya maji, hatuwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mradi wa Maji tu Bunda unachukua miaka kumi na bado haujakamilika ina maana mnahitaji miaka 100 kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji katika majimbo kumi, hilo haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, huu mradi wa Bunda ni wa muda mrefu sana. Akisimama Mheshimiwa Boniphace atakwambia hivyo hivyo, akisimama Mheshimiwa Kangi atakwambia hivyo

hivyo. Hatuhitaji Bunda Mkoa wa Mara kuwa kichaka cha wezi, tumechoka na hili tutaendelea kusema na tunaomba wachukuliwe hatua. Kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi walisema na Ofisi yangu ilitoa ushirikiano na bado baadhi ya wakandarasi na watumishi wengine wanapeta. Wanakula na nani? *Please*, huu wizi sisi hatuhitaji, tunahitaji miradi ikamilike wananchi wapate huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwako kunahitaji maji, Waheshimiwa Wabunge wote wanahitaji maji katika maeneo yao na hili nasema kwa dhamira ya dhati. Itokee sisi Wabunge na Mawaziri tukatiwe maji miezi mitatu, tu-*feel pinch* ambayo wananchi wetu wanaipata ya kukosa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia kumsaidia mwanamke kutua ndoo ya maji kichwani. Waheshimiwa Wabunge kwa miaka mitatu mfululizo mwaka 2015/2016 fedha zilizotengwa zikapitishwa na Bunge hili ni zaidi ya shilingi bilioni 485, zilizotoka ni shilingi bilioni 136 sawa na asilimia 28. Mwaka 2016/2017 fedha zilizotengwa shilingi bilioni 913, zilizotoka shilingi bilioni 250 sawa na asilimia 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka Aprili mwaka huu fedha zilizotengwa za maendeleo ni shilingi bilioni 673, zilizotolewa ni shilingi bilioni 135. Tunaenda mbele, tunarudi nyuma. Ie dhamira ya kuhakikisha mwanamke hatembe umbali mrefu kutafuta maji iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu mfululizo! Yaani badala ya kupanda, tunashuka. Asilimia 28, 25, 22, *why?* Halafu tunakuja hapa tunasema kweli tuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha tunamaliza tatizo la maji katika Taifa hili. Kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwenye Majimbo ya Vijijini kwenye mahospitali yetu kuna operesheni hazifanyiki kwa sababu maji hakuna hospitali. Naomba hili jambo



mliangalie kwa umuhimu wake. Wanawake wanateseka.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani sasa hivi bora umpelekee mgonjwa ndoo ya maji hospitalini kuliko chakula. Kama wawakilishi wa wananchi hali hii hatutaikubali. Hii *figure* nimetoa za miaka mitatu mfululizo, nikiwatajia hiyo ya miaka nane ni aibu tupu! Halafu bado tunakuja tunasema tuna dhamira ya dhati, kweli! Hata asilimia 40 tu tumeshindwa kufikisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza sekta ya umwagiliaji; tunawahamasisha vijana *graduate* kwenda kulima kilimo cha umwagiliaji. Mwaka 2015/2016 mahitaji ni shilingi bilioni 400. Bunge hili tulipitisha shilingi bilioni 53 kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji. Fedha zilizotoka ni shilingi bilioni tano; asilimia 10, *shame!* Shilingi bilioni tano! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wangu wa Nyatwali wana *project* kubwa sana ya kilimo cha umwagiliaji; kwa pesa hii inawezekanaje? Wale wa kwa Karukekere kwa Mheshimiwa Kangi, Mgeta kwa Mheshimiwa Boniphace na maeneo mengine! Lazima tuseme haya mambo, hatuwezi kuyafumbia macho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira zimekosekana, vijana wamehamasika kwenda kuwekeza kwenye kilimo. Kwa pesa hizi! Haya mwaka huu Bunge tulipitisha shilingi bilioni 24, zimetoka shilingi bilioni nne tu kwenye kilimo cha umwagiliaji. *Four billion*, halafu tunakuja hapa kwa mbwembwe nyingi kwamba tunataka kuboresha kilimo cha umwagiliaji. Kweli tuko *serious?* Tunaguswa na maisha ya Watanzania? Tunaguswa na tatizo la ajira la vijana wa nchi hii ambao wameona Serikali haiwezi kuajiri, wameenda kujijiri kwenye kilimo cha umwagiliaji, kwa pesa hizi tutazigawaje? Hata kama sungura mdogo kiasi hiki, hata mkia hauwezi ukatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine miaka yangu yote nane ya Ubunge nimesikia upotevu wa maji DAWASCO ni ule ule asilimia 47. Ukienda kwenye ripoti ya CAG

wamesema walishauriwa kununua chombo ambacho kitasaidia kudhibiti tatizo la upotevu wa maji. Mpaka leo kimya. Wizara yako inasemaje? Au kuna mradi wa watu hapa? Tunataka tujue. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Laizer, ajandae Mheshimiwa Adadi Rajab.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini kabla sijachangia naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais mwaka 2015 wakati anazindua Bunge hili aliposema maneno haya; "Wakati wa kampeni nimekutana na malalamiko mengi na ukosefu wa maji vijijini. Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kwamba inaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kufikia asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2020. Tutakamilisha miradi iliyokwishaanza na kuanza miradi mipya na tunataka tuwatue akina mama ndoo kichwani. Tunatambua umaskini hauwezi kuondoka nchini kama wananchi hawapati maji safi na maji salama."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili bajeti ya Wizara ya Maji ambapo hata wewe pamoja na kuwa uko kwenye Kiti umeshindwa kuvumilia maana hupati nafasi ya kuchangia, umezungumza habari ya uhitaji wa maji katika eneo lako. Uhitaji wa maji katika Taifa hili imekuwa ni janga kubwa sana na Bunge hili ni lazima lifanye uamuzi ambao utaisaidia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia vitabu vilivyopita, nimeangalia Wizara ya Afya ina *page* 47; nimeangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina *page* 45, nimeangalia vitabu kama vitatu, vinne hivi. Kitabu hiki cha Maji kuonesha kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza iliyoahidi ina *page* zaidi ya 280. Hii ni kuonesha kwamba maneno mengi ni kutafuta kujitetea badala ya kutekeleza kile ambacho tumeahidi. Kama Serikali ingetekeleza asilimia

hata kumi ya kilichoandikwa humu, Taifa hili lingefika mahali pazuri na tungeondokana na tatizo la maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *REPOA* ya mwaka 2018, asilimia 42 ya Watanzania wanakiri kwamba tatizo la maji limekuwa kero zaidi ya asilimia 34 ya mwaka 2014. Kadri siku zinavyokwenda, *population* ya Watanzania inaongezeka. Kwa hiyo, hata kama tungekuwa na maji kidogo miaka ya nyuma, kadri siku zinavyoenda lazima uhitaji wa maji uwe mkubwa. Mipango ya Serikali katika kutafiti, hebu tusaidieni mnataka Watanzania waishije ili akina mama waache kupoteza usiku na mchana kutafuta maji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM ambayo imeahidi kwenye Ilani ya CCM ya 2015, imesema itasaidia upatikanaji wa maji kutoka 67% mpaka 85%. Leo mnapeleka bajeti kwa asilimia 22, leo mnapeleka bajeti kwa asilimia 15, mnataka sisi tuamini nini mnachotuahidi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda mbele, katika Kamati wanasema asilimia ya bajeti iliyopelekwa ni 22%, lakini Mheshimiwa Waziri anasema 56%. Kwa mujibu wa kanuni, taarifa zote zinazokuja Bungeni lazima zipitishie kwenye Kamati, Kamati i-verify. Nataka Mheshimiwa Waziri atuambie, tuamini taarifa ipi kati ya Kamati inayosema mmepeleka 22% na wewe unayesema tumepeleka 56%? Tunamdanganya nani hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili linahitaji maji. Mwaka 2017 tulisema tunataka angalau tuweke shilingi 50 kwa ajili ya maji vijijini, mkakataa. Mkatuambia mna fedha kutoka India dola milioni 500. Kwenye kitabu hakuna hata nusu *page*, hata nusu maneno uliyoahidi kwamba hizo fedha ziko wapi? Kwa hiyo, mnakuja mnadanganya Bunge ili tupitishie bajeti, lakini ukienda kwenye utekelezaji mnasahau hata maneno yenu ambayo mliyasema mwaka 2017. Fedha zile za India hiyo dola milioni 500 ziko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnashindwa kutekeleza bajeti hii kwa sababu tunawashauri wekeni fedha kwenye

mafuta, hamtaki. Mnatafuta fedha hampati; lakini mnakuja hapa Mheshimiwa Waziri unatuambia mmepeleka hela ya maji kwa asilimia 26, halafu usiliombe Taifa radhi kwa kuacha Watanzania wateseke, halafu mnasema mnawasaidia akina mama. Badala ya kuwasaidia kuwaondoa ndoo kichwani, mnawatwisha ndoo kichwani, yaani mnaweka juu ya ndoo. Hata Naibu Waziri amejiridhisha, anasukuma kila siku toroli ya madumu ya wanaotafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza ahadi hizi ni lazima Serikali ioneshe *commitment* nzuri ya kupeleka fedha. Naomba kama Bunge tukubaliane tuweke shilingi 50 ili tupate fedha ya kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya vijijini. Bila hivyo hili tatizo litakuwa kubwa na maneno mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni mazuri sana na ni mengi mno, lakini utekelezaji wake kama hauna fedha huwezi kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuhusu Mamlaka ya Maji katika maeneo ya Halmashauri ambapo Serikali iliahidi kutekeleza kwa kusaidia fedha za ruzuku kwa ajili ya kujiendesha. Mheshimiwa Waziri atusaidie, kama Serikali iliahidi kutekeleza na kusaidia, kwa nini fedha haziendi na mpaka mwisho *TANESCO* inawakatia wananchi umeme na sisi tunakosa maji kwa kosa ambalo siyo la wananchi. Maana wananchi wanalipa *bills* zao lakini Serikali haipeleki. Kwa nini Serikali isiadhibiwe mnaadhibu raia ambao hawana makosa wala hawahusiki katika hili jambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnashindwa kuchangia jambo hili, msemi hamuwezi kuliko kutudanganya na kuwaumiza wananchi wetu. Tukimpigia Mheshimiwa Waziri wa Nishati anasema sihusiki, tukimpigia mtu wa Hazina anasema hahusiki. Nani anahusika katika madeni haya ambayo mnawanyanyasa na kuwatesa Watanzania? Mnakata umeme kwenye maji ambayo akina mama wako hospitalini! Akina mama wanajifungua ninyi mnakata maji, hamjali. *Sense of human* iko wapi katika jambo hili na kosa siyo la kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme machache katika Jimbo langu, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, ahadi ya Serikali ya kukarabati mabwawa katika Kijiji cha Esilalei ambao Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa ziara yake ya kuomba kura, inatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa maji wa Monalo na Mheshimiwa Waziri anakuja, maana alikuja Monduli. Tangu 2011 mpaka leo wananchi wanaendelea kulalamika hawapati maji na ule mradi umegharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili. Huo mradi unakamilika lini na Serikali inapata ukakasi gani kuwashughulikia wote wanaokwamisha mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni miradi ya umwagiliaji; katika miradi ya umwagiliaji Mheshimiwa Waziri anafahamu, alikuja na nilimtembeza pamoja na umri wake lakini alitembea. Tulienda Selela akaahidi, tulienda Mto wa Mbu akaahidi, tulienda Engaruka akaahidi kwamba watatupatia fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde hayo. Kwenye bajeti hii sijaona hata mahali ametaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anatutakia nini? Mbona tulimpokea vizuri naye alituahidi mengi? Mbona sioni hata nusu ya alichotuahidi kutusaidia? Alituahidi kutengeneza kile chanzo cha maji Ngaramtoni Mheshimiwa Waziri alifika mwenyewe, Monduli ilikosa maji akatuahidi. Mheshimiwa Waziri tumemkosea nini au tulimpokea vibaya? Wananchi wa Monduli wamekukosea nini? Alituahidi! Hakuna kwenye kitabu chake hata mahali ametaja hata ahadi moja aliyoahidi, kosa letu nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri ulikuwa unatudanganya uondoke au ulikuwa unamaanisha kutusaidia kutatua matatizo ya maji? Ninaomba uniambie, wananchi wa Monduli wanakuamini na uliwaahidi, katika ahadi zako zote, mwaka huu unatutekelezea nini? Hakuna hata moja umetaja. Mheshimiwa Waziri kwa nini? Tumekutembeza Jimbo zima, tumeweka mafuta zaidi ya magari 20 tumekusindikiza,

tumeenda na wataalamu, tumekuletea maandiko Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mapendekezo matatu; moja, kwa kuwa miradi hii ya vijiji kumi na miradi mingi inaonekana haitoi maji kwenye nchi hii, naomba Serikali ifanye *special auditing* kwenye miradi yote ya maji ya nchi hii ili tujue ni miradi mingapi inafanya kazi na miradi mingapi haifanyi kazi mtuletee Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani nilishawishi Bunge tuweke azimio kwamba hatutapitisha bajeti ya Wizara hii mwakani mpaka mmetuletea *special auditing* ya miradi yote ya maji, maana mnatengea fedha miradi lakini ukienda kwenye mradi, hakuna maji. Tunataka kufanyike *special auditing* kwenye miradi yote ya maji nchi hii. Tufahamu ni miradi mingapi inatoa maji na mingapi haitoi maji. Tuna *value for money*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kumwambia Mheshimiwa Waziri kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli waliwahi kuleta fedha za *consultant* aliyekuwa anasimamia ile miradi hakufanya kazi, lakini Wizara ilituma fedha tulipe, nikasema hailipwi. Wizara inaniambia kwa nini unazuia, kwani ni hela zako? Nikasema huyu mtu hakufanya kazi, hakustahili kulipwa. Imekuwa ni uchochoro wa kupitisha fedha za Serikali. Wale wanaoitwa *consultant* wanawambia walete *engineer* wanaleta hawa ma-*technician* wao mimi siwajui majina yao, lakini hakuna wanachofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni muhimu Serikali ifanye tathmini ya miradi ambayo imetekelezwa na imekamilika na ambayo hajjakamilika na iseme kwamba ni lini miradi hii itakamilika. Tumechoka na ahadi ya kwamba miradi itatekelezwa, miaka 10, miaka 15 mnatekeleza tu. Tutaanza lini mpya? Maana hakuna hata mradi mmoja mmeanza upya mnatekeleza ile ya zamani tu. Hata ule wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Nzega ni ya zamani mnatekeleza. Mnamaliza lini mwanze hii mipya? Ni muhimu

mkatuambia kila mradi unaanza lini na unakamilika lini ili wananchi wawe na imani ya kwamba Serikali inafanya kazi na wao kuna siku watapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Adadi Rajab, jandae Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hoja hii ya maji ambayo ni muhimu sana. Tatizo hili sijui kama ni sugu au ni donda ndugu au ni nini, lakini ni tatizo kubwa sana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mambo mengi sana katika kipindi cha miaka miwili na nusu. Tumeshuhudia mambo mengi kwenye sekta mbalimbali za afya, miundombinu, lakini sekta ya maji bado Awamu ya Tano haijashughulikiwa ipasavyo. Nashauri sasa hivi mwelekeo uende kwenye maji. Suala hili sasa hivi ni tatizo siyo katika Jimbo la Muheza tu, Jimbo la Muheza naweza kusema sijui ni sugu au ni donda ndugu, lakini ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu juhudi ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wanashughulika sana kutatua tatizo la maji, lakini hawana hela. Mipango ambayo ipo kwenye kitabu hiki kama ingetekelezwa ninaamini kabisa tungeweza kupunguza sana tatizo la maji. Kama mambo ambayo yametajwa kwenye kitabu hiki fedha zingeenda kutolewa, basi tatizo hili tungeweza kulipunguza kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona aibu sana kwa sababu Tanga sasa hivi kuna miradi mikubwa ambayo inakuja na unapopita kwenda Tanga huachi kupita kwenye Jimbo la Muheza, ni lazima upite Muheza. Ninyi ni mashahidi Waheshimiwa Wabunge, unapopita Muheza unapopita

Lusanga unakwenda Mkanyageni, Ngomeni, Kilapula unakaribishwa na madumu ya maji barabarani. Madumu ya maji watu wanasubiri kwenda kuchukua maji Tanga. Sasa hii kitu inanisononesha sana na ninaona aibu sana. Kwa kweli suala hili ni gumu na ninaomba sana Wizara iweze kuliangalia kwa sababu ndiyo miradi ipo mingi, lakini inachelewa kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Wizara kwa kuanzisha mradi wa Pongwe. Pongwe mpaka Muheza tumechukua maji na huo mradi umeanza kufanya kazi. Nawashukuru sana tena sana kwa sababu mradi huu tuliutegemea tuufungue mwezi huu, lakini naona itashindikana labda baada ya miezi miwili au mitatu ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashukuru kwa sababu Mheshimiwa Waziri wenyewe na Maofisa wake wote kwa kweli wanashughulika sana ili kuhakikisha kwamba haya maji yanafika Muheza Mjini kama ilivyopangwa ili wananchi wa Muheza waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Wizara kwa kuweza kuangalia vyanzo, vijiji vingi vya Mashewa kule Amani ambavyo vinazungumza Mto Zigi vimeweza kupata maji, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi bado nina miradi ya vijijini, najua nimepangiwa hela hapa karibu shilingi bilioni 1.169 na ninaamini kabisa kwamba kuna miradi ambayo tuliipanga kwenye mwaka uliopita haikutekelezwa. Mradi wa kutoa maji kutoka Mto Pangani wa Kirongo, Mradi wa Uмба – Ngomeni, Mradi wa Mkwakwa – Mafleta na mradi wa Tongwe. Hii miradi ipo kwenye hatua za kuwekewa *sign*. Sasa tunaamini kabisa kwamba haitasita na tutaendelea ili iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho nimesikitika sana ni hii miradi 17. Miradi 17 ya mkopo wa India dola milioni 500 imekuwa kama ni kichekesho sijui ni sindimba au ni nini. Miaka miwili iliyopita tumeambiwa hapa, Waziri



Mkuu wa India amekuja ameweka saina ikulu pale, miradi 17 Muheza ikiwemo, sasa hivi hapa Mheshimiwa Waziri kwenye taarifa yake anasema majadiliano yanaendelea. Mwenyekiti wa Kamati anasema *issue* ipo kwenye *vetting* kwa *Attorney General*. Sasa sijui tuamini ipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup* atuhakikishie kwamba kweli hiyo *financial agreement* imeshasainiwa? Maana yake tatizo lilikuwa ni *financial agreement*, kila siku *financial agreement*, sasa imeshasainiwa ili tuweze kujua kama ni nini? Kama ipo kwa *Attorney General*, hiyo *issue* ya *vetting*, *Attorney General* imefikia wapi? Hiki kitu miaka miwili na nusu inazungumzwa hapa! Ninaamini miradi hii ingeanza, ingeweza kupunguza sana tatizo la maji kwa sababu ni miradi ambayo ime-*cover* karibu nchi nzima mpaka Zanzibar, sasa kwa nini haitekelezwi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni suala la tozo ya mafuta. Hili suala ni la muhimu sana kwa sababu takwimu zinaonesha kwamba hizi tozo hata Hazina hawaziingilii, zinakwenda moja kwa moja na Wizara ya Maji wanazishughulikia hizi. Ukishapeleka hati mara moja tu unapewa hela zako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria kwamba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono wazo lililotolewa na Mwenyekiti wa Kamati, lazima tozo hii ya shilingi 50 iongezwe iwe shilingi 100. Kwa kweli bila kufanya hivyo Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Fedha wakati wa kupitisha *Financial Act* hapa itakuwa ni matatizo. Hatutakaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona muda haupo kwangu, nakushukuru sana na ninashukuru kwa kupata nafasi hii na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Lupembe, ajiandae Mheshimiwa Lucia Mlowe kwa dakika tano.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa ajili ya wananchi pamoja na akina mama. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na sasa hivi tupo muda huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpungeze Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake, Kaka yangu Mheshimiwa Kamwelwe kwa kazi kubwa nzuri anaoyoifanya, anafanya kazi nzuri sana lakini Wizara yenyewe ndiyo ngumu, wananchi wanatakiwa watuliwe ndoo ya maji kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nizungumzie Mkoa wangu wa Katavi hususan Wilaya ya Mpanda, Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi. Naomba niipungeze Serikali ilileta miradi; Mradi wa Ikorongo I na Ikorongo II, lakini siku hadi siku watu wanaongezeka. Tulivyotegemea kuwa labda Ikorongo I katika vyanzo vile vya maji, yale maji yanaweza kututosheleza wananchi wa Wilaya ya Mpanda, imekuwa tofauti. Naishukuru Serikali haikuchoka, ikaongeza mradi mwingine tena wa Ikorongo II, lakini bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana ndani ya Wilaya ya Mpanda hususani pale mjini. Serikali ilijitahidi kutuletea maji, mabomba yale makubwa, lakini bado ndani ya maeneo yetu, miundombinu ya maeneo husika ambayo yanatakiwa yapelekwe maji hatukuweza kubadilisha ile miundombinu, ipo vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya zamani, ilikuwa ni yale mabomba ya zamani ya chuma. Mabomba ya chuma yanaota kutu. Sasa kama yanaota kutu, sidhani kama yanaweza kuchukua au kubeba mzingo mzito ambao unakuja kutoka katika matenki yetu. Maana yake maji kwenye matenki yanajaa, lakini sasa kwenye kupita njiani kule, lazima kuna mfumuko yale maji yanaweza kuvuja na mabomba yanapasuka. Sasa imekuwa shida sana pale Wilaya ya Mpanda maji ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Serikali bado ina jitihada kubwa na sasa hivi kwenye bajeti ya Wilaya ya Mpanda nimeona shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya marekebisho mbalimbali kwa ajili ya matengenezo pale mjini. Bado kunatakiwa kazi kubwa sana kwa sababu wananchi wa Mpanda hawana maji kabisa sasa hivi, hususani Makanyagio, Majengo na Kashaulili ambapo ndiyo katikati ya Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi pale Wilaya ya Mpanda. Hawana maji kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia huu mradi wa Ikorongo, tulijenga magati Ilembo na Airtel. Magati haya katika Kata ya Ilembo, sasa hivi hayatoi maji kabisa. Airtel nako kwenye yale magati hayatoi maji. Katika huu Mradi wa Ikorongo nao vilevile haujaweza kutimiliza kwa sababu wataalam wamesema yanaweza kufika asilimia 50 tu wananchi wa Mpanda wakapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mwenyezi Mungu ametupa bahati kubwa sana. Ninashukuru Serikali kwa Mkoa wa Mwanza na Shinyanga wametoa maji kutoka Ziwa Victoria, Mungu ametupa neema yake, tumepata maziwa na mito. Sasa naomba nasi ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, Mungu ametupa neema, tuna Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakitupa maji ya Ziwa Tanganyika, shida ya maji itakwisha kabisa katika Mkoa wa Katavi kwa sababu maji ya Ziwa Tanganyika yatatumika ndani ya Wilaya yetu mpya ya Tanganyika; Wilaya nzima itapata maji ya Ziwa Tanganyika, tutakuja sisi Wilaya ya Mpanda na Halmashauri ya Nsimbo wote watapata maji ya Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu sikivu na kaka yangu Mheshimiwa Kamwelwe, sasa hivi afanye mipango ya kuleta maji kutoka Ziwa Tanganyika ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupumua kwa sababu maji vijijini hakuna na ukiangalia Makao Makuu ya Mkoa hatuna maji. Naomba sana hilo liweze kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, katika Mkoa lazima sasa tuanze *system* ya majitaka. Ndani ya Mkoa wetu wa Katavi hatuna *system* ya majitaka kabisa wala gari na matokeo yake mvua zikinyesha ni adha kubwa sana ndani ya Mji wa Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu sikivu, iweke mipango mikakati, nimemsikia Mheshimiwa Waziri kuna sehemu ambayo tayari miundombinu ya majitaka kwa mikoa kadhaa basi sasa na sisi Mkoa wetu wa Katavi ni mkoa, Wilaya ya Mpanda ni Makao Makuu ya Mkoa, tuanze sasa hivi mpango wa kujenga majitaka au basi tutafutiwe gari la kuweza kunyonya majitaka kwa sababu hatuna gari, hatuna kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye umwagiliaji; ninaishukuru Serikali, mipango ni mizuri sana ya umwagiliaji, lakini sisi tulijengewa miradi ya umwagiliaji Urwila, Ugala, Halmashauri ya Nsimbo, Kamsisi na Kata ya Mbede, lakini ile miradi sijaona kama imefanya kitu chochote. Naomba niulize swali moja, Mheshimiwa Waziri, hii miradi ya umwagiliaji hivi kwa nini tunatumia gharama kubwa sana lakini wananchi hawanufaiki kabisa. Leo hii ukiniambia Urwila wamenufaikaje kwa umwagiliaji, hakuna wananchi wa Urwila waliofaidika kwa ajili ya umwagiliaji na pesa nyingi sana zimetumika pale. Vilevile Kamsisi na Ugala pesa nyingi sana zimetumika, halafu tukija Mbede pesa nyingi zimetumika lakini miradi ya umwagiliaji bado hatujafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba Serikali ijipange upya, miradi ya umwagiliaji bado hatujafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inaendelea kufanyika, lakini ninaomba kuunga mkono hoja Mamlaka ya Maji Vijijini. Mamlaka hii itatusaidia sana kwa sababu wananchi wa Vijijini wengi wao ndani ya vijiji vyetu hatuna maji, lakini mamlaka hii ikiundwa itatusaidia sana kwa sababu itafanya kazi vizuri. Tulianzisha *TARURA*, tumeona jitihada za *TARURA*, nafikiri

tukianzisha Mamlaka ya Maji Vijijini nayo inaweza kutusaidia sana akina mama, tutawatua ndoo kichwani. Naomba niunge mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba katika ile shilingi 50 tuongeze iwe shilingi 100 ili sasa mamlaka hii iweze kuwa na nguvu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako umekwisha.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana naomba nipongeze.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlowe, dakika tano.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na miundombinu mibovu ya maji katika Halmashauri zetu. Katika Halmashauri zetu, miundombinu ya maji ni mibovu sana ndiyo maana kuna upotevu wa maji. Kwa mfano, katika Ripoti ya CAG ya mwaka 2016/2017 inaonesha upotevu wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 huko Babati peke yake. Tuone ni namna gani tunapata hasara ya upotevu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hapa Dodoma peke yake, karibu kila siku mabomba yanapasuka. Hii inatokana na kuweka mabomba yenye kiwango cha chini. Namwomba Mheshimiwa Waziri kufuatilia suala hili na kuhakikisha upotevu huu wa maji unadhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije suala la bili za maji. Kuna watu wanaletewa bili za maji mpaka shilingi milioni mbili kwa mwezi, kwa kweli ni janga. Tumekuwa tukilalamika kila

siku tukaambiwa hizo bili zitarekebishwa, lakini tatizo linaendelea. *(Makofi)*

Naomba kuuliza kwa Mheshimiwa Waziri, ni tatizo gani linalosababisha hizi bili ziendeele kupanda siku hadi siku. naiomba Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri, suala hili la bili za maji lishughulikiwe haraka iwezekanavyo kwa sababu wananchi wetu wanaumia. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge wengi kati yetu tunapata bili hizo kubwa na ukienda kuwaonesha wanasema tunarekebisha, lakini hawarekebishi. Sasa kama inatokea hivi kwetu sisi Wabunge, je, wananchi wa kawaida inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la mikataba mibovu ya maji. Karibu nchi nzima kuna tatizo la mikataba mibovu na kusuasua kwa miradi ya maji. Nitoe mfano wa mikataba mibovu ya maji ambayo baada ya muda mfupi inavunjwa. Mfano, Mkoa wangu wa Njombe kuna mradi wa Lugenge, Utalingolo na lhalula. Mradi huu ni wa mwaka 2013. Yule mkandarasi aliyewekwa kukamilisha mradi huu, mkataba ule ulivunjwa baada ya miezi mitatu na baada ya kuvunja ule mkataba yule mkandarasi alishitaki na baada ya kushitaki alishinda kesi yake. Hata baada ya kushinda hadi leo hii hajalipwa pesa zake, alitakiwa alipwe shilingi milioni hamsini hajalipwa na mradi huu hadi leo hakuna kinachoendelea na mabomba yamelala tu hapo. Naomba suala hili Mheshimiwa Waziri alifuatilie haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine vilevile wa Lwangu umetekelezwa na mkandarasi na hela zile za mwanzo zimepotea. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri afuatilie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ukosefu wa maji. Ukosefu wa maji ni janga la nchi hii. Ukiangalia maeneo mengi yana vyanzo vya maji, yana maji ya kutosha, lakini bado kunakuwa na tatizo la maji. Kwa mfano, Njombe inazungukwa na mito ya maji, lakini nenda pale Njombe Mjini unakuta watu wanapata maji mara moja kwa wiki.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Waziri ni tatizo gani? Ninaomba tafadhali fuatilia suala hili kuhakikisha hiyo miradi ambayo mmeahidi, basi itekelezwe kwa wakati. Tumekuwa tukiahidiwa sasa muda mrefu lakini hakuna utekelezaji. Siyo hiyo tu, kuna Wilaya ya Ludewa, vijiji vya Mkomang'ombe wananchi wale kwa kweli wanatia huruma. Wamekuwa wakiahidiwa kupatiwa maji... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Sokombi.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Joyce B. Sokombi jandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kuwapongeza viongozi na watendaji wa Wizara hii, tukianza na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe kwa kazi yake nzuri anayoifanya, vilevile Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo na Naibu Katibu Mkuu, *Engineer* Kalobelolo, hongereni sana.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi mnazozifanya tunazona na jinsi mnavyohangaika kurekebisha sekta ya maji na mna nia njema ya kumtua mama ndoo lakini changamoto kubwa ambayo mnakabiliwa nayo ni ukosefu wa fedha, lakini kwa fedha chache zilizopo matokeo tunayaona, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tukabiliane na tatizo hili la fedha ambazo Wizara hii muhimu na nyeti na ambayo inamgusa kila mwanafamilia asubuhi anapoamka basi niungane na wazo ambalo limetolewa na Kamati na wazo ambalo limetolewa na baadhi ya Wabunge, kwamba sasa ni muda muafaka wa kuhakikisha kwamba ile tozo ambayo mwaka jana tuliahirisha kwamba tusiongeze shilingi 50, mwaka huu tuongeze ili tupate fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni ushahidi ulio wazi, kama Kamati ilivyosema vizuri kwamba fedha ambayo ina uhakika ni fedha ya Mfuko wa Maji, kwa hiyo tuongeze tozo kwenye Mfuko wa Maji ili tupate fedha za kuwezesha kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna maendeleo bila maumivu. Kwa hiyo tuongeze shilingi 50 kwenye maji, tutaumia kwenye mafuta lakini kwenye utekelezaji wa miradi ya maji matokeo yataonekana, hivyo na mimi naunga mkono kwamba tuongeze hiyo tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utajikita kwenye miradi ambayo inafadhiliwa na fedha kutoka nje. Inawezekana Wizara inatoa taarifa hizi mapema sana kwa sababu miradi inachukua muda mrefu. Katika Mkoa wetu tuna mradi wa maji wa Makonde na tulishaambiwa kwamba kuna fedha, dola milioni 87 kutoka mkopo wa India na ni zile fedha za miradi 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi hata viongozi wetu wa kitaifa nakumbuka mwaka juzi, Mheshimiwa Makamu wa Rais alifanya mkutano mkubwa pale



7 MEI, 2018

Tandahimba na akawaambia wananchi wa Tandahimba kwamba tatizo la Mradi wa Makonde sasa limefika mwisho tumepata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Makonde unahusisha Halmashauri nne ambazo ni Halmashauri ya Newala, Halmashauri ya Mji Newala, Halmashauri ya Tandahimba na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. Kwamasikitiko makubwa Kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika amekuwa akielezea mara kwa mara kwamba mradi huu ulijengwa wakati wa mkoloni, unahitaji ukarabati mkubwa, lakini kwa masikitiko makubwa fedha hizi hadi leo hazijapatikana na ukiangalia ule ukurasa wa 72 utakuta bado majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Serikali yangu sikivu kwamba sasa mharakishe haya majadiliano. Hiyo *finacial agreement* isainiwe ili hii miradi 17 sasa ianze kutekelezwa. Kwa sababu ukiangalia kitabu cha mwaka 2016/2017 maelezo yapo, 2017/018 maelezo yapo na sasa hivi 2018/2019 maelezo ni hayohayo. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Fedha iharakishe hayo mazungumzo sasa..

## **T A A R I F A**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza, Mheshimiwa Chikota, anaongea kwa hisia sana juu ya Mradi wa Makonde ambao umejengwa mwaka 1953, kwamba fedha hazijapatikana. Sasa nimpe taarifa tu kwamba Waziri wa Fedha ndiyo mtoaji wa fedha na hapa hayupo ndani ya Bunge hili.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake, lakini Serikali ipo hata kama Waziri wa Fedha hayupo, Serikali ipo kwa hiyo *message* itafika kwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mtwara tuna mradi mwingine ambao mzungumzaji aliyetoa taarifa naye unamgusa vilevile, mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma na kupeleka Manispaa ya Mtwara. Mradi hii vilevile ni wa mkopo kutoka *Exim Bank* ya China, lakini huu mwaka wa tatu sasa fedha hizo hazijapatikana na mradi haujatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hii miradi ambayo inachangiwa na wahisani tuweke kwenye taarifa zetu pale tunapokuwa na uhakika kwamba fedha sasa ziko tayari, la sivyo mnatupa kazi wanasiasa, tunapokwenda kule tunaulizwa na wananchi. Kwa sababu taarifa hizi sasa wananchi wanazo, kwamba kuna fedha za utekelezaji wa mradi kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara. Mheshimiwa Waziri wa Maji wewe unafahamu mradi huu vizuri, ulishatembelea kule na umezunguka maeneo yote na unaona shida ya maji ya Vijiji vya Chawi, Maembechini na maeneo mengine ya Kitae, kwa hiyo nafikiri hili litafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji; kama nilivyosema, Wizara inafanya kazi vizuri sana, mmerekebisha upelekaji wa fedha, mmerekebisha hata mgao wa fedha. Ukiangalia hiki kitabu ukurasa wa 114 kila Halmashauri imeweka kiasi ambacho watapata ila changamoto iliyopo hamuweki fedha za usanifu wa miradi. Mradi hauwezi ukafikia hatua ya kutangazwa bila kusanifiwa, fedha hizo hamuweki. Hivyo, inailazimu Halmashauri ikope kwenye vyanzo vingine mradi usanifiwe, utangazwe hiyo *tender document* itoke ndiyo baadae mkandarasi akipatikana *a-raise certificate* Wizara ndiyo mnaanza kulipa. Kwa hiyo, naomba hapo Wizara hebu mrekebishe, muweke fedha kidogo kwa *council* ili waweze kufanya hizo kazi za awali.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango Mradi wa Maji wa Mitema – Lienje – Nanyamba. Kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali yangu ya Awamu ya Tano na kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa sababu ulifika Mitema, naona umetenga shilingi milioni 600, nakushukuru na kukupongeza sana, lakini andiko la awali la mradi huu gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni kumi na moja (11)).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipokea hii shilingi milioni 600 kwamba tutaanza na utekelezaji wa mradi lakini Mheshimiwa Waziri hebu katika bajeti ijayo basi muweke fedha za kutosha ili mradi uweze kutekelezwa kwa wakati lakini pia kwa eneo kubwa la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mkubwa sana utahusisha takribani kata tisa, vijiji 35 na wewe eneo hili umelitembelea na ni muhimu kwa Mkoa wa Mtwara, kwa hiyo nakuomba kwenye bajeti ijayo basi tutenge fedha za kutosha ili mradi huu wa Mitema – Lienje – Nanyamba uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie vilevile kuhusu wazo la kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini. Hili ni suala zuri na ni suala ambalo kila mtu anaunga mkono, lakini tuwe na tahadhari wakati wa kuanzisha, kwamba tujiandae. Wakati wa Wizara ya TAMISEMI tulikuwa tukiilaumu *TARURA* hapa kwa sababu tumeanzisha *TARURA* bila kuwa na maandalizi ya kutosha kwa hiyo Wakala wa Maji Vijijini hebu tuwe na fedha ya kutosha ili watekeleze miradi yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Amina Mollel hayupo. Mheshimiwa Sokombi kwa dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Mipata.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi nami kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua fika kwamba maji ni uhai, 2016/2017, fedha za maendeleo zilikuwa shilingi bilioni 915.1 lakini hadi kufikia Machi, 2017, zilitolewa asilimia 17.8 tu na 2017/2018 fedha za maendeleo zilikuwa shilingi bilioni 408.6 lakini hadi kufikia Machi, 2018 zilitolewa asilimia 22 tu, maana tumeona pia hata kwenye kitabu cha Kamati imeelezea hivyo kwa fedha za maendeleo na asilimia 1.8 tu kwa fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Maji Fungu Namba 05 zimeainishwa shilingi bilioni 5.6 tu na hadi kufikia Desemba, 2017 hakuna fedha za ndani zilizotoka, zilitoka fedha za nje tu ambazo ni asilimia 1.8. Kufikia mwaka 2018 Serikali na wadau wa maji walijenga vituo 125,086 vya maji vijijini ambavyo ilikuwa vihudumie watu milioni 30.9, sawa na asilimia 85.2 ambao ni wananchi milioni 36.3 waishio vijijini. Jambo la kusikitisha vituo vinavyofanya kazi kati ya hivyo vituo vyote ni vituo 86,877 tu ambavyo vinahudumia watu milioni 21.7 sawa na asilimia 59.8 ya watu waishio vijijini. Kwa hiyo kuna hasara ya vituo 38,209 havifanyi kazi, sawa na asilimia 30.5 ya vituo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu cha Waziri sijaona mahali popote ambapo wameelezea namna ya kuvikarabati vituo hivyo au kuhakikisha vituo hivyo vinafanya kazi. Sasa tunasema kwamba tunahitaji kumtua mwanamke ndoo kichwani, kwa hali hii ukiangalia kweli mwanamke wa kijijini tutamtua ndoo kichwani? Ndivyo wanavyoishi watu wengi vijijini, sisi tuko mijini maji yakikatika kidogo tu tunaanza kulalamika, je, wale akina mama wanaoamka saa kumi alfajiri kwenda kufuatilia maji? Haya, ameamka saa kumi alfajiri, kurudi saa sita mchaa! huyu mwanamke ataleta maendeleo kwenye familia kweli? Tunahitaji watu wa vijijini wawe na maendeleo, walete maendeleo, kwa hali hii anahangaikia maji muda wote maendeleo atayafanya saa ngapi? *(Makofi)*

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishauri Serikali, hasa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango atueleze fedha zinazoidhinishwa za mwaka jana kwanza zilienda wapi? Zinavyoidhinishwa ihakikishwe fedha zote ziende kwa wakati ili miradi ifanye kazi kama inavyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, mimi ni mwanamke, nawaonea huruma sana wanawake wenzangu wa vijijini. Tunaomba tafadhali sana, tunajua pale Mheshimiwa Waziri wa Maji hakikisha unaongea na Waziri wa Fedha unapata pesa kwa wakati ile miradi ifanye kazi vijijini. Kwa mfano, Mkoa wangu wa Mara tumezungukwa na Ziwa Victoria mwaka jana niliongea hapa, tumezungukwa na Ziwa Victoria, lakini fikiria Serikali inaweza kutoa maji Ziwa Victoria inapeleka maji Shinyanga, lakini sisi wa Mkoa wa Mara hatuna maji, inasikitisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tafadhali sana hakikisheni Mkoa wa Mara tunapata maji hasa Bunda hatuna maji ya kutosha, Musoma Vijijini hatuna maji ya kutosha. Pale Musoma tu tupo lakini hatuna maji ya kutosha, Tarime ni sehemu ya mjini tu, sehemu za vijijini watu hatuna maji ya kutosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako wa dakika tano umekwisha. Mheshimiwa Mipata hayupo, Mheshimiwa Bobali ajiandae Mheshimiwa Maftaha Nachuma na ajiandae Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Mheshimiwa Waziri amekuwa akifanya kazi kubwa ya kuzungunguka kwenye Mikoa yetu kufuatilia shida ya maji na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hilo tu mnalifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa kwamba kama Wabunge tunakubaliana mimi ningetoa hoja ama mtu yeyote atoe hoja kwamba Wizara hii tusiipitiche mpaka Waziri

7 MEI, 2018

wa Fedha aje kutoa *commitment* ndani ya Bunge kwamba kwa nini fedha za miradi ya maeneleo hazipelekwi kwenye Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya chama kinachoongoza, Chama cha Mapinduzi, hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa wakati anazindua Bunge aliongea kwa msisitizo kwamba anakusudia kuhakikisha kwamba anamtua mama wa Kitanzania ndoo kichwani na Watanzania walimfuatilia na wakamshangilia tukadhani kwamba yale yanayoongelewa tutakuja kuyaona sasa kwenye utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate majibu yafuatayo na wa kutujibu upande wa Serikali ambao ninyi ndiyo mmepeva dhamana na wananchi, upande wa Chama cha Mapinduzi, mtueleze sekta ya maji mmeipa kipaumbele cha ngapi kwenye vipaumbele vyenu. Haiwezekani kwamba Watanzania waliopo vijijini mpaka leo wanaopata maji ni asilimia 56 pekee, haiwezekani, hizi asilimia 44 wanaishije? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ilianzishwa na *World Bank* na *World Bank* wakati wanaanzisha mradi walitoa fedha dola za Kimarekani bilioni 1.4, miaka saba ya utekelezaji wake shida ya maji iko palepale. Hili linatokana na kwamba kulikuwa na usimamizi mbovu wa miradi mingi ya maji iliyokuwa inatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukawa tunapambana na *individuals*, kuamini kwamba labda Waziri hafanyi kazi, Naibu Waziri hafanyi kazi ama Katibu Mkuu hafanyi kazi, tatizo ambalo linapelekea Watanzania kukosa maji ni mfumo na inawezekana hakuna *political will* waliyonayo Chama Tawala ya kutatua matatizo ya maji, inawezekana hakuna *political will*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa nane na wa tisa inaelezea upatikanaji wa maji vijijini na mijini. Takwimu hizi ambazo

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Waziri amezisoma zina-*contradict* sana na uhalisia. Lakini pia hata hizi takwimu zenyewe zinajikanganyakanganya ukizisoma na ukazipitia ukafanya *calculation* kidogo zina tofauti. Kwa mfano, upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa Jiji la Dar es Salaam unaonesha kwamba kwa sasa umeshuka kutoka asilimia 85 mpaka asilimia 76, lakini upatikanaji wa vyanzo vya maji siyo upatikanaji wa maji kwa wananchi kwa sababu haya maji yanahitaji usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukienda ukaangalia namna mtandao wa maji ulivyosambazwa na vyanzo vya maji vilivyopo ni tofauti, na ndiyo maana leo ukifanya mahesabu wakazi wa Dar es Salaam anaopata huduma ya maji, waliunganishiwa kwa huduma ya bomba hawafiki hata robo ya wakazi wa Dar es Salaam. Hili ndilo tatizo, unaweza ukaona kwamba kwenye takwimu tunasema kwamba watu wengi wa Dar es Salaam wanapata huduma kumbe wanaopata huduma ni wachache, walio wengi tunaishi Dar es Salaam, tunatumia maji ambayo mengine siyo salama ni yale maji ya kuchimba wenyewe. Ukifanya *research* Dar es Salaam watu wengi wamechimba maji chini, yale maji ambayo siyo salama sana lakini mtandao wa maji wa Ruvu Chini, Ruvu Juu na vyanzo vyote vya Dar es Salaam, bado havijawafikia wakazi wengi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda maeneo ya Temeke, Mbagala huko Chamazi, Kigamboni na maeneo mengi, ukienda ukiangalia mtandao wa maji Dar es Salaam unaona kabisa kwamba maji hayawajafikia, sisi tunaishi Dar es Salaam karibu wote hapa tuna makazi yetu Dar es Salaam tunajua. Kwa hiyo, hizi takwimu zenyewe ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema kidogo zina mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nirudi upande wa Wizara ya Fedha na labda Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, hivi Serikali ina *diplomatic complication* na wahisani tunajiuliza? Ukisoma hotuba ya bajeti ya mwaka 2017 na ya mwaka huu, fedha ambazo wahisani walihaidi kuzitoa

hazijatolewa mpaka sasa. Sasa wakati mwingine unajieleza inawezekana Bunge linapaswa kufahamishwa kama kuna matatizo ya kiplomasia baina ya Tanzania na wahizani wetu tuelezwe ili tujue kwamba kinachoendelea kumbe hatupati fedha za wahisani kwa sababu tumenasanasa hapa ili Bunge lichukue hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati tunajadili bajeti hapa ilielezwa kulikuwepo na dola milioni 503 na wako Wabunge waliishabikia kwamba fedha hamuioni kuna dola milioni 503 ipo, mpaka leo mbona haionekani kwenye utekelezaji wala kwenye kitabu humu hakuna. Hiyo dola milioni 503 iliyokuwa imesemwa mwaka jana na tukaambiwa kwamba Waziri wa India alishakuja na ametia sahihi sasa kilichokwama ni wapi, tumenasa wapi ili dola milioni 503 ili iweze kwenda kukamilisha miradi yetu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukiangalia Wabunge tunaweza tukasema sana hapa, lakini jambo la maji kwa sasa, kwa upatikanaji wa fedha za maendeleo wa asilimia 22 nilidhani Wabunge leo tungesimama pamoja tukasema tunahitaji *commitment* ya Serikali ama taarifa ya Serikali *very intense* watuleleze ndani ya Bunge kwamba kwa nini Wizara ya Maji haipewi fedha za maendeleo, haingii akilini kuona Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inapewa asilimia 0.85. Sasa hii mishahara ambayo inalipwa wafanyakazi, wanalipwa ili wafanye kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza kuona kwamba tatizo watu wengi wanaweza kusema kwamba kuna tatizo labda kwenye utendaji tunaweza tuka-*deal* na *personalities*, tunaweza tukaona kwamba Katibu Mkuu labda tatizo, ama Waziri tatizo ama Naibu Waziri, kumbe tatizo ni mfumo kwamba fedha hazitolewi labda Waziri wa Fedha anakipaumbele chake yeye tofauti na kipaumbele ambacho vimetajwa kwenye ilani ya chama chenu ama kile kipaumbele ambacho Mheshimiwa Rais alikitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji maelekezo ya kina



7 MEI, 2018

mje kutueleza namuona Naibu Waziri wa Fedha yupo, jambo la maji ni jambo tete, huko vijijini tunakotoka Watanzania wana shida kubwa ya maji na hili tatizo linapelekea kuwa na tatizo lingine la magonjwa ya mlipuko, kwa sababu maji wanayopata Watanzania ni maji ambayo siyo maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaongea sana hapa tukajenga hoja tunavyoweza kujenga. Lakini suala linabaki palepale kama Waziri amepewa asilimia 22 ya fedha za maendeleo afanye nini, hiyo asilimia 22 tunaigombania hapa na unajua likitokea swali hapa la Wizara ya Maji, Wabunge wote tunasisima humu kila mtu ana shida ya maji, lakini asilimia 22 ikafanye nini! Wewe mwenyewe leo umeelezea suala la maji llala na maeneo mengine, lakini pia kuna haja kubwa ya kuipitia mikataba ya karandasi za maji ambazo zilitolewa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kubwa upo mradi wa maji uko pale Longido, nilikuwa kwenye Kamati ya maji tuliutembelea mwaka huu una shida kubwa Mkandarasi yupo amepewa fedha zaidi ya asilimia 80 amelaza mabomba tu hakuna kinachofanyika. Kwa bahati mbaya watendaji wa Wizara yako ambao ndiyo waliingia mkataba wanautoa sasa wanataka kujivua baada ya kuona wanaenda kukwama wanawapelekea watu wa *Arusha Water Supply* ili wakausimamie. Kwa hiyo, mwisho wa siku mtakuja kuona kwamba kumbe usimamizi mbovu umepatikana *Arusha Water Supply Agency* kumbe tatizo ni Wizara yako. Hivyo, kuna tatizo kubwa pia la kuingia mikataba

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa nini taasisi za Serikali hazilipi ankara za maji, huu ni mtihani mwingine. Nikiwa Kamati ya Maji tulitembelea katika Mamlaka ya Maji pale Moshi tulikuta Chuo cha Polisi cha Moshi kinadaiwa shilingi milioni 900, *RPC* wa Moshi anadaiwa shilingi milioni 300 anaambiwa kwamba sasa tukufungie mita za *prepaid* anakataa anagoma. Sasa unaweza kuona kwamba kumbe tatizo linalokwamisha maji wakati mwingine maeneo ya mijini ni taasisi za Serikali. *(Makofi)*

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa Arusha yule Mtendaji Mkuu wa Idara ya Maji Arusha alieleza Kamati kuwa kama Serikali inaweza ikalipa madeni yake yote, yeye hahitaji ruzuku kutoka Wizarani kwako, inakuwaje sasa Idara za Serikali zinatengewa bajeti tunaidhinisha humu kwenye Bunge, bajeti inakwenda wanatumia huduma za maji hawataki kulipa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo siyo tu kwamba mfumo wenyewe haupeleki fedha kwenye Wizara ya Maji, pia hata mfumo hautaki kuzisimamia Taasisi na Idara za Serikali zikaweza kulipa *bill* zake ili wananchi wakaweza kupata huduma za maji. Hii nayo ni changamoto nyingine Mheshimiwa Waziri unakutana nayo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nimeona kwenye kitabu chako hapa kuna uchimbaji wa visima vya *DDCA* nami nimekuomba, Mheshimiwa Waziri naomba vile visima uviweze kuvikamilisha ili wananchi wa Jimbo la Mchinga wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maftaha Nachuma, ajiandae Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru Mwenyezi Mungu *Subhuhana Wataala*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hapa amezungumza kwa kiasi kikubwa sana na amejaribu kueleza kwamba Tanzania ni nchi ya nne Afrika kwa upatikanaji wa maji ambayo yapo chini ya ardhi ikitanguliwa na nchi ya Zambia, Mozambique, Sudan ya Kusini na ya nne ni Tanzania. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu ametujalia maji mengi sana Tanzania, suala lililopo ni Wizara husika kuhakikisha kwamba wanaweka mikakati ambayo inatekelezeka, mikakati ambayo mwisho wa siku itakuja kuzalisha maji na wananchi waweze kuyapata.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chikota amezungumza mradi ambao amezungumza zaidi ya miaka mitatu hivi sasa pale Mtwara, mradi ambao unatoka katika Jimbo la Nanyamba kule eneo la Mayembe Chini unakuja mpaka Mtwara Mjini. Huu mradi hivi sasa ni zaidi ya miaka minne haujakamilika na kila mwaka tunavyokuja ndani ya Bunge tukija kuhoji tunaambiwa watu wa Benki ya Exim ya China hawajatoa pesa na Serikali ipo kwenye majadiliano, tumefikisha suala hili katika Wizara ya Fedha, kwa muda mrefu na huu ni mwaka wangu wa tatu nazungumza ndani ya Bunge hili kwamba ule mradi vijiji vimechukuliwa zaidi ya vijiji 26, wananchi wamechukuliwa maeneo kutoka Jimbo la Nanyamba, Mtwara Vijijini mpaka baadhi ya mitaa ya Mtwara Mjini wamechukuliwa maeneo zaidi ya miaka mitatu hivi sasa, hawajapewa fidia kwa kigezo kwamba *Exim Bank* ya watu wa China haijatoa pesa za mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Wizara ya Fedha, inavyopanga mikakati yake kwa sababu hili ni jambo la pili kwa Mtwara, liko jambo la ardhi pia Wizara ya Fedha iliahidi itatoa pesa kwa ajili kulipa fidia kupitia *UTT* lakini hawatoa pesa, mwisho wa siku wananchi wamechukuliwa maeneo yao. Kwa hiyo, hata hapa pia kwamba pamechukuliwa zaidi ya miaka mitatu wananchi hawa wanapaswa kulipwa fidia ili sasa na wao waweze kufanya shughuli zingine kwa sababu mashamba yao yamesitishwa kupisha mradi huu. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ihakikishe Wizara ya Fedha inapeleka fedha kwenye miradi ya maji ili kuondoa matatizo ambayo tumezungumza kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilizungumza hapa mwaka jana na mwaka juzi kwamba Mtwara Mjini hatuna tatizo la maji pale chini, kuna mradi ambao Serikali ilitenga bilioni tano ambapo mkandarasi alikuwa *site*, mkandarasi tayari ameshatafuta maji, maji yamepatikana, tumefanya *pump test* na maji yalikuwa ni mengi sana. Maji mengine ile *clip* niliichukua nikamrushia Mheshimiwa Waziri kumjulisha kwamba maji yamepatikana Mtwara Mjini katika eneo la Lwelu tunachohitaji sasa ni Wizara kutoa pesa ziweze kujenga

visima, ziweze kujenga mtaro, ziweze kusambaza maji kuna maeneo zaidi ya kata tano Mtwara Mjini tuna tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwamba hawa wakandarasi tunaowapa miradi hii kuweza kutekeleza kwa sababu yule mkandarasi alishasema kwamba tayari amesha-*raise certificate* ameshapeleka Wizarani suala lililobaki ni yeye kulipwa zile pesa ili aweze kuchimba visima aweze kusambaza maji katika kata za Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nimtajie Mheshimiwa Waziri maeneo ambayo Mtwara Mjini tunashida ya maji ziko kata zaidi ya nne hapa, katika Kata ya Mitengo pekee eneo la Mitengo Juu hatuna maji, wananchi hawana maji, eneo la Mji Mwema, Vitengo hakuna maji, Kilima Hewa hatuna maji, maji hayapo kabisa Kata ya Ufukoni, Kihole hakuna maji, Comoro ambako hata mimi mwenyewe ndiyo naishi huko hakuna maji, yaani anapoishi Mbunge maji hakuna. Lakini Soko Jinga hakuna maji, Kwa Selemu hakuna maji, Mbaye Juu hatuna majina, Mtwara Mjini na maji chini yako mengi na mkandarasi yuko *site*, pesa hapewi kwa ajili ya kusambaza maji. Kwa hiyo, naomba sana huyo mkandarasi *certificate* ameshatoa, kazi ya Wizara ni kutoa pesa ili huyu jamaa aweze kuchimba visima na aweze kusambaza mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ni pamoja na eneo la Chipuputa nalo pia liko Mtwara Mjini maji hatuna, tuna eneo la upande wa Magereza hakuna maji, kuna Mbawala Chini ile mitaa ambayo inatoka nje ya mji kidogo ambayo mwanzo ilikuwa vijiji kote hakuna maji Mbawala Chini, Naulongo, Dimbuzi, Mkunja Nguo, Mwenge, Naliendele Mikoroshoni kote hatuna maji wakati maji Mtwara yapo kedekede, suala lililobaki ni Wizara kutoa pesa kumpa mkandarasi ili aweze kusambaza haya maji na wananchi wa Mtwara Mjini waweze kupata maji kwa sababu tuna maji baridi kweli pale chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba sana Wizara ihakikishe mwaka huu huyu mkandarasi

7 MEI, 2018

anapewa fedha ili aweze kusambaza haya maji wananchi wangu wa Jimbo la Mtwara Mjini wanahitaji maji kwa kiasi kikubwa sana. Pale ambapo kuna miradi hii ya visima ambavyo vimejengwa kuna wakati fulani tulitembelea maeneo ya Ruvu Juu, Ruvu Chini kupitia Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, utakuta vyanzo vimejengwa vizuri sana pesa zimetumika nyingi sana kujenga hii miradi, lakini vile visima havijafunikwa yaani siku moja anaweza akatoa mtu tu huko chizi chizi akaja akaingia pale akamwaga uchafu akamwaga nini wananchi wanaweza kupoteza maisha, kwa sababu ya ulinzi wa visima vya maji Tanzania miradi hii mikubwa ya maji lazima ifunikwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia taarifa za nchi zingine maeneo mengi visima vya maji vimefunika, Tanzania visima vya maji viko *naked* na ulinzi wenyewe ukiangalia hakuna ulinzi wa kutosha, wakati maji ndiyo maisha ya Watanzania. Naomba sana hii miradi inavyotekelezwa kutengewe pesa maalumu, bajeti ya kufunika visima Ruvu Chini, Ruvu Juu visima vifunikwe Mtwara Mjini pale Mangamba visima vifunikwe *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati fulani taarifa zinasema wakati wa kampeni mgombea mmoja alienda akawatumia wale watumishi wa pale, akamwaga uchafu ndani ya maji, wananchi wa Mtwara tukanywa kwa sababu ulinzi wenyewe hautoshi. Sasa hii siyo Mtwara ni Tanzania nzima. Kwa hiyo, naomba sana kwamba Wizara itenge bajeti ya kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji hivi visima hivi vya maji, mabirika haya ya maji yanafunikwa kunakuwa na ulinzi kwa ajili kuwafanya Watanzania waweze kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni mtu wa Mtwara, lakini nilikuwa naishi Lindi kama mwalimu, kuna Mradi wa Ng'apa ambao umeanza kujengwa zaidi ya miaka saba hivi sasa pale Lindi, mradi ambao ulitakiwa uende kuwanufaisha wananchi wa Lindi Mjini, wananchi wa Mitwelo pale lakini huu mradi unasuasua sana zaidi ya miaka saba sasa, mkandarasi aliyepo pale yupo taratibu sana, tunashangaa

tatizo ni nini? Kwa nini maeneo mengine ya nchi hii wakandarasi wanakuwa wanakimbia kimbiba hivi lakini ukija maeneo ya Kusini wakandarasi wapo taratibu na hawachukuliwi hatua yoyote. Tuna mradi huu wa Ng'apa ni wa muda mrefu wananchi wa Lindi wana matatizo kulliko maeneo yote ya Kusini mwa Tanzania hawana maji ya kutosha, maji pale Ng'apa yapo na ule mradi utatoa maji mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa sababu kila mwaka tunaambiwa hapa mkandarasi atamaliza mwaka huu naomba usimamizi uwe wa kina yule mkandarasi amalize mradi wa Lindi Mjini ili wananchi wa Lindi Mjini waweze kupata maji na wananchi wa Mitwelo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala hili la *bill* za maji, kumekuwa na malalamiko makubwa sana Tanzania, kumekuwa na malalamiko Mtwara Mjini kumekuwa na malalamiko Mikoa ya Kusini Lindi kumekuwa na malalamiko mpaka Dar es Salaam, kwamba watu wanakadiria tu *bill* za maji yaani wale wanaokuja kuchukua *bill* za maji kusoma mita hawasomi mita wanakadiria tu unaambiwa mwezi huu unalipa shilingi 40,000 mwezi huu unalipa shilingi 50,000 wakati hawajasoma *exactly* ni *cubic meter* ngapi zimeweza kutumika kwa mwezi husika, kwa hiyo, naomba Wizara iangalie hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 nilizungumza kuhusiana na Mtwara Mjini lakini hili suala haliko Mtwara Mjini ni Tanzania mzima, wasomaji wa mita hawasomi mita wanakadiria na kuwabambikiza wananchi *bill* za maji kubwa ambazo ni kinyume kabisa na uhalisia wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la upotevu wa maji ni jambo ambalo limekuwa ni *chronic* hivi sasa, sisi tunaishi Dodoma hapa, ukipita mitaani huko maji mabomba yanapasuka sana, mabomba yanavuja sana kuna sehemu zingine barabarani kumetengeneza mpaka mabwawa, ukienda hapa Dodoma hapa njini tu eneo la Chadulu ukifika pale kila siku maji yanavuja na unatoa taarifa kwa watu wa

7 MEI, 2018

maji hawaji kurekebisha. Tanzania nzima iko hivyo Dar es Salaam napo hivyo, leo mbona likipasuka unaweza ukatoa taarifa kwa watu wa Idara ya Maji wanachukua muda mrefu sana kuja kurekebisha. Tunaomba sana maji yanapotea kwa sababu haya maji yanatumia gharama sana kuyachimba kupatikana kwake na kuyasambaza yasiachwe yanamwagiga yanapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kuchauka hayupo, Mheshimiwa Shabiby, ajiandae Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara yetu hii nyeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisimama mara nyingi sana kuchangia Wizara hii Wizara ya Maji. Pale Gairo pana mradi wa maji sasa hivi una muda mrefu, lakini kila nikisimama au kila Wizara ikileta bajeti ule mradi uko asilimia tu 84 na mwaka unaofuata unashuka unakuwa asilimia 75. Kwa hiyo, sasa sielewi mwaka mwingine unapanda bado haujaisha mwaka mwingine unashuka. Kwa leo sitaongelea sana huu mradi ila nitatoa ushauri kwa sababu nimeona kwenye gazeti la Mwananchi la tarehe 3 kwamba sasa hivi anatafutwa mzabuni wa kuweza ku-*supply pump* pamoja na mashine ya kuchuja chumvi ambayo ina uwezo wa kuchuja zaidi ya lita nafikiri kulingana na matenki zaidi ya mita milioni moja au zaidi kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa mpango huo nimeona kwenye gazeti la juzi hapa la terehe tatu, naomba iwe kweli kwa sababu huu mradi kwanza utakuwa ni mradi wa mfano kwa sehemu zingine za nchi yetu, kukuta maji mengi chini ya ardhi ni suala lingine na

7 MEI, 2018

kukuta maji salama ni suala lingine, unaweza ukachimba maji lakini ukakuta yana chumvi na ukienda kupima hayafai kwa matumizi ya binadamu. Kwa hiyo, siyo kila sehemu yenye maji mengi kwamba ni baraka unaweza ukakuta maji lakini yana chumvi ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule wa Gairo itakuwa ni mwanga kwa Wziara na sehemu zingine zote ambazo zina maji chini lakini hayafai kwa matumizi ya binadamu, nafiki ni mradi wa kwanza Tanzania ambao maji yatachunjwa sasa na kuwa maji salama na wananchi kutumia, naomba utekelezaji. Kwa sababu ule mradi ni wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na Wabunge wengine waliotangulia, siwezi nikasema Wizara ya Fedha haijaleta pesa haijaleta nini, tayari ule mradi wa shilingi 6,666,000,000 mkandarasi amechukua zaidi ya asilimia 80 ya pesa ameshachukua tayari, lakini haujakamilia sasa mimi siwezi kulaumu, siwezi kusema hapa pesa iko wapi haiwezekani! Hata huyo Waziri wa Fedha kama amezuia pesa bora azuie tu, kama asilimia 80 imechukuliwa na bado utekelezaji wake hata hauna dalili sasa hizo pesa zinakwenda wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wangu hapa amejitahidi sana pale Gairo na nushukuru tumemuomba aje pale Gairo na anakuja na nafikiri atakuja kwa ajili ya miradi ile ya maji kuja kuangalia. Atakuja Mvomero, atakwenda Gairo anaangalia miradi kwa sababu pesa tayari Kilosa, Mvomero, Turiani, Gairo, lakini kasi iko wapi ndugu zangu? Ingekuwa pesa haijatoka mngesema kweli hapa pesa haijatoka kuna matatizo, labda Wizara fulani haijaleta pesa hizo pesa zipo, maji yako wapi, tumekaa sasa hivi pale unajua kuna watu wengine duniani hawapo, mbinguni hawapo hawaelewi wanajua labda Mbunge huwa anapewa hela anaweka mfukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu kabisa wanasimama pale wanakuambia Mbunge huyu wa Gairo



7 MEI, 2018

amekula pesa zetu za maji, wanajua labda Wabunge tunapewa pesa kwa hiyo sisi ndiyo tunatoa toa pesa kwenye miradi. Wabunge hatupewi pesa, pesa ziko kwenu na ninyi ndiyo mnahudumia hizo au kama mmeshindwa mtu ukweli basi fedha zetu tuwe na *account* zetu za Mfuko wa Jimbo halafu tuweke watu muangalie nchi nzima kama haina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa maji wa mradi huu maji hakuna, lakini ukiangalia hapa kwenye bajeti utaona usimamizi tu wa maji Gairo, Mvomero, Turiani na Kilosa ni shilingi milioni 490, usimamizi tu! Sasa si ulaji huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu namuomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu wamekuja pale, huu mradi wa Gairo utakuwa na gharama kubwa sana kwa wananchi. Nawakumbusha kwamba mradi huu wakati wa Waziri Maghembe alishasema ukiwa na gharama kubwa Serikali/Wizara italipia yenyewe gharama zile za pale siyo wananchi maana tuwekane sawa kabisa, muangalie kwenye *Hansard*. Ukiwa na gharama Wizara kama alivyosema Waziri aliyetangulia kwamba ninyi ndiyo mtakaowalipia gharama hizo wananchi wa Gairo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewapa *plan* nyingi, tumewapeleka kwenye vyanzo vya Mserereko lakini kila watalaam wenu wakifika unasikia ooh! maji haya hayatoshi. Hivi maji haya ndiyo Mto Mkondoa yanasumbua watu kila siku yanaleta mafuriko pale Kilosa halafu unasema hayatoshi kusambaza Gairo? Tumewapeleka kwenye chanzo cha Mto Mkondoa unapotoka Gairo kila siku mafuriko pale Kilosa, Mto Ludewa, Mto Mvumi yote inatoka Gairo pale juu, kwa hiyo hata macho na sisi hatuoni kwa macho? siyo watalaam wa maji lakini hata kwa macho hatuoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tumeomba pesa mtupe kile chanzo tunachotumia sasa hivi cha mserereko kina bomba za nchi tatu, tupeni bomba za *plastic* tu ambazo hazifiki hata shilingi bilioni moja tutoe pale kwenye chanzo cha Mserereko tulete pale. Mwaka jana mmetoa milioni 312 hazijatumika popote. Mnaweka tu hapa, litatumika bomba

7 MEI, 2018

la chuma yaani mnapiga *plan* za ulaji ulaji, pesa ipo lakini *plan* za ulaji tu! Mwaka huu tena ukiangalia kuna shilingi milioni 300 eti hizi kufunga mita Mijini, kwanini msikusanye ile shilingi milioni 300 ya mwaka jana haijatumika na hii shilingi milioni 300 ongezeni hapo.

**MBUNGE FULANI:** Rudia hapo.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Waheshimiwa Wabunge, hatufuatilii tu mkiangalia, lakini kwenye Wilaya pesa za maji zinakuja nyingi, miradi ya utapeli mingi. Mimi mtu akiniambia hela haziji labda Wabunge wenyewe tu hatufuatilii tu, lakini ukifuatilia kwa makini, mimi pale Gairo naangalia pale na kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Saddiq na sehemu nyingine nyingi tu hata Mheshimiwa Mabula nimeongea nao hapa, kuna miradi mingi! Hata ya kwenye Halmashauri mnatoa hela, lakini Wizara hamsimamii siyo tuende mpaka TAMISEMI ile si mambo ya maji? Wizara ninyi mmetoa labda Gairo maji, kwa mfano pale Chakwale na Kibedi kuna mradi wa karibia shilingi milioni 500 lakini maji mpaka leo hayatoki na wakandarasi wameshakabidhi. Ukifungua yale maji mabomba yote yanapasuka, kwa hiyo mnataka sisi kama anavyokuja Mheshimiwa Magufuli hata haya mambo ya maji tukamlalamikie Rais? Sasa hawa wataalam wamewekwa kwa ajili ya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani, halafu mnajua kabisa Mji kama Gairo ni mji mkavu kama Dodoma, kwenye kutenga pesa mnatufananisha sisi na sehemu ambayo watu wakichimba hata na mkono kama panya hapa wanapata maji, huu utalaam unatoka wapi? Muwe mnaangalia, lazima muwe na usawa kwamba sehemu zingine maji hayapatikani kirahisi. Kwa hiyo Ndugu zangu tunaombeni sana... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shabiby kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae Mheshimiwa Mipata.

7 MEI, 2018

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kipekee kabisa niipongeze Serikali, nimpongeze Waziri wa Maji kwa jitihada kubwa anazofanya na tumeshuhudia ni kwa jinsi gani ambavyo amekuwa mstari wa mbele kutembelea maeneo mbalimbali kushughulikia tatizo la maji. Pamoja na yote haya maji ni shida sana na tunafahamu kwamba maji ni uhai na maji ni kwa wote, uwe mwenye ulemavu, usiye na ulemavu kila mmoja anahitaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana alikuja kuzindua mradi wa maji katika Kata ya Nduruma, Vijiji vya Maroroi, Mlangarini pamoja na vijiji vingine vya jirani, tunashukuru sana kwa hili kwa sababu ndani ya miaka 50 hatukuwa na maji ya bomba zaidi ya maji ya mito ambayo tulikuwa tumeyazoea, kwa hili naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote tunafahamu Mkoa wa Arusha tumejaaliwa Mlima Meru na katika huu Mlima Meru baadhi ya maeneo wanapata maji lakini maeneo mengine tunafahamu kama katika Jimbo la Longido, Jimbo la Ngorongoro kote huko maji ni shida na wanaopata shida kubwa ya maji ni akina mama kwa sababu wao ndiyo wachotaji wakubwa wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie shida kubwa iliyopo katika Hamashauri ya *Arusha DC* ambapo tuna tatizo kubwa la madini ya *fluoride* yanayowaathiri wananchi kwa kiasi kikubwa. Inasikitisha sana kwa sababu watoto wanapinda miguu, akina mama wanapinda migongo na hata hao watoto ukiangalia mahudhurio yao shuleni siyo mazuri kwa sababu maji yenye madini ya *fluoride* yamewaathiri kwa kiasi kukubwa sana. Eneo kubwa ambalo limeathirika na maji ni katika Kata ya Oldonyosambu pamoja na Oldonyowasi ambako huku kuna athari kubwa sana ya

7 MEI, 2018

madini haya ya *fluoride*, maji yanapatikana kwa kiwango kidogo lakini hata hayo yanayopatikana kwa kiwango kidogo bado ni shida sana.

Mheshimiwa mwenyekiti, ulemavu unaepukika na ulemavu huu tunafahamu upo ulemavu wa kuzaliwa, upo ulemavu wa ajali na changamoto nyingine lakini ulemavu huu unaosababishwa na maji yenye madini ya *fluoride* haukubaliki kwa sababu tuna uwezo wa kupeleka maji na kuwaondolea shida akina mama na watoto ambao wanapata athari kubwa, wanapinda miguu na wanapata athari pia hata kwenye kusoma inakuwa ni shida. Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri nilikuonesha video ambayo inaonesha ni kwa jinsi gani watoto wameathirika na maji haya yenye madini yenye *fluoride* na kwako wewe pia ilikuwa ni jambo la kushangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwamba umeahidi lakini kwa kweli tunahitaji jitihada za haraka katika kuhakikisha kwamba tunawasaidia wakazi hawa katika hizi Kata za Oldonyosambu pamoja na Kata ya Oldonyowasi ili basi tuondoe tatizo hili la ulemavu unaotokana na maji yenye madini ya *fluoride*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo hili ni kubwa na kwa kuwa sasa katika Wilaya ya Longido chanzo kingine cha maji cha Mto Simba kutoka Wilaya ya Siha, basi tunaomba hivi sasa kwamba chanzo cha maji ambacho ni cha Engutoto na tunafahamu kabisa kwamba kulikuwa kuna mradi unaofadhiliwa na *DFID* kwa kushirikiana na *Water Aid Tanzania*, tunaomba katika Halmashauri hii ya Arusha kile chanzo cha maji ambacho awali kilikuwa kipeleke maji katika Jimbo la Longido na hatimaye chanzo hiki tumekiacha, tunaomba sasa chanzo hiki kiweze kupeleka maji katika Kata hii ya Oldonyosambu pamoja na Kata ya Oldonyowasi ili tuondoe tatizo hili la madini ya *fluoride*. Tukipeleka chanzo hiki cha maji tutasaidia vijiji vya Losinoni ambavyo hali yake ni mbaya sana, tutasaidia vijiji vingine ambavyo ni vya Lengijave lakini siyo hiki tu kuna kijiji cha Lemanda ambacho kimeathirika kwa kiasi kikubwa sana.

7 MEI, 2018

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana ili basi uweze kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha, tunakishughulikia chanzo hiki cha maji ili tuweze kutatua madini haya ya *fluoride*. Kuna baadhi ya wenzetu wakati mwingine hata kucheka inakuwa ni shida kwasababu ya meno yameathirika na maji. Mheshimiwa Waziri, hatupendi kwahiyo tunaomba sana mtusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu katika Mkoa wa Arusha, tumesomeshwa wengine na bustani kwa sababu tulikuwa na kilimo cha umwagiliaji kwa miaka yote kutokana na maji yanayotoka katika Mlima Meru. Hivi sasa hatuwezi tena kulima kwa sababu wamiliki wa mashamba makubwa ya maua sasa hivi wanayahodhi yale maji yote, matokeo yake wananchi ambao walitegemea kilimo kutokana na kilimo hiki cha umwagiliaji sasa hivi hawawezi tena kulima. Tunawapenda wawekezaji, tunawahitaji wawekezaji, lakini wawekezaji hawa wasitufikishe hapo wananchi wetu wanapata shida. Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri ili uweze kushughulikia na kupitia basi kwa sababu wengine wamehodhi maji na wanasema kwamba wana hati miliki ya kuhodhi maji hayo kwa miaka 100 yaani kwa maana 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wetu wanaangamia, ndugu zangu nimesoma mimi kwa kulima bustani, hivi sasa imekuwa ni shida kwa hiyo tunaomba sana mashamba ya maua yaliyopo katika eneo la vijiji vya Chekereni, lakini pia njiapanda ukienda Mlangarini, mashamba ya maua yale wamiliki wote wamehodhi maji, tunaomba tunayahitaji haya maji ili wananchi wetu waweze kurudi na kulima kilimo cha umwagiliaji tofauti na sasa ambako tunasubiri mvua mpaka mvua na siku hizi kumekuwa na mabadiliko ya tabianchi maji haya yanakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, hiki ni kilio cha wananchi cha muda mrefu, tunawahitaji wawekezaji kama nilivyosema, lakini wawekezaji hawa wasihodhi maji yote, kwa hiyo ninaomba sana Serikali ipitie haya... (*Makofi*)

7 MEI, 2018

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri Mheshimiwa Mollel. Mheshimiwa Mipata jandae Mheshimiwa Mendrad Kigola

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mipata. Waheshimiwa kuna mtu ameacha ufunguo *I think* wa gari kwenye ma-*box* haya ya usalama hebu mji-*check* kama mtu amepoteza ufunguo wake uko hapa.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Namshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima, ninayo machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitambue kazi nzuri sana inayofanywa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii wamekuwa wakitusikiliza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninayo michango miwili, ama mitatu kutoka Jimboni kwangu. Kwanza ni mradi wa Kawa uko Nkundi. Mradi huu unasimamiwa na Wizara moja kwa moja na umeanza miaka minne, mitano iliyopita wananchi wanasubiri maji. Umetumia zaidi ya shilingi billioni tatu, tangu ujenzi wa chanzo chake, wananchi tumewaaminisha kwamba mradi huu karibu wanapata maji, mpaka sasa Mheshimiwa Waziri bado hawajapata maji. Ujenzi wake umekamilika na nilifika ofisini kwako kukuelezea juu ya changamoto zinazojitokeza, leo hii nilikuwa naongea na wannchi bado maji katika kijiji cha Nkundi hawajapata maji, lakini Kalundi wamepata maji na wao wanasema maji yanachukua muda mrefu sana kujaa kwenye *tank* kwa hiyo kwa vyovyote vile kuna changamoto ama za kimfumo, mfumo wa kusukuma maji au njia yenyewe.

7 MEI, 2018

Kwa hiyo, ninaomba watalaam wa Wizara wausimamie huu mradi vizuri kwa sababu umetumia pesa nyingi na ikiwezekana mradi huu ukitoa maji vizuri upeleke na maji kijiji changu cha Miula itakuwa imesaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi mwingine wa mradi wa Isale. Mradi huu una changamoto ya fedha, mkandarasi amesha-*raise certificate* sasa hivi tunaomba pesa, nilikuja hapo Wizarani Mheshimiwa Waziri ukaniahidi kwamba hivi karibuni utatoa. Tunachotaka kuwaeleza ni kwamba huu mradi ni muhimu sana unabeba vijiji zaidi ya sita na kama mkiupa pesa maana yake ile asilimia ambayo tunatoa maji katika Wilaya yetu itapanda kidogo. Vijiji vya Nkata, Ntemba, Kitosi, Ifundwa na Ntuti vinakusudia kunufaika na mradi huu, shida yake ni pesa. Mtuharakishie pesa ili mkandarasi aweze kuendeleza ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni Mradi wa Mpasa mradi huu wa pia unaendelea vizuri. Mkandarasi sasa hivi amesimama kidogo kwa kukosa pesa lakini anadai vilevile *certificate* yake ili aweze kuendeleza mradi wenyewe. Mradi huu tunaomba utakapokamilika utapeleka maji King'ombe, Kilambo, Mlambo na tunaomba upeleke Kilambo upeleke na Kapumpuli utatusaidia sana. Maeneo haya ya mwambao huwa yanapata kipindipindu kila wakati, kwa hiyo utakuwa msaada sana na ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maombi pia mapya, niliwahi kuzungumza hapa Bungeni, katika Vijiji vya Kasu, Katani, Milundikwa na Kantawa ili ku-*support* pia sekondari mpya ya Milundikwa, mradi huu unahitaji watalaam na timu ya watalaam iende nimeandika na barua kwa Wizara, naomba itusaidie kupeleka timu iende ikachunguze, siyo huu tu wajaribu tena kunisaidia katika Kijiji cha Nkana, kijiji cha Sintali na kijiji cha Mkomachindo ambao wana sekondari pia hawana maji ya kutosha yanayoweza kusaidia. Kijiji cha Sintali muda mrefu sana wanatumia maji ya Madimbwi, wana chanzo kizuri lakini haijawahi kusaidiwa. Naomba Wizara iniangalie katika hilo na nimeandika barua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine muhimu ni mradi wa maji ya Mserereko wa Wampembe. Mji mdogo wa Wampende hauna maji na una kituo cha afya na watu wengi wa kutosha, lakini ndiyo maeneo ambayo chanzo cha magonjwa ya kipindupindu yanaanzia kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika. Mradi ule Halmashauri wameanza kuufanyia kazi, tunaomba *support* ya Wizara ya kitaalam na kifedha ili uweze kusaidia Vijiji vya Kizumbi, Ng'anga, Katenge, Wampembe na Ng'undwe unaweza ukatusaidia sana. Lakini vijiji kama Mwinza, Izinga, Lusembwa na Itanga hawana maji, naomba sana watusaidie. Vipo vijiji pia vya Kacheche na vijiji vingine vina visima ambavyo tunaomba pia mtusaidie katika uchimbaji na ukamilishaji wa visima vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Chala una chanzo kizuri cha maji, kinatakiwa kiongezewe tu, kuna kisima kilichochimbwa muda mrefu kiongezewe kwenye chanzo kinachotoa maji sasa ili maji yaweze kutosheleza Mji wa Chala na jambo hili ni pesa kidogo tu itahitajika kwa sababu kisima tayari kimeshachimbwa na miundombinu ipo inayotumika mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ni suala la umwagiliaji. Nimezungumza juu ya bonde la Mto Kate, bonde la Mto Namansi kuna vyanzo vya umwagiliaji na miundombinu yote na michoro na utaratibu wote wa kihandisi ulishafanywa na Halmashauri kwa gharama kubwa na kuletwa kwenye Kanda, tunachosubiri ni pesa ili tuanze ujenzi wa miundombinu. Nilitegemea kwenye bajeti hii nitaona huu mradi sasa sijui kwa nini. Ninaomba Wizara na watalaam wa Wizara wawe wanapitia michango ya Wabunge, haiwezekani mradi mmoja unazungumzwa mara kumi. Nazungumza kila wakati huu mradi kwamba Halmashauri imetumia gharama kubwa saa katika mradi huu lakini bado hatujaanza umwagiliaji katika maeneo yote mawili ya Kate pamoja na Wamanse.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* Wizara inafanya kazi vizuri, naunga mkono hoja na ninapongeza utendaji mkubwa sana wa Wizara na Serikali.



7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae Mheshimiwa Godfrey Mгимwa.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuongea machache.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali kwa mipango mizuri kabisa. Tunapojadili kuhusu maji tunajadili maisha ya watu na unapojadili maisha ya watu hakuna utani lazima tuwe *serious*, tufanye kazi na lazima tutekeleze kile ambacho tunakijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maji ni Wizara muhimu sana katika Wizara zote. Katika Wizara zote wananchi pamoja na Wabunge tunaweka macho kwenye Wizara ya Maji. Maji vijijini na mijini kama hakuna maji hakuna maisha. Tunasema maji ni uhai na tunapoesema maji ni uhai maana yake mwananchi lazima apate maji na tunaposema kumtua mama ndoo kichwani na iwe ni ukweli tunaitua hii ndoo kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, tukipanga bajeti ya maji na fedha lazima tuwape kama tulivyopanga. Ni vigumu sana Serikali ikiwa inapeleka kwenye Wizara hii fedha kidogo sana halafu miradi haiishi kwa muda unaotakiwa. Kuna wakandarasi wengi wako *site* mpaka sasa hivi hawajapata pesa, wanashindwa kutekeleza miradi ya maji kwa sababu fedha hawajapata, kwa hiyo, niombe Serikali tuache mambo mengine yote, lakini tuhakikishe kwamba miradi ya maji inaisha kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Mufindi Kusini kuna Mradi wa Maji Sawala unakwenda karibu mwaka wa 12, bahati nzuri sana leo Waziri nimeongea naye, Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu nimeongea nae pia, kwa kweli nilikuwa nimepanga tofauti lakini kufuatana na mazungumzo tuliyoongea naishukuru Serikali kwa mazungumzo tuliyoifanya

7 MEI, 2018

leo. Wamenihakikisha kuwa Mwezi Mei huu fedha zitapelekwa kule kwenye Kata ya Mtwango, kuhakikisha Mradi wa Sawala unatekelezwa kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kubwa mradi wa shilingi milioni 800 au mradi wa shilingi bilioni mbili unachukua miaka sita, saba ni aibu! Bahati nzuri sana Waziri tulienda siku ile kwenye Kata ya Mtwango tukasaini mkataba mbele ya wananchi. Wilaya imeleta maombi toka mwezi wa Machi mpaka leo hawajapata fedha na tuliwaahidi wananchi. Kwa vile Waziri leo umeniambia maneno mazuri ndiyo maana naipongeza Serikali kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika Jimbo la Mufindi Kusini kuna tatizo kubwa sana la maji, kuna matenki ya maji kule karibu Kata 11, matenki yapo Serikali ilijenga kwa ushirikiano na wananchi, miaka ya nyuma miaka ya 1980 ni ukarabati wa miundombinu. Mimi Mbunge nimeleta maombi mara nyingi kwamba kule siyo miradi mipya, ni miradi ambayo inatakiwa kufanyiwa ukarabati lakini hatufanyi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali kwenye Kata ya Igowelo, wananchi wanapata taabu sana ya maji, matenki yapo na *sources* za maji zipo, ni ukarabati wa miundombinu, naomba sana Serikali Igowelo pale ipeleke maji. Ukienda pale Nyololo bahati nzuri Waziri unapita kila siku pale, siku nyingine nenda pale shuka omba maji kama watakupa maji pale, maji hayapo, tunatumia maji ya visima tu ndiyo vinatusaidia vingine visima vile vya kienyeji, wakati tuna mabwawa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kata ya Nyololo ipewe maji, Itandula, Idunda, Mbalamaziwa, Nyololo, Luhunga hizi Kata zote maji hayapo ni habati nzuri sana nawashukuru sana wafadhili wamenisaidia sana wamenichimbia visima kule, sasa hivi tusingekuwa na visima vile ambavyo nilichimba mimi kwa kushirikiana na wafadhili wananchi wasingekuwa na maji mpaka leo.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kwenye Jimbo la Mufindi Kusini naomba sana maji yapelekwe kwa muda kama tulivyopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye bajeti kuna fedha imetengwa. Sasa hii fedha ambayo tumeipata hata ikiwa ni kidogo basi ikafanye kazi. Tukipanga shilingi bilioni mbili, basi ziende shilingi bilioni mbili siyo upange bajeti ya shilingi bilioni mbili wewe unapeleka shilingi bilioni moja inakuwa bado haisaidii. Wakandarasi wale wamekopa fedha kutoka benki na wanadaiwa na benki lakini Serikali bado haijawalipa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameniahidi kwamba Mwezi Mei Mufindi hela zinakwenda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Godrefy Mgimwa, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, ajiandae Antony Calist Komu.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, vilevile nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Makatibu wote Wakuu.

Wizara hii ya Maji ni Wizara muhimu kama ilivyoielezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, binafsi ninapongeza shughuli ambazo zinaendelea kwenye Taifa letu na kwenye Jimbo langu la Kalenga. Binafsi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kufika Jimboni kwangu. Siyo tu Waziri Kiongozi lakini Naibu Waziri pia amefanya kazi kubwa sana kuweza kuhakikisha kwamba Jimbo la Kalenga linakaa vizuri. Pongezi zangu zifike kwako kwa sababu hata ile fedha uliyonipa shilingi 500,000 kuwapelekea wananchi wangu ninakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri naamini ni mwanzo mzuri. Ilikuwa ni fedha binafsi kutoka kwenye mfuko wake na mimi nakupongeza sana.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba kuna miradi mbalimbali ambayo inaendelea, lakini nizungumzie mradi mahsusi ambao sasa hivi una takribani miaka sita tokea uanze. Mradi wa Itengulinyi, Isupilo kuelekea Magunga. Huu ni mradi mkubwa sana ambao Serikali iliingia mkataba na Mkandarasi RJR kwa zaidi ya shilingi za Kitanzania bilioni 2.4. Leo hii tunavyozungumza, nimeshaongea mara kwa mara Bungeni kukumbusha umuhimu wa mradi huu wa maji. Mpaka leo fedha ambazo zimetolewa ni zaidi ya shilingi bilioni 1.2 na mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yangu ya Iringa Vijijini leo hii tunavyoongea imepelekwa mahakamani kwa ajili ya mradi huu, mradi haujakamilika na mkandarasi ameipeleka Halmashauri mahakamani na tunaendelea kusubiri nini kitatokea kwa sababu mkandarasi huyu anadai Serikali fedha ya riba ziadi ya shilingi milioni 250, nashindwa kufahamu tumeshapeleka fedha za mradi zaidi ya shilingi bilioni 1.2 lakini utaratibu unavyokwenda mpaka leo ni muda mrefu sasa Serikali imeshindwa kuingia makubaliano na Mkandarasi huyu ili mradi huu ukamilike na wananchi wangu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mradi ambao ungeweza kutatua tatizo la maji kwa zaidi ya vijiji vinne na ni mradi ambao binafsi ungekamilika ningeshukuru sana na wananchi wangu ambao katika bajeti hii iliyoelezwa kwa kweli hatujatengewa fedha za kutosha kwenye suala la maji, na kama tunavyofahamu maji ni uhai na wananchi wa Jimbo la Kalenga wanahitaji maji kama majimbo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona utaratibu ambao umeoneshwa kwenye Wizara kuhusu suala la maji, lakini kwanza fedha ambazo tumekopa kutoka India jumla ya dola za Kimarekani milioni 500 ningependa kujua, je, ni utaratibu gani umetumika kwa Serikali kupeleka hizi fedha katika yale maeneo ambayo tumeyatenga 17, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tufahamu kwamba kuna maeneo mengine mengi ambayo yameshaelezwa na yameoneshwa kwenye kitabu cha hotuba, mengine yamepata miradi ya maendeleo, mengine fedha kutoka Serikali, mengine miradi ya umwagiliaji, lakini kuna maeneo kama Jimbo langu la Kalenga hatujapata hata senti moja kutokana na maeneo haya ambayo yametengwa. Kwa sababu inaonesha kabisa kwamba fedha zimetolewa na kuna fedha zingine kutoka Serikali Kuu, fedha kutoka miradi mbalimbali kwa ajili ya mwaka huu wa fedha na mambo mengine chungu nzima, lakini Jimbo langu la Kalenga bado halijapata au halijatengewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba tumetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya bajeti hii ya 2018/2019 lakini Serikali lazima itambue kwamba kuna maeneo au kuna Wilaya ambazo zina majimbo mawili, fedha hizi bilioni 1.3 zikitenganishwa katika majimbo mawili bado zinakuwa hazitoshi. Jimbo langu la Kalenga peke yake bajeti yake ni jumla ya shilingi za Kitzania milioni 735, sasa sina uhakika kama fedha hizi zitafika kwa wakati au hazitafika kwa wakati lakini ninachoomba Wizara ni kwamba hebu tujitahidi kupeleka fedha katika maeneo ambayo matatizo ya maji ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo ambayo tulipitisha mwaka jana ya shilingi 50, sasa hivi ningependa tu kuishauri Serikali kwamba kama tukakubaliana zikawa shilingi 100 zikaenda katika kwenye maji basi nina uhakika kabisa tatizo la maji linaweza likawa limepungua. Shilingi 50 ambayo tumeitenga mwaka jana imeweza kukusanywa na tukapata jumla ya shilingi bilioni 158, ina maana kama tungefanya kwa shilingi 100 tungepata zaidi ya shilingi bilioni 300 ambazo tungegawanya katika Wilaya au katika Majimbo tungepata fedha nyingi sana. Hili ningependa Wizara iweze kuliangalia sana na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo dogo kuhusu miradi ya umwagiliaji, pale Jimboni kwangu tuna

mradi wa maji wa umwagiliaji wa Mlambalasi, ambao kwenye kitabu hiki cha hotuba inaonesha kwamba mradi umekamilika, lakini ukweli ni kwamba mradi haujakamilika na zaidi ya shilingi milioni 800 bado zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ulifika Jimboni na umezunguka mara kwa mara umeona, ninaamini hata hili ninalolizungumza unalifahamu, tunachohitaji ni shilingi milioni 800 ili mradi huu uweze kukamilika, naona kwamba umuhimu wa umwagiliaji ni mkubwa lakini tunasahau eneo hili la umwagiliaji kwa sababu tumejikita sana kwenye miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie suala la miradi mbalimbali ya maji ambayo haikamiliki katika maeneo mbalimbali ya nchi. Ningeomba kuishauri Serikali kwamba sasa ifike wakati Serikali ipeleke *special audit* kwenye miradi yote ya maji katika nchi hii. Nilikuwa kwenye Kamati ya LAAC kwenye kipindi kilichopita nimeshuhudia miradi mbalimbali ya maji ambayo imetelekezwa na wakandarasi, imetelekezwa na Halmashauri, aidha fedha hazijakwenda au kama fedha hazikwenda basi kuna utapeli wa hali ya juu ambao umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni suala la msingi kwa sababu tutakapoongeza hizi fedha hizi za tozo nina uhakika kabisa kwamba tunaweza kufanya *special audit* na tukapata miradi mbalimbali ya maji ambayo ilikuwa haijakamilika na hatimaye ikakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kuna Wasimamizi Elekezi *(Consultants)*, katika maeneo mbalimbali ukiangalia watu hawa, ndiyo wamefanya kazi nzuri na wanaendelea kufanya kazi nzuri, lakini kuna maeneo ambayo wamekuwa kama kichaka cha kujipatia fedha bila kuangalia ufanisi wa kazi. *Consultant* anapewa kazi, anafanya kazi lakini baada ya muda fulani anatokomea na zile fedha ambazo alitakiwa alipwe, analipwa lakini mradi unakuwa haujakamilika.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaotokea vijijini tunaona mengi na tunajua kuwa miradi ya maji ni mikubwa lakini kama fedha zinakuwa haziendi au zinatumiwa vibaya nina uhakika kabisa kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo lazima sasa kama Wizara iweze kuweka jicho lake na kuangalia na kwa umakini zaidi na kuona je ni wapi ambapo tumekosea? Eneo hili ni mojawapo na ninaamini kama tutaweka macho ya uhakika na tukaangalia vizuri tunaweza tukawa na uhakika wa kupata maji katika maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu na miji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia mradi mmoja wa Nyamlenge katika Jimbo langu. *Design* inahitaji shilingi milioni 49, ningependa Serikali iweze kuangalia mradi huu kwa sababu unakidhi viwango vilevile utapeleka maji katika vijiji zaidi ya 15. Mheshimiwa Waziri naamini unanisikia, uko hapo pamoja na Naibu Waziri ninaomba mradi huu wa maji muweze kuangalia. Nilishapeleka *proposal*/sijajua mpaka leo imefikia wapi na nimejaribu sana kufuatilia bado sijajua hizi milioni 49 ambazo zingeweza kukidhi mahitaji ya mradi huu kama zingepatikana zingeweza kuleta tija sana katika suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kusema mengi naamini kwa haya machache ambayo nimeyaeleza Serikali itayachukua itaenda kuyafanyia kazi na hatimaye Jimbo la Kalenga na Mkoa wa Iringa uweze kupata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru sana na ninawatakiwa kila la kheri Wizara ya Maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mary Nagu, ajiandae Mheshimiwa Antony Komu na ujiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii ya awali kabisa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ambayo naitafuta kwa udi na

uvumba ahsante sana. Vilevile nimshukuru Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu na Waziri mwenyewe kwa dhamira yao ya dhati ya kumtua mama ndoo kichwani na kama itatokea hivyo kwa kweli Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhili kama sitampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa sababu kwa kweli kama siyo ufinyu wa fedha utaona kwamba wanajihadi kubwa sana. Kwa hivyo, naomba muendeleo kukazana ili nchi ipate maji kwa malengo ambayo mmeyaweka na kwamba watu wasiende zaidi ya mita 400 kutafuta maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, maji ni usafi wa mazingira, maji ni afya na kwa ujumla maji ni maendeleo lakini ilivyo maji ni siasa vilevile. Kwa hivyo, ninaomba tutekeleze haya maji kwa kuondoa kiu ya maji, vilevile kusambaza miradi hii nchi nzima ili kusudi kila mwananchi wa Tanzania aweze kunufaika na miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga mambo mengi na imetekeleza mengi, Serikali ilipitisha sera hii nzuri kwamba maji yasiwe mbali zaidi ya mita 400 kutoka kaya mbalimbali na Serikali imetaka *by* 2020 wananchi asilimia 85 wamefikiwa na maji, lakini hadi sasa utaona na kama Waziri alivyoeleza ni asilimia 58.7 ambao wamepata maji na hasa vijijini. Ninaomba tufanye yafuatayo ili hayo mambo yatekelezeke kwa kasi kubwa zaidi. Niko kwenye Kamati hii na ni lazima ni-*declare interest*, nimeona changamoto nyingi ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba Serikali kama imetenga shilingi fulani itoe zote basi kwa sababu bajeti ndiyo *instrument* kuu ya kutekeleza mambo ya maendeleo bila bajeti hatuwezi kufika mbali. Pili kwa sababu bajeti inaonekana kwamba haifikii malengo basi tuendeleo na kuhakikisha kwamba katika bajeti hii shilingi 50 zimeongezeka kwenye mfuko wa maji kutokana na mafuta, dizeli na petroli



7 MEI, 2018

na mafuta ya taa. Kwa sababu mimi ninavyoona ndivyo namna pekee na kila moja ni shahidi kwamba miradi ya mwaka huu au mambo yaliyopangwa mwaka huu yametokelezwa kwa asilimia 66 na mfuko wa maji na bajeti iliyopangwa imetokeleza kwa asilimia 22 tu. Kwa hivyo, Wabunge wanapokazania hii tozo ya shilingi ya 50 ni kuitaka Serikali iweze kufikia azma yake na wanachi waweze kupata maji kama tunavyotegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna vifaa au ya kujenga miundombinu ya maji mingi inatozwa kodi, maana yake ni kwamba mnapunguza bajeti ya kutumia vifaa kwenye miundombinu, naomba tuangalie na hilo. Jambo la nne ni uundaji wa wakala wa maji, hakuna *labour force* ya kutosha au wataalam wa kutosha kwenye Halmashauri zetu ambao watatekeleza miradi ya maji na ndiyo maana *contractors* wengi kwanza hawana uwezo kwa hivyo tukiwa na wakala miradi mingi itatekelezeka upesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye Wilaya yangu ya Hanang ambako Mbunge ni mimi. Niliomba kwa miaka minane lambo ya Gidahababieg na Waziri anajua, ninaomba wakati akitujibu aweze kuniridhisha na awaridhishe watu wa Hanang kwamba miaka hii minne hatudanganywi bali lambo litapatikana. Ninajua anataka sana kufanya hivyo lakini aendelee kutupa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni maji katika Mji wetu Mkuu wa Katesh, ninaishukuru sana Serikali imeipa kazi hii Mamlaka ya Maji Babati lakini kwa muda mrefu Katesh haina maji, shilingi milioni 100 haitatosha, naomba Waziri uangalie na hata kwenye mfuko huo mdogo ambao tunao ili Katesh ipate maji. Huwezi kuwa na Makao Makuu ya Wilaya ambayo hayana maji, kwa kweli siyo jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna miradi mingi kwa mfano, tulitengewa shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya mradi wa Endasaki, Endagau, Endasiwold, lakini mpaka sasa tumepokea shilingi milioni 700 naomba hizi shilingi milioni 600

7 MEI, 2018

zitoke kusudi maeneo yaliyobaki kama Endasiwold Endagau waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna mradi mwingine wa Malama, Maskararoda, Masakta na Lambo ambao tulitengewa shilingi bilioni 1.2 hatukupata hata senti moja na kule kuna matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang ipo kwenye *Rift Valley* ukichimba kisima unaenda zaidi ya mita mia moja huoni maji, kwa hiyo gharama ni kubwa. Ninaomba sana watu wetu wasibaki bila maji wakati malengo ya Serikali ni mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba fedha hizi za Malama, Endagau, Endasaki na Endasiwold zimepangwa kwa miaka mitatu mpaka leo maji hayajapatikana. Naishukuru sana Serikali kutokana na mradi huu Endasaki imepata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna visima zaidi ya tisa ambavyo vimeshachimbwa watu wanaona na wanataka kututoa macho kwa sababu miundombinu haipo, hakuna *pump* hakuna nini, watu hawachoti maji wanaangalia maji yako pale, ninaomba sana ninaomba sana miradi hii ikamilike na ninaomba Waziri kama walivyosema wengine kwa kweli tuunde Tume wakaangalie miradi ya maji nchi nzima ikiwepo Hanang yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie kwamba Endamdaiga haina maji, Gawidu haina maji, Gisambalang haina maji na vijiji vingi ambavyo havina maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba kwa vile Hanang haina maji ya chini ya kutosha bonde la ufa ninaombeeni mtupangie fedha za kuweza kuchimba mabwawa au malambo. Sisi tuna wafugaji, wanaotumia maji watu wengi takribani laki nne, tunao wakulima vilevile.

Jambo lingine ambalo nilitaka niongelee ni kuhusu umwagiliaji. Tuna mradi wa Endagau ambao ulipokea shilingi milioni 900, kama utatekelezwa vizuri Hanang watakuwa na manufaa makubwa kwa sababu hatuna uhakika wa mvua. Naomba sana kama Serikali ilivyoanza iendelee kuufuatilia mradi ule ili uende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalosikitisha ni kwamba *design* zinakuwa si sawa na hasa ukienda kwenye miradi yote ya umwagiliaji ndani ya nchi utakuta kwamba zina *faults* au zina matatizo. Endagau ni moja ya maeneo yenye matatizo lakini naomba sana Serikali nayo iweze kuuangalia mradi huu ili Hanang nayo iweze kunufaika na miradi ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, kama tunavyojua maji yalivyo na umuhimu barabara hazijengeki bila ya maji, hakuna mradi wowote utakuwepo bila ya maji, hata viwanda havitajengeka bila ya maji. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wote hapa wanataka hiyo tozo ya shilingi 50 iongezwe kusudi maji yatakapokuwa na uhakika ndani ya nchi hii, mengine yote yatawezekana na watoto watakuwa na malezi mazuri kwa sababu mama zao hawatachukua muda mwingi na hawataenda masafa marefu ya kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwangu mimi kipaumbele cha kwanza ni maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Komu na ajiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, naomba Waheshimiwa Wabunge tuiptishe ili Watanzania wapate maji. *(Makofi)*

7 MEI, 2018

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji ambayo ni bajeti muhimu. Kwa maoni yangu ni bajeti ambayo ingepaswa iwe labda namba mbili baada ya bajeti ya Wizara ya Elimu kwa umuhimu. Maji ni uhai si uhai wa binadamu tu isipokuwa uhai wa viumbe na hata uhai wa uchumi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuangalia hali ya maji nchini. Waziri amejaribu kujenga picha kwamba tuna hali nzuri sana katika Afrika Mashariki kwa sababu kiasi cha maji sasa hivi kwa maana ya mita za ujazo kilichopo kwa ajili ya matumizi ya kila mtu ni 1,800 kama alivyosema na akasema sisi ni wa kwanza Afrika Mashariki. Nataka Bunge lielewe, kwa mujibu wa taarifa za wataalam wa Wizara hali yetu ya maji si nzuri kwa sababu ifikapo mwaka 2025, tutakuwa tupo chini ya kiwango ambacho kinahitajika kwa binadamu mmoja, tutakuwa tumefikia mita za ujazo 1,500 na tutatangazwa kama nchi yenye uhaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uwekezaji unaofanywa kwenye maji inaonekana wazi kabisa kwamba huko ndiko tunakokwenda. Kwa hiyo, kutulinganisha sasa hivi na walemavu wengine haitusaidii sana, ni lazima tuzungumze hali halisi na kwamba hali yetu ni mbaya na uwekezaji wetu hauashirii hata kidogo kwamba tutazuia kwenda kwenye nchi ambayo ina uhaba mkubwa wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu leo tunavyozungumza katika vijiji vyetu vyote ni asilimia 46 tu ya watu wenye maji salama na maji safi. Sasa hili si jambo la kujisifia. Ukiangalia fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya bajeti ya maji hazioneshi kama tunaweza tukajiondoa hapa tuliko kwa sababu ni fedha kidogo, lakini vilevile pesa hizo zikishatengwa hazipelekwi na mahali pengine inakwenda sifuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimejitahidi kusoma kidogo na hawa watu wa Wizara wamefanya kazi kubwa

sana, wametengeneza miradi yote ya maji katika nchi hii kwenye hiki kitabu na zipo hapa. Wameonesha ili miradi yote ya maji iweze kukamilika tunahitaji shilingi trilioni 32.4 lakini leo pesa tuliyotenga, tumetenga shilingi bilioni 20 maana yake ni kwamba tunahitaji miaka 1,200 ili tuweze kukamilisha kilichoandikwa humu, tunatania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka jana pesa ambazo zilitengwa kwa ajili ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji shilingi bilioni sita, wamesema hapa kwamba hiyo bajeti imetekelezwa kwa asilimia 12 lakini waseme vilevile kwamba fedha za ndani hazikwenda hata shilingi moja, zimekwenda asilimia sifuri, fedha za nje ndizo zilizokwenda shilingi bilioni 2 ambazo ndizo zinazofanya asilimia 12. Katika hali ya namna hii tunatania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maana ya kuwekeza kwenye maji ni nini? Maana ya kuwekeza kwenye maji ni kuwa na ajira ya uhakika, chakula cha kutosha na kuacha ku-*import* chakula kutoka nje. Leo kwa taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania tunaagiza chakula kutoka nje cha shilingi bilioni 888.5 kila mwaka. Hizi fedha tungeweza tukazi-*save*, ndiyo maana sisi watu wa upinzani tunashangaa kweli kweli mnavyoshangilia hapa kuhusu kununua ndege *cash*. Hivi tuna-*luxury* gani ya kwenda kuwekeza shilingi trilioni moja kwenye ndege wakati kila mwaka tunapoteza shilingi bilioni 800 kwa ajili ya kununua chakula kwa sababu hatuwekezi kwenye maji? Tukiwekeza kwenye maji tukaokoa hizo fedha maana yake ni kwamba kila mwaka tungeweza kununua hizo ndege sita kwa mpigo, lakini kweli tumeanza na ndege ndiyo maana sisi tunawashangaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni hali ambayo kama hatutabadilika, tukaamua kuchagua vipaumbele ambavyo ni sahihi, vipaumbele vinavyowagusa watu wetu, vipaumbele ambavyo vinatufanya tuweze kupiga hatua kwa namna ya kuweza kuchochea uchumi wetu bado tutaendelea kuingia katika hatari na kama nilivyosema tunakwenda sasa ku-*approach danger zone* kwamba tutakuwa nchi ambayo wanaita kwa kiingereza *water stress*.

Nashauri tuangalie upya na hili ni Bunge tusimame kama Bunge tuisimamie na kuishauri Serikali iache haya mambo ambayo ni ya kujenga *impression* wakati hali yetu ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti nikienda kwenye miradi hii ambayo imetangazwa humu, iko miradi ya umwagilaji ya toka mwaka 2004 haijaisha. Katika miradi 312 ni miradi 55 tu ambayo imeweza kukamilika maana yake ni asilimia 17. *This is very serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kama Wabunge wengine walivyosema unavyokwenda kumpa mkandarasi pesa kidogokidogo, unakuta kuna mradi ambao unapaswa ujengwe kwa shilingi bilioni sita unapeleka shilingi bilioni 900, hauko *serious*. Tabia hii ni lazima tuibadilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jimbo langu. Kule kwenye la Moshi Vijijini tuna mradi mmoja wa Kata ya Old Moshi Magharibi na niliwahi kuuliza kwenye swali la msingi hapa ulitangazwa toka mwaka 2012, tukaambiwa mkandarasi atakwenda *site*, kila tukiuliza tunaambiwa utaanza mwaka unaofuata mpaka leo huo mradi wa vijiji vya Telamande haujaanza. Naomba Waziri akija hapa atuambie huo mradi utaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii asilimia 46 wanayosema kwamba kuna maji, wanahesabu mpaka yale mabomba ya Moshi Vijijini yaliyojengwa na Lucy Lameck mwaka 1975 ambapo miundombinu yake imeshachakaa na vyanzo vingi vya maji hayo vimeshakauka, kwa hiyo na vyenyewe wanahesabu kwamba kuna maji. Ndiyo maana kuna watu wengine watu wa Kaskazini wasubiri kwa sababu wanafikiri kule kuna maji, sisi kule tuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kata yangu moja inaitwa Mabogini ina vijiji kumi ni vijiji vinnetu vina maji. Kule Mtakuja kwa Wamasai, Mserikia, Mawala kwa Mheshimiwa Mbatia, Mikocheni *TPC* hakuna maji, watu wanatafuta maji kama wanavyotafuta mafuta ya taa au petroli. Kwa hiyo, tunaomba muangalie mambo haya. *(Makofi)*

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi mkubwa ambao ulijengwa na Wajapani unaitwa *Moshi Lower Irrigation Scheme*. Mradi ule ni wa kisasa sana lakini na wenyewe kwa sababu hakuna *maintenance fund*, hakuna watumishi wenye weledi wa kuweza kusimamia *machines* ambazo zimeachwa kule, hakuna mashine hata moja inafanya kazi na sasa hivi unaanza kubomoka na huko kwenye hatari vilevile ya kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, huu utaratibu wa kutokupeleka fedha kwenye Wizara mbalimbali na hasa hii ya Maji maana yake ni kwamba *there is no value for money* kwa zile pesa za matumizi tunazotoa, unalipa mtu ambaye humtumii. Maana yake ni kama unatoa sadaka au ruzuku tu na hii ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi wa nchi hii. Ni lazima tusimamishe hayo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana Bunge lako liielekeze Serikali ichukue vipaumbele vichache vyenye matokeo makubwa kwenye uchumi wetu, iweke nguvu hapo na imalize miradi hiyo. Leo tunaenda kushika *Stigler's Gorge*, hatujaangalia uchumi wa gesi kule umeendaje, tunaenda kuangalia *Stigler's Gorge* kuna Mchuchuma na Liganga ambao unaweza kutupa umeme hatuendi, sasa tukifanya hayo mambo kwa mtindo huo hatutaweza kufika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kuchauka, wajiandae Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Boniphace Getere.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kama ilivyo ada watu wamezoea kuwasifia na kuwapongeza Mawaziri mimi leo naomba nisiwapongeze na sababu ya kutowapongeza wanaijua. Siyo kwamba

7 MEI, 2018

nawachukia ila sababu za kuacha kuwapongeza Mawaziri na watendaji wote wanazijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na sera ya kumtua mama ndoo kichwani, hivi takwimu tunazopewa huwa zinalenga nini? Kwa sababu takwimu hizi haziendani na uhalisia na ninyi Wabunge humu ndani ni mashahidi siku yoyote pakitokea swali la maji Bunge zima linalipuka kuonesha kwamba hali ya maji nchini ni mbaya. Hata hivyo, ukisoma vitabu, mimi hapa nimesoma nimeambiwa kwenye upande wa vijiji watu milioni 36 wanaopata maji ni milioni 30.9 asilimia 85; lakini bado Waziri akaendelea kusema lakini upatikaji wa maji katika vijiji ni asilimia 58, sababu aliyotoa ni usimamizi mbovu wa miradi ya maji. Kama kweli tuna sera ya kumtua ndoo kichwani ifikapo mwaka 2020 na huku kutokupeleka fedha kwenye miradi ya maji mbona hizi takwimu zinakwenda tofauti tofauti? Unawezaje kutekeleza hii sera wakati huo huo Serikali haipeleki fedha kwenye miradi ya maendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa hizi takwimu na hizi sera mnataka kumfurahisha nani kwa sababu hazina uhalisia. Kama kwenye miradi ya maji hampeleki fedha halafu mnasema ifikapo mwaka 2020 mnamtua mama ndoo kichwani. Mimi sielewi labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha anifafanulie zaidi sera hii maana yake ni nini lakini kama kwa namna hii ya upelekaji wa fedha kwenye Halmashauri zetu au kwenye miradi mbalimbali wa asilimia 22 halafu mnasema ifikapo 2020 mnamtua mama ndoo kichwani mimi siwezi kuelewa na wala sikubaliani na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nijielekeze kwenye miradi ya umwagiliaji. Nataka niseme Mheshimiwa Waziri kwenye hii miradi ya umwagiliaji tumefeli. Hakuna Mbunge hapa atasimama atasifia kwamba kweli halmashauri zake kuna miradi ya umwagiliaji imefanya vizuri sana, hakuna. Kwanza mimi naomba niwashauri hebu ondoeni kwanza utata nani msimamizi wa hii miradi ya umwagiliaji. Haiwezekani mradi wa umwagiliaji uko Liwale



7 MEI, 2018

kilometa 400 kutoka Mtwara halafu wasimamizi wa mradi eti wa Kanda watoke Mtwara waisimamie miradi Liwale halafu iende sawasawa, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mradi tangu unaanza inatakiwa yule mtaalam awe pale, *at least* kila baada ya siku mbili au tatu hata kama wiki atoke Mtwara aende Liwale akakague mradi, atakwenda kule mwezi mmoja umepita, wakandarasi wamefanya wanavyotaka halafu miradi inafeli na pesa zinapotea, mnasema kwamba mvua ilikuwa nyingi miradi imeharibika, si sawasawa. Hebu hii miradi mhakikishe inasimamiwa na Halmashauri, kama yule Mhandisi wa Maji yupo Wilayani tumpe huu mradi asimamie, tuone hii miradi ya umwagiliaji itafeli kama ilivyofeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nikisimama hapa naongelea Mradi wa Ngongowe. Mradi huu umeshaondoka na shilingi milioni 770 lakini umekufa. Nimeshaomba mara nyingi hapa ule mradi kama itawezekana, nasikia mwaka huu *JICA* wamekubali kuufadhili basi mtupe sisi halmashauri tuusimamie kwa sababu hawa watu wa Kanda wako mbali sana hata wawe na weledi wa namna gani, kwa shida ya usafiri tuliyonayo na barabara mabovu hizi, atoke Mtwara kila wiki aende Liwale kusimamia mradi wa umwagiliaji si sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri amesema kuna mipango ya ushirikishwaji wa ulinzi wa rasilimali maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona maelezo tu ni namna gani ushirikishwaji huu upo haeleleweki. Mpaka sasa hivi hatujaambiwa wameunda vikosi kazi kwenye vijiji gani, kwenye mabwawa au mito. Huu ushirikishwaji mnaosema hapa kwamba mna mpango wa ushirikishwaji wa ulinzi wa rasilimali maji, kwenye vitabu nimeuona, lakini kwenye uhalisia hatujauona kwamba ni mikakati gani imechukuliwa na Serikali katika kulinda hii miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona tu kweye karatasi imeandikwa lakini sijasikia kumeundwa *task force* ya namna gani, kijiji gani au halmashauri gani katika kutimiza hili lengo la ushirikishwaji. Kwa sababu haiwezekani Wizara ninyi mnaweza kulinda rasilimali maji bila kuwashirikisha wananchi, ni lazima muwashirikishe wananchi ili miradi hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia hii miradi ya maji hata ukiangalia ile miradi ya maji vijijini, fedha nyingi ni za wafadhili, fedha ya Serikali hapa hatuioni hata kama ipo ni kidogo sana na ndiyo hiyo ambayo haiji. Mheshimiwa Waziri nimeshamfuata mara nyingi ananiambia kinachotakiwa pale ni Mhandisi kuleta *certificate* ya miradi wao watalipa. Nataka niseme kwamba kwenye Halmashauri yangu *certificate* zipo nyingi kwenye Wizara yako lakini sijapata fedha. Hata bajeti ya mwaka jana nilivitaja vijiji ambavyo havina maji mpaka leo, vya Nangano, Kipelele, Kikuyungu, Naujombo, Kiangara, Mikunya, Kipule, Makata, Mkutano, Mlembwe na miradi ya maji ipo. Sasa sijaelewa hizo *certificate* ambazo Wizara inadai ni za namna gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niongelee vile vijiji ambavyo tayari vina maji. Vile vijiji ambavyo tayari vina mashine za maji tuna tatizo kubwa sana na mashine hizi zinazoendeshwa na dizeli. Mashine zinazoendeshwa na dizeli kwenye vijiji vyetu tunashindwa kumudu gharama ya maji kwa sababu unakuta ndoo inauzwa kuanzia shilingi 100 mpaka shilingi 200. Kwa mtu wa kijijini yuko tayari aende kilomita tano afuate maji kuliko kutoa shilingi 200 kununua ndoo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi ni katika Kijiji cha Mpigamiti ambacho kina mradi wa maji sasa hivi una takribani zaidi ya miaka tano lakini pale kijijini wanakosa fedha za kuendesha mradi ule. Kwa sababu mwisho wa siku wanakosa fedha za kununua dizeli kwa hiyo watu hawapati maji. Ushauri wangu ingewezekana kabisa miradi hii wakaanza kuipeleka kwenye *solar*, miradi ambayo inaendeshwa kwa mitambo ya *solar* inafanya vizuri sana.

7 MEI, 2018

Namshauri Mheshimiwa Waziri hii miradi ya vijiji iliyobaki badala ya kuelekeza kwenye mafuta tuelekeze itumie *solar*, hapo ndiyo itaweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sera ya kumtua mama ndoo kichwani naomba niirudie, hebu mtuletee *time frame*, mtuletee takwimu, mpaka leo hii mmeshafikia asilimia ngapi ya utekelezaji ili tuweze kuona kwamba je, itakapofika mwaka 2020 kweli mtafikia lengo? Hapa mnaleta tu takwimu za ujanja ujanja, hatuletewi ni asilimia ngapi kwamba mpaka sasa hivi mmefika asilimia ngapi, hatujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua nchi hii tuna tatizo kubwa la maji, leo hii nchi hii kuzindua kisima cha maji anaenda Rais. Hiki kitabu unakiona yaani Makamu wa Rais anamtwisha mama ndoo, anazindua kisima cha maji, hizi kazi wanafanya hata Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikichimba kisima pale kijijini kwetu Diwani anaenda kukizindua, lakini leo tunamtuma Rais akazindue kisima cha maji, muone jinsi gani tulivyo mbali. Tuko mbali na uhalisia ndiyo maana inakuwa hivyo yaani inaonekana ni jambo la ajabu mama kutua maji mpaka Rais, Waziri Mkuu, Waziri wanaenda, hizi ni kazi za Madiwani. Tatizo la maji ni kubwa kuliko hivyo mnavyofikiria. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Getere wajiandae.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji. La kwanza, niipongeze sana Wizara pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu, maji ni uhai wa binadamu mpaka wanyama. Mimi nitachangia kwa

kuanza na Mamlaka za Maji na madeni ya taasisi za Serikali. Taasisi za Serikali zinadaiwa fedha nyingi na Mamlaka zetu za Maji, inafika wakati hizi mamlaka zetu zinashindwa kujiendesha. Niiombe sana Serikali, la kwanza iweze kulipa pesa hizi za Mamlaka za Maji ili ziweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zetu za Serikali zinadaiwa fedha nyingi na Mamlaka za Maji inafika wakati mamlaka hizi haziwezi kujiendesha kabisa. Ni jambo la ajabu sana, mamlaka zinalalamika zinasema zikilipwa fedha na taasisi hizi zinaweza kujiendesha wao wenyewe. Ni jambo la ajabu sana ni kwa nini Serikali isiweze kulipa pesa hizi kwa Mamlaka za Maji ili hizi mamlaka ziweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi na wakiweza kujiendesha maana yake ni kupunguza mzigo kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, leo nina mambo machache, ni suala la shilingi 50 kuongezwa katika petroli na dizeli. Suala hili tunaiomba sana Serikali, lazima ifanye jitihada zake zozote zihakikishe inaongeza shilingi 50 kwenye Mfuko wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna muarobaini wa tatizo la maji kwenye nchi hii isipokuwa kuongeza shilingi 50. Nashangaa kwa nini Serikali haiwezi kukubaliana na maoni ya Wabunge wake. Sisi Wabunge tukisimama hapa kuchangia, siyo kama tumesimama Wabunge ni wananchi wa Tanzania ndiyo wamesimama hapa wanaishauri Serikali. Wametuleta hapa kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Mimi nashangaa sana, Serikali yetu hii kama Wabunge tunachangia, tunaishauri lakini haitaki kusikiliza mawazo yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, suala la kuongeza shilingi 50 kwenye mafuta ya petroli na dizeli lipewe kipaumbele ili tuweze kufika hatua ambayo tunaitaka. Ukiangalia bajeti iliyopita, asilimia 80 ya miradi ya maendeleo imefanywa na Mfuko wa Maji, siyo pesa za Serikali ni Mfuko wa Maji. Tukiongeza shilingi 50, tukiwa tuna shilingi 100,

7 MEI, 2018

tutafika mahali pazuri. Niiombe sana Serikali yangu, mimi naamini Serikali hii sikivu, Waziri wa Fedha yupo nimwombe aweze kulichukua hili jambo liweze kufanikiwa ili wananchi wetu waondokane na kadhia ya maji waliyo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuligusia ni suala la *DAWASCO* kuunganishwa na *DAWASA*. Ni jambo zuri sana limefanywa, Serikali imewaza jambo zuri lakini je, wamefanya tathmini ya kina jinsi ya kuendesha maana ziko mamlaka mbili kwenda mamlaka moja? Je, Serikali imefanya tathmini ya kina kuhusu gharama za uendeshaji hasa katika suala la mishahara, lazima tuliangalie kwanza. Kama sisi Kamati hatukuletewa lolote na tumewaomba Wizara waweze kutuletea ili tujue, je, kuondoka kuwa mamlaka mbili na kuwa mamlaka moja kuna-*benefit* yoyote? Isijekuwa tunaondoa baadae tukawa tunapata hasara katika Serikali yetu tukaja tukataka turejeshe. Niiombe Wizara ikae chini iweze kufanya tathmini ili tujue tunakwenda kwenye faida au hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pesa za India. Hizi pesa hata na mimi kule Zanzibar kwa kuwa niko Mkoa wa Mjini nitafaidika nazo sana. Niiombe sana Serikali, sijui pana tatizo gani, hebu Serikali ituambie, hizi fedha zina tatizo gani? Huu mwaka wa tatu tunazichangia hizi fedha ndani ya Bunge hili. Fedha hizi hazipatikani, tunashindwa kusaini, sijui kuna tatizo gani? Kuna tatizo gani hapa ili hizi fedha ziweze kupatikana kwani zikipatikana tunaweza kutatua tatizo kubwa sana la maji kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni la Tume ya Umwagiliaji. Tume ya Umwagiliaji bado ni tatizo lakini ili kuondoa matatizo ya Tume naiomba Serikali leo hii iweze kunisikiliza kwa makini. Naishauri Tume hii iondoke kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji ipelekwe kwenye Wizara ya Kilimo. Hili ni jambo jema sana, tukiiondoa Tume hii kutoka katika Wizara ya Maji tukaenda nayo katika Wizara ya Kilimo ndiyo hasa yale mahitaji ya wananchi wetu yatafika mahali tunapotaka. Tume hii ikibakia kwenye Wizara ya Maji na Tume hii shida yetu ni wakulima na maendeleo kwa wakulima

7 MEI, 2018

bado itakuwa ni shida. Tunaomba sana Serikali iiondoe Tume hii kutoka kwenye Wizara ya Maji ielekee kwenye Wizara ya Kilimo hapo ndipo tunaweza tukapata mafanikio katika nchi yetu kutokana na Tume hii ya Kilimo kwa sababu itafika pale ambapo wanataka iwaguse wananchi. Tukiibakiza katika Wizara hii tutakuwa tuna wakati wa kufanya *zero* na pasipo na Tume ya Umwagiliaji, ikafanya kazi vizuri kwenye nchi hii hapana kilimo wala hakuna maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu hii ukiitazama ina matatizo makubwa mawili; la kwanza ni tatizo la fedha ambalo limesemwa na kila Mbunge; lakini la pili kama walivyosema baadhi ya Wabunge ni tatizo la uwezo wa matumizi ya pesa zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwa mwaka huu Mheshimiwa Waziri alifanya ziara na alikuja Geita na yeye mwenyewe akawa anashangaa kuona maji hakuna, anashangaa kuona malalamiko ya maji yako nchi nzima lakini anasema ana takriban shilingi bilioni 50 kwenye akaunti na tatizo ni kwamba hakuna mtu analeta *certificate* kuonesha kwamba kuna kazi zinaendelea.

Kwa hiyo, ina maana tuna matatizo mawili, la kwanza inawezekana tuna tatizo la pesa ambalo ni dogo lakini tuna tatizo la uwezo wa kutumia pesa kutoka kwenye Wizara yenyewe na pengine inawezekana ni uwezo wa watu walioko chini kwenye Wizara wanaoweza kusababisha pesa zitumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atafute namna ya kuimarisha sana uwezo wa watu wake huku chini. Kuna lugha mbili zinazungumzwa hapa, Mheshimiwa Waziri anasema msiangalie sana *ring fence* ya bajeti yenu kwenye Halmashauri, anzisheni miradi, tengenezeni *certificate* mlete tulipe, lakini walioko kule chini wanaangalia kile ambacho wamepewa na Serikali ndiyo wanatangaza na pengine hawatangazi mpaka waambiwe pesa zipo. Kwa hiyo, inawezekana kuna tatizo la mawasiliano kati ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri na watu wake ndiyo maana malalamiko ni mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali, kwa miaka yote miwili mfululizo tumekuwa na tatizo kubwa sana la maji katika Mji wa Geita. Katika taarifa yake ukurasa wa 53 amekadiria kwamba hivi sasa upatikanaji wa maji katika Mji wa Geita ni kama takribani asilimia 37. Inawezekana takwimu hizi Waziri ameletewa lakini siyo kweli, Geita takwimu hizi ambazo nazipinga upatikanaji wa maji uko chini ya asilimia 15 na sababu ni kwamba maji yaliyoko Geita ambayo yanasukumwa na mgodi wa *GGM*, makubaliano ya uanzishwaji wa mradi ule ilikuwa Serikali ichangie asilimia 50 na mgodi asilimia 50, mgodi ukatumia shilingi bilioni 12; lakini Serikali ikatoa shilingi 400,000 peke yake. Kwa hiyo, matokeo yake ule mradi umekamilika lakini uwezo wake wa kufanya kazi unafikia kaya 1,700 peke yake. Mara nyingi Mji wa Geita hauna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi hivi karibuni *GGM* wamesema wanajiondoa kwenye uendeshaji wa mradi ule na sasa hivi *GEUWASA* walikuwa wanakusanya mapato bila kuingia gharama ya kupeleka umeme wala kusukuma umeme kutoka kwenye chanzo cha maji. Maana yake ni kwamba muda mfupi ujao *GGM* wakijiondoa, *GEUWASA* wanatakiwa waanze kujilipia mwenyewe gharama ya uendeshaji na mradi ule uko *category C*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu ya namna gani tunamaliza tatizo la

7 MEI, 2018

maji katika Mji wa Geita. *GGM* watakapoacha kusukuma maji kwa sababu wanasema gharama ni kubwa na walikuwa wanatumia pesa za *CSR* ambazo Serikali kupitia sheria tuliyorekebisha hapa Bungeni tumewanyang'anya sasa tumezipeleka halmashauri, kwa hiyo, hawana tena uwezo wa kutumia zile pesa na wao hawana fungu lingine kwa maelezo yao na kwa mwezi mmoja wanatumia milioni 70 maana yake ni kwamba *GEUWASA* hawana uwezo tena wa kusukuma maji, hata hii asilimia 15 tunayoipata sasa hivi haitakuwepo. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri aje na majibu ni namna gani ataondoa tatizo hili kwa sababu tumesubiri pesa za India leo mwaka wa tatu hazionekani na muda unakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi pale wa *LV-WATSAN* na kwa nini nimesema tunalo tatizo la matumizi ya pesa na usimamizi, huu mradi una pesa tayari shilingi bilioni sita, Waziri ametaja kwenye taarifa yake lakini mradi ambao ungekabidhiwa mwezi Novemba, 2016; leo Mei, 2018 mradi huu haujakamilika na mkandarasi hayuko *site*, maana yake ni nini? Amesema mradi huu utakabidhiwa Mei, namhakikishia Mheshimiwa Waziri sio kweli kwa sababu sisi tunatoka kule *site* tangu alivyoondoka matenki na mabomba yako vilevile na mkandarasi haonekani na kama anaonekana atakuwa anafanya kazi nje ya mkataba kwa sababu alishasimamishwa na Wizara na watu wanaomsimamia. Sasa kama pesa zilikuwepo shilingi bilioni sita na hakuna tatizo la pesa hapa lakini mradi hauendi leo mwaka wa tatu maana yake ni kwamba liko tatizo pia la uwezo wa kumsimamia huyu mkandarasi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri pengine leo atakuja na majibu sahihi kwamba huu mradi wa *LV-WATSAN* utakamilika lini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita tunashangaa kuona tunapokuja na bajeti ya visima, sisi tuko kilometa nane tu kutoka ziwani. Watu wa Shinyanga, Tabora na sehemu nyingine wangezungumzia visima nisingeshangaa, sisi tunataka maji ya ziwa. Pale kama Serikali itawekeza maji kutoka ziwani ukapandisha kwenye ule mlima ulioko pale



7 MEI, 2018

Geita, maji yatashuka yenyewe kwa *gravity* kwenda mpaka Kahama, kwa nini tunahangaika na visima katikati ya Mji wa Geita ambavyo kiangazi vyote vinakauka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini moja ya miji inayokuwa haraka sana kutokana na shughuli za madini na mwingiliano wa watu ni Mji wa Geita. Nimeona humu kwenye ripoti ya Waziri wamekadiria wanapeleka maji kwa watu 130,000, sisi Geita pale tunaamini kuna zaidi ya watu 300,000 sasa hivi na tunahitaji maji mengi sana ili tuweze kuendelea na shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii ametupatia shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuongeza mtandao wa maji. Mwaka jana walitupatia tena shilingi bilioni mbili ambazo zilitupa kama kilometa 80 za mtandao wa maji. Tatizo kubwa tulilionalo ni maji machache ambayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Taska Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa King Musukuma.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umechangia vizuri sana mpaka umejisahau, kaa. (*Kicheko*)

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia jioni ya leo katika bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchangia Wizara hii ya Maji kwangu mimi naomba Mungu anisaidie nipate akili ya kusema vizuri kwa sababu ninaweza nikaruka humu Bungeni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu aliwahi kusema ni bora kuongoza maskini mwenye matumaini kuliko kuongoza maskini asiye na matumaini na maskini mwenye matumaini ni yule aliyelima mihogo au ana shamba anaweza kumkopa mwenzake fedha kwa kumuomba kwamba mahindi yake yakifika atauza atamlipa lakini yule ambaye hana kitu kabisa huyo ni maskini asiye na matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili mimi naona ni maskini nisiye na matumaini maana kila bajeti inayokuja sioni kwenye Jimbo langu la Bunda kuna chochote mle ndani. Kwa hiyo, inavyofika wakati huu naona kwamba hivi Bungeni humu nafanya biashara gani humu ndani? Si bora tu nitoke nikachunge ng'ombe huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Bunda na Bunda kwa ujumla kuna miradi mbalimbali na mimi nashangaa watu wanasema hamna fedha, nadhani fedha zipo ila usimamizi wake ni kidogo sana au tuna ugonjwa unaoitwa *D by D*, hii ambayo wataalam wametupatia. Wizara ya Maji inatoa fedha kwenda kwenye Halmashauri, mamilioni ya fedha yanaenda, watekelezaji wa miradi ile ni watu wa TAMISEMI, wahandisi wako TAMISEMI na pengine hata Waziri wa TAMISEMI au Naibu wake, watumishi wake hawajui fedha ngapi imeenda huko, inajulikana kwa Wizara ya Maji tu peke yake. Waziri wa Maji anapokwenda kukagua maji anakuta fedha zimeliwa. Ukimuuliza Waziri sasa huyu achukuliwe hatua gani anakwambia mimi hao siyo wangu mpaka niende kushauriana na Mheshimiwa Jafo, hii biashara hatuiwezi hii, hii biashara itakuwa ngumu sana.

Kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia huu ugonjwa wa *D by D* tunaufanyaje katika hizi Wizara mbili, vinginevyo tutapata shida sana na ndiyo maana tumeshauri hapa mara kwa mara kwamba Wakala wa Maji Vijijini uwepo ili Waziri apewe vitu vyote, fedha na watu wake aweze kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie miradi ya Wilaya ya Bunda kwa ujumla, tuna Mradi wa Kibara shilingi milioni

400, zimetumika pale kama shilingi milioni 300 na zaidi maji hayatoki, lakini kwenye taarifa utaonesha maji yanatoka. Kuna Mradi wa Buramba, shilingi milioni 353, maji hayatoki, kuna Mradi wa Kinyambwiga shilingi milioni 395, maji hayatoki, kuna Mradi wa Kwing'ombe shilingi milioni 700, mradi umeisha na Mwenge ukafungua, maji hayatoki, kuna Mradi wa Nyamswa Salamakati, shilingi milioni 252 zimetumika, maji hayatoki, kuna Mradi wa ufadhili wa Bomamaji, walikuja wafadhili pale Bomamaji wakatoa shilingi milioni 987 zimeliwa, ripoti ikatolewa haifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mkubwa wa maji wa Bunda ambao bomba lake linatoka Nyabeho nao unasuasua. Mbaya zaidi kuna mradi wa Mgeta, Nyang'aranga zikatolewa shilingi milioni 495 zimefika shilingi milioni 910 maji hayatoki na Waziri ameshafika pale akiwa Naibu Waziri. Sasa hili linakuwa ni tatizo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ni kwamba ukimuuliza Waziri hapa nimezungumza habari ya malambo kule kwetu sisi Bunda malambo hayo ndiyo visima tunaita, ndiyo ng'ombe na binadamu wanakunywa. Tukamwambie atutengenezee malambo ambayo yalitengenezwa na Chifu Makongoro yatatusaidia huko tunapokwenda, akakubali hapa Bungeni kwamba atatengeneza hayo malambo akasema leteni mpango. Tumepeleka mpango tukamkabidhi Katibu Mkuu wa Wizara, kuidhinisha huo mpango uende kujengwa ukija kumuuliza Waziri anakwambia malambo sichimbi mimi, anachimba Wizara ya Kilimo lakini Wizara hii ya Maji ndiyo yenye malambo. Sasa najjuliza hii ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba kiasi cha shilingi bilioni moja bajeti ya 2016/2017 hatukuitumia, Halmashauri ya Bunda haikupata taarifa. Bajeti ya mwaka 2017/2018 tumewekewa shilingi bilioni moja tumeleta mpango wa maji wa malambo sita hayachimbwi wala hamna kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Bunda una mradi mkubwa wa maji na kuna kitu kinaitwa chujio. Mimi

nimwombe Waziri, pale wanasema kuna shilingi bilioni 12, wanasema ni nyingi labda hizi ni za wizi. Sasa kama ni za wizi ngapi zinatoshwa kwa sababu katika kuchimba, mimi siyo mtaalamu lakini katika mambo ya kuchimba hilo chujio kuna vitu vinaitwa *clarifier, flocculant, rapid sand, refilter*, mitambo na kuna vitu vingi mleni. Wataalam wa Wizara si waende waangalie kwamba ni fedha ngapi zinatoshwa kuweka hiyo chujio. Kwa sababu maji ya Bunda kila siku yanaletwa maji machafu, kila Waziri anayekuja mnanyweshwa maji machafu kwa nini sasa msipeleke wataalam watu ambie hili chujio badala ya shilingi bilioni 16 ni bilioni ngapi? Wakati fulani tunaweza tukawa tunawalaumu watu tu kwamba mkandarasi amekula, amefanyaje, twendeni tukajiridhishe na mradi huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumze habari ya fedha, tumezungumza mwaka jana kwenye bajeti Sh.50 kuongezeka kwenye mafuta kwa ajili ya kupata fedha za kuhudumia maji lakini imekuwa wimbo. Sasa Wabunge tukubaliane, wakati fulani mimi nasema na tutaendelea kusema, humu ndani tukifa wote watasema Wabunge wa Tanzania wamekufa, hawatasema CCM wala CHADEMA. Ifike muda tukubaliane kwamba kwenye mambo yale ambayo tunakubali ni halali tuache UCCM wala UCHADEMA tukubaliane hoja. Kwa nini tunaweka shilingi 50 kwenye mafuta iende kwenye maji halafu haiwekwi, nani anaizua na sisi ndiyo wawekaji wa fedha? Kwa hiyo, nafikiri Waziri anapokuja hapa atuambie anafanyaje kuhakikisha kwamba hiyo fedha kwa kipindi hiki itakuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri, najua wakati fulani tukisema haya mambo yanamgusa Waziri, Naibu na watendaji wake, lakini watu hawa nao ni wapya. Hebu tuweke mtazamo mzuri, hivi Waziri anaposema shilingi bilioni moja imekwenda Bunda, lakini haikutumika, anatulaumu sisi Wabunge, hivi nani ana utaratibu wa kuwaambia Halmashauri fulani kwamba jamani kuna fedha zenu hapa mbona hatujaona *proposal* yenu ya kuanzisha miradi? Kwani wataalam wa Wizara ya Maji wana kazi gani? Kwani nani anaweza kujua mradi Bunda iko miradi mitano

wanaandika imekamilika lakini haitoi maji, nani anaweza kujua? Ina maana Wizara ya Maji haina watu wa *IT* ambao wanaoweza kujua vitu hivi? Siku hizi watu wanafanya vitu kwenye *computer* kwa nini haya mambo hayafanyiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua bajeti tutampitishia Mheshimiwa Waziri najua na wewe una bidii sana ya kufanya kazi lakini mimi kwangu uadilifu si hoja. Kwangu mimi mtu awe mwadilifu na awe mbunifu. Unaweza kuwa na mwadilifu anakaa na hela tu kwenye droo hapo watu wanakufa bila maji. Kwa hiyo, tunajua Waziri wewe ni mwadilifu jitahidi kufanya *innovative* na *creative* kwenye ofisi yako ili watu waweze kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe ile *proposal* yangu ya Bunda ya malambo, sisi malambo ndiyo visima, atupitishie ili watu wakapate maji. Toka mwaka 2008 hii miradi imeanza kuzungumzwa humu ndani na bajeti zinakuwepo, lakini haitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae Mheshimiwa King Musukuma na Mheshimiwa Musa Ntimizi.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nichangie Wizara ya Maji. Kwanza kabisa napenda kumpa pongezi Waziri wa Maji, Mheshimiwa Isack Kamwelwe kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya kwenye Wizara hii. Pia napenda nimpongeze Naibu wake, Mheshimiwa Aweso, wote kwa pamoja mnajitahidi kufanya kazi ya kutatua matatizo ya maji ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niungane na Wabunge wenzangu waliochangia kuhusu kuongeza shilingi 50 kwenye petroli na dizeli ili iweze kusaidia bajeti ya maji kwa kupata chanzo kikubwa cha

kuendeleza miradi ya maji. Naungana na Wabunge wenzangu waliounga mkono hoja ya kuongeza shilingi 50. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Maji. Bajeti ya Wizara ya hii ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya maji nchini Tanzania na mikoani kote. Kila mahali unapoenda iwe ni vijijini, wilayani na *city center* ni kilio cha maji. Niiombe Serikali iongeze bajeti ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naenda moja kwa moja kwenye Mkoa wangu wa Katavi. Mkoani kwangu Katavi, Wilaya ya Mpanda tunalo Bwawa linaloitwa Milala. Bwawa hili limechimbwa miaka mingi tangu enzi za ukoloni, enzi za Mpeluki kwa wale wanaotoka Katavi wanafahamu lilikuwepo toka kabla ya uhuru. Bwawa hili lilikuwa linatumika ku-*supply* maji pale Mpanda Mjini kwa matumizi ya wananchi wote wa Manispaa ya Mpanda. Sasa hivi bwawa hilo haliwezi kutumika tena kwa sababu lina viboko wengi wamezaliana pale, wanakula mazao ya wananchi, mipunga, mahindi, wanachafua maji kiasi kwamba yale maji ya bwawa hilo hayawezi kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ya Maji na Umwagiliaji ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii iwatoe hawa viboko ili yale maji yaweze kutumika. Manispaa ya Mpanda, kata nyingi hazina maji, Kata za Mpanda Hoteli, Ilembo, Magamba na Shanwe, zote hizo hazina maji. Kwa kusafisha haya maji yaliyoko kwenye Bwawa la Milala litafanya kata hizi ziweze kupata maji. Nimeshawahi kupeleka hili swali ili lije hapa Bungeni niliulize, lakini nashangaa limechukua miaka miwili halijaletwa hapa kuhusu kuhamishwa viboko hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukichukulia kwamba hilo bwawa liko mjini pale Mpanda, zamani lilikuwa ni nje ya mji lakini sasa hivi limezungukwa. Kwa hiyo, kuwa na viboko ni hatari na kuna shule ya sekondari ya Mwangaza iko karibu na hilo bwawa, watoto wa shule wanakwenda pale kuchota

maji na viboko wenyewe huwa wanatembea kutoka kwenye bwawa hilo wanakuja mpaka Mpanda Mjini. Niombe sana Serikali na Waziri Mheshimiwa Kamwelwe iweze kututatulia hilo tatizo la viboko Mpanda Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia suala la viboko, niende moja kwa moja kwenye suala la maji ya visima. Kwanza Mpanda tunashukuru kwa visima vya maji lakini niombe sana vile visima ambavyo vinatumia mkono muangalie uwezekano wa kuweka *solar* ili wale akina mama wa vijijini na hasa wazee waweze kuchota maji yale. Muweke *pump* inayotumia umeme na *tape* ili akina mama wale waweze kuchota maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vingi vimechimbwa kule lakini havijakwisha na vingi ni vya ku-*pump* na akina mama vijijini ambao hawana nguvu wanashindwa ku-*pump* yale maji. Mnaweza mkatumia umeme wa *solar* kwa sababu umeme wa *REA* haujapita kwenye vijiji vyote vya Mpanda na ukizingatia kwamba Mkoani kwetu Katavi hakuna umeme wa gridi. Niombe basi uweze kutumia umeme wa *solar* ili akina mama wa Mkoa wa Katavi waweze kufaidika na maji haya ya visima ambavyo vinaendelea kuchimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napende kuzungumzia miradi iliyoko Mkoani Katavi; tunao mradi wa Ikorongo II ambao utaleta maji kwenye vijiji vya Magamba. Nafahamu Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba lipo tank la Mwanamsenga kule Ilembo ambalo halifanyi kazi limechoka. Niombe likarabatiwe ili vijiji vile vya Magamba viweze kufaidika na maji hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba vile visima vinajengwa kule Mkoani kwetu Katavi ni *temporary*. Nimwombe Mheshimiwa aharakishe kuleta mradi mkubwa Mkoani Katavi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika ili yaweze kusambazwa Mkoa mzima wa Katavi. Maji ya visima ni *temporary measure*, utakapoletwa mradi mkubwa wa kutoka Ziwa Tanganyika utaweza ku-*supply* vijiji vingi vya Mkoa wa Katavi na Waziri anafahamu miundombinu ya mkoa wetu si

7 MEI, 2018

rafiki. Kwa kupata maji haya inaweza ikawarahisishia akina mama shughuli nyingine za biashara ambazo wanaweza wakafanya kutokana na haya maji yatakayotoka Ziwa Tanganyika. Maji haya pia yataweza kusaidia mikoa ya jirani kama Mkoa wa Rukwa, mkoa wetu wa zamani ambao tulikuwa pamoja, haya maji yanaweza yakafika pale kwa kupitia Jimbo la Kavuu mpaka Sumbawanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la umwagiliaji. Kule mkoani kwetu Katavi miradi ya umwagiliaji iko nyuma sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri miradi ambayo ilikuwa imeanzishwa Mkoani kwetu Katavi ifuatiliwe ili iweze kuendelea. Miradi ilianzishwa lakini mimi kama mimi sijaona ile miradi kwamba imekwisha na hatuelewi ilifikia wapi na taarifa kama vile Wabunge wengine wamekuwa wanazungumza inatakiwa ieleweke ile miradi huwa inakuwa chini ya nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa umwagiliaji Kata ya Ugala lakini jinsi ulivyoisha sielewi uliishaje na sielewi ulikuwa chini ya usimamizi wa nani na maelezo yake hayaeleweki. Niiombe Wizara ya Maji ijaribu sana kuwa inafuatilia kwa ukaribu miradi yote ya maji ambayo inaanzishwa humu nchini ili kuona kwamba mradi huu umegharimu shilingi ngapi na zimebakia shilingi ngapi na wamelipwa shilingi ngapi. Kama mradi umetolewa pesa na haujakamilika basi wale watu wanaohusika na hiyo miradi waweze kuwajibika. Tunaona tu kwenye makaratasi kwamba kuna mradi huu wa maji lakini miradi inakuwa haijaisha na pesa hazijulikani zimekwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie suala hili la maji. Napenda sana kumshukuru Rais kwa hatua aliyoichukua jana pale Morogoro kumpigia simu Katibu Mkuu wa Maji lakini nafikiri hili suala lilikuwa ndani ya Waziri mwenyewe wa Maji na Naibu wake kufuatilia ile miradi ya maji. Basi niombe wawe wanaifuatilia kwa karibu ili suala la maji lisilete tatizo sehemu nyingine. *(Makofi)*



7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu maji taka kwenye Mkoa wetu wa Katavi. Miundombinu ya maji taka ya Mkoa wa Katavi bado, nimwombe Wazir Kitengo cha Majitaka kiweze kufuatiliwa kwa sababu ule mkoa ni mpya lakini suala la...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa King.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa King Musukuma, Mheshimiwa Ntimizi tunamaliza na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaingia Bungeni hapa nilijifunza kupitia Wizara tatu ambazo zilikuwa *pressure* kubwa sana kwa Wabunge wote ambazo ni Wizara ya Maji, Wizara ya Afya na Wizara ya Ujenzi. Sasa najiuliza mara mbili mbili sielewi ndiyo maana sasa hivi wanawake wana kamsemo wanasema wanawake wanaweza. Hivi kwa nini *pressure* ya Wizara ya Afya imeisha kabisa yaani hata nilikuwa nasikiliza Wapinzani wanashauri lakini Wizara hii kila mwaka humu ndani lazima tulumbane, kuna tatizo gani Wizara ya Maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona hata Rais akienda kwenye ziara huko mikoani kwetu anapata *pressure* na maswali mengi na mabango ya maji. Ndugu yangu, rafiki yangu Kamwelwe kwani wewe huwezi kumaliza matatizo yako ukawa mbunifu kama Mheshimiwa Ummu alivyofanya kwenye Wizara sumbufu kabisa ya Afya? Gari mpya umepewa, mafuta yapo, ukija mikoani tatizo dakika mbili

7 MEI, 2018

huyo kwenye ziara kwa Mkuu wa Mkoa, hukai na walengwa/wawakilishi wakakuambia matatizo? Huwezi kuyamaliza haya matatizo kwa kuja unajifungia kwenye *air condition* kwa Mkuu wa Mkoa unaenda kuonyeshwa miradi tu iliyofanya vizuri, miradi mibovu hauonyeshwi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongee kidogo na Mheshimiwa Waziri. Tunaona kuna zoezi linaendelea kwamba wakandarasi wengi wamelipwa asilimia 80 lakini kazi hazifanyiki. Nataka nikwambie Waziri mtawafunga wakandarasi wote. Hii miradi ya maji ya Benki ya Dunia asilimia 90 ya wakandarasi waliofanya hizo kazi wengi wameuziwa nyumba na wengine wame-*paralyze* kwa sababu mnawasainisha mikataba ya mabilioni ya hela halafu hela haziendi. Mtu anafanya kazi, amekopa benki bilioni aki-*rise certificate* ya 500 inakuja baada ya miezi tisa nyingine miaka mitatu, nyumba imeuzwa na *pressure* anayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Waziri asiunde Tume ikachunguza hizi hela zinarudi Wizarani kwako. Nataka nikwambie usiposikia ushauri wetu utapambana na maswali bajeti ijayo. Kule Wizarani kwako kuna watu wanacheza na watu wa huko Halmashauri hela zikija zinarudi kwako huko huko. Mimi nimekuwa Meya nafahamu, nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri nafahamu, makampuni ya ushauri ambayo yanatutia hasara kwenye Halmashauri zetu yako ndani, ni ya watumishi wa Wizara yako na unao. Sasa ni bora ukasikiliza mawazo ya Wabunge ukaunda Tume ikaenda kuchunguza, kama hauwezi umuombe Spika aunde Tume ya Wabunge ikachunguze hili suala tukija bajeti ijayo mzee tusikuulize haya maswali mengi mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuuliza rafiki yangu Mheshimiwa Waziri na ulipita jimboni kwangu, hivi kweli kitabu kizima cha kurasa 200 na kitu hata shilingi milioni tano hamna kwenye jimbo langu au ni *style* gani tuitumie kuomba? Jimbo langu mimi asilimia 85 ni ziwa, lakini hatuna maji, kweli Waziri hata kisima kimoja? Labda wengine humu tumekuwa kwa bahati mbaya au mtufundishe *style* ya kuomba ili tuweze kupata angalau hata visima viwili. Mbunge unajadili bajeti

nzima ya mabilioni unatoka humu unasifia tu wenzio hata kisima kimoja hamna, kweli Mheshimiwa Waziri? Nisikitike sana lakini nina imani wewe mzee ni msikivu na ni mtani wangu utatekeleza, nadhani utaangalia hata kwenye ukokoukoko huo utupie hata visima vitatu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na suala la kuongeza shilingi 50 kwenye mafuta. Nashauri kabisa kama walivyoshauri Wabunge wengine, Wabunge wote tuazimie na wewe ufanye kazi ya kubanana na sisi ile shilingi 50 iongezwe. Sisi wengine huku vijijini bado tuna uhitaji mkubwa sana wa maji. Mheshimiwa Waziri nilishawahi kukwambia kwamba kwangu kuna mradi umeshapitwa na Wabunge watatu walionitangulia wa shilingi bilioni 1.2 skimu ya umwagiliaji, mashamba ya watu mmechukua, kutengeneza hamtengenezi, mmeleta shilingi milioni 200 zimeisha kugawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri Wizara yako hii Wahandisi wa Maji wengi walioko kule Wilayani kwetu siyo Wahandisi wa Maji ni *Environmental Engineer* ndiyo wanaokuangusha. Jaribu kufanya paranja, ma-*engineer* wa maji wapo wengi vyuo vikuu vinatoa acheni kufanya upendeleo kuweka watu wasiohusika. Mtu wa mazingira na visima wapi na wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu namheshimu sana nilitaka nichangie tu hapo lakini nikwambie Mheshimiwa Waziri kama alivyosema Mbunge mwenzangu wa Geita unavyosema asilimia za maji zilizoko Geita watu wanatushangaa sisi humu Wabunge ndani. Hebu jaribu uje hata ziara ya kushtukiza uone hizo asilimia unazozitaja kwenye kitabu haziko Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi mingi imekwama, Chankorongo na Mharamba kwenye jimbo langu haitekelezeki. Mtu anamaliza mradi wa shilingi bilioni tano anakabidhi wiki moja hautoi maji, lakini ukija wanakuchukua unakaa kwa Mkuu wa Mkoa unateleza na *air condition*.

7 MEI, 2018

Mimi nikuombe sana Mheshimiwa Waziri sihitaji kubishana na wewe mzee wangu, baada ya Bunge hebu njoo mkoani kwangu ufanye ziara, hasa Jimbo la Geita Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ntimizi, ajiandae Mheshimiwa Kingu.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Maji ambayo ni Wizara muhimu sana katika maisha yetu na ya wananchi wetu, hasa sisi watu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza na mimi nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Injinia Kamwele, mdogo wangu Naibu Waziri na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na changamoto nyingi za maji tulizonazo katika maeneo yetu na nchi yetu lakini kwa kweli wanajitahidi kutimiza wajibu wao. Pamoja na bejeti ndogo wanayopata lakini maeneo mengi wanajitahidi kufika na kutatua kero zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo naomba nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Waziri na watendaji wake, bajeti zilizopita nilikuwa nazungumzia sana shida ya maji katika Jimbo langu la Igalula, ukizingatia mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Viktoria unaokuja katika Mkoa wetu wa Tabora, Jimbo langu la Igalula lilikuwa halimo katika maeneo yanayopata maji kutoka Ziwa Victoria. Nilijaribu kuomba mara mbili, tatu kwamba, kama kuna uwezekano tuone uwezekano wa kupata maji mbadala wakati maji ya Ziwa Viktoria tunategemea yatakuja hapo baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sasa miradi imeanza kuja jimboni kwangu, mradi wa Igalula tumepata zaidi ya shilingi milioni 380, tumekarabati bwawa kubwa la maji lilipo pale Igalula na sasa tunaelekea kupata maji ya uhakika katika Jimbo letu la Igalula hasa katika Kata ya

Igalula. Pia upembuzi yakinifu unaendelea kufanyika katika mradi wa Kata ya Nsololo na Goweko, wataalam wameshakwenda, nina hakika maji yatapatikana muda si mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Loya na Tura tuna bwawa kubwa sana kuliko Bwawa la Kazima lililo katika Manispaa ya Tabora Serikali kupitia Wizara ya Maji imekubali sasa kuuwekea miundombinu mradi ule mkubwa wa maji wa Tura, nina hakika sasa wananchi wangu wa Jimbo la Igalula tutapunguza kero kubwa ya maji tuliyokuwanayo, nashukuru kwa kazi kubwa inayofanyika.

Naomba pia nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *TRL* kwa kukubali lile bwawa walilochimba *TRL* liweze kutumiwa na wananchi wangu wa Tura kwa kuwekewa miundombinu na Wizara baada ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kukubali kuweka miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote niliyoyaeleza, nilitaka nitoe ushauri kidogo ili tuendeleo kutatua changamoto ya maji, najua hatuwezi kumaliza matatizo ya maji kwa mara moja, lakini kuna namna ambayo tunaweza tukafanya tukaendelea kupunguza matatizo ya maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema maeneo yangu ya Jimbo la Igalula tumejaribu kuchimba visima vingi virefu na vifupi, upatikanaji wa maji umekuwa ni mdogo sana na siyo katika Jimbo la Igalula tu maeneo mengi ya Mkoa wetu wa Tabora visima vinachimbwa lakini baada ya mwezi mmoja visima hivyo vinakuwa havitoi maji. Ushauri wangu ni kwamba Serikali sasa iwekeze kwenye uchimbaji na utegaji wa mabwawa ambayo mara nyingi yanasaidia sana upatikanaji wa maji ya uhakika. Zile fedha nyingi tunazozipoteza katika kuchimba visima nadhani sasa Serikali ijipange na mradi mkubwa wa kuangalia maeneo yanayoweza kuchimbwa mabwawa yakachimbwa mabwawa na yakawekewa miundombinu inasaidia sana

kupunguza kero ya maji kuliko hizi fedha zinazoendelea kupotea katika visima tunavyovijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mimi kwangu Igalula tuna bwawa lilichimbwa mwaka 1970, mwaka huu zimetolewa shilingi milioni 380 tumelirekebisha lile bwawa, tumeliwekea miundombinu, watu takribani 20,000 wanapata maji kupitia mradi ule wa bwawa lakini tungechimba kisima cha shilingi milioni 40 kisingeweza kutoa maji ya kutosha watu takribani 40,000 wa Kata ya Igalula. Kwa hiyo, Wizara ije na mpango mahsusi katika maeneo yetu nchi nzima, hata kama tutapata kidogo kidogo, lakini tuanze kufikiria sasa kuchimba na kutega mabwawa ili wananchi wetu waweze kupata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la miradi ya umwagiliaji. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa, na mimi nataka miradi hii haijapewa umuhimu wa kutosha. Naomba Wizara iangalie umuhimu wa miradi hii ya umwagiliaji. Miradi hii ya umwagiliaji ina faida zake, kwanza wananchi wetu wanapata maji ya uhakika, lakini wananchi wetu watasaidiwa upatikanaji wa chakula; wananchi wetu watapata kipato kutokana na mazao yatakayopatikana katika ule mradi wa umwagiliaji, lakini pia halmashauri zetu zitakusanya kodi kwa sababu uzalishaji utakuwa mkubwa, watapata kodi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine wananchi wetu wataondokana na umaskini. Wanapokuwa na uhakika wa chakula maana yake wananchi wetu hawatakuwa ombaomba na wananchi wetu wataweza kusomesha watoto wao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya umwagiliaji iwekewe fedha na sio itengewe tu fedha, fedha ziende kwenye miradi hii. Tusipofanya hivi wananchi wetu watakosa faida kwa sababu miradi mingi ya umwagiliaji inatengewa fedha, inafanyiwa *feasibility study*, inafanyiwa kila kitu, lakini mwisho wa siku haitengewi fedha na kwenda kutekelezwa, hili ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa maji, kuna miradi wamezungumza Waheshimiwa Wabunge haitekelezeki kutokana na kutopelekwa fedha. Niiombe Wizara ijipange miradi yote ambayo ilitengewa fedha na haijakamilika ipelekewe fedha ikakamilike nchi nzima. Tunapoteza fedha za walipa kodi na mwisho wa siku wananchi wanakuwa hawatuelewi, shida ya maji inaendelea kuwepo na fedha zimepelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maeneo mkandarasi amekimbia *site*, aidha, kwa kutolipwa fedha au mwingine ameshindwa kuiendeleza ile miradi. Wale ambao wameshalipwa fedha, kama walivyosema wenzangu, Wizara lazima iwachukulie hatua hawa wakandarasi, aidha kuwashitaki au kuhakikisha wanarudi *site* kuikamilisha miradi iliyoanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Wizara hii imepumulia zile shilingi 50 tulizowawekea kwenye tozo ya petroli, Mawaziri wanajua bila fedha hii miradi yote ambayo imetekelezwa isingeweza kutekelezeka. Kwa hiyo, kwa sababu tumeweza kupumulia shilingi 50 na miradi mingi imeonekana katika katika maeneo yetu, wazo langu nataka Bunge hili liungane tuhakikishe safari hii kieleweke, shilingi 50 lazima iongezwe kwenye bei ya petroli na fedha hiyo iende kwenye miradi ya maji. Kwa sababu sisi ni waathirika hasa sisi tunaotoka vijijini, safari hii hakitaeleweka hapa kama shilingi 50 itakataliwa kuongezwa, tunataka ifike shilingi 100. Kama kwa shilingi 50 tumeweza kufanya miradi mikubwa mingi kiasi hiki na sisi tuliahidi kumtua mama ndoo kichwani kijijini, miaka inazidi kwisha, tunataka shilingi 50 iongezwe ili twende tukatekeleze miradi iliyopo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuishukuru sana Wizara hii. Changamoto wanazokutana nazo ni kwa sababu ya shida kubwa ya maji tuliyonayo katika maeneo yetu. Tunaomba wasikate tama, waendeleo kufanya kazi, sisi tuko pamoja nao na Mungu atawabariki sana. *(Makofi)*

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa na mimi niungane na baadhi ya Wabunge wenzangu kuwapa pongezi Waziri wa Maji, Mzee wangu Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Aweso. Kwa kweli, wanasema mnyonge mnyongeni, watu hawa wanajitahidi kujituma *regardless* ya changamoto za kifedha ambazo zipo katika Wizara yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Mkumbo. Profesa Kitila, kaka yangu huyu kwa kweli, hongera sana *brother*, tunaona kuna mabadiliko yanaonekana na unatuwakilisha vizuri watu wa Singida pia kwenye Wizara hii, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wenzangu kuishauri Serikali na hapa naomba tuelewane. Najua Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, sisi tunapozungumza kama Wabunge tunazungumza kwa niaba ya wananchi walipa kodi wa hii Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wabunge tumesema tunahitaji shilingi 50 ziingizwe kwenye petroli na dizeli kwa ajili ya kuwasaidia wapiga kura wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuishii kuagiza fedha hizi ziingizwe, tunatoa rai fedha hizi zikiingizwa, Wizara ya Fedha tunawataka sisi kama Wabunge, fedha hizi ziende Wizarani zikatatue kero na changamoto ya maji kwa wananchi wetu. Itakuwa ni jambo la aibu kama tutawapa wananchi wa Tanzania *burden* hii, fedha hizi ziingie zikatumike katika mipango ambayo Bunge hili halikuwa limependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua Mheshimiwa Waziri wa Maji, najua unyenyekevu wako mzee wangu na Waziri wa Fedha, mama yangu Mheshimiwa Kijaji, wewe



7 MEI, 2018

ulikuwa mwalimu wangu, huyu mzee mkimpa fedha mimi nina imani kwa jinsi ninavyomjua huyu mzee tatizo na changamoto za maji, mnyonge mnyongeni...

**MWENYEKITI:** Mu-*address* kama Mheshimiwa Waziri au Mbunge.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, Wizara ya Fedha tunachowaomba hizi shilingi 50 tunaomba ziende Wizara ya Maji wakafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna watu wengine wanakuja wanachangia kuhusiana na mradi wa *Stigler's*. Mimi nataka niwaambie, Ilani ya *TANU* kipindi cha nyuma, kwa watu mnaosoma historia, acha sisi watu wa Chama cha Mapinduzi, Mradi wa *Stigler's* umekuwepo kwenye Ilani ya *TANU* enzi za Mwalimu Nyerere, la kwanza. La pili, ndugu zangu tuache kushikiwa akili na Wazungu. Miradi yote ambayo Taifa linajua italeta tija Wazungu wanakuja wanasema *environmental problem*, achacheni na haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachotaka Bwawa la Kidunda lijengwe, mradi huu wa *Stigler's Gorge* ukatekelezwe. Kinachotakiwa Serikali chukueni maamuzi magumu kafanyeni *serious land conservation*. Kuna mambo yataumiza watu, lakini fanyeni kwa maslahi ya vizazi vinavyokuja na kwa maslahi ya hili Taifa. Haiwezekani leo tuogope kutekeleza mradi kwa sababu tu kuna watu wanapiga kelele kwa maslahi ya Wazungu, tuwaache Wazungu wawili/watatu wakavae bukta wapige picha tuache kutengeneza mradi wa nchi kwa maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, megawati 2,400 zitaweza ku-*curb problem* ya umeme ambayo nchi tumekuwa nayo toka uhuru. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Serikali, kama Rais wetu alivyosimamia sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tunawakilisha watu wengi humu ndani, nendeni

7 MEI, 2018

mkatekeleze mradi wa *Stigglers Gorge* kwa maslahi ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia hata ma-*researchers* wanavyosema, angalia gharama za uzalishaji umeme kwa kutumia mambo ya *thermo technology*, angalia mambo ya gesi, angalia mambo ya *wave* za bahari, angalia mambo ya *nuclear*, gharama ya uzalishaji umeme kwa njia ya maji ni ndogo, Wazungu wanajua. Hapa tunazungumzia tunajenga treni ya umeme itakwenda kuendeshwa na umeme upi? Kwa hiyo, tuwe wajanja hasa ninyi watu wa Serikali, simamemi imara kuhakikisha kwamba kile mnachoki-*dream* sisi tunawaunga mkono, tekelezeni kwa maslahi ya wapiga kura wa Jamhuri hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nataka nilizungumze, Mheshimiwa Waziri nakuomba mzee wangu, kuna Wabunge wamechangia na mimi naunga mkono. Profesa Kitila Mkumbo kaka yangu, unda Tume ukachunguze kuna miradi hapa ya maji imefanyika, mfano mmoja ni kwangu, kuna miradi ya maji imetumia *billions of shillings* za walipa kodi haifanyi kazi. Nenda pale kwangu kuna Kijiji kinaitwa Nkwairree zaidi ya shilingi milioni 200 zimekwenda, jana nimetoka kufanya mkutano jimboni kwa wapiga kura mradi haufanyi kazi, watu wamepiga pesa, haya mambo hayawezekani. Hatuwezi kuruhusu Taifa letu fedha za walipa kodi zinatumika watu wanakwenda wanafanya miradi ambayo haina tija *at the end of the day* mradi unakwisha maji hayatoki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga pale kuna mradi ulitekelezwa kutoka Igunga kwenda mpaka kule Isakamaliwa. Nimeondoka nikiwa kama *DC* pale, *DP* zote hakuna *centre* hata moja inatoa maji. Watu wame-*relax* Wizarani *as if nothing has happened*, pesa za walipa kodi zimekwenda. Haya mambo kama kweli tunataka kumsaidia Rais na kuwasaidia wapiga kura na kwa maslahi ya chama chetu tuendelee kutawala na kushika dola lazima tutende haki na kuhakikisha kwamba tunawapelekea watu wetu maji. (Makofi)

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, Mheshimiwa Waziri ulikuja jimboni kwangu, nakushukuru sana mzee wangu ukazindua mradi wa maji pale Sepuka na ulituahidi na najua kwa sababu Profesa Kitila Mkumbo uko hapa, Mheshimiwa Waziri alituahidi kutuchimbia visima vingine tisa katika maeneo yafuatayo; Mayaha, Misake, Iseke, Mpetu, Kaugeri, Ufana, Puma na Mpugizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba kwa heshima na taadhima na unajua sasa Profesa Kitila Mkumbo hapa na wewe ni *home boy*, hebu basi bwana fanya mambo yako huko kwa maslahi ya wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Singida Magharibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri nakuomba utakapokuwa unamaliza majumuisho ya Wizara yako uje na kauli ya kuwahakikishia watu wa Jimbo la Singida Magharibi kwamba kero za maji, kwa mfano, kuna maeneo mzee wangu niliyasema kuna watu wanabeba ndoo za maji kutoka Kata ya Kijiji cha Mlandala...

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Mheshimiwa Profesa Mkumbo ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa Taifa zima.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, basi bwana kwa heshima kwa sababu huyu Mbunge pia ninamheshimu basi, lakini kwani hujui kwamba Profesa Kitila Mkumbo ni mwenyeji wa Singida? Nimeipokea taarifa yake kaka yangu huyu, naomba niendeleo kumalizia mchango wangu. Natambua kama huyu bwana ni Katibu

7 MEI, 2018

Mkuu wa nchi nzima lakini wewe kubali tu bwana huyu ni wa kwetu pia Singida kule bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumaliza kwa kusema Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dokta John Joseph Pombe Magufuli, mimi nataka nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, toka nimekua kwenye kijiji nilichozaliwa mpaka nimefikisha umri wa kuwa Mbunge sijawahi kuona miradi mikubwa ya maji kitekelezeka kama kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napozungumza Waziri umeleta fedha shilingi milioni 300 tumechimba maji Mtunduru, shilingi milioni 300 tumechimba maji Irisya, shilingi milioni 81 tumechimba maji Mwaru, shilingi milioni 210 tumesambaza maji Sepuka, shilingi milioni 81 tumesambaza maji Nkwairee japokuwa mradi huu nimesema una matatizo, lakini kwa juhudi kabisa Mheshimiwa Waziri nataka nikupongeze wewe na Naibu wako, ahsanteni sana. Njoooni tena tuendeleo kutatua changamoto za maji kwenye jimbo langu, Mungu awabariki, endeleeni kuisimamia na kuitekeleza Ilani ya chama changu ili CCM tuendeleo kushika dola na tuendeleo kuwatumikia wananchi wa hii Jamhuri na walipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii. Kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na miradi ya maji; kama walivyozungumza Wabunge wenzangu, kwa nini miradi haikamiliki Mheshimiwa Waziri? Kwangu kuna visima vinne vimechimbwa katika vijiji vya Mima, Iyoma, Bumila pamoja na Mzase. Tangu mwaka juzi, mwaka 2016 umeleta

wakandarasi, sawa, sasa wako pale karibu mwaka mzima hawafanyi kazi yoyote, hakuna fedha na inatakiwa upeleke shilingi milioni 426. Sasa Mheshimiwa Waziri hivi tutakuwa tunawachambia watu visima halafu inakuwa kama *white elephant*, watu wanaangalia tu kwamba tuna kisima hapa, miaka mitatu, miaka minne, kisima hakikamiliki, kwa nini sisi Wabunge tusilalamike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri Miradi ya *World Bank* imechukua miaka kumi, mingine imekamilika juzi, mingine haijakamilika. Kwa mfano, Kijiji cha Kimagai ndiyo mradi umekamilika juzi, miaka kumi Miradi ya Benki ya Dunia. Sasa tatizo ni fedha au tatizo la wakandarasi? Naona tatizo ni wajkandarasi hamuwalipi. Bunge sisi kama Bunge tunatenga fedha, tunakaa hapa miezi mitatu, tukishapitisha bajeti haiendi kwenye miradi, inakuja nusu tu, hizi fedha zinakwenda wapi huko Hazina? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Musukuma, nadhani ipo haja ya kuunda Tume ichunguze Wizara hii fedha zinakwenda wapi? Miradi haikamiliki, miaka kumi, miaka nane? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa katika nchi hii ni maji, ni shida kubwa sana, kila kijiji ukienda tatizo ni maji. Sasa ahadi tulishaahidi, Ilani ya Uchaguzi kwamba mkinichagua nitahakikisha mnapata maji, sasa Mheshimiwa Waziri unatutakia mema kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana peleka Jimbo la Mpwapwa shilingi milioni 426 ili wakandarasi waweze kukamilisha miradi hii ya maji. Mpwapwa Mjini tunatumia maji ya chumvi, ni kweli wanasema siyo kila aina ya maji ya chumvi yana madhara tumboni kwa sababu yale maji yanapimwa, unachukua *sample* inapelekwa kwa Mkemia Mkuu wanaangalia mambo mawili, wanafanya *chemical analysis* pamoja na *bacteriological examination*. Kama yana madini yanayoweza kudhuru afya ya binadamu ama kama kuna *bacteria*, maana maji mengine yanaleta homa ya matumbo lakini wamepima yanafaa.

7 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri ukienda Wilaya ya Mpwapwa, hasa Mpwapwa Mjini, ujaribu kuonja yale maji ndiyo binadamu wanakunywa. Kwa hiyo, nakuomba na nilikwishaiomba Serikali ifanye utafiti kuna sehemu ambazo ukichimba kisima cha maji kuna maji baridi, tuwaonee huruma wananchi wa Mji wa Mpwapwa jamani wanateseka. Kweli maji yapo lakini ni ya chumvi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.  
*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji wa leo imekwisha na muda wetu umekwisha. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 8 Mei, 2018 ,Saa Tatu Asubuhi)*